



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI



RIPOTI KUU

YA MWAKA

YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

KUHUSU UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA ZA

SERIKALI KUU

KWA MWAKA ULIOISHIA 30 JUNI 2018

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

**RIPOTI KUU YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI
MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

**KUHUSU UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA ZA SERIKALI
KUU KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2018**





Uwasilisho

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI



Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, 4 Barabara Ukaguzi, S.L.P. 950, 41104 Dodoma. Simu ya Upepo: 'Ukaguzi' D'Salaam, Simu: 255(026) 262179, Tarakishi: 255(026)2171527, Barua pepe: ocag@nao.go.tz, tovuti: www.nao.go.tz

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na.CFA.27/249/01/2017/2018

28 Machi 2019

Mh. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu,
S.L.P. 9120,
1 barabara ya baraka obama, 11400 dar es salaam.

YAH: KUWASILISHA RIPOTI KUU YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI JUU YA UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA ZA SERIKALI KUU KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2018

Kulingana na Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa 2005), pia Kifungu Na. 34 (1)(c) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 pamoja na Kanuni ya 88 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009, ninawasilisha kwako ripoti yangu ya ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Taasisi za Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 18.

Wako mtiifu;


Prof. Mussa Juma Assad

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Yaliyomo

1 Uwasilisho	ii
2 Yaliyomo	iii
3 Orodha ya Majedwali	v
4 Orodha ya Vielelezo	x
5 Mamlaka ya Ofisi	xvi
6 Vifupisho	xviii
7 Dibaji	xxi
8 Shukrani	xxiii
9 Muhtasari	xxiv
1 Sura ya Kwanza	58
Maelezo ya Awali	58
2 Sura ya Pili	63
Hati za Ukaguzi	63
3 Sura ya Tatu	69
Hali halisi ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi na Maagizo ya Kamati ya PAC	69
4 Sura ya Nne	81
Ukaguzi wa Bajeti ya Serikali	81
5 Sura ya Tano	105
Mamlaka ya Mapato Tanzania	105
Deni la Serikali	138
Pensheni	150

Hesabu Jumuiifu.....	158
6 Sura ya Sita.....	167
Tathmini ya Mifumo Ya Udhhibiti wa Ndani na Utawala Bora	167
7 Sura ya Saba.....	183
Ukaguzi wa Rasilimali Watu na Mishahara	183
8 Sura ya Nane	192
Ukaguzi wa Wakala za Serikali na Taasisi Nyingine.....	192
9 Sura ya Tisa	232
Ukaguzi wa Manunuzi na Usimamizi wa Mikataba	232
10 Sura ya Kumi.....	257
Usimamizi wa Matumizi	257
11 Sura ya Kumi na Moja	283
Ukaguzi wa Mali na Madeni ya Wazabuni na Watumishi	283
12 Sura ya Kumi na Mbili	296
Kaguzi Maalum na Ukaguzi wa Vyama vya Siasa	296
13 Viambatisho.....	337

Orodha ya Majedwali

Jedwali Na. 1: Uchambuzi wa Ukaguzi wa Serikali Kuu na Taasisi zake	59
Jedwali Na. 2: Taasisi mpya zilizotambulika	60
Jedwali Na. 3: Idadi ya Kaguzi Maalumu zilizofanyika	61
Jedwali Na. 4: Orodha ya Taasisi zenye Hati yenye Shaka	65
Jedwali Na. 5: Mchanganuo wa Hati za Ukaguzi zilizotolewa kwa mwaka 2017/18	66
Jedwali Na. 6: Jwenendo wa Hati za Ukaguzi Kwa Mfululizo wa Miaka Mitatu.....	68
Jedwali Na. 7: Maana ya maneno yaliyotumika kutathmini hali ya utekelezaji	70
Jedwali Na. 8: Uwiano wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018	72
Jedwali Na. 9: Melekezo ya Kamati ya PAC kwa Mwaka 2017/18	75
Jedwali Na. 10: Hali Halisi ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi ya Miaka iliyopita kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali.....	79
Jedwali Na. 11: Mchanganuo wa Bajeti ya Makusanyo	83
Jedwali Na. 12: Makusanyo yaliyopokelewa Mfuko Mkuu	90
Jedwali Na. 13: Tofauti zilizoonekana kati ya Taarifa za kutoa Fedha na Taarifa za fedha zilizoandaliwa na wizara.....	91
Jedwali Na. 14: Makadirio, Fedha zilizotolewa na Matumizi Halisi ya ya Fedha za matumizi ya kawaida kwa miaka Mitano (Kiasi katika Sh billioni)	93
Jedwali Na. 15: Makadirio, Fedha zilizotolewa na Matumizi Halisi ya Fedha za maendeleo kwa miaka Mitano (Kiasi katika Sh. billioni).....	96
Jedwali Na. 16: Mwenendo wa makusanyo yasiyotokana na kodi kwa miaka mitano Mfululizo (Kiasi katika Sh)	98
Jedwali Na. 17: Makusanyo yasiyotokana na Kodi ambayo hayakuwasilishwa Mfuko Mkuu	101
Jedwali Na. 18: Utofauti ulioonekana katika Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti na Taarifa ya fedha katika wizara	103
Jedwali Na. 19: Idadi ya mapendekezo yaliyotolewa kwa miaka iliyopita kwa kila Idara.....	106

Jedwali Na. 20: Mwelekeo wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyopita	106
Jedwali Na. 21: Jumla ya makusanyo kwa mwaka 2017/18 kwa idara (Shilingi kwa mamilioni)	107
Jedwali Na. 22: Mwelekeo wa makusanyo ya mapato kwa Tanzania na nchi za Afrika Mashariki, 2013/14 - 2017/18 (Shilingi kwa milioni).....	109
Jedwali Na. 23: Mwenendo wa Misamaha ya Kodi kuanzia mwaka 2013/14-2017/18 (Shilingi kwa mamilioni)	121
Jedwali Na. 24: Magari yaliyoingia nchini kwa muda maalum lakini hayakutoka nje ya Tanzania.....	127
Jedwali Na. 25: Makontena (makasha) yenye bidhaa zilizoharibika	129
Jedwali Na. 26: Bidhaa/mizigo iliyokaa muda mrefu katika bandari, na bandari kavu bila kodi kukusanywa.....	129
Jedwali Na. 27: Bidhaa ambazo zimeuzwa nje ya nchi (Export goods) ...	131
Jedwali Na. 28: Ukuaji wa Deni kwa miaka mitatu 2015/16 hadi 2017/18.....	139
Jedwali Na. 29: Vyanzo vya Deni la nje hadi 30 Juni 2018	142
Jedwali Na. 30: Vyanzo vya Deni la nje kwa mwaka 2017/2018	144
Jedwali Na. 31:Ulinganisho wa Muundo wa deni la nje kwa miaka mitano	145
Jedwali Na. 32 : Sampuli ya malimbikizo yaliyolipwa kwa mifuko ya Pensheni.....	148
Jedwali Na. 33: Majalada ya wastaafu yaliyokaguliwa 2017/2018	152
Jedwali Na. 34: Makosa katika ukokotozi wa mafao ya hitimisho la akazi	153
Jedwali Na. 35: Majalada yaliyocheleweshwa	154
Jedwali Na. 36: wekezaji wa Mitaji uliokosa Ufafanuzi wa Kina	159
Jedwali Na. 37: Uwekezaji ambao thamani yake imebaki ile ya mwaka uliopita	159
Jedwali Na. 38: Taasisi zilizotoa ufananuzi wa Mali za Kibaiolojia	160
Jedwali Na. 39: Mashirika yanayodhibitiwa yenye tarehe tofauti za kutoa taarifa.....	163
Jedwali Na. 40: Taasisi za Washirika na Ubia zisizoshirikishwa katika hesabu Jumufu.....	165

Jedwali Na. 41: Wakala wasiokuwa na Bodi za ushauri	169
Jedwali Na. 42: Mlinganisho wa Tathmini ya Udhhibiti wa Ndani.....	173
Jedwali Na. 43: Tathmini ya Kamati ya Ukaguzi	176
Jedwali Na. 45: Orodha ya Taasisi ambazo hazikuwa na Mpango wa Uhitaji wa Mafunzo na Mafunzo kwa Watumishi.	185
Jedwali Na. 46: Orodha ya Baadhi ya Taasisi zilizokata Makato makubwa katika mishahara.....	186
Jedwali Na. 47: Ulinganifu wa Bajeti kuu na makusanyo ya fedha kutoka vyanzo vya ndani	193
Jedwali Na. 48: Ulinganifu wa Fedha za matumizi ya kawaida zilizoidhinishwa na fedha iliyotolewa	194
Jedwali Na. 49: Ulinganifu wa Fedha za Maendeleo ziliyoidhinishwa na fedha iliyotolewa	196
Jedwali Na. 50: Ukusanyaji wa Maduhuli kutumia vyanzo vya ndani	197
Jedwali Na. 51: Taasisi ambazo hazikutakiwa kuhamisha Fedha kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina	198
Jedwali Na. 52: Miradi inayoendelea	200
Jedwali Na. 53: Uwekezaji wa Nyumba usio na Tija, Bunju	202
Jedwali Na. 54: Fedha ambazo hazikupelekwa TARURA.....	204
Jedwali Na. 55: Fedha za ucheleweshaji wa kazi ambazo hazijakusanywa.....	205
Jedwali Na. 56: Mapungufu katika Makubaliano ya Ubia	209
Jedwali Na. 57: Kasi ya chini ya Uzalishaji wa vitambulisho vya Taifa ...	212
Jedwali Na. 58: Idadi ya wateja wanaosubiria huduma ya umeme	213
Jedwali Na. 59: Miradi ya REA iliyochelewa ya Awamu ya I na II.....	214
Jedwali Na. 60: Fedha pungufu zilizotolewa kwa Miradi ya Maji.....	215
Jedwali Na. 61: Fedha za maendeleo zilizotumika kwenye matumizi ya kawaida	216
Jedwali Na. 62: Trekta ambazo hazina umiliki wa pamoja.....	217
Jedwali Na. 63: Fedha ambazo hazijarudishwa	218
Jedwali Na. 64: Fedha ambazo hazijarejeshwa na Wizara ya Afya	219
Jedwali Na. 65: Madeni yasiolipika	220
Jedwali Na. 66: Madai yasiokusanywa	221
Jedwali Na. 67: Wakala waliofanya malipo bila Mkataba na Zabuni	223

Jedwali Na. 68: Taasisi za Serikali zisizokuwa na hati Miliki ya Ardhi	224
Jedwali Na. 69: Malipo yasiyokuwa na risiti za kielektroniki-EFD	225
Jedwali Na. 70: Mchanganuo wa Sampuli ya Msingi wa Tabaka la Saruji ya Lami.	229
Jedwali Na. 71: Kazi zilizolipwa kabla ya Kufanyika	453
Jedwali Na. 72: Taasisi ambazo hazikuandaa Ripoti za Manunuzi.....	239
Jedwali Na. 73: Taasisi zilizotakiwa kufanyiwa uchunguzi na PPRA	245
Jedwali Na. 74: Muhtasari wa mapungufu yaliyobainika kwenye ankra za matibabu.....	260
Jedwali Na. 75: Mihutasari wa miamala yenye utata	261
Jedwali Na. 76: Muhtasari wa Kodi za Zuio ambazo hazikukatwa	266
Jedwali Na. 77: Malipo ya madeni ya nyuma ambayo hayakuoneshwa ...	270
Jedwali Na. 78: Fedha ambazo hazijarejeshwa kutoka kwenye akaunti ya Amana.....	272
Jedwali Na. 79: Malipo yaliyofanyika kimakosa kwenye vifungu visivyostahili	274
Jedwali Na. 80: Orodha ya malipo yasiyo na tija	275
Jedwali Na. 81: Malipo yaliyofanyika bila kuidhinishwa	277
Jedwali Na. 82: Malipo yasiyostaki kutoka kwenye akaunti za amana....	278
Jedwali Na. 83: Bakaa la Amana ambayo hazijatumika muda mrefu	278
Jedwali Na. 84: Orodha ya Taasisi zenye madai yaliyokataliwa	279
Jedwali Na. 85: Matumizi yaliyolipwa zaidi	281
Jedwali Na. 99: Ukosefu wa Nyaraka za Umiliki wa Ardhi na Majengo ya Umma	285
Jedwali Na. 100: Taasisi ambazo hazina Mpango wa Matengenezo na Kumbukumbu za Matengenezo ya Mali za Kudumu.....	286
Jedwali Na. 101: Taasisi ambazo zimeshindwa kufanya mapitio ya thamani na muda uliobaki wa matumizi ya Mali za Kudumu.....	287
Jedwali Na. 102: Taasisi zilizoonekana na mapungufu katika usimamizi wa Mali zilizotaifishwa	289
Jedwali Na. 103: Taasisi zenye madeni tarajiwa	291
Jedwali Na. 104: Mtiririko wa deni la Hospitali za India.....	294
Jedwali Na. 105: Madeni ya Hospital za India.....	294

Jedwali Na. 106: Masurufu ambayo hayakupita kwenye mfumo - Wizara	314
Jedwali Na. 107: Maelezo yenye nyaraka pungufu au yasiyokuwa na nyaraka	315
Jedwali Na. 108: Mwenendo wa Mauzo kutoka Mwaka 2016 mpaka 2018	329
Jedwali Na. 109: Mwenendo wa gharama za uendeshaji kutoka Mwaka 2016 mpaka 2018.....	329
Jedwali Na. 110: Orodha ya vyama vya siasa vyenye matumizi yenye nyaraka pungufu	332

Orodha ya Vielelezo

Kielelezo Na. 1: Uwiano Utekelezaji wa Mapendekezo ya niliyotoa miaka iliyopita kwa Taasisi kwa Mwaka 2017/18.....	71
Kielelezo Na. 2: Uwiano wa Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi kwa Taasisi- 2017/2018	72
Kielelezo Na. 3: Jumla ya Mapendekezo ya Ukaguzi kwa 2017/18 ikilinganishwa na 2016/17	73
Kielelezo Na. 4: Ulinganifu wa hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi kati ya 2016/2017 na 2017/2018	74
Kielelezo Na. 5: Uwiano wa Idadi ya Maelekezo kwa Taasisi za Serikali Kuu 2017/2018	76
Kielelezo Na. 6: Kiwango cha Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya PAC kwa M/F 2017/2018	77
Kielelezo Na. 7: Halisi ya Utekelezaji wa mapendekezo niliyoyotoa kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali.....	79
Kielelezo Na. 8: Mgawanyo wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo.....	84
Kielelezo Na. 9: Makadirio ya Bajeti pamoja na Makusanyo kutoka katika vyanzo vilivyotambulika kwa Mwaka wa fedha 2017/18 (Kiasi katika Sh. Bilioni)	86
Kielelezo Na. 10: Mwenendo wa Makadirio ya Serikali kwa Miaka Mitano (Kiasi katika Sh Bilioni).....	87
Kielelezo Na. 11: Mwenendo wa Makusanyo ya Serikali kwa Miaka Mitano (Kiasi katika Sh Bilioni).....	87
Kielelezo Na. 12: Mwenendo wa Makadirio na Makusanyo ya Serikali kwa Miaka Mitano	88
Kielelezo Na. 13: Mwenendo wa Makusanyo ya ndani na Mikopo kwa mfululizo wa miaka mitano.....	90
Kielelezo Na. 14: Makadirio, Fedha zilizotolewa na Matumizi Halisi ya ya Fedha za mKielelezo Na. 15: atumizi ya kawaida kwa miaka Mitano (Kiasi katika Sh billioni)	94
Kielelezo Na. 16: Matumizi halisi ya Kawaida na Maendeleo	97
Kielelezo Na. 17: Makusanyo yasiyotokana na Kodi kutoka katika Wizara na Idara za serikali.....	98
Kielelezo Na. 18: Makusanyo yasiyotokana na kodi katika sekretarieti za Mikoa	99

Kielelezo Na. 19: Makusanyo yasiyotokana na Kodi katika Balozi	100
Kielelezo Na. 20: Uwiano wa Makusanyo halisi Kwa Idara kwa mwaka 2017/18.....	108
Kielelezo Na. 21: Mwenendo wa Ukuaji wa Deni la serikali kwa Miaka Mitano, 2013/14 hadi 2017/18	138
Kielelezo Na. 22: Ukuaji wa Deni kwa miaka mitatu 2015/16 hadi 2017/18.....	140
Kielelezo Na. 23: Vyanzo vya Deni la nje hadi 30 Juni 2018	142
Kielelezo Na. 24: Sababu za kuongezeka kwa deni la nje, 2015/16 hadi 2017/18.....	143
Kielelezo Na. 25: Vyanzo vya Deni la nje kwa mwaka 2017/2018.....	144
Kielelezo Na. 26: Muundo wa deni la nje kwa Unafuu wa masharti.....	145
Kielelezo Na. 27: Tathmini ya Ukaguzi wa Ndani	174
Kielelezo Na. 28: Tathmini ya Kamati ya Ukaguzi	176
Kielelezo Na. 29: Tathmini ya usimamizi wa vihatarishi.....	178

Orodha ya Viambatisho

Kiambatisho Na. 1: Orodha ya Taasisi Zenye Hati Zinazoridhisha	337
Kiambatisho Na. 2: Taasisi zilizopata hati yenye shaka na mapungufu yaliyopelekea hati hiyo.....	349
Kiambatisho Na. 3: Vyama vya Siasa vilivyopata Hati Yenye Shaka na Mapungufu yaliyosababisha Hati hiyo	353
Kiambatisho Na. 4: Vyama vya Siasa vilivyopata hati isiyoridhisha na mapungufu yaliyopelekea hati hiyo	354
Kiambatisho Na. 5: Vyama vya Siasa vilivyopata hati mbaya na mapungufu yaliyopelekea hati	356
Kiambatisho Na. 6: Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa miaka uliopita	358
Kiambatisho Na. 7: Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi ya miaka iliyopita	365
Kiambatisho Na. 8: Makadirio, Fedha zilizotolewa na Matumizi halisi ya Fedha za Matumizi ya Kawaida	369
Kiambatisho Na. 9: Makadirio, Fedha zilizotolewa na Matumizi halisi ya Fedha za Maendeleo	373
Kiambatisho Na. 10: Makadirio na Makusanyo ya Mapato yasiyotokana na Kodi	376
Kiambatisho Na. 11: Makusanyo yasiyotokana na Kodi katika Balozi	380
Kiambatisho Na. 12: Kesi katika mamlaka za rufaa za kodi ambazo bado kuamuliwa	382
Kiambatisho Na. 13: Muhtasari wa mapato yaliyokusanywa na Mamlaka kwa niaba ya Taasisi nyingine	382
Kiambatisho Na. 14: miradi iliyowezeshwa na mikopo mipya iliyotolewa kwa Serikali kwa mwaka 2017/18.	383
Kiambatisho Na. 15: Miradi Muhimu iliyofadhiliwa kwa deni la nje 2017/18.....	389
Kiambatisho Na. 16: Uwiano usio sahihi wa Vifungu vya hesabu za taasisi na hesabu jumuiifu.....	390
Kiambatisho Na. 17: Utofauti wa 'line items' kati ya hesabu jumuiifu na hesabu za taasisi binafsi.....	392
Kiambatisho Na. 18: Utofauti kati ya 'line items' ya hesabu za taasisi na Hesabu Jumuiifu.....	393

Kiambatisho Na. 19: Hesabu zilizojumuishwa kwenye hesabu jumuiifu bila kusainiwa/kutolewa na mamlaka husika	394
Kiambatisho Na. 20: Uwasilishwaji usio sahihi wa madeni uliotokana na uondoshwaji wa zaidi/pungufu	397
Kiambatisho Na. 21: Washirika na Ubia wenye tarehe tofauti za kufunga hesabu.....	398
Kiambatisho Na. 22: Taasisi zenye upungufu kwenye ukaguzi wa ndani	401
Kiambatisho Na. 23: Taasisi Zenye Mapungufu Kwenye Kamati ya Ukaguzi	404
Kiambatisho Na. 24: Taasisi zenye Mapungufu Kwenye Usimamizi wa Vihatarishi.....	408
Kiambatisho Na. 25: Taasisi zenye Mapungufu Kwenye Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)	409
Kiambatisho Na. 26: Tathmini ya Ubadhirifu	412
Kiambatisho Na. 27: Watumishi Wanao Kaimu Nafasi za Ukuu wa Idara	414
Kiambatisho Na. 28: Orodha ya Taasisi Zilizopitiwa na kukutwa na upungufu wa Watumishi.....	414
Kiambatisho Na. 29: orodha ya Taasisi zenye Usimamizi Usiofaa Katika Malipo ya Watumishi.....	417
Kiambatisho Na. 30: Ulinganisho wa uwezo wa Makusanyo ya ndani kufanikisha Bajeti matumizi ya kawaida na maendeleo ya Wakala wa Serikali	419
Kiambatisho Na. 31: Mchanganuo wa Makisio yaliyopitishwa na kiasi cha fedha kilichotolewa.....	421
Kiambatisho Na. 32: Mchanganuo wa Makusanyo Halisi na Makisio ya Mapato ya Ndani	424
Kiambatisho Na. 33: Taasisi zilizohamisha fedha kwenda Mfuko Mkuu wa Hazina	426
Kiambatisho Na. 34: Riba ya uchleweshaji wa malipo kwa wahandisi na washauri	427
Kiambatisho Na. 35: Kutorejeshwa kwa fedha zilizokopwa	429
Kiambatisho Na. 36: Miradi ya TBA iliyochelewa Kukamilika	430

Kiambatisho Na. 37: (A) Tozo za ucheleweshaji wa kazi (Liquidated damages) hazijahamishiwa TARURA.....	434
Kiambatisho Na. 38: Idadi ya wapangaji wasio na mkataba.....	437
Kiambatisho Na. 39: Orodha Ya Taasisi Za Serikali Zenye Madeni	438
Kiambatisho Na. 40: Orodha ya Taasisi za serikali zenye madai.....	442
Kiambatisho Na. 41: Mapungufu katika ukaguzi wa Matumizi.....	449
Kiambatisho Na. 42: Manunuzi yaliyofanyika bila kuwepo kwa Ushindani.....	454
Kiambatisho Na. 43: Manunuzi ya bidhaa, Kazi na huduma bila idhini ya bodi ya zabuni	455
Kiambatisho Na. 44: Malipo ya Bidhaa, Kazi na Huduma bado kupokelewa	459
Kiambatisho Na. 45: Manunuzi toka kwa Wazabuni wasio idhinishwa	462
Kiambatisho Na. 46: Bidhaa na Huduma ambazo hazikukaguliwa	464
Kiambatisho Na. 47: Bidhaa na Huduma zilizo nunuliwa bila uwepo wa mikataba	467
Kiambatisho Na. 48: Mapungufu yaliyojitokeza katika mchakato wa Manunuzi, Mikataba na Utekeleaji wa Miradi	467
Kiambatisho Na. 49: Miradi ya Ujenzi Iliyochelewa Kukamilika	476
Kiambatisho Na. 50: Vifaa vilivyonunuliwa bila kuingizwa kwenye vitabu	478
Kiambatisho Na. 51: Mapungufu yaliyobainishwa na Mhakiki Mali.....	480
Kiambatisho Na. 52: Makosa Mengine ambayo hayakuwa na Athari za Kifedha	483
Kiambatisho Na. 53: Matumizi yasiyo na nyaraka toshelezi	487
Kiambatisho Na. 54: Malipo yasiyo na risiti za kielektroniki	488
Kiambatisho Na. 55: Orodha ya malipo yenye dosari katika usimamizi wa Masurufu	489
Kiambatisho Na. 56: Majengo yaliyotelekezwa, Ujenzi usiokamilishwa na Viwanja visivyoendelezwa	492
Kiambatisho Na. 57: Kuwapo kwa Rejista ya Mali za Kudumu Isiyo Timilifu	493

Kiambatisho Na. 58: Magari ambayo hayatumiki kwa muda mrefu bila kufanyiwa matengenezo au kuuzwa.....	494
Kiambatisho Na. 59: Taasisi zenye mapato ambayo hayajapokelewa	495
Kiambatisho Na. 60: Taasisi zenye matumizi ambayo hayajalipwa	496

Mamlaka ya Ofisi

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi Taifa ya Ukaguzi-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

(Imeundwa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania).

Wajibu na majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yameainishwa kwenye Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyofanyiwa marekebisho mara ya mwisho mwaka 2005) na kufafanuliwa zaidi na Kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008 (iliyofanyiwa marekebisho) na Kanunu za Ukaguzi wa Umma ya za Mwaka 2009.

Dira ya Ofisi

Kuwa Taasisi ya Hali ya Juu katika ukaguzi wa sekta ya Umma.

Dhamira

Kutoa Huduma za Ukaguzi wa Sekta ya Umma Zenye ubora wa Hali ya Juu Zinazoimarisha utendaji, Uwajibikaji na Uwazi Katika Usimamizi wa Rasilimali za Umma

Misingi ya Maadili

Uadilifu	Sisi ni asasi adilifu inayotoa huduma kwa namna isiyo na upendeleo
Ubora	Sisi ni wanataaluma wanaotoa huduma zenye ubora kwa kuzingatia viwango kubalifu vya ukaguzi.
Uaminifu	Tunahakikisha kuwa na kiwango cha juu cha uaminifu na kuzingatia Utawala wa sheria.
Kuwalenga watu	Tunamakinikia zaidi matarajio ya wadau wetu kwa kujenga utamaduni mzuri wa kuhudumia mteja na kuwa na watumishi wataalamu na wenye motisha ya kazi.
Ubunifu	Tunamakinikia zaidi matarajio ya wadau wetu kwa kujenga utamaduni mzuri wa kuhudumia mteja na kuwa na watumishi wataalamu na wenye motisha ya kazi.
Kujielekeza kwenye matokeo	Sisi ni taasisi inayojikita kwenye mafanikio kulingana na malengo tuliyojiwekea
Kufanya Kazi kwa Kushirikiana	Tunafanya kazi pamoja kama timu, kujadiliana kitaalamu na kubadilishana maarif

Vifupisho

Na.	Kifupisho	Maelezo
1.	AAFP	Alliance for African Farmers Party
2.	ACGEN	Mhasibu Mkuu wa Serikali
3.	ADA(TADEA)	African Democratic Alliance Party
4.	ADC	Alliance for Democratic Change
5.	ADEM	Wakala wa Usimamizi na Maendeleo ya Elimu
6.	AFIS	Mfumo wa Utambuzi wa Alama za Vidole
7.	AFRM	Mpango wa kujitathimni kwa Nchi za Afrika
8.	AG	Mwanasheria Mkuu wa Serikali
9.	AGITF	Mfuko wa Udhadini wa pembejeo za kilimo
10.	AO	Afisa Masuuli
11.	APP	Mpango wa Manunuzi wa Mwaka
12.	ASA	Wakala wa Mbegu za Kilimo
13.	BOQ	Mchanganuo wa Gharama za Ujenzi
14.	BoT	Benki Kuu ya Tanzania
15.	BRT	Mabasi Yaendayo Haraka
16.	BVR	Mfumo wa Kidijitali wa Kusajili Wapiga Kura
17.	CAG	Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
18.	CCK	Chama Cha Kijamii
19.	CCM	Chama cha Mapinduzi
20.	CCTV	Kamera za Usalama
21.	CDF	Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi
22.	CG	Serikali Kuu
23.	CHADEMA	Chama Cha Demokrasia na Maendeleo
24.	CHAUMMA	Chama Cha Ukombozi wa Umma
25.	CID	Idara ya Upelelezi Makao Makuu ya Jeshi la Polisi
26.	CTA	Kibali cha Kazi cha Muda Mfupi
27.	DART	Wakala wa Usafiri wa Mwendo Kasi Dar es Salaam
28.	DDCA	Wakala wa Kuchimba Visima na Mabwawa
29.	DK	Dola za Kimarekani
30.	NPS	Kurugenzi za Mashitaka ya Umma
31.	EFD	Mashine za Kielekroniki
32.	e-RCS	Mfumo wa Ukusanyaji Mapato
33.	ERPP	Mradi wa Upanuzi na Uzalishaji Mpunga
34.	ETD	Hati za Dharura za Kusafiria
35.	FETA	Wakala wa Elimu ya Uvuvi na Mafunzo
36.	FRF	Jeshi la Zimamoto na Uokoaji
37.	GCC	Masharti ya jumla ya Mkataba
38.	GCLA	Wakala wa Maabara za Serikali
39.	GEPGS	Mfumo wa Ukusanyaji Mapato
40.	GN	Tangazo la Serikali
41.	GoT	Serikali ya Tanzania

Na.	Kifupisho	Maelezo
42.	GPSA	Wakala wa Ugavi na Huduma za Manunuzi
43.	GST	Wakala wa Utafiti wa Miamba
44.	HESLB	Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu
45.	HQ	Makao Makuu
46.	ICT	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
47.	IFMS	Mfumo Jumuiifu wa Taarifa za Fedha
48.	IGP	Mkuu wa Jeshi la Polisi
49.	IJA	Taasisi ya Uongozi wa Sheria Lushoto (IJA)
50.	IPSAS	Uandaaji wa Hesabu za Sekta ya Umma Kwa Viwango vya Kimataifa
51.	ITT	Maelekezo Kwa Wazabuni
52.	LGAs	Mamlaka za Serikali za Mtaa
53.	LGTI	Taasisi ya Mafunzo ya Serikali za Mtaa
54.	M/F	Mwaka wa Fedha
55.	MDAs	Wizara Idara na Wakala
56.	MP	Mbunge
57.	NCCR	National Convention for Construction and Reform
58.	NGO	Mashirika yasiyo ya Kiserikali
59.	NIDA	Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa
60.	NLD	National League for Democracy
61.	NMB	Benki ya NMB
62.	NRA	National Reconstruction Alliance
63.	NSSF	Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii
64.	NWIF	Mfuko wa Taifa wa Uwekezaji
65.	OI	Taasisi Nyingine
66.	PAC	Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu Serikali Kuu
67.	PMG	Mlipaji Mkuu wa Serikali
68.	PO-RALG	Ofisi ya Raisi - Tawala za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa
69.	PSPF	Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma
70.	PTF	Mfuko wa Rais wa Kujitegemea
71.	REA	Wakala wa Umeme Vijijini
72.	RITA	Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhadini
73.	RS	Sekretarieri ya Mikoa
74.	SAU	Sauti ya Umma
75.	Sh.	Shilingi ya Kitanzania
76.	TAA	Mamlaka ya Viwanja vya Ndege
77.	TAKUKURU	Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa
78.	TANCIS	Mfumo wa Forodha
79.	TANROADS	Wakala wa Barabara Tanzania
80.	TARURA	Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini
81.	TBA	Wakala wa Majengo Tanzania
82.	TEHAMA	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
83.	TEMESA	Wakala wa Ufundi na Umeme

Na.	Kifupisho	Maelezo
84.	TLP	Tanzania Labour Party
85.	TOSCI	Chuo cha Kuthibitisha ubora wa Mbegu
86.	TRA	Mamlaka ya Mapato Tanzania
87.	UDP	United Democratic Party
88.	UMD	Union for Multiparty Democracy
89.	UPDP	United Peoples Democratic Party
90.	UWT	Umoja wa Wanawake
91.	VAT	Kodi ya Ongezeko la Thamani

Dibaji



Prof. Mussa Juma Assad
Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa
Hesabu za Serikali

Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (kama ilivyorekebisha) inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwasilisha kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kila ripoti anayoiandaa kulingana na Ibara ndogo ya pili ya Ibara hii¹. Pia, Kanuni ya 88 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009 inataka ripoti kuu za ukaguzi ziwasilishwe kwa Mheshimiwa Rais ifikapo tarehe 31 Machi kila mwaka ambapo zitawasilishwa


Bungeni kupitia kwa Waziri mwenye dhamana hiyo. Kwa mujibu wa matakwa hayo, ninafurahi kuwasilisha ripoti hii inayohusiana na ukaguzi wa taarifa za fedha wa taasisi za Serikali Kuu kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2018

Lengo kuu la kufanya ukaguzi wa taarifa za fedha ni kuwaaminisha watumiaji wa taarifa hizo kama zimeandaliwa pasipo kuwa na makossa kulingana na matakwa ya viwango vya kubalifu vya uhasibu, yaani Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma visivyozingatia pesa taslimu (IPSAS accrual basis). Ripoti hii inajumuisha matokeo ya ukaguzi wa taasisi za Serikali Kuu kwenye maeneo ya taarifa za fedha na nyaraka zake, mfumo wa udhibiti wa ndani, mchakato na taratibu za manunuzi na uzingatiaji wa sheria na kanuni mbalimbali. Pia, inajumuisha matokeo ya kaguzi maalumu zinazohusiana na taasisi za serikali kuu pamoja na utekelezaji wa mapendekezo yangu ya kaguzi zilizopita na maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali.

Ripoti hii imejumuisha matokeo ya ukaguzi wa taarifa za fedha 255 za Wizara,

Idara zinazojitegemea, Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Ofisi za Balozi, Mifuko Maalum, Bodi za Mabonde ya Maji, Vyama vya Siasa pamoja na taasisi nyingine za Serikali. Ukaguzi ulifanyika kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguzi vinavyotolewa na Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu ambavyo ni mahsusi kwa ukaguzi wa taasisi za sekta ya umma. Kutokana na ukaguzi huu, ripoti za taasisi mojawoja zilitolea zikiwa na maoni ya ukaguzi, vilevile barua ya mapungufu yaliyobainika ambayo hayakupata majibu wakati wa ukaguzi ilitolewa kwa kila Afisa Masuhuli zikiwa na mapendekezo kwa ajili ya maboresho kwa vipindi vinavyofuata. Pia, ripoti hii ina matokeo ya kaguzi maalumu saba (7) ambazo zilifanyika kwa mwaka unaoishia tareher 30 Juni 2018.

Ni matumaini yangu kuwa mapungufu yalibainika na mapendekezo yaliyotolewa yatafaniwa kazi kwa nia ya kuimarisha uwajibikaji, uwazi na uadilifu kwenye utendaji wa Serikali na taasisi za umma.



Prof. Mussa Juma Assad,

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Shukrani

Ofisi yangu imeendelea kuonyesha umuhimu, uwezo na uaminifu kwa wadau wake katika kuimarisha uwajibikaji, uwazi na uadilifu katika sekta ya umma na Serikali kwa ujumla kwa kutoa taarifa bora za ukaguzi. Mafanikio haya yasingepatikana bila kuwapo kwa juhudi za pamoja kutoka kwa watendaji tofauti ambao walielekeza nguvu zao, muda na rasilimali zao nyingine.

Natoa shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, kwa kuendelea kuamini ofisi yangu; Wabunge, na Kamati za Kudumu za Bunge za Serikali Kuu na Serikali za Mitaa kwa kushiriki katika majadiliano mazuri na kwa kujitolea ili kuhakikisha kuwa ripoti za ukaguzi zinabaki kuwa na umuhimu, na ofisi yangu inaendelea kuwa huru kifedha bila kuingiliwa na taasisi and mtu yeyote.

Ninashukuru pia wafanyakazi wa Ofisi yangu katika ngazi zote, makampuni ya ukaguzi yaliyofanya kazi na sisi, Menejimenti za taasisi zilizokaguliwa kwa ushirikiano wao muhimu katika ukaguzi, Wizara ya Fedha na Mipango na washirika wa maendeleo kwa jitihada zao za bidii na rasilimali ili kutimiza mamlaka yangu ya kikatiba.



Prof. Mussa Juma Assad,

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Muhtasari

Ripoti hii inatoa muhtasari wa matokeo ya ukaguzi wangu wa taarifa za fedha za Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Mawanda ya ukaguzi katika Serikali Kuu ni pamoja na Wizara na Idara za Serikali 65, Wakala 33, Mifuko maalum 16, taasisi nyingine 42, Vyama vya Siasa 14, Sekretariati za Mikoa 26, Balizi za Tanzania 41, Bodi za mabonde ya Maji 14. Pia, inajumuisha ukaguzi wa Mamlaka ya kodi ya mapato Tanzania (TRA), Hesabu Jumuiifu za Taifa, ukaguzi wa awali wa mafaili ya mafao ya wastaafu na kaguzi maalum.

Hati za Ukaguzi

Lengo la kufanya ukaguzi wa taarifa za fedha ni kuwaaminisha watumiaji wa taarifa hizo kama zimeandaliwa kwa usahihi katika maeneo yote, na taarifa za fedha zina ujumbe unaohusu kipindi husika kwa kuzingatia miongozo ya utoaji taarifa na sheria zilizotumika. Taarifa ya ukaguzi huwapa watumiaji habari za uhakika kuhusu kiwango cha taarifa za fedha, kwamba ni sahihi na za kuaminika kwa kuzingatia taratibu zilizotumika na kubaini kuwa, hazina dosari.

Matokeo ya ukaguzi yanaonesha kwamba, kati ya taarifa za fedha 241 zilizokaguliwa bila kujumuisha Vyama vya Siasa, 234 (97%) zilipata hati zinazoridhisha. Hawa ni wakaguliwa ambao taarifa za fedha hazikuwa na dosari yoyote; hii inamaanisha kuwa miamala ya fedha katika taarifa ni sahihi 7 (3%) zilipata hati yenye shaka; hapakuwa na hati isiyoridhisha wala hati mbaya.

Matokeo ya ukaguzi wa vyama vya siasa kwa taarifa za fedha za mwaka 2017/2018 yanaonesha kwamba, vyama vya siasa 14 vilikaguliwa 3 (21%) vilipata hati zinazoridhisha; 4 (29%) vilipata hati yenye shaka; 5(36%) vilipata hati mbaya; na 2 (14%) vilipata hati isiyoridhisha. Hii inamaanisha kuwa, taarifa za fedha za vyama vya siasa zilikuwa na dosari katika miamala ya fedha. Maelezo ya kina yanapatikana sura ya pili ya ripoti hii.

Mapendekezo ya jumla

Kwa mantiki ya matokeo ya ukaguzi, taarifa za fedha 18 zilizokaguliwa hazikuzingatia miongozo ya kimataifa katika sekta ya umma katika kuandaa taarifa za hesabu; hivyo, kusababisha kupata hati zisizoridhisha, zenye shaka na mbaya.

Ninawashauri Maafisa Masuuli wote waendeleo kufanyia kazi maeneo yenye dosari yaliyoainishwa katika taarifa ya ukaguzi ili, hatimaye kuwa na taarifa zenye kuonesha usahihi.

Ufuatiliaji wa mapendekezo ya miaka ya nyuma

Katika sura ya tatu; ninatakiwa kwa mujibu wa kifungu cha 40 cha PAA, 2008 (iliyorekebisha mwaka 2013) kuelezea katika Taarifa yangu ya mwaka hali ya utekelezaji wa mpango kazi unaoandaliwa na na Maafisa Masuuli juu ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi na maagizo yanayotolewa na Kamati ya PAC.

Kwa ujumla, hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi na Maelekezo ya PAC kwa Taasisi moja moja sio ya kuridhisha kwa mwaka huu wa fedha ikilinganishwa na mwaka wa fedha uliopita, umkini, hali hiyo inatokana na jitihada zisizoridhisha za utekelezaji wa Mpango kazi wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi uliondaliwa na kuridhiwa na Menejimenti za Taasisi nilizozikagua.

Hivyo basi, ijapokuwa ninazitambua juhudi zinazofanywa na Maafisa Masuuli, PMG na Serikali nzima katika kuyaweka mapendekezo yangu kwenye vitendo, ninaendelea kusisitiza juu ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kikamilifu ili kuepuka kujirudiarudia kwa mapungufu katika miaka ijayo. Kwa kufanya hivyo, itaonesha umuhimu wa uwajibikaji na utawala bora kwa Taasisi ninazozikagua. Tazama sura ya tatu (3) kwa maelezo zaidi.

Mapendekezo ya Jumla

Ukaguzi wa sasa unaonesha ongezeko la asilimia 4 la hoja zinazosubiri utekelezaji ikilinganishwa na wa mwaka uliopita (Angalia sura ya 3 ya ripoti hii). Pia, uchambuzi unaonesha kwamba, sehemu kubwa (38%) ya mapendekezo ya kaguzi zilizopita utekelezaji wake umeanza

lakini haujahitimishwa. Hii inamaanisha kwamba jitihada za sasa za Serikali kuimarisha utaratibu wa kushughulikia mapendekezo ya ukaguzi kupitia vikosi kazi vya wataalamu katika MDA zote na Taasisi za Umma bado hazijatoa matokeo tarajiwa.

Kwa hiyo, ninapendekeza Serikali iendelee na mkakati wake wa kukamilisha Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ufuatiliaji wa Taarifa za Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi (GARI-ITS) chini ya Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani na Wizara ya Fedha na Mipango. Mfumo huu una lengo la kuwezesha ufuatiliaji wenye ufanisi wa utekelezaji kwa kupitia Wakaguzi wa Ndani wa Taasisi za Serikali Kuu zote na zile za Serikali za Mitaa.

Kufuatia mapitio ya Taarifa zitakazopatikana kutoka kwenye Mfumo wa GARI-ITS, ni matumaini yangu kuwa, zitaaidia serikali kufanya ufuatiliaji wa mapendekezo ya kaguzi zilizopita. Pia, mfumo huo unapaswa kuhakikisha kuwa unawekewa mpango kazi na Taarifa ya inayochambua muda wa utekelezaji wa kila pendekezo la ukaguzi ili kuhakikisha mapendekezo yanatekelezwa kwa wakati na ufanisi.

Usimamizi na Utekelezaji wa Bajeti

Katika Mwaka wa Fedha 2017/18 Serikali ilipanga kukusanya jumla ya Sh. bilioni 31,711.99, sawa na ongezeko la Sh. bilioni 2,172.39 ikilinganishwa na makadirio ya Sh. bilioni 29,539.6 yaliyoripotiwa mwaka 2016/17. Makusanyo halisi kutoka katika vyanzo vya mapato vilivyotambulika ni Sh. bilioni 27,695.96, pungufu kwa Sh. bilioni 4,016 sawa na asilimia 12.66 ya makusanyo yote.

Makusanyo ya ndani ni Sh. bilioni 16,739 sawa na asilimia 60 ya makusanyo yote ya Sh. bilioni 27,695.96. Hii inaonesha kuna ongezeko la makusanyo ya kodi kwa Sh. bilioni 878.17, (sawa na asilimia 6.15) ikilinganishwa na makusanyo ya kodi yaliyoripotiwa mwaka wa fedha 2016/17. Hii inaonesha upungufu wa Sh. bilioni 1,956.87 (11.44%) ikilinganishwa na makadirio yaliyopitishwa na Bunge ya Sh. bilioni 17,106.34.

Makusanyo ya mapato yasiyotokana na kodi yamepungua kwa Sh. bilioni 483.03, sawa na asilimia 23.3 ukilinganisha na makusanyo

yaliyoripotiwa mwaka 2016/17. Hata hivyo, kumekuwa na makusanyo pungufu kwa Sh. bilioni 1,280.80 sawa na asilimia 44.62 ikilinganishwa na makadirio ya Sh. bilioni 2,870.67 yaliyopitishwa na Bunge.

Makusanyo kutoka katika Mikopo ya ndani na nje ni Sh. bilioni 10,956.62, sawa na asilimia 40 ya makusanyo yote ya Sh. bilioni 27,695.96. Mapato kutoka katika mikopo ya ndani ili kugharamia bajeti na mikopo inayoendelea yamepungua kwa Sh. bilioni 211.35 sawa na asilimia 3.57 ikilinganishwa na mikopo iliyoripotiwa mwaka 2016/17. Pia, kumekuwa na upungufu wa mikopo ya ndani kwa Sh. bilioni 464.40 ikilinganishwa na makadirio ya yaliyopitishwa na Bunge ya Sh. 6,168.90

Mikopo ya Nje, Misaada ya Wahisani na Misaada ya Washirika wa Maendeleo imeongezeka kwa Sh. bilioni 2,204.69 ikilinganishwa na mikopo ya Nje iliyoripotiwa mwaka 2016/17. Hata hivyo kumekuwa na upungufu wa Sh. bilioni 314 kutoka kwenye Mikopo ya Nje, Misaada ya Wahisani na Misaada ya Washirika wa Maendeleo ikilinganishwa na makadirio yaliyopitishwa na Bunge.

Aidha, Bajeti ya matumizi ilikuwa Sh. bilioni 31,711.99 sawa na ongezeko la Sh. bilioni 2,172.39 ikilinganishwa na makadirio yaliyoripotiwa ya Sh. bilioni 29,539.6 ya mwaka 2016/17. Kulingana na marejeo ya bajeti Na.1 ya mwaka 2017/18, Sh. bilioni 20,278.99 zilitengwa kwa matumizi ya kawaida na Sh. bilioni 11,432.99 zilitengwa kwa matumizi ya maendeleo, hili ni ongezeko la Sh. bilioni 2,194.43 sawa na asilimia 12.13 kwa matumizi ya kawaida yaliyoripotiwa mwaka 2016/17 na upungufu wa Sh. bilioni 29.27 sawa na asilimia 0.26 ya matumizi ya maendeleo yaliyoripotiwa mwaka 2016/17.

Kwa Serikali Kuu kiasi cha Sh. bilioni 22,627.28 kilitolewa. Hii ni sawa na asilimia 87 ya makadirio ya Sh. bilioni 25,867.88. Sh. bilioni 15,328.66 sawa na asilimia 68 zilitumika katika matumizi ya kawaida na kupunguza Deni la Serikali, na Sh. bilioni 7,100.42 sawa na asilimia 32 kilitumika katika matumizi ya Maendeleo. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 14.27 Kwa matumizi ya kawaida na asilimia 17.44 matumizi ya maendeleo ikilinganishwa na matumizi yaliyoripotiwa katika mwaka 2016/17. Kiasi cha Sh. bilioni 198.20 kilichotolewa

hakikutumika hadi kufikia tarehe 30 Juni 2018, na kuwasilishwa Mfuko Mkuu wa Hazina.

Katika kuangalia mwenendo wa uzingatiaji wa sheria ya kuwasilisha makusanyo yote Mfuko Mkuu, nimebaini kuwa kiasi cha Sh. bilioni 2.54 kilichokusanywa na balozi 7 katika mwaka wa fedha 2017/18 kakikuwasilishwa Mfuko Mkuu. Mwenendo huu unaonesha ongezeko la uzingatiaji wa sheria kwa upungufu wa asilimia 82.5 ikilinganishwa na Sh. bilioni 14.5 za balozi 21 zilizoripotiwa katika mwaka wa fedha 2016/17. Maelezo zaidi na mapendekezo yamebainishwa katika Sura ya Nne.

Mapendekezo ya jumla

Makusanyo ya ndani yamekuwa yakionesha mwenendo chanya kwa ongezeko la mfululizo ndani ya miaka mitano kuanzia 2013/14 hadi 2017/18. Licha ya ongezeko hilo katika makadirio na makusanyo kumekuwa pia na changamoto ya ukusanyaji hafifu ikilinganishwa na makadirio yaliyowekwa. Pia kumekuwa na ucheleweshwaji katika kutoa Fedha zilizobajetiwa katika mwaka husika Kutokana na hayo, utekelezaji wa malengo ya taifa ya kiutendaji na kimkakati yatashidwa kutekelezwa kama ilivyopangwa awali, na kuongeza utegemezi katika mikopo ya ndani, nje na washirika wa maendeleo.

Kwa mantiki hii, Serikali inapaswa kutafiti vyanzo mbadala ili kuongeza makusanyo ya mapato ya ndani. Pia kuhamasisha wananchi kulipa kodi bila shuruti. Aidha, Hazina itoe fedha za utekelezaji wa bajeti kwa wakati. Vilevile kuhakikisha fedha zilizotolewa zinatumiwa ndani ya mwaka wa fedha husika.

Pia, ningependa kutoa ushauri kwa Balozi zote juu ya uzingatiaji wa miongozo na Kifungu Na. 11 cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha cha mwaka 2001. Pia, kuhakikisha kwamba makusanyo yote ya serikali yanawasilishwa katika Mfuko Mkuu kwa wakati, ili fedha zote zinazokusanywa ziweze kupangiwa matumizi kulingana na mpango wa Bajeti uliopitishwa.

Ukaguzi wa mapato yatokanayo na kodi

Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikusanya Sh. bilioni 15,386.50 dhidi ya malengo yaliyowekwa ya Sh. bilioni 17,315.77. Hali hii inaonesha upungufu wa makusanyo kwa Sh. bilioni 1,929.27 ambazo ni sawa na asilimia 11 ya malengo. Jumla ya makusanyo hayo haikuhusisha Sh. bilioni 18.95 ambazo ni vocha za misamaha ya kodi kutoka Hazina. Hivyo makusanyo halisi ya mwaka 2017/18 ni Sh. bilioni 15,405.44 yakijumuisha vocha za misamaha ya kodi kutoka Hazina.

Kodi zilizoshikiliwa katika kesi za muda mrefu kwenye mamlaka za rufaa za kodi

Katika ukaguzi wangu wa mwaka wa fedha wa 2017/18, nilibaini kwamba, Mamlaka ya Mapato ina kesi za kodi katika mamlaka za rufaa za kodi kwa muda mrefu zenye kodi ya Sh. trilioni 382.6. Hili ni ongezeko la kiasi cha shilingi trilioni 378.2 (asilimia 85) ikilinganishwa na kesi za Sh. trilioni 4.4 katika mwaka wa fedha 2016/17. Ongezeko hili kubwa la kesi za kodi limetokana na walipakodi na jamii kupata uelewa zaidi wa kuhusu kuwapo kwa mamlaka za rufaa za kodi pamoja na mabadiliko ya taratibu za Bodi ya Rufaa za Kodi za mwaka 2018 ambazo zimerahisisha utaratibu wa kushughulikia mapingamizi ya kodi. Aidha, kati ya jumla ya kesi za kodi zinazopo Bodi ya Rufaa za Kodi (TRAB) ya Sh. trilioni 382, kesi nne zenye jumla ya kodi ya Sh. trilioni 374.7 sawa na asilimia 98.08 zinahusu kampuni ya uchimbaji madini ya ACACIA.

Mapungufu katika kushughulikia mapingamizi ya kodi

Katika ukaguzi wangu nilibaini kuwa Mamlaka ina mapingamizi ya kodi yenye thamani ya Sh. 77,857,964,376.52 kutoka kwa walipakodi. Mapingamizi hayo yalikuwa hayajashughulikiwa kwa muda mrefu kinyume na taratibu za Mamlaka za utoaji huduma. Kuchelewa kushughulikia mapingamizi ya kodi kuna madhara katika kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato ya serikali kwani mapingamizi haya yanashikilia kiasi kikubwa cha kodi.

Usimamizi na ufuatiliaji usioridhisha wa makusanyo ya madeni ya kodi

Pia, katika ukaguzi wa mwaka huu nimebaini kuwa kodi ya Sh. 119,604,133,635.16 haikukusanywa kutoka kwa walipakodi. Kuwapo kwa madeni ya kodi kunasababishwa na mifumo na mikakati isiyoridhisha kwenye ufuatiliaji wa madeni ya kodi hasa katika Idara ya Kodi za Ndani.

Mapungufu katika ukaguzi wa kodi na ukadiriaji wa kodi

Nilipitia ukaguzi na ukadiriaji wa kodi unaofanywa na Mamlaka na kubaini makusanyo pungufu ya kodi ya jumla ya Sh. 46,548,934,370.70. Makusanyo haya pungufu yalisababishwa na mawasilisho pungufu ya kodi ya makampuni, kodi ya ongezeko la thamani (VAT) na kodi ya zuio ambayo haikukusanywa.

Kadhalika, nilibaini kuwa kodi ya kipato (PAYE) na tozo ya maendeleo ya ujuzi (SDL) ya walipakodi 30 haikuwasilishwa Mamlaka ya Mapato kwa kipindi cha jumla ya miezi 149. Pia, kodi ya mapato (PAYE), tozo ya maendeleo ya ujuzi (SDL) na kodi ya zuio yenye jumla ya Sh. 1,951,215,244.93 haikuwasilishwa Mamlaka ya Mapato na walipa kodi wa Idara ya Kodi za Ndani.

Tathmini ya Ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya serikali

Ukaguzi katika ukusanyaji wa mapato yanayotokana na tozo za huduma za kusafiri za viwanja vya ndege na bandari ulibaini mapato ya Sh. 1,845,250,227 na Dola za Kimarekani 2,747,249 hayakuwasilishwa Mamlaka ya Mapato kutoka mashirika ya ndege 19, Mamlaka ya Viwanja vya ndege (TAA) na Kampuni ya huduma za meli.

Pia, nilibaini kuwa mafuta yaliyoingizwa kutoka nchi nyingine kwa ajili ya matumizi ya ndani ya nchi yenye kodi ya Sh. 4,772,815,004.75 yaliyoingizwa na makampuni 20 ya mafuta pamoja na bidhaa zenye kodi ya Sh. 35,223,221,808.42 ziliruhusiwa na Mamlaka ya Mapato kuchukuliwa na makampuni husika (walipakodi) kabla ya kukamilisha taratibu za kiforodha, na hapakuwa na ushahidi kuthibitisha kuwa kodi husika zilikusanywa.

Kadhalika, mafuta yenye kodi ya Sh. 2,519,765,899.69 yaliyoingizwa kutoka nchi nyingine na makampuni matatu ya mafuta (kupitia nyaraka 4 za kuagizia mizigo nje ya nchi) hayakuingizwa kwenye

mfumo wa TANCIS kwa ajili ya kukadiriwa na kulipia kodi. Pia, nilibaini kuwa malipo pungufu ya kodi ya Sh. 1,167,107,857 kutoka makampuni tisa (9) ya mafuta na ada ya bandari (wharfage fees) ya Sh. 1,286,992,434.00 hazikukusanywa kutoka kwa makampuni mbalimbali ya mafuta.

Mifumo isiyoridhisha ya udhibiti wa bidhaa zinazosafirishwa kwenda nchi nyingine na bidhaa zinazouzwa nje ya Tanzania

Ukaguzi uliofanyika katika bidhaa zinazoingizwa nchini kwa ajili ya kusafirishwa kwenda nchi nyingine (mafuta na bidhaa nyingine) ulibaini kuwa, mizigo yenye kodi ya Sh. 57,098,864,624.83 haikutoka nchini kwenda nchi zilizokusudiwa. Wakati wa uhakiki sikupata ushahidi wowote kuthibitisha kuwa bidhaa hizi zilitoka kwenda nchi zilizokusudiwa kupitia mipaka husika.

Pia, nilibaini mizigo inayosafirishwa kutoka nchini kwenda nchi nyingine yenye kodi ya ongezeko la thamani (VAT) ya Sh 649,451,067.85 ambayo iliruhusiwa kwenda nje ya nchi bila kukamilisha taratibu za kiforodha; na hakukuwa na ushahidi wa nyaraka za kuthibitisha kuwa kodi stahiki ilikusanywa.

Udhibiti hafifu katika ukusanyaji wa kodi na usimamizi wa bidha zilizo katika bandari kavu (ICDs)

Baada ya kupitia taarifa za ukadiriaji kodi za bidhaa zilizoingizwa kutoka nchi nyingine uliofanyika katika bandari kavu (ICDs) mbalimbali, nilibaini makadirio ya kodi ya Sh. 4,734,719,220.80 yaliyofanywa na waingizaji wa bidhaa yalikuwa hayajalipwa kwa Mamlaka kwa muda mrefu. Kadhalika, uhakiki wa mizigo iliyowekwa kwenye bandari kavu 13 na bandari kuu (TICTS na Mamlaka ya Bandari). Nilibaini bidhaa katika makontena zaidi ya 286 zilizoharibika na kutofaa kwa matumizi ya binadamu, kwani hazikukidhi vigezo na viwango vya Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) na Shirika la Viwango Tanzania (TBS). Hii ilisababisha mapato ya serikali katika bidhaa hizi kutokusanywa.

Mapendekezo ya jumla

Naishauri Serikali ihakikishe mamlaka za rufaa za kodi zinapata rasilimali watu wenye uwezo na fedha za kutosha ili ziweze kusilikiliza na kumaliza kesi za kodi. Pia, Serikali iongeze wafanyakazi wenye uwezo, uzoefu na weledi wa kutosha ili kuiwezesha Mamlaka ya Mapato kushughulikia mapingamizi ya kodi, na kukusanya kwa wakati madeni ya kodi na kodi zilizokadiriwa.

Kadhalika Serikali idhibiti mifumo ya ukusanyaji wa tozo za huduma za kusafiri kwenye viwanja vya ndege na bandari. Pia pawe na udhibiti wa mafuta na bidhaa zinazoingia kwa matumizi ya hapa nchini, na zinazokwenda nchi nyingine ili kuhakikisha kuwa hazitumiki bila kulipa kodi stahiki.

Pia, serikali ihakikishe mafuta yote yanayoingia nchini yanaingizwa kwenye mfumo wa TANCIS kwa ajili ya kudhibiti makadirio na malipo stahiki ya kodi za mafuta. Vilevile Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) zihakiki bidhaa kabla hazijaingizwa nchini kwa ajili ya kulinda afya na usalama kwa watumiaji. Kodi stahiki zikusanywe pia kwenye mizigo inayosafirishwa kwenda nchi nyingine na kwenye bidhaa zilizoingizwa nchini na kuwekwa kwenye bandari kavu (ICDs).

Ukaguzi wa Awali wa Malipo ya Mafao

Katika mwaka wa fedha 2017/2018, ofisi yangu imekagua majalada 2,868 ambapo majalada 2,814 yenye jumla ya Sh. 165,446,698,552.92 yalikaguliwa na kuidhinishwa na ofisi yangu kwa malipo. Majalada hamsini na nne (54) yalihojiwa na kurudishwa kwa Maafisa Masuuli husika kwa ajili ya masahihisho. Jumla ya Majalada 569 yalikuwa bado katika ukaguzi wakati wa kufunga mwaka wa fedha tarehe 30 Juni, 2018.

Pia, nilibainisha kwamba kiwango cha malipo ya hitimisho la kazi kwa viongozi wa kisiasa hakijawekwa wazi kwenye sheria. Hii ni kutokana na marekebisho yaliyofanyika kwenye kifungu cha 21 (3) cha Sheria ya Mafao kwa Viongozi wa Kisiasa ya mwaka 1999 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2005) kwa kufuta kiwango kilichokuwa

kimebainishwa; na badala yake kuipa nguvu mamlaka husika kutathmini kiwango cha malipo hayo. Hiyo itafanya malipo hayo yaathiriwe na maamuzi ya mamlaka hiyo.

Mapendekezo ya jumla

Serikali kupitia kwa Maafisa Masuuli iimarisha udhibiti na utaratibu wa kufanya mapitio ya uandaaji wa mafao. Hii itahakikisha kuwa waandaaji wa mafao ya kiinua mgongo na pensheni wanafuata kanuni na vigezo vya ukokotoaji na sheria kabla ya kuwasilisha kwa ukaguzi wa awali wa malipo. Aidha, kuepuka kucheleweshwa kwa mafao ya hitimisho la kazi na hasara kwa serikali.

Serikali kupitia Mamlaka husika wafanyie marekebisho kifungu cha 21(3) cha Sheria ya Mafao ya Hitimisho la Kazi kwa Viongozi wa Kisiasa ya mwaka 1999 (kama ilivyorekebisha mwaka 2005) kwa kuainisha kiwango cha malipo ya posho la hitimisho la kazi.

Usimamizi wa Deni la Serikali

Deni la Serikali kufikia tarehe 30 Juni 2018 lilikuwa Sh. bilioni 50,926.51, ambapo deni la ndani lilikuwa Sh. bilioni 14,732.45 na deni la nje Sh. bilioni 36,194.06. Hii inaonesha ongezeko la Sh. bilioni 4,845.08 sawa na asilimia 10.5 ikilinganishwa na deni la Sh. bilioni 46,081.43 lililoripotiwa tarehe 30 Juni 2017.

Katika ukaguzi wangu nilibaini masuala ya msingi kuhusu Deni la Serikali na usimamizi wake. Nayo ni haya yafuatayo: Upotoshwaji wa mapokezi ya mikopo kutokana na mapungufu ya Udhibiti wa Ndani katika kurekodi na kutaarifu, Kuchelewesha kulipa madeni ya Benki Kuu, Sh. bilioni 212.7; Kutokuwapo kwa uwiano wa taarifa za mfumo wa malipo (Epicor) na mfumo wa kutunza taarifa za deni la taifa (Common Wealth Secretariat-Debt Record Management System - (CS-DRMS)); Kushindwa kutambua madeni yatokanayo na malimbikizo ya michango ya pensheni; na kutapanywa kwa shughuli za ofisi ya mbele, kati na ya nyuma. Hizi ndizo changamoto kuu katika kutunza kumbukumbu na kutoa taarifa sahihi zinazohusu deni la serikali.

Mapungufu mengi yaliyojitokeza mwaka huu, yalijitokeza pia miaka iliyopita. Hii inaashiria kuwa, serikali imekuwa na umakini hafifu katika utekelezaji wa mapendekezo yangu. Kama nilivyoeleza awali mapungufu mengi kwenye Deni la Serikali yanasababishwa na kutapanywa kwa shughuli za ofisi kuu, kati na ya nyuma. Pamoja na kwamba Muundo mpya wa Wizara ya Fedha na Mipango ulioidhinishwa mwaka 2017/18 umewezesha kuwapo kwa kitengo cha kusimamia madeni, bado muundo huo haujatekelezwa.

Kwa kuzingatia hayo, napendekeza serikali ifanye yafuatayo:

- i) kupata uhakika wa mapokezi ya fedha za mikopo kutoka kwa wanufaika kabla ya kuingiza kumbukumbu hizo katika mfumo wa kutunza kumbukumbu za madeni. Pia kuzingatia kubuni vidhibiti ambavyo vitawezesha usahihi wa taarifa za fedha kuchukuliwa kutoka CS-DRMS;*
- ii) Kulipa sehemu yake ya gharama ya kudhibiti ukwasi pamoja na riba ya nakisi katika akaunti yake kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 2006 na mkataba wa makubaliao (MoU) baina yao. Kuwezesha bajeti ya Fungu Na. 22 ili kuweza kumudu gharama hizo ndio njia sahihi hapo mbeleni;*
- iii) Kuzingatia kufanya marekebisho ya Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 2006 ili kuruhusu Benki Kuu kupunguza madeni yake kwa Serikali kutoka katika gawio lake. Juhudi hizi zitapunguza kasi ya ukuaji wa madeni yatokanayo na gharama ya kudhibiti ukwasi pamoja na riba ya nakisi ya Serikali;*
- iv) limarishe mifumo ya ndani ili kuhakikisha hesabu zinapitiwa kwa umakini kabla ya kuwasilishwa kwa Ukaguzi; kuzingatia kutumia programu zake zilizopo, ikiwa ni pamoja na Lawson na GSPP,*
- v) Katika kupata taarifa halisi kwa wakati kuhusu madai ya michango ya kisheria na kulipa kwa wakati huohuo ili kuepuka malimbikizo yasiyokuwa ya lazima kwa serikali na kuripoti madai kwa upungufu.*

Taarifa za Fedha Jumuifu

Wakati tunatambua juhudi zilizofanywa na serikali kwa kuandaa taarifa za fedha jumuifu kwa taasisi zinazosimamiwa na Serikali, kuna changamoto katika uandaaji wa taarifa za fedha jumuifu ambazo ni pamoja na; ufafanuzi usiofaa na upimaji wa uwekezaji wa mitaji (Equity investments Held for Trading) Mali za Kibaiolojia zimeainishwa kwenye hesabu Jumuifu pasipo kuainishwa kwenye hesabu za taasisi husika Sh.100.9 Bilioni, Mpangilio wa vipengele usio sawa baina ya hesabu jumuifu na hesabu za taasisi hivyo kusababisha uwasilishwaji usio sahihi Sh. 251.7 Bilioni, Hesabu zilizojumuishwa zikiwa na tarehe tofauti bila kufanyiwa marekebisho, utofauti wa kiasi kilichoondolewa kwenye ruzuku zilizoenda kwenye taasisi za serikali na ruzuku zilizotoka taasisi za serikali kwa kiasi cha Shilingi 2,323 Bilioni, takwimu zisizo sahihi kuhusu ziada / nakisi ya uwekezaji katika Washirika na Ubia, Bakaa Hasi ya Mfuko wa Fedha za Walipakodi Shilingi 10,860 Bilioni.

Mapendekezo ya jumla

Napendekeza Serikali ihakikishe kuwa Taasisi za umma ziandae taarifa za ziada na marekebisho ya taarifa za kifedha yafanyike kwa usahihi ili kuendana na mahitaji ya miongozo ya uandaaji wa taarifa za fedha katika sekta ya umma.

Tathmini ya mifumo ya udhibiti wa ndani na utawala bora

Sura hii inafupisha matokeo ya tathmini ya mifumo ya udhibiti wa ndani na utawala uliofanywa kwa Wizara, Sekretarieti ya Mikoa, Taasisi Nyingine, Mabalizi na Mawakala kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Inashughulika na mapungufu yaliyotambuliwa katika maeneo yafuatayo: tathmini ya mifumo ya udhibiti wa ndani na utawala, na masuala ya utawala, changamoto zilizokabiliwa na huduma za mashitaka ya umma za Taifa (NPS) katika utekelezaji wa sheria za Utaifishaji na Urejeshaji, mfumo wa teknolojia ya habari (TEHAMA), kamati za ukaguzi, Mfumo wa ukaguzi wa ndani, tathmini za ubadhirifu pamoja na tathmini ya usimamizi wa vihatarishi.

Tathmini yangu ya mifumo ya udhibiti wa ndani ilibaini kuwa kuna taasisi 33 zenye mapungufu ambayo yalitokea katika mfumo wa

ukaguzi wa ndani. Taasisi hizo ni: Wizara 11, Wakala 3, Taasisi Nyingine 5, na Sekretarieti za Mikoa 15. Katika tathmini ya Kazi ya Kamati ya Ukaguzi kulikuwa na Taasisi 30 zenye mapungufu. Nazo ni Wizara 12, Sekretarieti za Mikoa 11, Wakala 3 na Taasisi Nyingine 4. Pia, tathmini ya usimamizi wa vihatarishi ilibainisha Mawakala 8 zenye mapungufu, ikiwa ni pamoja na Wizara 2, Sekretarieti za Mikoa 3, Wakala 1 na Taasisi Nyingine 1.

Tathmini ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) inaonesha kuwa kuna taasisi 40 zenye mapungufu katika mfumo. Nazo ni Wizara 10, Sekretarieti za Mikoa 11, Wakala 8, Taasisi Nyingine 6 na Balozi 5. Katika masuala ya utawala kulikuwa na vipengele 5 vinavyosababishwa. Tathmini yangu ya kuhusu viashiria vya rushwa ilibaini kuwa Sekretarieti za Mkoa (7) zilikuwa na mapungufu katika masuala ya rushwa. Mbali na kuwa nimejumuisha changamoto zilizokabiliwa na NPS katika utekelezaji wa Sheria za utaifishaji na urejeshaji wa mali masuala mengine ya serikali ni kutokuanzishwa kwa Bodi ya wasimamizi, kutoteuliwa kwa Mkurugenzi wa NGOs na Bodi ya Ushauri wa Waziri. Matokeo ya kina yanaoneshwa katika Sura ya Sita.

Mapendekezo ya jumla

Baadhi ya taasisi zimeonyesha maboresho hasa katika eneo la kuanzisha na kufuata sheria na kanuni kuhusiana na kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, Bodi za Wakurugenzi, Kamati ya Ukaguzi na usimamizi wa vihatarishi. Ninashauri taasisi zote ziendelee kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani.

Maoni yangu ni kwamba, kutokana na kukosekana kwa Bodi ya Wadhamini, maamuzi ya kiseru hayakuweza kufanyika; na kwa ujumla, mwelekeo na mkakati wa shughuli za Taasisi havikuweza kutathiminiwa.

Nashauri kwamba mamlaka husika ihakikishe uteuzi wa Bodi unafanyika ili kuongeza utawala na kusimamia kazi na majukumu ya Taasisi.

Serikali inapaswa kuwa na muundo mzuri wa mipango ya kukabiliana na majanga. Aidha, pawe na mikakati ya kuhakikisha kuwa vifaa vya kompyuta na programu vinatunzwa ili kuweza kukabiliana na majanga pale yanapotokea.

Usimamizi wa rasilimali watu

Katika mwaka huu niliofanya ukaguzi nilibaini kuna mwendelezo wa kupungua kwa hoja katika usimamizi wa rasilimali watu na mishahara. Hii inaashiria kuwa serikali inaendelea kuchukua hatua katika kutatua mapungufu sugu katika usimamizi wa rasilimali watu na mishahara. Miongoni mwa hoja zilizoibuliwa mwaka huu ni pamoja na watumishi wanaokaimu nafasi za ukuu wa idara kwa muda mrefu, upungufu wa watumishi, kutozingatia mafunzo kwa watumishi, Makato katika mishahara kwa kiwango kisichoruhusiwa, kucheleweshwa kulipwa kwa stahiki za watumishi kiasi cha Sh. 591,662,727.

Mengine ni malipo ya Makato katika mishahara na mishahara isiyochukuliwa kiasi cha Sh. 132,951,455 ambayo hakuna hati za kukiri kupokea, mishahara isiyochukuliwa ya kiasi cha Sh. 227,883,921.55 hakikupelekwa Hazina, malipo ya kazi za ziada kiasi cha Sh. 306,645,407.99 ambayo hayakuthibitishwa na wasimamizi. Dosari katika usimamizi wa rasilimali un aweza kusabisha kutofikia malengo. Masuala yote haya yameelezwa zaidi sura ya saba.

Mapendekezo ya jumla

Pamoja na kuwa kumekuwapo na maendeleo mazuri katika eneo hili, nazidi kuwashauri Mafisa Masuuli kutatua masuala yanayojitokeza kama vile; watumishi kukaimu kwa muda mrefu, upungufu wa watumishi, kutokuwapo na mpango wa mafunzo, makato ya mshahara zaidi isivyostahili na madai ya watumishi.

Kukosekana kwa udhibiti wa ndani katika eneo la usimamizi wa rasilimali watu kunasababisha utendaji usio na tija kwani taratibu zote zinahitaji uwapo wa watumishi. Kwa hiyo changamoto katika eno hili zinahitaji kufanyiwa kazi haraka ili kuepusha watumishi kukosa motisha na kufikia malengo ye taasisi. Hivyo nashauri Maafisa Masuuli yafuatayo:

- a) Kutoa taarifa mapema kwa mamlaka zinazohusika na uteuzi pindi inapotokea nafasi zilizo wazi.
- b) Kuandaa mpango kwa nafasi zinazotarajiwa kuwa wazi ili kuepuka kukaimu nafasi za kazi kwa muda mrefu,
- c) Kuandaa mpango wa kuwajengea uwezo watumishi waliopo kazini.
- d) Maafisa Masuuuli wanakumbushwa kutoidhinisha mikopo kwa watumshi kinachozidi kiwango

Ukaguzi wa Wakala wa Serikali, Mifuko Maalum na Taasisi nyingine

Sura hii inaeleza matokeo ya ukaguzi wa Wakala wa Serikali 33, Mifuko Maalumu ya Fedha 17, Taasisi Nyingine za Serikali 41, na Mabonde ya Maji, ambapo nilibaini masuala muhimu yafuatayo katika kila ngazi:

i. Udhaifu uliobainika kwenye kaguzi za Wakala wa Serikali

Nilibaini udhaifu katika usimamizi kwa baadhi ya Wakala wa Serikali kwenye masuala muhimu kama nilivyobainisha hapo chini:

- a) Kushindwa kwa Wakala wa Serikali kujiendesha kwa kutumia mapato yao ya ndani kutekeleza bajeti ya maendeleo na ya kawaida kwa asilimia 84. Pia, nilibaini kuna anguko la makusanyo ya ndani kwa asilimia 8 ikilinganishwa na ya mwaka wa fedha uliopita.
- b) Wakala wa Serikali wameshindwa kupeleka kiasi cha Sh. 9,268,048,701 kwenda Mfuko Mkuu wa Hazina kama inavyotakiwa na Kifungu cha 11 (3) cha Sheria ya Fedha ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa mwaka 2016).
- c) Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) anadaiwa kiasi cha Sh. 57,094,951,223 ikiwa ni tozo ya riba kwa ucheleweshaji wa malipo ya Wakandarasi wa ujenzi na washauri.
- d) Kasi ndogo ya utekelezaji wa ujenzi wa majengo yenye thamani ya Sh 24,068,482,278 na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA).

- e) Uwekezaji usio na tija wa Nyumba za Makazi 851 huko Bunju, Dar es Salaam ambao ulitarajiwa kukusanya maduhuli ya Sh. 145,338,500,000.
- f) Baadhi ya Halmashauri zimeshindwa kuhamisha fedha ambazo zilitegemewa kwa ajili ya tozo ya Wakandarasi na fedha za zuio la kazi zenye jumla ya Sh. 6,655,417,488.24 kwenda kwa Wakala wa Barabara Vijijini na Mjini (TARURA).
- g) Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) alitarajia kuwa na jumla ya mabasi 305 kuanzia Juni 2015. Hata hivyo, ni mabasi 140 ndiyo yanayofanya kazi, huku kukiwa na ongezeko la abiria likikadiriwa kutoka 77,000 mwezi Mei 2016 hadi 200,000 mwezi Juni 2017.

ii. Udhaifu uliobainika kwenye kaguzi za Taasisi za Serikali

Nilibaini udhaifu na changamoto katika usimamizi wa Taasisi za Serikali katika kutekeleza malengo yao kama yalivyobainishwa hapo chini:

Nilibaini ubia usio na faida ulioingiwa baina ya SUMA JKT na Equator Automech Company Ltd (EACL), ambapo malengo ya ubia hayakutekelezwa kwa kipindi cha miaka 8 na kusababisha kutopatikana kwa mapato.

Nilibaini kuwa, kati ya watu 19,662,105 waliosajiliwa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), ni kadi 4,511,809 za vitambulisho ndizo zilizotengenezwa sawa na asilimia 23 tu ya idadi ya watu walioandikishwa. Pia, nilibaini kampuni ya IRIS Corporation Berhad ya Malaysia (Mkandarasi) imesimamisha shughuli zote za kutengeneza vitambulisho kuanzia 14 Machi 2018.

Kuwapo kwa wateja 1,317 waliolipia gharama za umeme na bado hawajaunganishwa mkoani Kagera

iii. Udhaifu uliobainika kwenye kaguzi za Bodi za Mabonde ya Maji na Mifuko Maalumu ya Serikali

Kaguzi za usimamizi wa Bodi za Mabonde ya Maji na Mifuko Maalumu ya Serikali zilibaini yafuatayo:

- a) Bodi za Mabonde ya Maji 4 (28%) kati ya 14 zilihamisha fedha za maendeleo kiasi cha Sh. 88,378,660 kwenda kugharamia matumizi ya kawaida
 - b) Umiliki wa matrekta yaliyotolewa kwa mkopo hayajaandikishwa kwa pamoja baina ya wakopaji na Mfuko wa Udhamini wa Pembejeo za Kilimo (AGITF) kama inavyotakiwa na Sera za Mkopo.
 - c) Kiasi cha Sh. 1,108,783,664 kiliondolewa kimakosa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwenye akaunti ya benki ya Mfuko wa Taifa wa Uwekezaji (NWIF) kwa nia ya kufidia deni la muda mrefu la kodi ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji.
- iv. **Mapungufu mbalimbali yaliyobainika kwenye usimamizi wa Malipo, Manunuzi na udhibiti wa Bajeti.**
- a) Kwenye usimamizi wa malipo, nilibaini kuwa kuna matumizi yenye nyaraka pungufu ya Sh. 1,347,912,012.83, masurufu yasiyorejeshwa ya Sh. 380,947,840.76; malipo ya Sh. 88,356,439.84 yaliyofanywa bila kukata kodi za zuio pamoja na malipo ya Sh. 7,956,320,106 hayakuambatishwa risiti za EFD.
 - b) Kwenye usimamizi wa Manunuzi, nilibaini kuwa kuna malipo ya Sh. 935,358,546.88 yaliyofanyika bila ya kukagua mali zilionunuliwa na manunuzi ya Sh. 2,976,003,845.95 yaliyofanyika bila kupata idhini ya Bodi ya Zabuni.
 - c) Kwenye udhibiti wa Bajeti, nilibaini kuwa Kuna malipo ya Sh. 232,512,534 yaliyofanyika nje ya bajeti iliyopitishwa na Malipo ya shilingi 235,697,497.24 yaliyofanyika nje ya makubaliano ya mkataba (MOU) baina ya Serikali na Bodi ya Mfuko wa Barabara.

Mapendekezo ya Jumla - Usimamizi wa matumizi katika Wakala wa Serikali

Mbali na mapendekezo niliyoyatoa katika taarifa zangu zilizopita, bado nimeendelea kubaini Taasisi za Serikali kuwa na udhibiti wa ndani usioridhisha unaosababisha kuwapo kwa mapungufu.

Hivyo basi, naendelea kuhimiza Wakala wa Serikali, Taasisi, na Mifuko Maalumu ya Fedha kuimarisha mfumo ya udhibiti wa ndani wa taasisi zao, ikiwa ni pamoja na kujenga uwezo wa wafanyakazi. Mbali na hayo, nyaraka zinapaswa kuboreshwa kwa kufuata Sheria na Kanuni za Fedha za Umma, Sheria na Kanuni za Manunuzi ya Umma, pamoja na Sheria na Kanuni za Bajeti.

Mapendekezo kwa wakala maalum

- a) *Ili kupunguza utegemezi wa Serikali, nazishauri Menejimenti za Wakala wa Serikali kukusanya mapato ya ndani ili kujiendesha, kubuni vyanzo vipya vya mapato, kuendesha shughuli zao kwa kutumia mbinu za kisasa za kibiashara, pamoja na kupitia upya viwango vya tozo wanazotumia.*
- b) *Nashauri serikali kutoa fedha za utekelezaji wa miradi ya barabara zinasosimamiwa na Wakala wa Barabara Tanzania kwa wakati kama ilivyoidhinishwa na bunge ili kuepuka malipo ya ziada yanayotokana na riba.*
- c) *Nashauri Menejimenti ya Wakala wa Majengo (TBA) kubadilisha mkakati wake wa masoko ikiwa ni pamoja na kutafuta ushauri kutoka Wizara mama ili kuwezesha nyumba zilizokamilika kuuzwa kwa mtu yeyote badala ya watumishi wa Serikali peke yao.*
- d) *Nawashauri Mamlaka za Halmashauri tajwa kuhamisha mali na madeni yote yanayohusiana na miradi ya barabara kwenda kwa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA). Pia, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) inapaswa kufuatilia utekelezaji*
- e) *Nashauri Wakala wa Mabasi Yaendayo kwa kasi (DART) kuharakisha mchakato wa kumpata mtoa huduma wa pili na kuongeza mabasi zaidi ili kuendana na kasi ya ukuaji wa mahitaji ya usafiri wa mwendo kasi.*

Mapendekezo kwa Taasisi nyingine za Serikali

- a) *Nashauri SUMA JKT kufanya upembuzi wa kina kabla ya kuingia katika ubia. Hii itasaidia kupunguza athari ya kuingiza rasilimali zake kwenye uwekezaji usio na faida*
- b) *Nashauri Mamlaka ya Vitambulisho ya Taifa kuharakisha zoezi la usajili na utengenezaji wa vitambulisho vya taifa. Pia, kutathimini utendaji kazi wa mkandarasi ili kuweza kuchagua kama kumuongezea muda wa mkataba au kuingia kwenye makubaliano mapya na mkandarasi mwingine.*
- c) *Nashauri Wakala wa Nishati Vijijini (REA), kusimamia kwa ufanisi na kuhakikisha kwamba miradi yote inayotekelezwa inakamilika ndani ya muda uliowekwa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.*

Mapendekezo kwa Bodi za Mabonde ya Maji na Mifuko Maalum

- a) *Nashauri Bodi za Mabonde ya Maji kuhakikisha zinaboresha makusanyo yao ya ndani ili kuepukana na uchepushaji wa fedha ambapo yanaweza kuathiri Miradi ya Maji*
- b) *Nashauri Mfuko wa Udhamini wa Pembejeo za Kilimo (AGITF) kuhakikisha matrekta yote ya mkopo yanaandikishwa kwa usajili wa pamoja. Pia, yanasimamiwa vizuri na wakopaji ili kulinda dhamani yake ikiwa mkopaji atashindwa kulipa.*
- c) *Nashauri Mfuko wa Taifa wa Uwekezaji (NWIF) pamoja na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kufanya ufuatiliaji na kuitaka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kurejesha fedha zilizochukuliwa kwenye akaunti ya Benki ya NWIF.*

Manunuzi na Usimamizi wa Mikataba

Katika ukaguzi wa manunuzi na usimamizi wa mikataba kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2018, nilibaini taasisi za umma kadhaa zilizofanya ukiukaji wa Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2011 (iliyorekebisha mwaka 2016) na Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013. Hoja zenyewe zimeelezwa kwa kina katika sura ya tisa.

Pia, katika ukaguzi nimebaini kuwa Taasisi za Serikali Kuu zimeonesha juhudi na nia ya kutekeleza ushauri na mapendekezo mbalimbali yaliyotolewa kwa taasisi husika. Pamoja na hayo, ukaguzi ulipokuwa unafanyika ilibanika kuwa udhibiti wa ndani uliokuwa unatarajiwa kuwapo haukuthibitika wakati wa ukaguzi. Kuwapo kwa hoja nyingi za ukaguzi katika manunuzi na usimamizi wa miradi kunaleta mashaka kuwa thamani ya fedha haikuweza kupatikana katika manunuzi na mikataba iliyoingwiwa na wazabuni/wakandarasi.

Ufuatao ni muhtasari wa hoja za ukaguzi na ushauri:

- a) Ukaguzi wa Manunuzi katika mwaka wa fedha 2017/2018 umebaini kiasi cha Sh 4,615,040,383.12 kimetumika katika kununua bidhaa, huduma, ushauri wa kitaalam na kazi za ujenzi ndani ya Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa pasipo kutumia taratibu za kushindanisha wazabuni. Hii ni kinyume na Kanuni ya 163 na 164 za Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013. Hili linaleta shaka katika kufikia thamani ya fedha katika Taasisi husika.
- b) Taasisi nane (8) zilibainika kufanya manunuzi yenye thamani ya Sh 5,373,435,190.36 bila kupata kibali cha bodi ya zabuni ambayo ni kinyume na Kifungu cha 35(3) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011 na Kanuni 55 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2013. Kufanya Manunuzi bila kibali cha bodi ya zabuni kunaweza kusababisha kuingia mkataba na mzabuni asiyekuwa na uwezo wa kutoa huduma kama ilivyotarajiwa, Ukiachilia mbali kutofuata sheria na kanuni zilizotajwa hapo juu, pia thamani ya pesa katika Manunuzi haitoweza kufikiwa.
- c) Ilibainika kuwa Taasisi tano (5) zilifanya manunuzi ya kazi za Ujenzi, bidhaa huduma kiasi cha Sh 1,174,767,341 bila kuwapo kwa makubaliano ya kimkataba na wazabuni. Hii ni kinyume na Kanuni namba 10 (4) ya Kanuni za Manunuzi ya umma ya mwaka 2013. Hata hivyo, kuna maboresho ya asilimia 58 katika kufuata sharia; kwani Taasisi zimepungua kutoka saba (7)

ikilinganishwa na mwaka uliopita ambapo zilikuwa Taasisi kumi na mbili (12).

- d) Nilibaini mapungufu mbalimbali katika taratibu za manunuzi na usimamizi wa miradi niliyokagua katika taasisi 13 ya kiasi cha Sh. 119,228,294,260.45.
- e) Nilibaini kuwapo kwa Taasisi 14 zilizonunua bidhaa na kupata huduma zenye thamani ya Sh 628,364,144.05 bila kuzikagua na kukubaliwa na Kamati ya Kukagua na Kupokea. Hii ni kinyume na Kanuni ya 244 (1) ya Kanuni za Manunuzi za mwaka 2013. Hivyo, nazishauri Taasisi za Serikali Kuu kuanzisha Kamati ya Mapokezi na Ukaguzi.
- f) Nilibaini Taasisi 13 zilifanya Manunuzi ya bidhaa na huduma zenye thamani ya Sh 5,356,549,884.76 ambazo hazijapokelewa, na kufanya thamani ya fedha kutopatikana.
- g) Nilibaini Taasisi 14 zilikiuka Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 kwa kufanya manunuzi ya bidhaa na huduma za kiasi cha Sh.432,737,939,877.68 kutoka kwa wazabuni wasiokuwamo katika orodha ya waliopitishwa na Wakala wa Ugavi, dawa kununuliwa nje ya MSD pamoja na matengenezo kutoka kwa mkandarasi asiyesajiliwa na Bodi ya Wakandarasi.
- h) Taarifa ya PPRA inaonesha kuwa, kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2018, taasisi zilizofanya manunuzi zimekidhi matakwa ya Sheria ya Manunuzi kwa hali ya wastani wa asilimia 74 ambayo ni sawa na ile ya mwaka wa fedha uliopita 2016/2017. Hata hivyo, hii ni chini ya malengo ya mwaka 2017/2018 yaliyotarajiwa kufikia asilimia 80. Kwa kulinganisha na mwaka uliopita, mwaka huu wa Ukaguzi unaonesha kuwa wastani wa kuzingatia sheria za manunuzi umeshuka toka asilimia 78 hadi 75 ambayo haikuwa na athari yoyote katika wastani wa uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma wa asilimia 74 uliofikiwa mwaka wa fedha uliopita.

Mapendekezo ya Jumla

Taasisi zinashauriwa kufuata muda uliopangwa katika mpango wa manunuzi wa mwaka, hasa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuendana na sheria.

Ili kuendana na changamoto za kisekta, PPRA inahitajika kufanya yafuatayo; (i) Kuendelea kufuatalia na kuhakikisha kuna uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi na kuchukua hatua stahiki kwa wahalifu, (ii) Kuendelea kuwajengea uwezo watumiaji wote wa Sheria ya Manunuzi kupitia mafunzo mbalimbali (iii) Wadau wanaotumia Sheria ya Manunuzi waelimishwe na kutumia zana na mifumo iliyoanzishwa na PPRA (iv) Kuungana na Taasisi mbalimbali zinazohusika kuandaa na kutoa viwango vya bidhaa na huduma mbalimbali zinazotumika katika Taasisi za serikali. (v) Kuungana na makundi maalum yanayosaidia kuzijengea uwezo taasisi za serikali na kuzipa usajili maalumu. (vi) PPRA waendeleo kujitangaza katika huduma wanazotoa kupitia kuandaa na kusambaza sera na mikakati ya vitendea kazi ili kuhamasisha wadau waweze kuchangia huduma zinazohitaji fedha.

Mapitio ya taarifa ya Mhakiki Mali wa Serikali. Kupitia taarifa yake ya mwaka 2016/2017, nimebaini kuna makosa yenye thamani ya Sh 6,223,172,903.52 katika Taasisi ishirini (20) ikilinganishwa na ya mwaka wa fedha 2017/2018 ambapo yalikuwa na thamani ya Sh. 968,085,433.63 katika Taasisi ishirini (20). Hii inamaanisha kuwapo kwa upungufu wa kiasi cha Sh. bilioni 5.26, sawa na asilimia 84. Zaidi, hii inamaanisha kuwa, Taasisi zimeongeza uzingatiaji wa sheria na kanuni za manunuzi. Masuala yote muhimu yameelezwa kwa kina katika sura ya Tisa.

Usimamizi wa matumizi

Usimamizi wa matumizi unahusisha taratibu zote muhimu zilizowekwa katika kusimamia malipo yaliyofanywa na Wizara na Idara, na kuhakikisha kuwa yanazingatia masuala ya ufanisi, ufasaha na yanafanyika kwa wakati.

Ukaguzi umebaini kuwa, kutokana na kutokuwapo kwa nyaraka stahiki, baadhi ya Wizara na Idara zimeendelea kuonesha dosari katika matumizi yaliyosababishwa na udhaifu wa udhibiti. Wakaguliwa walifanya miamala ambayo haikuzingatia kanuni na miongozo mingine iliyowekwa. Zifuatazo ni dosari hizo:

Dosari kwenye matumizi ya Sh. 4,665,410,500 yaliyofanywa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwenda kampuni binafsi za kisheria bila kufuata makubaliano ya Mkataba, mapungufu katika usimamizi wa ankra za Matibabu nje ya nchi Sh.7,013,014,856.65, utata wa miamala iliyofanywa na DAS Tarime Sh.514,000,000, ongezeko la gharama za kukodi magari katika balozi za Tanzania zilizopo Moroni na Brasilia Sh. 87,461,046,99, malipo yasiyo na vithibitisho Sh. 4,369,240,033.86, Kodi ya zuio ambayo haijadaiwa Sh. 722,173,494.09, malipo yasiyokuwa na risiti za kielektroniki (EFD) Sh.1,432,,407,818.97 na malipo ya posho kwa Watumishi yasiyo ya kawaida yalitofanywa na Tume ya Huduma za Walimu Sh. 721,050,000.

Aidha, nimebaini 18% ya VAT ambayo haikudaiwa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji (Fungu na 49) kwenye mradi wa Programu ya Sekta ya Maendeleo ya Maji (WSDP) Sh.49,385,014.88, malipo ya madeni ya miaka ya nyuma ambayo yalikuwa hayajaoneshwa Sh. 145,067,788.50, kiasi kilichoazimwa kwenye akaunti za amana bila kurejeshwa Sh. 562,635,234.24, dosari katika usimamizi wa Masurufu Sh.6,356,450,927.45, na malipo yaliyofanyika kimakosa kwenye vifungu visivyotahili Sh.885,994,926,713.82. Vilevile nimebaini malipo yasiyo na tija Sh.668,764,264.53 malipo yaliyofanyika bila kuidhinishwa Sh. 193,182,333.28, malipo yasiyostahili kutoka kwenye akaunti za amana Sh.192,582,796.42, na Bakaa za Amana zilizokaa muda mrefu bila kudaiwa Sh.2,532,574,210.92. Ukaguzi pia ulibaini hasara ya fedha za umma zilizosababishwa na ujazaji usio sahihi wa madai kutoka NHIF Sh. 291,933,248 pamoja na malipo yaliyozidishwa kiwango Sh. 133,528,196.68

Naamini kama mapendekezo yangu yatafanywa kazi kwa umakini, yataondoa udhaifu ulioibuliwa. Maelezo ya kina yametolewa kwenye Sura ya Kumi.

Mapendekezo ya jumla

Katika mwaka huu wa fedha taasisi nyingi zilikuwa na changamoto za usimamizi wa matumizi kutokana na kutozingatia Sheria husika na Kanuni, ikiwemo Sheria ya fedha za umma (Iliyorekebisha 2004) pamoja na Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015.

Ili Serikali iimarisha uangalizi, uwazi, uwajibikaji, utawala bora na kuchochea matumizi mazuri ya usimamizi wa rasilimali fedha katika nyanja zote za Wizara, Idara, Balozi na Sekretarieti za Mikoa, inashauriwa kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani ambao, kwa kiwango kikubwa, umesababisha mapungufu katika usimamizi wa matumizi yaliyofanyika.

Vilevile, kwa masuala yanayoashiria kuwapo kwa ubadhirifu, Serikali inashauriwa kutumia vyombo vyake vya kiuchunguzi ili kuthibitisha zaidi kiwango cha udhaifu ulioibuliwa na Ukaguzi.

Aidha, baadhi ya udhaifu ulioibuliwa umekuwa ukijirudia katika ripoti zangu, Hiyo jitihada zaidi zinapaswa kufanywa ili udhaifu unaoonekana upunguzwe au kuondolewa kabisa. Pia, kuna haja ya kuwa na usimamizi wa jumla ambao ni endelevu ili kuhakikisha kuwa Maafisa Masuuli/Mamlaka na Menejimenti za uandamizi wanawajibika kutoa uhakika wa viwango vinavyotakiwa ili kuwa na hali itakayoboresha matokeo ya ukaguzi.

Usimamizi wa Mali za Kudumu na Madeni

Mapungufu katika Usimamizi wa Mali za Kudumu

Wizara ya Fedha imeweka taratibu mbalimbali za namna ya usimamizi wa Mali za Kudumu ambao unaonyesha muelekeo, kuzingatia matakwa ya taaluma ili kuwe na ufanisi katika matumizi ya mali za umma. Hata hivyo, mapitio yaliyofanywa katika usimamizi na taarifa za Mali za Kudumu zilizoko chini Wizara, Sekretarieti za Mikoa na ofisi za Ubalozi nje ya Nchi yalibainika mapungufu mbalimbali. Nayo ni: majengo ya umma yalitelekezwa, ujenzi wa majengo unaosuasua, kutoshughulikia mapungufu yaliyojitokeza kwenye majengo ya umma ambayo bado yapo kwenye kipindi cha

matazamio, na usimamizi usioridhisha wa Mali za Kudumu zilizotaifishwa na Serikali. Mengine ni regista ya Mali za Kudumu kutokuwa kamilifu, Mali za Kudumu ambazo hazitumiki lakini hazijauzwa wala kufanyiwa matengenezo, kukosekana kwa nyaraka za umiliki wa ardhi na nyumba za Serikali, pamoja na Mali za Kudumu kutokuwa na namba za utabulisho. Zaidi, ukaguzi ulibaini kutokutenganisha ardhi na majengo kwenye taarifa za fedha kulingana na matakwa ya viwango vya kimataifa vya kuandaa taarifa za fedha katika sekita ya umma na kutokuwapo kwa mpango na taarifa za matengenezo ya Mali za Kudumu. Maelezo ya kina yameripotiwa katika sura ya Kumi na Moja

Mapungufu katika Usimamizi wa Matumizi ambayo Hayajalipwa

Nilibaini mlundikano wa matumizi ambayo hayajalipwa yaliyofikia kiasi cha Sh. 3.106 Trilioni ikiwa ni ongezeko la Sh.0.426 trilioni sawa na asilimia 15 ikilinganishwa na kiasi cha Sh. 2.683 trilioni kwa mwaka uliopita. Moja ya sababu za msingi inayofanya taasisi kuwa na mlundikano wa matumizi yasiyolipwa kwa wakati na Wizara ya Fedha kutokupeleka fedha kwenye taasisi kama bajeti zilivyooidhinishwa.

Pia, nimebaini kuwapo kwa matumizi ambayo hayajalipwa. Matumizi hayo yanajumuisha gharama za matibabu kwa wagonjwa wanaotibiwa Hospital za India kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Sh. 29 bilioni. Ikilinganishwa na mwaka wa fedha uliopita ambapo gharama zilikuwa kiasi cha Sh. 28 bilioni, kuna ongezeko la kiasi cha Sh.0.5 bilioni sawa na asilimia mbili (2).

Madai ya kisheria kiasi cha Sh. 52,631,626,396.69 yaliripotiwa chini ya taasisi kumi na moja (11) na yanasubiria maamuzi ya mahakama dhidi ya makampuni na watu binafsi. Taasisi husika hazina bajeti kwa ajili ya madai kama haya. Hivyo, kama madai yakithibitishwa na mahakama itabidi yalipwe kutoka katika fedha za bajeti ya taasisi husika ambapo fedha hizo zilikuwa zimelengwa kutoa huduma, hatimaye kupunguza uwezo wa kifedha wa taasisi. Maelezo ya kina yapo katika Sura ya Kumi na Moja.

Mapendekezo

Usimamizi wa Mali za Kudumu

Licha ya mapendekezo yangu ya miaka ya nyuma, taasisi bado zina kazi ya kufanya kuhusiana na usimamizi wa Mali za Kudumu. Kazi hizo zinajumuisha kuwa na regista ya Mali za Kudumu zenye taarifa sahihi zilizojazwa kwa wakati kwa kuzingatia sheria zilizopo; pamoja na kuhakikisha usimamizi endelevu unakuwepo, ikijumuisha kuondosha Mali za Kudumu kwenye regista.

Kwa ujumla, baadhi ya viashiria vya hatari ambavyo nimeviona kama sehemu ya ukaguzi ni pamoja na uwezekano wa Mali za Kudumu kutumika vibaya, na baadaye taarifa ambazo sio sahihi kuingizwa kwenye mfumo wa kutoa taarifa za fedha, hivyo kuathiri usahihi wa taarifa za fedha.

Mlundikano wa matumizi ambayo hayajalipwa

Serikali inadhibiti matumizi yake kupitia ukomo wa bajeti inayoingizwa kwenye mfumo - Epicor. Kwa hiyo, ili kudhibiti mlundikano wa matumizi ambayo hayajalipwa kwenye taasisi, matumizi yote yaingizwe kwenye mfumo (Epicor) wakati yanapotokea. Ili kufanikisha hili, nashauri Wizara ya Fedha pamoja na mzabuni (SOFTECH) kuutengeneza mfumo utakaowezesha matumizi ambayo hayajalipwa kuingizwa wakati yanapotokea ili kupunguza mlundikano. Aidha mfumo huo utengenezwe ili kukidhi matakwa ya Mfumo wa Kimataifa wa Uandaaji wa Taarifa za Fedha katika Sekita za Umma (IPSAS Accrual).

Madai yaliyopo Mahakamani

Kama nilivyopendekeza katika taarifa zangu zilizopita, naendelea kupendekeza Serikali ihamasishe kila taasisi ya serikali iwe na mikakati thabiti ya usimamizi wa madeni kulingana na mazingira yao kwa ajili ya kuhakikisha hatari zilizopo katika taasisi zao zinasimamiwa na kupunguzwa mpaka kufikia kiwango cha kudhibitiwa.

Ukaguzi Maalum wa Ununuzi wa Mfumo wa Kidigitali wa Usajili wa Wapiga Kura (BVR) Uliofanywa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi

Nilibaini kwamba kabla ya kusainiwa kwa mkataba Na. IE/018/2012-2013/HQ/G/19 kwa ajili ya manunuzi ya BVR 8,000 baina ya Tume ya Uchaguzi (NEC) na Kampuni ya Lithotec Exports LTD ilikubalika kuwa, vifaa vya usajili wa wapiga kura (BVR) vitakavyoletwa vilandane kimatumizi na vile vilivyokwishanunuliwa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA). Hata vivyo, wakati wa utekelezaji Mzabuni, hakuweza kuleta BVR zinazolandana na zile zinazotumiwa na RITA na NIDA. Hivyo kusababisha matumizi yasiyo na tija ya Sh. 862,085,100 yaliyofanywa na NIDA ya kununua leseni mpya za “Windows na Biometric Algorithms” ili kubadilisha BVR 5,000 zilizopokelewa kutoka NEC ziweze kufanya kazi na mfumo wa BVR wa NIDA. Matumizi haya yangeweza kuepukwa kama mkataba ungesimamiwa vya kutosha na NEC. Pia, nilibaini mzabuni alilipwa kiasi cha Dola za Kimarekani 148,243.73 zaidi ya bei ya mkataba na mafunzo kwa maafisa TEHAMA 15 wa NEC hayakufanyika licha ya malipo ya Dola za Kimarekani 358,650 kulipwa kwa mzabuni.

Ukaguzi Maalum wa Ununuzi wa Mfumo wa Utambuzi wa Alama za Vidole (AFIS) Uliofanywa na Jeshi la Polisi Tanzania

Katika ukaguzi wangu wa mkataba baina ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani na Mzabuni Lugumi Enterprises Limited, nilibaini kuwa mahitaji ya kitaalamu kutoka idara ya mtumiaji wa mfumo hayakuzingatiwa wakati wa kutathmini na kutoa zabuni hiyo. Pia, nilibaini tofauti ya bei ya jumla ya Sh.556, 647,610 kwa vifaa vinavyounda mfumo huo ambavyo vimetengenezwa na mtengenezaji mmoja, vikiwa na sifa moja na utendaji kazi unaofanana kama ilivyonekana katika orodha la Jedwali la Mahitaji. Pia, Mzabuni alipewa zabuni pasipokuwa na leseni ya Biashara inayoendana na uuzaji na ufungaji wa mitambo ya udukuzi (AFIS). Zaidi, nilibaini kuwa Manunuzi haya hayakuwamo kwenye bajeti iliyopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia, nilibaini kuwa utaratibu uliotumika kuhamisha fedha toka Hazina kwenda Jeshi la Polisi haukuwa sahihi.

Pia, nilibaini Vifaa vya Utambuzi wa Alama za Vidole vyenye thamani ya Sh. 1,736,056,030.45 havikufungwa kwenye Magereza 35 yaliyoainishwa; badala yake, vifaa hivyo vilionekana kuhifadhiwa katika Ofisi ya Upelelezi ya Makao Makuu ya Jeshi la Polisi (CID). Vilevile, mafunzo kwa Wataalamu 30 yaliyogharimu jumla ya Sh. 604,390,244 hayakufanyika. Zaidi, nilibaini “Monitor 58” aina ya Dell zenye thamani ya Sh.159,166,100 zilizopelekwa kwenye Kitengo cha Uchunguzi wa kisayansi cha Makao Makuu ya Jeshi la Polisi (Forensic Unit) havikuonekana wakati wa Ukaguzi huu. Zaidi, hakukuwa na ushahidi wa kufanyika kwa huduma ya matengenezo na ufuatiliaji wa jumla ya Sh.3,304,000,000 kwenye mikoja minane (8) ya Temeke, Mwanza, Simiyu, Rukwa, Tabora, Kigoma, Geita na Kinondoni. Pia, nilibaini “Monitor” 213 aina ya dell optiplex modeli ya L2250P zenye ukubwa wa inchi 22 hazikuletwa na Lugumi Enterprises Limited, hivyo kusababisha hasara ya Sh.195,221,682 kwa Serikali.

Ukaguzi Maalum wa Tuhuma za Ubadhirifu wa Fedha za Umma wakati wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege Songwe Uliofanywa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA)

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa, jumla ya Sh.5,482,610,339.86 zililipwa kwa Mkandarasi bila ya kuidhinishwa na Mhandisi Mshauri. Zaidi ya hilo, nilibaini jumla ya Sh. 570,508,125 zililipwa zaidi ya gharama zilizoidhinishwa na Mhandisi Mshauri. Pia, nilibaini kati ya malipo ya awali ya Sh.1,704,766,352.25 aliyolipwa Mkandarasi kwa ajili ya kuanzisha shughuli za ujenzi, ni Sh.176,565,475.27 tu ndizo zilizorejeshwa; na bakaa ya Sh.1,528,200,879.98 haikurejeshwa hadi kufikia muda wa Ukaguzi. Zaidi, nilibaini malipo mara mbili ya Sh.1,433,387,095.46 yaliyofanyika kwa udanganyifu kupitia Maafisa wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA). Aidha, jumla ya Sh. 1,950,000,000 zililipwa bila ya kuwapo kwa Jedwali la Vipimo na Hati za madai zilizoidhinishwa na Mhandisi Mshauri.

Ukaguzi Maalum wa Ununuzi wa Sare za Polisi uliofanywa na Jeshi la Polisi Tanzania

Katika Ukaguzi huu maalum nilibaini maoni ya Kisheria ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yanayohusu uwasilishaji wa Kiapo cha Nguvu ya Kisheria (Power of Attorney) na leseni halali ya biashara

hayakuzingatiwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani wakati wa kusaini Mkataba na ME.014/PF/2015/2016/G/30 Lot 2 uliohusu ununuzi wa Sare za Polisi. Pia, nilibaini kuwa Jeshi la Polisi lililipa jumla ya Sh. 16,660,000,000 bila ya kuwa na ushahidi wa uagizaji na upokeaji wa Sare za Polisi kwa Boharia Mkuu wa Jeshi la Polisi.

Ukaguzi Maalum wa Masufuru uliofanyika Katika Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi (Fungu Na. 43), Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu Na. 46), Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Fungu Na. 52) na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Fungu Na. 98)

Wakati wa Ukaguzi huu Maalum nilibaini Masufuru ya jumla ya Sh.245,194,247 yaliyotolewa kwa maafisa wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi (Fungu Na. 43) na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Fungu Na. 52) hayakurejeshwa hadi muda wa ripoti hii mwezi Agosti 2018. Zaidi, nilibaini jumla ya masufuru ya Sh.32,529,895 yalitumika kulipia shughuli za Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi (Fungu Na. 43) ambazo hazikubajetiwa. Pia, nilibaini jumla ya Masufuru ya Sh.11,756,128,459.71 kutoka Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi (Fungu Na. 43), Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu Na. 46), Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Fungu Na. 52) na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Fungu Na. 98) yalitolewa na kurejeshwa nje ya mfumo wa “Epicor” licha ya kuwapo kwa Moduli ya Masufuru (Imprest Module) iliyogharamiwa na Serikali kwa jumla ya Sh. 5,371,391,852.05.

Kwa kuongezea, nilibaini nyaraka pungufu kwenye masufuru ya jumla ya Sh. 2,610,449,214 yaliyorejeshwa kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Fungu Na. 52), Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu Na. 46) na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi (Fungu Na. 43). Zaidi ya hilo, nilibaini masufuru ya jumla ya Sh.672,248,976.80 kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu Na. 46), na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Fungu Na. 52) yalirejeshwa bila ya kuwapo na nyaraka zozote.

Ukaguzi Maalum wa Ununuzi wa Magari 777 aina ya Ashok Leyland uliofanywa na Jeshi la Polisi Tanzania.

Nilibaini kuwa hadi kufikia mwezi Desemba 2018 gharama za kujitolea ya mkopo (Commitment charges) ya Dola za Kimarekani 287,087.17 (sawa na Sh. 642,256,630.39) zilizalishwa kwenye mkopo ambao haujatumiwa na Serikali. Hakuna ushahidi uliowasilishwa kuthibitisha kama mahitaji ya Magari haya yaliibuliwa na mtumiaji. Pia, nilibaini Ashok Leyland hakuwa na uwezo wa kuleta magari yote kwani kati ya magari 777, ni magari 507 (sawa na asilimia 65) yenye gharama ya Dola za Kimarekani 25,498,100 ndiyo yaliweza kutoka kwake. Magari 270 yaliyobakia (sawa na asilimia 35) yenye gharama ya Dola za Kimarekani 4,103,000 yaliagizwa kutoka kampuni ya Great Wall Motors (mtengenezaji kutoka China).

Zaidi, nilibaini kuwa mikataba yote iliyosainiwa haikuwa na Jedwali la uletaji magari (delivery schedule); na muda wa mkataba haukuoneshwa wazi kwenye mkataba wa awali, nyongeza na mwisho. Pia, nilibaini magari 497 yaliletwa bila ya kuwapo kwa taarifa ya ukaguzi kutoka kwa mtengenezaji. Hivyo, hakuna uhakika kama magari hayo yalikaguliwa kabla ya kuwasili kwenye Bandari ya Dar es Salaam. Zaidi, nilibaini kuwa kabrasha la Zabuni na Barua ya mwaliko vilitumwa kwa mzabuni kabla ya mkopo kuidhinishwa na Wizara ya Fedha na Mipango. Pia, nilibaini Magari yote yalikaguliwa na Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA), lakini magari 181 yenye thamani ya Dola za Kimarekani 7,447,428 yalikuwa na hitilafu. Shehena hiyo haikutoa uhakika kama magari ni mapya au la. Pia, nilibaini magari 22 yenye thamani ya Dola za Kimarekani 572,506 yalikuwa na kasoro, na hayakupokelewa na Jeshi la Polisi.

Pia, nilibaini kuwa magari 497 yalitolewa Bandarini bila ya Hati ya kutolea Mizigo (Release Order) toka Idara ya Forodha na Ushuru, kinyume na taratibu za Idara ya Forodha na Ushuru CED-702-F. Hii pia ilisababisha taratibu za bandari kukiukwa. Pia, nilibaini masharti ya mkopo yalikuwa ya kibiashara; na masharti ya malipo kwenye mkataba wa magari yalikuwa hayaendani na masharti yaliyotajwa kwenye mkataba wa mkopo.

Ukaguzi Maalum wa Tuhuma za Matumizi Mabaya ya Marejesho ya Mikopo kutoka Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF) Tawi la Morogoro

Katika uchunguzi wangu, nilibaini kuwa taarifa za Mfuko zimeonesha kiasi cha mikopo kilichotolewa kuanzia tarehe 1 Januari, 2016 mpaka 31 Desemba, 2017 ni Sh.196,900,000 kwa vikundi 26; na kiasi cha Sh.128, 642,800 kilirejeshwa na wakopaji kupitia NMB benki. Hata hivyo, katika uhakiki niliufanya kwenye vikundi husika, nilibaini kiasi cha Sh.196,131,800 kilirejeshwa hadi kufikia Desemba 2017. Hii, inamaanisha kuwa, kiasi cha Sh.67,489,000 hakikuoneshwa kwenye Taarifa za Mfuko wala benki. Katika majadiliano na wakopaji, niliambiwa kuwa watumishi wa Mfuko walikuwa wanawataka wakopaji kulipa marejesho ya mkopo kwa fedha taslimu.

Vilevile, nilibaini wanakikundi 16 wa “Nyota na Ing’ae” walipata mkopo wa Sh. 15, 500,000 tarehe 7 Desemba 2016 kupitia benki ya NMB. Ukaguzi ulithibitisha kuwa kiasi cha Sh.2,500,000 hakikupokelewa na wanakikundi kwa sababu kiasi hicho kililipwa kwa Meneja wa tawi kama marejesho ya deni ambalo, kimsingi, halikuwepo; kwani kikundi hakikuwahi kuchukua mkopo hapo nyuma. Nilibaini pia, stakabadhi zenye kiasi cha Sh. 76,560,550 hakikuwa na nakala halisi na hazikuwapo kwenye taarifa za Mfuko. Hata hivyo, Watumishi wa Mfuko hawakuwa na la kusema kuhusiana na jambo hili.

Zaidi, nilibaini wafanyakazi wa Mfuko wa tawi la Morogoro walifanya udanganyifu kwa kughushi nyaraka za utambulisho wa wanachama watano (5) wa kikundi cha Kilakala Kijana Jiari na kujipatia mkopo wa kiasi cha Sh. 15,000,000 kupitia kikundi kinachoitwa Mwale Cleaners Company. Pia, nilibaini uanzishwaji wa kikundi hewa chenye jina la Maendeleo Uhuru ambacho nyaraka za wanakikundi 10 wa kikundi cha Raha Kikoba zilitumika na kujipatia mkopo wa kiasi cha Sh. 5,000,000 kupitia benki ya NMB Bank. Kwa taarifa zaidi rejea Sura ya 12.

Mapendekezo

Napendekeza kuwa Serikali iwajengee uwezo watumishi wa Idara ya Manunuzi pamoja na Wanasheria katika kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Mikataba kwa kuwapa mafunzo stahiki na ya mara

kwa mara. Mafunzo haya yataongeza uelewa katika usimamizi wa mikataba na kupunguza matukio yatokanayo na usimamizi wa usioridhisha wa mikataba na ambao umesabisha upotevu wa fedha wa umma wa mara kwa mara.

Nachukua fursa hii kupendekeza hatua stahiki za kisheria na kinidhamu zichukuliwe dhidi ya Maofisa waliohusika moja kwa moja na wote walio Shirikiana na wazabuni kupora mali za umma. Nasisitiza, pawe na ufuatiliaji wa marejesho kutoka kwa wazabuni. Hili litatekelezwa kwa ufanisi kwa kuanzisha Kitengo Maalum kwa ajili ya ufuatiliaji.

Ukaguzi wa Vyama vya Siasa

Ukaguzi wa Vyama vya Siasa umebaini kuwa Vyama vinne (4) kati ya kumi na tisa (19) vyenye usajili wa kudumu havikuwasilisha Taarifa za Fedha. Vyama hivyo ni NRA, ADC, TLP na Demokrasia Makini. Nimeshindwa kuthibitisha uhalali wa matumizi ya fedha za Vyama husika. Katika ukaguzi, nimebaini kuwa chama cha CHADEMA kilinunua gari jipya aina ya Nissan Patrol Y61 Series GRX kwa Dola za Kimarekani 63,720 (sawa na Sh.147,760,080). Gari hilo halikusajiliwa kwa jina la Bodi ya Wadhamini ya CHADEMA, bali limesajiliwa kwa jina la mwanachama ambaye ni Mbunge. Ukaguzi huo umebaini kuwa, gari lililonunuliwa lilioneshwa kwenye taarifa za fedha kama mkopo kwa Mbunge huyo bila kuwa na makubaliano ya mkopo yaliyosainiwa kati ya Mbunge huyo na Bodi ya Wadhamini ya CHADEMA. Pia, ukaguzi umebaini kuwa bado kuna magari yenye thamani ya Sh.172,227,083 ambayo hayajapokelewa hadi wakati wa ukaguzi mwezi Januari 2019. Pia, hapakuwa na nyaraka za manunuzi na uagizaji kutoka nje.

Katika Ukaguzi, nimebaini kuwa UWT (Umoja wa Wanawake wa CCM) haukuwasilisha michango ya kila mwezi kwenda Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF). Hadi kufikia Mei, 2018 UWT (CCM) ilikuwa na deni la Sh.3,741,358,870.97 likiwamo deni la adhabu lililotokana na ucheleweshaji wa uwasilishaji wa michango ya Sh.2,730,509,964.73. Mbali na hilo, nimebaini kuwa UWT (CCM) uliingia mkataba na mwekezaji Manji Holdings Limited wa kukodisha ardhi kwa ajili ya uendelezaji wa jengo (kwa sasa ZANRAN TOWER). Hata hivyo,

hakukuwa na mkataba mpya kwa ajili ya kukodisha jengo na kusababisha hasara ya kiasi cha Sh.230,000,000 pamoja na Ada ya ucheleweshaji wa malipo ya 10% kwa mwaka ambayo ingelea ongezeko la DK. 10,000 kwa miaka mitano (sawa na Sh.23,000,000). Kwa nyongeza, nimebaini kuwa, hapakuwa na msingi wa wazi wa kukokotoa kodi ya upangishaji iliyooneshwa kwenye makubaliano. Kwa hiyo, kodi ya mwaka ya upangishaji haikuweza kuthibitishwa wakati wa Ukaguzi. Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwapo kwa tatizo la uendelevu wa biashara (Going concern) katika Kampuni ya Uchapishaji ya Uhuru inayomilikiwa na CCM. Pia, Hati za Ardhi za nyumba 199 zinazomilikiwa na CCM Zanzibar zilionekana hazijasajiliwa kwa jina la Bodi ya Wadhamini; badala yake, nimebaini zimesajiliwa kwa majina ya Maafisa wa chama. Pia, nilibaini kuwa CCM kilishindwa kukusanya Sh.1,457,173,050 hadi Juni, 2018. Kwa upande mwingine, nimebaini kuwapo kwa manunuzi ya gharama za uchapichaji yanayofikia Sh. 524,777,538 yaliyofanywa na Kampuni ya Uchapishaji ya Uhuru bila kufuata taratibu za manunuzi.

Ukaguzi wangu pia umebaini kuwa, Vyama vitano (5) yaani CCM, UDP, UPDP, CKK na ADA-TADEA havitunzi Rejista ya maelezo ya mali. Zaidi, nimebaini vyama saba (7) vimefanya matumizi ya Sh.777,910,739.72 bila kuwa na nyaraka toshelezi. Hivyo, nilishindwa kuthibitisha kama malipo hayo yalikuwa halali na kama yalikusiana na shughuli za Vyama vya siasa. Zaidi, nimebaini kuwa CCM, CHADEMA na ACT Wazalendo havikudai na kutunza risiti za kielektroniki kwa kiwango kinachofikia Sh.85,186,705. Nimebaini kuwa kulikuwa na mikutano michache ya Bodi ya Wadhamini ya Chama cha ACT Wazalendo; na hakuna mikutano yoyote iliyoanywa na Chama cha CCK tangu kuanzishwa kwake. Pia, nimebaini kuwa SAU hakijateua Bodi ya Wadhamini. Vilevile, taarifa za fedha kutoka SAU, UPDP, UMD, ADA-TADEA, NLD na AAFP zilikuwa haziendani na mwongozo wa mfumo dhanifu wa Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu za Umma. Kadhalika, bakaa la madeni yanayofikia Sh.85,366,000 yaliyoelezwa kwenye Taarifa za Fedha za NCCR Mageuzi hayakuwa na nyaraka za kuyathibitisha. Kwa maelezo zaidi, rejea Sura ya 12.

Mapendekezo ya jumla

Napendekeza uongozi wa Vyama vya siasa kuhakikisha kuwa, udhibiti unaanzishwa na kuimarishwa, hasa kwenye malipo ili malipo yote yawe na vielelezo na nyaraka toshelezi, zikiwamo risiti za kielektroniki. Aidha viboreshe utunzaji wa nyaraka kwa muda unaotakiwa kama ilivyoelezwa kwenye Kanuni za fedha za Vyama husika. Licha ya hiyo, mfumo wa uandaaji wa taarifa za fedha unaotumika unapaswa kuzingatiwa na kutumiwa katika namna hiyohiyo ili taarifa zote za fedha ziandaliwe zikiwa na maelezo ya kina. Pia, nahimiza mawasilisho ya michango ya kisheria yafanyike kwa wakati na ufuatiliaji wa washitiri na malipo ya madeni yafanyike ndani ya muda husika.

Sura ya Kwanza

Maelezo ya Awali

1.1 Mamlaka

Ripoti hii Kuu ya Mwaka inajumuisha hoja za ukaguzi na mapendekezo niliyotoa kwenye kaguzi za Taarifa za Fedha za Taasisi zilizoko chini ya Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2018, ikiwa ni kwa mujibu wa Ibara 143 (2) & (4) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (ilivyorekebisha 2005) na Kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, 2008. Pia imejumuisha matokeo ya ukaguzi wa awali wa malipo ya mafao ya kustaafu na ukaguzi maalum uliofanywa katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Kama mkuu wa Taasisi ya Juu ya Ukaguzi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninayakubali majukumu yangu, kazi na mamlaka kama ilivyoelezwa katika Katiba, Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya 2008 na Sheria ya Fedha za Umma ya 2001 (kama ilivyorekebisha 2004) kwa kuhakikisha kuwa, ubora wa juu wa ripoti za ukaguzi unazingatiwa ili kuwezesha Serikali na Taasisi za Serikali kuwajibika kwa umma.

1.2 Malengo na Mawanda ya Ukaguzi

Ukaguzi ulifanyika hasa kwa lengo la kutoa uhakika wa kutosha wa kutokuwapo kwa upotoshaji (makosa/utoaji/udanganyifu) katika taarifa za fedha na kama zimeandaliwa kuendana na Viwango vya Kimataifa vya uandaaji wa taarifa za fedha kwa msingi usiotumia fedha taslimu (IPSAS accrual basis). Pia lengo lingine ni kuchunguza ikiwa sheria na kanuni zinazohusika zimezingatiwa na ikiwa Maafisa Masuuli wameunda na kutekeleza udhibiti makini wa ndani ambao unaweza kuzuia na kubaini makosa pale tu yatakapojitokeza.

Ukaguzi ulifanyika kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguzi (ISSAIs). Viwango hivi vinahitaji wakaguzi kuzingatia mahitaji ya kimaadili, mipango ya ukaguzi, kukagua na kutoa ripoti juu ya matokeo ya ukaguzi. Katika mwaka huu wa fedha, taarifa za fedha 255 kati ya 266 ziliwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi kama inavyotakiwa na Kifungu cha 25 (2) cha Sheria ya Fedha za Umma ya

mwaka 2001 na Kanuni ya 71 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009. Taarifa zote za fedha zilizowasilishwa zilikaguliwa na kuunda msingi wa ripoti ya ukaguzi. Uchambuzi wa kina wa taasisi zilizokaguliwa ikilinganishwa na taasisi zilizotakiwa kukaguliwa ni kama ilivyoonyeshwa kwenye Jedwali hapo chini;

Jedwali Na. 1: Uchambuzi wa Ukaguzi wa Serikali Kuu na Taasisi zake

Na	Taasisi	Taasisi zilizotakiwa Kukaguliwa	Taasisi zilizokaguliwa	Tofauti
1	Fungu ndani ya Wizara	66	65	1
2	Wakala	37	33	4
3	Balozi/Misheni	41	41	0
4	Sekretarieti za Mikoa	26	26	0
5	Mifuko	17	16	1
6	Vyama vya Siasa	19	14	5
7	Bodi za Mabonde ya Maji	9	9	0
8	Mamlaka za Maji Safi na Maji Taka	5	5	0
9	Taasisi Nyingine	42	42	0
10	Taarifa ya Fedha ya Pamoja & Mfuko Mkuu wa Hazina	2	2	0
11	Mamlaka ya Mapato-Mapato & Matumizi	2	2	0
Jumla		266	255	11

Kutokana na Jedwali la hapo juu, inaonekana kwamba idadi ya taasisi zilizokaguliwa ni tofauti na idadi halisi ya taasisi zilizopo. Hii ni kutokana na sababu zifuatazo;

- a) Ukaguzi wa Tume ya UNESCO (Fungu Na. 18) ulikuwa unaendelea kipindi taarifa hii inaandaliwa. Hivyo basi, matokeo ya ukaguzi huo yataoneshwa katika taarifa ya mwaka ujao wa fedha.
- b) Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) na Wakala wa Usimamizi wa Maendeleo ya Elimu (ADEM) kaguzi zake zilikuwa bado zinaendelea kipindi cha kuandaa taarifa hii. Matokeo ya ukaguzi yataonyeshwa kwenye taarifa ya mwaka ujao. Shughuli

za Wakala wa Maendeleo ya Kigamboni (KDA) zimesitishwa kwa kipindi huku Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (TMAA) shughuli zake zilifungwa tangu 7 Julai 2017. Hii inasababisha Taasisi tajwa kutojumuishwa kwenye taarifa hii.

- c) Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ukaguzi wake ulikuwa haujaanza wakati wa kuandaa taarifa hii kutokana na ukosefu wa fedha.
- d) Kati ya Vyama vya Siasa vitano (5), vinne (4) havikuwasilisha taarifa za kifedha kwa ukaguzi, wakati Chama cha Wananchi (CUF) hakikuwasilisha taarifa ya fedha kwa sababu ya migogoro yake ya ndani ambayo bado haijaweza kutatuliwa.

Taarifa za kifedha zilizotakiwa kuwasilishwa kwa ukaguzi zimeongezeka hadi 266 kutoka 255 za mwaka uliopita. Hii ni kutokana na kuanzishwa na kutambuliwa kwa taasisi mpya kama ilivyobainishwa kwenye jedwali lifuatalo:

Jedwali Na. 2: Taasisi mpya zilizotambulika

Na	Jina la Taasisi	Kipengele
1	Tume ya Taifa ya Mipango na Matumizi Bora ya Ardhi	Fungu Na. 3
2	Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji	Fungu Na 60
3	Wizara ya Uvuvi na Mifugo (Sekta ya Uvuvi)	Fungu Na. 64
4	Mfuko Mkuu wa Hazina	Mfuko
5	Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini	Wakala
6	Ubalozi wa Tanzania Seoul - Korea	Ubalozi
7	Mamlaka ya Maji safi na taka Maswa	NWSSA
8	Mfuko wa Barabara OR-TAMISEMI	Mfuko
9	Taasisi ya Mafunzo ya Misititu	Taasisi Nyingine
10	Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu	Taasisi Nyingine
11	Bodi ya Usajili wa Maafisa Mipango Miji	Taasisi Nyingine
12	Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki - Idara ya Zanzibar (SV 1003)	Taasisi Nyingine

Chombo cha Kusimamia Ufuatiliaji wa utekelezaji wa programu na Miradi ya Maendeleo kwenye Maendelo ya Kimkakati ya Kitaifa

(Presidential Delivery Bureau) shughuli zake zimesitishwa mwaka huu; hivyo kusababisa kutoingia kwenye taarifa hii.

Ingawa tumeweza kufanya ukaguzi kama sheria inavyotutaka kwenye taasisi zilizoandaa taarifa za fedha, kulikuwa na changamoto kwenye mawanda ya ukaguzi kutokana na upungufu wa fedha. Changamoto kubwa tuliyoipata ni kwenye kaguzi za shughuli za Serikali kuu mikoani. Timu za ukaguzi ziliweza kutembelea mikoa mitatu (3) kati ya ishirini na sita (26) ambapo, kwa maoni yangu, ni kiwango kidogo tofauti na uhalisia.

Katika ngazi ya taasisi mojawoja, ukaguzi ulihusisha uchambuzi wa taarifa za fedha ambapo maoni ya ukaguzi yakatolewa. Pia ulihusisha vipengele vifuatavyo: tathmini ya mfumo wa udhibiti wa ndani, ukaguzi wa utekelezaji wa mapendekezo ya miaka ya iliyopita, usimamizi wa manunuzi na mikataba, usimamizi wa rasilimali watu na mshahara, matayarisho ya bajeti na utekelezaji, usimamizi wa malipo, mali na madeni, pamoja na usimamizi wa mapato na utendaji kazi wa Wakala.

Mbali na ukaguzi wa taarifa za kifedha, ripoti hii ina matokeo ya awali ya uhakiki wa pensheni za wastaafu; ambapo, mafaili 3,437 ya pensheni yaliwasilishwa kwa ukaguzi, huku mafaili 2,868 yalikaguliwa. Kati ya hayo, mafaili 2,814 yalipitishwa kwa ajili ya malipo.

Pia, taarifa hii ina matokeo ya ukaguzi maalumu wa taasisi 7 uliofanywa kwenye mwaka huu wa fedha. Hii ni kama walivyoomba wadau mbalimbali na ilivyoonyeshwa katika jedwali hapo chini. Matokeo ya kina ya ukaguzi maalum yameelezwa kwa kwenye Sura ya kumi na mbili ya ripoti hii.

Jedwali Na. 3: Idadi ya Kaguzi Maalumu zilizofanyika

Na.	Maelezo	Maombi Kutoka
1	Madai ya Udanganyifu wakati wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Songwe Mbeya na Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania	Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa
2	Ununuzi wa Sare na Vifaa vya Jeshi la Polisi la Tanzania	Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa

Na.	Maelezo	Maombi Kutoka
3	Ununuzi wa magari 777 'Ashok Leyland' uliofanywa na Jeshi la Polisi la Tanzania	Katibu Mkuu, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.
4	Manunuzi ya Mfumo wa Utambuzi wa Alama za Vidole (AFIS) yaliyofanywa na Jeshi la Polisi	Waziri Mkuu
5	Usimamizi wa masurufu katika Wizara ya; Kilimo (Fungu Na.43), Elimu (Fungu Na.46), Afya (Fungu Na.52) na Ujenzi (Fungu Na.98)	Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu
6	Ununuzi wa Mfumo wa Kidigitali wa Kuandikisha Wapiga Kura (BVR) uliofanywa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi	Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa
7	Madai ya Matumizi Mabaya ya Fedha za ulipaji wa mkopo kutoka kwenye Mfuko wa Rais wa Dhamana	Katibu Mkuu Kiongozi

Wakati wa ukaguzi, tulielekeza juhudi zetu kwenye kutumia njia za ukaguzi na kutetea maadili yetu ya msingi ili kuhakikisha kuwa ukaguzi wa ufanisi unafanyika. Tulihakikisha mawasiliano bora na menejimenti za wakaguliwa katika kipindi chote cha ukaguzi na bila kuacha misingi ya uhuru wa ukaguzi. Kama wakaguzi wa sekta ya umma, tumejitolea kwa taaluma yetu ili kudumisha uaminifu kwa umma katika kazi zetu na kutoa ripoti inayoaminika na inayoendelea kuimarisha uwajibikaji, uwazi na ukweli katika usimamizi wa rasilimali za umma.

Sura ya Pili

Hati za Ukaguzi

2.1 Utangulizi

Lengo la kufanya ukaguzi wa taarifa za fedha ni kuwaaminisha watumiaji wa taarifa hizo kama zimeandaliwa kwa usahihi. Uaminifu huo hutolewa kwa njia ya maoni ya ukaguzi kwenye ripoti kama taarifa za fedha zilizoandaliwa kwa ujumla wake zinatoa picha halisi ya utendaji wa taasisi husika, yaani hazina makosa au ubadhirifu mkubwa.

Hata hivyo, katika ukaguzi wa sekta ya umma, lengo la ukaguzi ni pana zaidi ya kutoa maoni kwenye taarifa za fedha, kwani huenda zaidi na kuripoti juu ya uzingatiaji wa sheria na kanuni mbalimbali pamoja na ufanisi wa mfumo wa udhibiti wa ndani ambao kwa pamoja inaitwa ukaguzi wa kawaida wa taarifa za fedha kulingana na kifungu cha 26 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008.

Kwa kuzingatia matakwa haya ya kisheria, jukumu langu lilikuwa ni kukagua taarifa za fedha ili kutambua hali halisi ya mali na madeni, utendaji wa fedha, mtiririko wa fedha na uzingatiaji wa sheria na kanuni zinazohusiana na usimamizi wa fedha.

Kwa kuzingatia umuhimu wa taarifa za fedha ambao unawezesha kuwepo kwa uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali fedha ukaguzi wangu umefanyika kwa umakini mkubwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi katika Sekta Umma ili kuhakikisha kuwa maoni ya ukaguzi yanayotolewa yanaendana na mazingira halisi ya utendaji wa taasisi husika na hivyo kuwaongeza hari watumiaji wa taarifa hizo ya kuziamini taarifa za fedha.

Katika kutoa maoni ya ukaguzi, taarifa za fedha na nyaraka zake zilitathiminiwa dhidi ya Viwango vya Kimataifa vya uandaaji wa taarifa za fedha (Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Taarifa za Fedha katika sekta ya Umma kwa msingi usio taslimu.

2.2 Maoni ya Ukaguzi yaliyotolewa kwa mwaka huu ikilinganishwa na maoni ya miaka ya nyuma (bila kuhusisha Vyama vya Siasa)

Kwa mwaka huu wa fedha Taarifa za fedha 255 kati ya 266 ziliwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi vikiwamo vyama 14 vya siasa. Ukiondoa vyama vya siasa, Taarifa za fedha zilipaswa kuandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu za Umma kwa msingi usio wa fedha taslimu. Hata hivyo, hapakuwa na mwongozo wowote kutoka Serikalini juu ya Uandaaji wa taarifa za fedha za vyama vya siasa. Kukosekana kwa mwongozo huo kumepelekea kila chama kutumia mwongozo wake katika kuandaa taarifa zake za fedha. Kwa maana hiyo, maoni ya ukaguzi wa vyama vya siasa yametenganishwa na maoni ya taarifa nyingine za fedha ambazo zinazotumia mwongozo unaofanana wa uandaaji wa hesabu.

2.2.1 Hati inayoridhisha (Hati safi) (bila kuhusisha vyama vya siasa)

Katika mwaka 2017/2018, kati ya taarifa za fedha 241 zilizokaguliwa ukiondoa vyama vya siasa¹, 234 (97%) zilipata hati inayoridhisha ikiwa na maana kuwa taarifa za fedha hazikuwa na makosa au ubadhilifu, na zimeandaliwa kwa kuzingatia mfumo wa uandaaji wa taarifa hizo. Hili ni ongezeko la asilimia 15 ikilinganishwa na taarifa 204 (88%) za mwaka uliopita kati ya 231 ambazo zilikaguliwa. Kama inavyoonesha idadi ya taarifa ya fedha zilizokaguliwa zimekuwa zikitofautiana mwaka hadi mwaka ambapo taarifa 217 zilikaguliwa kwa mwaka 2015/16, 231 mwaka 2016/17 na 241 zilikaguliwa kwa mwaka 2017/18. Tofauti hii inatokana na uanzishwaji wa taasisi mpya, kufungwa kwa taasisi na kutoandaa na kutowasilisha taarifa za fedha kwa baadhi ya taasisi. Taasisi 11 kati ya 12 zilizoanzishwa na kukaguliwa kwa mara ya kwanza mwaka huu zilipata hati inayoridhisha. Hii inaonesha ni mwanzo mzuri, na ni msingi imara wa uandaaji wa taarifa za fedha kwa kipindi kijacho. Aidha, kati ya taarifa za fedha 234 zilizopata hati inayoridhisha, taarifa 164 (70%) ziliweza kuendelea kuwa na hati safi kwa kipindi cha miaka mitatu

¹ Hati za ukaguzi za vyama vya siasa zimeripotiwa kwenye aya 2.3 hapa chini.

mfululizo, wakati taarifa za fedha 197 (84%) ziliendeleza kuwa na hati safi kwa mwaka huu na mwaka jana. Hii inaonesha kuna maboresho katika usimamizi na uwajibikaji wa fedha za umma. Mchanganuo wa taarifa za fedha zilizopata hati inayoridhisha upo katika Kiambatisho Na. 1

Pia kati ya taarifa za fedha 234 zilizopata hati safi, taarifa 16 zilikuwa na masuala ya msisitizo kwenye maeneo ambayo ni muhimu kwa watumiaji wa taarifa hizo kuyajua. Masuala hayo ya msisitizo hayakuathiri hati zilizotolewa,

2.2.2 Hati yenye shaka (bila kujumuisha Vyama Vya Siasa)

Taarifa za fedha zilizokaguliwa za Taasisi sita (6) zimepewa hati yenye shaka. Aina hii ya hati hutolewa pale mkaguzi anapobaini kuwa taarifa za fedha zinamakosa makubwa kwenye baadhi ya maeneo ya taarifa hizo lakini taarifa hizo kwa ujumla wake hazina makosa. Hii inamaanisha kuwa, kuna kikwazo au kutokubaliana kwenye eneo fulani lakini sehemu nyingine za taarifa za fedha zinaonesha ukweli na uhalisia kulingana na viwango vya Kimataifa vilivyotumika kuandaa Taarifa hizo za fedha. Ikilinganishwa na mwaka wa fedha uliopita ambapo taarifa za fedha za Taasisi 19 zilipata hati yenye shaka, katika mwaka huu wa fedha inaonesha kuna upungufu wa Taasisi 13. Hii inamaanisha kuwa Taasisi zinaimarika katika kuandaa kwa usahihi taarifa za fedha. Mienendo ya miaka mitatu ya Taasisi zilizopata hati yenye shaka ni kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini:-

Jedwali Na. 4: Orodha ya Taasisi zenye Hati yenye Shaka

Na	Taasisi	Aina	2017/18	2016/17	2015/16
1	Tume ya Huduma za Walimu	Fungu Na. 2	Hati yenye shaka	Hati Inayoridhisha	Haikuwepo
2	Chuo cha Sanaa Bagamoyo	Wakala	Hati yenye shaka	Hati Inayoridhisha	Hati Inayoridhisha
3	Ubalozzi wa Tanzania-Lusaka	Kifungu kidogo Na. 2007	Hati yenye shaka	Hati Inayoridhisha	Hati Inayoridhisha
4	Idara ya Deni la Taifa na Huduma za Jumla	Fungu Na. 22	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati Inayoridhisha
5	Idara ya Huduma za Uhamiaji	Fungu Na. 93	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati Inayoridhisha
6	Tume ya Taifa ya mpango wa Utumiaji Bora wa Ardhi	Fungu Na. 3	Hati yenye shaka	Haikuwepo	Haikuwepo
7	Hesabu Jumuiifu za Taifa		Hati yenye shaka	Hati isiyoridhisha	Hati isiyoridhisha

chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Taasisi husika

Vigezo vilivyotumika kutoa hati yenye shaka vimeoneshwa katika Kiambatisho Na. 2

2.2.3 Hati isiyoridhisha (ukiacha Vyama vya Siasa)

Hapakuwa na hati isiyoridhisha kwa ukaguzi wa mwaka huu, Hii ina maanisha kuwa, taratibu za ukaguzi zilizotumika hazikubaini mapungufu ya kiasi kikubwa na yanayojirudia (kutokukubaliana) yanayoathiri taarifa za fedha na kusababisha kukosa uhalisia kwa msomaji.

2.2.4 Hati Mbaya (ukiacha Vyama vya Siasa)

Hapakuwa na hati mbaya kwenye ukaguzi wa mwaka huu. Hati mbaya hutolewa pale ambapo kuna kikwazo kwenye ukaguzi na mkaguzi ameshindwa kupata ushahidi sahihi na wa kutosha wa kiasi kilichoripotiwa kwenye taarifa ya fedha.

Matokeo ya kaguzi kwa ujumla kwa mwaka 2017/2018 yameonyeshwa kwenye Jedwali la hapo chini ikilinganishwa na kaguzi za miaka iliopita.

Jedwali Na. 5: Mchanganuo wa Hati za Ukaguzi zilizotolewa kwa mwaka 2017/18

	Hati inayoridhisha			Hati inayoridhisha ikiwa na kipengele cha msisitizo			Hati yenye shaka			Hati isiyoridhisha			Hati mbaya		
	2018	2017	2016	2018	2017	2016	2018	2017	2016	2018	2017	2016	2018	2017	2016
Mwaka wa Fedha marungu ya	53	52	46	8	6	11	4	6	9	0	1	1	0	0	1
Wakala	31	27	24	1	2	7	1	3	2	0	1	0	0	0	0
Ubalazi	40	32	28	0	1	5	1	2	1	0	0	0	0	0	0
Tawala za Mkoa	25	23	14	1	2	6	0	1	0	0	0	1	0	0	0
Bodi na Mamlaka za Maji	14	9	12	0	0	0	0	4	0	0	0	0	0	0	0
Mfuko	15	14	11	2	3	1	0	0	0	0	0	0	0	0	0
Taasisi Nyingine	40	31	22	4	2	3	0	3	12	0	2	1	1	0	0
Jumla	218	188	157	16	16	33	6	22	24	0	4	3	1	7	5

2.3 Hati za Ukaguzi Zilizotolewa Kwenye Vyama vya Siasa.

Kumekuwa na mpishano wa uandaaji na uwasilishaji wa Taarifa za Fedha za Vyama vya Siasa kwa ajili ya Ukaguzi. Kwa mfano, kati ya

Vyama vya Siasa 19 vyenye usajili wa kudumu, vyama 14 pekee ndivyo vilivyoandaa na kuwasilisha Taarifa za Fedha kwa ajili ya Ukaguzi kwa mwaka huu wa fedha ikilinganisha na vyama 10 vilivyokaguliwa mwaka uliopita, 2016/17.

Kati ya vyama vya Siasa 10 vilivyowasilisha Taarifa za Fedha mwaka uliopita, vyama vitatu (3)² havikuwasilisha Taarifa za Fedha mwaka huu. Kwa upande mwingine, vyama vitatu (3)³ vya siasa ambavyo havikuwahi kukaguliwa miaka ya nyuma lakini vimekaguliwa mwaka huu havikuandaa Taarifa za Fedha kwa miaka hiyo ya nyuma isipokuwa kwa vyama vinne (4)⁴

Kwa sababu ya mpishano huo, imekuwa vigumu sana kuandaa mwenendo ili kubainisha kama kuna maboresho ya maandalizi ya taarifa za fedha au la. Pia, kuwasilisha taarifa za fedha za miaka ya nyuma pamoja na za mwaka huu kumeongeza mzigo wa ziada katika kufanya ukaguzi wa miamala ya miaka miwili au mitatu.

Mpishano huo unahitaji hatua za haraka kutoka Serikalini (Msajili wa Vyama vya Siasa) kuhakikisha kuwa, vyama vya siasa vilivyosajiliwa vinaandaa na kuwasilisha taarifa za fedha kama inavyotakiwa kisheria.

Kwa ujumla, vyama vya siasa vimeendelea kufanya vibaya katika maandalizi ya taarifa za fedha ambapo kati ya vyama 14 vilivyokaguliwa mwaka huu wa fedha, ni vyama vitatu (3) tu vimepata Hati inayoridhisha (safi), ikiwa ni idadi sawa na mwaka uliopita. Vyama vinne (4) vimepata hati yenye shaka, hii ni sawa na mwaka uliopita. Vyama vitano (5) vimepata hati mbaya; wakati vyama viwili (2) zimepata Hati isiyoridhisha. Hati mbaya na hati isiyoridhisha ni hati chafu ambazo zinaonesha kuwa taarifa za fedha zilizoandaliwa haziwezi kutumiwa kwa ajili ya kufanya maamuzi mbalimbali kwani zinakuwa sio sahihi.

Matokeo mabaya ya vyama vya siasa kwa kiasi kikubwa yalisababishwa na ukosefu wa mwongozo kwa vyama vya siasa wa wa uandaaji wa

²ADC, TLP na Demokrasia Makini

³ ADA, TADEA, NRA na UMD

⁴ CHAUMA, UDP, ACT Wazalendo na NCCR Mageuzi

taarifa zao za fedha na ukosefu wa wataalamu wa uhasibu ndani ya muundo wa vyama vya siasa. Pia ilitokana na uhifadhi mbaya wa kumbukumbu za uhasibu na ukosefu wa ushahidi wa hesabu ili kukubaliana na kiasi kilichoripotiwa kwenye taarifa zao za fedha.

Hii pia inahitaji hatua za haraka kutoka Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ili kuhakikisha kuwa, vyama vya siasa vinaongozwa ipasavyo kwenye uandaaji wa taarifa zao za fedha na uhifadhi wa nyaraka za uhasibu na ushahidi.

Mchanganuo wa kina wa hati za ukaguzi za vyama vya siasa ni kama ilivyooneshwa katika jedwali hapa chini.

Jedwali Na. 6: Jwenendo wa Hati za Ukaguzi Kwa Mfululizo wa Miaka Mitatu

Na	Jina la chama cha siasa	2017/18	2016/17	2015/16
1	United Democratic Party	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hakikukaguliwa
2	Chama cha Mapinduzi (CCM)	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka
3	Democratic Party (DP)	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati mbaya
4	CHADEMA	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka
5	ACT-Wazalendo	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
6	NCCR-Mageuzi	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka	Hati yenye shaka
7	Chama cha Kijamii (CCK)	Hati yenye shaka	Hati mbaya	Hati mbaya
8	ADA-TADEA	Hati mbaya	Hakikukaguliwa	Hakikukaguliwa
9	National Reconstruction Alliance (NRA)	Hati mbaya	Hakikukaguliwa	Hakikukaguliwa
10	Union for Multiparty Democracy (UMD)	Hati mbaya	Hakikukaguliwa	Hakikukaguliwa
11	Alliance for Africa Farmers Party	Hati mbaya	Hati mbaya	Hati mbaya
12	Sauti ya Umma (SAU)	Hati mbaya	Hati mbaya	Hati mbaya
13	Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA)	Hati isiyoridhisha	Hati inayoridhisha	Hakikukaguliwa
14	National League for Democracy	Hati isiyoridhisha	Hati mbaya	Hati ya mbaya

Msingi wa Hati yenye shaka, Hati isiyoridhisha na Hati mbaya kuhusiana na taarifa hizi za fedha zimejumuishwa kwenye Kiambatisho Na. 3, Kiambatisho Na. 4 na Kiambatisho Na. 5 mtawalia.

Sura ya Tatu

Hali halisi ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi na Maagizo ya Kamati ya PAC

3.1 Utangulizi

Sura hii inatoa hali ya utekelezaji wa hatua zilizoridhiwa na Menejimenti za Taasisi nilizozikagua ili kuhakikisha kuwa mapendekezo ya ukaguzi niliyoyatoa pamoja na maagizo ya Kamati ya PAC yanatekelezwa kwa ufasaha na kwa wakati muafaka, ili hatua hizo zilizochukuliwa ziondoe mianya ya ubadhirifu iliyoibuliwa kwenye hoja za kaguzi zilizopita.

Kifungu Na. 40 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 (Iliyorekebisha mwaka 2013) kinanitaka kujumuisha katika ripoti yangu ya mwaka hali ya utekelezaji wa Mpangokazi wa utekelezaji wa mapendekezo yangu ulioandaliwa na Maafisa Masuuli na kufanyiwa majumuisho na Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuandaa ripoti ya pamoja. Ili kukidhi matakwa ya Sheria hiyo, sura hii inaeleza hali na hatua za utekelezaji wa mapendekezo yangu na Maagizo yaliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali (PAC)

Ili mapendekezo niliyoyatoa pamoja na maelekezo ya Kamati ya PAC yalete tija, ni muhimu kuhakikisha kwamba mapendekezo na maagizo hayo yanatiliwa maanani na yanatekelezwa ili yatoe matokeo yaliyotarajiwa.

Utekelezaji wa mapendekezo ya CAG na maagizo ya Kamati ya PAC huonesha dhamira ya wakaguliwa na Serikali kwa ujumla katika kuimarisha uwazi, uwajibikaji, utawala bora, uangalizi na kuhamasisha usimamizi bora wa fedha na rasilimali katika ngazi zote. Kwa hiyo, kutotekeleza au kuchelewa kutekeleza mapandeko ya ukaguzi na maagizo ya Kamati ya PAC kunaweza kusababisha mapungufu katika usimamizi wa mapato, matumizi na mali za Serikali. Hatimaye kusababisha kutoaminika kwa uthabiti wa mifumo na taratibu za fedha.

Kwa ujumla, hali ya utekelezaji wa mapendekezo yangu katika mwaka huu wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2018 si wa kuridhisha

ikilinganishwa na mwaka uliopita. Hii ni kutokana na kiwango kisichoridhisha cha Maafisa Masuuli na menejimenti za Wizara, Idara na Wakala wa Serikali husika kushughulikia utekelezaji wa mapendekezo yangu. Hali ya kina ya utekelezaji wa mapendekezo yangu inaelezewa kwa kina katika sura hii.

Vigezo vyetu vilivyotumika kutathmini hali ya utekelezaji vimeoneshwa kwenye la hapo chini:

Jedwali Na. 7: Maana ya maneno yaliyotumika kutathmini hali ya utekelezaji

Misamiati iliyotumika kutathmini	Maana ya Maneno
Yaliyotekelezwa	Mapendekezo na Maagizo yametekelezwa kikamilifu na Mkaguliwa ama, kama ilivyoelezwa kwenye taarifa au
Yaliyo katika utekelezaji	Mkaguliwa ana mipango mahususi ya kuanza nayo au ameshaanza kutekeleza na amedhamiria kutekeleza pendekezo kikamilifu au ametekeleleza sehemu ya pendekezo na maagizo.
Yasiyotekelezwa	Mkaguliwa hajatekeleza pendekezo, na inaonesha hatafanya hivyo.
Yaliyopitwa na wakati	Mkaguliwa amejitahidi kwa kiasi kikubwa kwamba mapungufu ya nyuma hayatokei tena katika mwaka (miaka) ujao (ijayo) au mapendekezo na maagizo siyo ya muhimu tena kutekelezwa au utekelezaji wake hauwezekani au siyo muhimu kwa sababu ya mabadiliko ya sheria, vipaumbele vya Serikali, maagizo na miongozo.

Chanzo: Taarifa Jumuifu ya CAG

3.2 Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa CAG wa miaka iliyopita

3.2.1 Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa CAG wa miaka iliyopita kwa kila Mkaguliwa wa Serikali Kuu


Katika mwaka huu wa ukaguzi, ripoti yangu ya ukaguzi inaonesha kuwa, katika miaka iliyopita nilitoa jumla ya mapendekezo 3,843 juu ya hoja yanayowataka Menejimenti za Taasisi kuchukua hatua muhimu za marekebisho na maboresho (Tazama Jedwali hapo chini)

Hata hivyo, kati ya jumla ya mapendekezo 4,282, uwiano wa kiwango cha mapendekezo yangu ya miaka ya nyuma kwa Taasisi za Serikali

Kuu unaoneshwa kwenye **kielelezo Na. 1**, kuwa Mafungu yalikuwa 23%, Sekretarieti za Mikoa (20%), Taasisi Nyingine (18%), Balozi (14%), Wakala (11%), Vyama vya Siasa (7%), Taasisi za Mabonde ya Maji na Ugavi wa Maji Taifa (4%) na Mifuko ya Fedha (4%) ya jumla ya mapendekezo yote ya ukaguzi uliopita.

Katika kufuatilia nimebaini kuwa hali halisi ya utekelezaji wa mapendekezo yangu ambayo, kati ya mapendekezo 4,282; Mapendekezo 1,459 (sawa na asilimia 34) yametokelezwa, 1,626 (sawa na asilimia 38) utekelezaji wake unaendelea, 752 (sawa na asilimia 18) hayajatekelezwa na 445 (sawa na asilimia 10) utekelezaji wake umepitwa na wakati.

Kielelezo Na. 1: Uwiano Utekelezaji wa Mapendekezo ya niliyotoa miaka iliyopita kwa Taasisi kwa Mwaka 2017/18



Chanzo: Taarifa za Mapungufu Kwa Menejimenti za Taasisi Husika kwa Mwaka 2017/18

Ufafanuzi wa kina juu ya utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi umetolewa kwenye Taarifa za Ukaguzi za Taasisi husika: Hata hivyo, muhtasari wa uchambuzi wa jumla kutoka kwenye Taarifa hizo ni kama inavyoonekana katika jedwali hapo chini:


Jedwali Na. 8: Uwiano wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

Hali ya Utekelezaji	Idadi ya Mapendekezo 2016/2017	Asilimia ya Mapendekezo- 2016/2017	Idadi ya Mapendekezo- 2017/18	Asilimi ya Mapendekezo- 2017/2018
Yaliyotekelezwa	1,543	38	1,459	34
Yaliyo katika Utekelezaji	1,454	35	1,626	38
Yasiyotekelezwa	721	18	752	18
Yaliyopitwa na Wakati	390	9	445	10
Jumla ya Mapendekezo	4,108	100	4,282	100

Chanzo: Taarifa za Mapungufu Kwa Menejimenti za Taasisi Husika kwa Mwaka 2017/18

Uwasilisho wa picha ya hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi ya mwaka uliopita unaweza kuonekana kwenye kielelezo hapa chini:

Kielelezo Na. 2: Uwiano wa Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi kwa Taasisi- 2017/2018




Chanzo: Taarifa za Mapungufu Kwa Menejimenti za Taasisi Husika kwa Mwaka 2017/18

3.2.2 Ulinganifu wa hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa niliufanya kati ya mwaka huu na mwaka uliopita

Hali ya utekelezaji katika mwaka huu wa fedha unaoishia tarehe 30/06/2018 si ya kuridhisha ikilinganishwa na mwaka uliopita. Hii inaweza kuwa ni kutokana na ufuatiliaji na usimamizi usioridhisha wa Menejimenti za Taasisi za Serikali katika utekelezaji wa mapendekezo

ya ukaguzi. Angalia Kielelezo Na. 3 na Kielelezo Na. 4 kwa ufafanuzi zaidi.


Kielelezo Na. 3: Jumla ya Mapendekezo ya Ukaguzi kwa 2017/18 ikilinganishwa na 2016/17



Chanzo: Taarifa za Mapungufu kwa Menejimenti za Taasisi Husika

Kielelezo Na. 3 hapo juu kinaonesha kuwa, jumla ya Mapendekezo ya Ukaguzi niliyotoa miaka iliyopita yameongezeka hadi kufikia Mapendekezo 4,282 kutoka Mapendekezo 4,108 ya mwaka uliopita, hii ni sawa na ongezeko la asilimia 4 ya Mapendekezo yanayosubiri utekelezaji kwenye mwaka uliopita. Hii inamaanisha kuwa, kasi ya serikali kutekeleza mapendekezo ya CAG ni ndogo ukilinganisha na idadi ya mapendekezo ya ukaguzi yanayotolewa kila mwaka kusubiri utekelezaji.

Kielelezo Na. 4: Ulinganifu wa hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi kati ya 2016/2017 na 2017/2018



Chanzo: Taarifa za Mapungufu Kwa Menejimenti za Taasisi Husika kwa Mwaka 2017/18

Kielelezo Na. 4 kinaonesha kwamba kiwango cha *utekelezaji uliokamilika* wa mapendekezo kimepungua kwa asilimia 4 kutoka asilimia 38 mwaka jana hadi 34 mwaka huu. *mapendekezo yaliyo katika utekelezaji* na *yaliyopitwa na wakati* yameongezeka kwa asilimia 3 na asilimia 1, mtawalia. *Mapendekezo yasiyotelekezwa* yamesalia kwenye asilimia 18 ya mapendekezo yote kwa mwaka huu na uliopita. Kwa mantiki hiyo, Menejimenti za Taasisi za Serikali Kuu wanashauriwa kuongeza jitihada zaidi za kutekeleza mapendekezo ya ukaguzi.

3.2.3 Hali halisi na uchambuzi wa Maagizo ya Kamati ya PAC kwa Taasisi za Serikali Kuu, Vyama vya Siasa na Bodi za Mabonde ya Maji katika Mwaka wa Fedha 2017/18

Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali ni chombo cha juu kabisa cha usimamizi wa Wizara, Idara na Wakala wa Serikali kwa mujibu wa Kanuni 117(15) ya Kanuni za kudumu za Bunge (toleo la Januari, 2016). Majukumu ya Kamati hii yameelezwa kwa kina chini ya Kanuni 14 na 16 nyongeza ya nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, ambapo Ripoti za CAG huwa nguzo muhimu katika kujenga misingi ya shughuli za Kamati ya PAC.

Kwa sababu ya umuhimu wa kimuundo, utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa yanapaswa kushughulikiwa ipasavyo na Maafisa Masuulii husika. Utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya PAC ni muhimu ili kuhakikisha shughuli zinafanyika kwa utaratibu unaokubalika, kuzingatia maadili, ufanisi, tija, uangalizi na uwajibikaji. Pia, kuhakikisha sheria na kanuni zilizopo zinazingatiwa, rasilimali zinasimamiwa dhidi ya upotevu, matumizi mabaya na uharibifu. Hivyo ni muhimu mambo yote yaliyoibuliwa na Kamati ya PAC yanashughulikiwa vizuri na maagizo yote yanatekelezwa ipasavyo.

Kwa hiyo, ni muhimu sana kuyafanyia kazi masuala yote yaliyoibuliwa na Kamati ya PAC na kuyatekeleza kikamilifu maagizo yote iliyoyatoa. Aidha, ninaendelea kuishukuru Kamati ya PAC na Bunge kwa ujumla kwa ushirikiano wanaonipa kwa kuzitumia ripoti zangu na kusimamia utekelezaji wa mapendekezo ninayoyatoa; hivyo kufanya jukumu nililonalo kikatiba kuwa la umuhimu zaidi.

Ripoti za ukaguzi za Taasisi mojamoya zinaonesha kwamba, katika mwaka wa ukaguzi kulikuwa na jumla ya maelekezo 272 ya Kamati ya PAC yaliyokuwa kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji uliofanywa na Taasisi mbalimbali za Serikali Kuu. Anagalia Jedwali na kielelezo kinachofuata.


Jedwali Na. 9: Melekezo ya Kamati ya PAC kwa Mwaka 2017/18

Hali ya Utekelezaji	2014/15		2015/16		2016/17	
	No	%	No	%	No	%
Yaliyotekelezwa	0	0	1	6	82	30.1
Yaliyo katika Utekelezaji	4	57	10	63	163	59.9
Yasiyotekelezwa	2	29	3	19	19	7.0
Yaliyopitwa na Wakati	1	14	2	12	8	2.9
Jumla ya Mapendekezo	7	100	16	100	272	100

Chanzo: Taarifa za Mapungufu Kwa Menejimenti za Taasisi Husika kwa Mwaka 2017/18

Maelezo ya hapo juu yanaweza kuoneshwa kupitia kielelezo cha hapo chini:

Kielelezo Na. 5: Uwiano wa Idadi ya Maelekezo kwa Taasisi za Serikali Kuu 2017/2018



Chanzo: Uwiano wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Hoja za Ukaguzi kwa Taasisi za Serikali Kuu 2017/18

Uchambuzi wa Kielelezo Na. 5 hapo juu unaonesha kuwa, miongoni mwa maagizo 272 yaliyotolewa na Kamati ya PAC kabla ya mwaka wa fedha 2017/18, sehemu kubwa ya asilimia 62 yalitolewa kwa *Wizara, Idara na Balozji*; ikifuatiwa na *Sekretariet za Mikoa* wana asilimia 23, *Taasisi nyingine* wana asilimia 7, *Wakala* wana asilimia 5, *Mifuko ya Fedha* wana asilimia 3, *Vyama vya Siasa* na *Bodi za Mabonde ya Maji* kwa pamoja wana asilimia sifuri mtawalia.


Licha ya Taasisi za Maji & Bodi za Mabonde ya Maji na Vyama vya Siasa kuwa na uwiano wa asilimia 4 na 7, mtawalia, wa jumla ya mapendekezo ya kaguzi za miaka ya nyuma (tazama kielelezo hapo juu). Hata hivyo, Kamati ya PAC haikuvii Vyama vya Siasa na Taasisi za Maji na Mabonde ili kutathmini ripoti zao za ukaguzi na kuzitolea maagizo ipasavyo. Ni matarajio yangu kwamba wakati ujao hii itarekebishwa. Wakati mkaguzi anapotoa hoja na mapendekezo, iko haja Kamati ya PAC kuhakikisha hatua zinachukuliwa kuyatekeleza mapendekezo husika. Bila kufanya hivyo, mapendekezo ya ukaguzi hayataleta matokeo tarajiwa.

3.2.4 Ulinganifu baina ya mwaka huu na mwaka uliopita wa fedha, juu ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya PAC ya ripoti za ukaguzi binafsi

Ufuatiliaji wetu umebaini kuwa, hali ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya PAC katika mwaka wa fedha 2017/2018 yameboreka; ambapo maagizo yasiyotekelezwa yamepungua hadi asilimia 7 mwaka huu kutoka asilimia 20 mwaka jana. Maagizo ambayo utekelezaji wake unaendelea yameongezeka hadi asilimia 60 kutoka asilimia 39 mwaka jana. Maelekezo yaliyopitwa na wakati yamesalia kwenye asilimia 3; ingawa maagizo yaliyotekelezwa yamepungua hadi asilimia 30 kutoka asilimia 39 mwaka jana kama ilivyoelezwa kwenye Kielelezo Na. 6: Kiwango cha Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya PAC kwa M/F 2017/2018 hapa chini:

Maelezo ya hapo juu yanaweza kuoneshwa kwenye hapo Kielelezo Na. 6 cha chini:

Kielelezo Na. 6: Kiwango cha Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya PAC kwa M/F 2017/2018



Chanzo: Taarifa za Mapungufu Kwa Menejimenti za Taasisi Husika kwa Mwaka 2017/18

Kutokana na Kielelezo Na. 6 cha hapo juu, inawezekana kuhitimishwa kuwa maagizo mengi ya Kamati ya PAC (60%) bado yapo katika ya hatua ya utekelezaji. Hii inaashiria kwamba jitihada nyingi zinatakiwa kuchukuliwa ili kuhakikisha kuwa maagizo yote yasiyokamilika

yanatekelezwa kikamilifu. Vivyo hivyo, maagizo yasiyotekelezwa sawa na asilimia 7 yanapaswa kutekelezwa ili maelekezo ya Kamati ya PAC yalete tija.

3.3 Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa miaka iliyopita kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)

Kif. 40 cha Sheria ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma (Iliyorekebishwa 2013) Kinahitaji Maafisa Masuuli kuandaa mpango kazi wa jinsi gani watatekeleza mapendekezo ya CAG na kuyawasilisha kwa PMG kwa ajili ya kuandaa Ripoti Jumuiifu ambayo itajumuishwa kwenye Ripoti Jumuiifu ya kila mwaka ya CAG. Zaidi ya hayo, Kanuni ya 38 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma inamuhitaji PMG kuwasilisha majibu kwa maandishi ndani ya miezi mitatu tangu tarehe ya kupokea mapendekezo yangu.

Kwa kuzingatia matakwa ya kisheria ya hapo juu, nilipokea majibu ya Serikali kuhusiana na ripoti yangu ya mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2017 kutoka kwa PMG kupitia barua yenye kumbukumbu Na. CHA 114/474/01/81 tarehe 10 Juni, 2018.

Ripoti ya mwaka huu kuishia 30 Juni 2018 ilikuwa na jumla ya mapendekezo ya ukaguzi 100 ya miaka iliyopita. Kati ya hayo, 94 yalikuwa na mapendekezo kabla ya 30 Juni 2017 yaliyohitaji majibu ya Serikali, 6 yalikuwa maagizo ya Kamati ya PAC 6.

Kati ya mapendekezo 91 niliyotoa kwa Serikali, mapendekezo 2 (asilimia 2.2) yalitekelezwa, mapendekezo 17 (asilimia 18.7) utekelezaji wake unaendelea, mapendekezo 4 (asilimia 4.4) hayakutekelezwa; na 68 (asilimia 74.7) yalipitwa na wakati. Hali ya hutekelezaji wa mapendekezo inatolewa kwenye **Jedwali na Kielelezo hapo chini:**

Jedwali Na. 10: Hali Halisi ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi ya Miaka iliyopita kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali

Utekelezaji	2015/2016		2016/2017		2017/2018	
	No.	%	No.	%	No.	%
Yaliyotekelezwa	19	19	14	16.5	2	2.2
Yaliyo katika Utekelezaji	53	52	51	60	17	18.7
Yasiyotekelezwa	20	20	9	10.6	4	4.4
Yaliyopitwa na Wakati	10	9	11	12.9	68	74.7
Total	102	100	85	100	91	100

Chanzo: Taarifa za Mapungufu Kwa Menejimenti za Taasisi Husika kwa Mwaka 2017/18

Jedwali la hapo juu linaweza kuwakilishwa na Kielelezo Na. 7 hapo chini:

Kielelezo Na. 7: Hali ya Utekelezaji wa mapendekezo niliyoyatoa kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali



Chanzo: Taarifa za Mapungufu Kwa Menejimenti za Taasisi Husika kwa Mwaka 2017/18

Kwa ujumla, Jedwali Na. 10 na Kielelezo Na. 7 hapo juu vinaonesha kuwa, utekelezaji wa mapendekezo ya CAG ni wa wastani; ambapo mapendekezo yasiyotekelezwa yalipungua hadi asilimia 4.4 kutoka

asilimia 10.6 mwaka jana. Hata hivyo, mapendekezo ambayo yapo katika ngazi mbalimbali za utekelezaji kwa mwaka huu wa 2017/18 yamepungua mpaka asilimia 17 kutoka asilimia 60.0 mwaka jana.

Vilevile, mapendekezo yaliyotekelezwa kikamilifu yamepungua kutoka asilimia 16.5 mwaka jana hadi asilimia 2.2 mwaka huu. Mapendekezo yaliyopitwa na wakati yaliongezeka hadi asilimia 74.7 kutoka asilimia 12.9. Angalia Kiambatisho Na. 6 na Kiambatisho Na. 7 kwa maelezo zaidi.

Ijapokuwa majibu ya Serikali juu ya mapendekezo ninayoyatoa na mipango kazi yao ya utekelezaji yameimarika, jitihada zaidi zinahitajika ili kuhakikisha utekelezaji kamili wa mapendekezo ambayo utekelezaji wake kwa sehemu umeanza lakini haujakamilika.

Halikadhalika, ili kuhakikisha kuwa mapendekezo ambayo utekelezaji wake uliokwishaanza unakamilika kwa wakati, nashauri PMG na Maafisa Masuuli waweke msisitizo katika kutekeleza mapendekezo niliyoyatoa kwa kuzingatia muda uliopangwa kwenye mpango kazi wa utekelezaji wa kila hoja ya ukaguzi.

Sura ya Nne

Ukaguzi wa Bajeti ya Serikali

4.1 Utangulizi

Makadirio ya Mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/18 ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 - 2020/21) ikiwa na lengo la kuchochea mapinduzi ya Viwanda na Maendeleo ya Watu. Hatua zilizopendekezwa katika bajeti ya 2017/18 zina lengo la kujenga misingi imara ya kiuchumi kwa ajili ya uchumi wa viwanda na kupanua fursa za ajira pamoja na biashara chini ya kauli mbiu: **“Kujenga uchumi wa viwanda utakaochoea ajira na ustawi endelevu wa jamii”** Lengo likiwa ni kusaidia kufikia Dira ya Taifa kufikia uchumi wa kipato cha kati ifikapo 2025⁵.

4.2 Vipaumbele vya Bajeti ya mwaka 2017/18

Bajeti ya mwaka 2017/18 ilijielekeza kutekeleza vipaumbele muhimu vifuatavyo: -

- i) Shughuli za kuendeleza ukuaji wa uchumi na ujenzi wa viwanda ;
- ii) Kufungamanisha uchumi na maendeleo ya watu;
- iii) Kujenga mazingira wezeshi kwa uendeshaji biashara na uwekezaji;
- iv) Kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa Mpango wa ufanisi;

4.3 Muonekano wa Jumla wa Bajeti

Ili kuhakikisha ufanisi katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2017/18 Serikali iliandaa sera na miongozo mbalimbali ili kuongeza ukusanyaji wa mapato na kuhakikisha serikali inafanya matumizi yenye tija.

⁵ Muonekano wa jumla wa bajeti, sera na miongozo ya utekelezaji wa bajeti kama ilivyotolewe kwenye Hotuba ya Bajeti iliyowasilishwa Bungeni Juni, 2017; <http://www.mof.go.tz>

Kati ya miongozo na sera zilizowekwa katika ukusanyaji wa mapato ni; Kufanya marekebisho ya mfumo wa kodi ikiwa ni pamoja na viwango vya kodi, ada na tozo zinazotowazwa chini ya sheria mbalimbali za kodi, Kuendelea kuhimiza matumizi ya vifaa vya kidigitali vya kukusanya mapato (EFDs) , Mfumo wa ukusanyaji mapato (e-RCS) na (GEPGS), Kurasimisha mifumo ya kibiashara isiyo rasmi pamoja na kuanzisha maeneo ya kuhakiki na kuruhusu madini kusafirishwa nje ya nchi katika viwanja vya ndege vya kimataifa, migodini na kwenye maeneo mengine yanayofaa.

Mikakati ya matumizi inahusisha kuweka nidhamu ya matumizi ya fedha za umma, kufuatisha sheria, kanuni na taratibu za fedha pamoja na miongozo. Lengo likiwa ni kupunguza matumizi yasiyo ya lazima kwenye matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo ili kupata thamani ya fedha.

Hatua zilizotekelezwa ni pamoja na kuhakikisha mishahara inalipwa kwa wafanyakazi wanaostahili, kuzuia na kupunguza malimbikizo ya madeni, kuhakikisha taasisi za umma zinajiendesha kwa faida bila kutegemea ruzuku kutoka serikali Kuu, kuendelea kudhibiti gharama/matumizi ya taasisi, Kusisitiza matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika kufanikisha mawasiliano kwenye shughuli za Serikali, pamoja na Kuhakikisha kwamba mikataba yote inayoingwiwa na Serikali na Taasisi zake inakuwa katika shilingi za kitanzania isipokuwa kwa mikataba inayohusisha biashara na huduma za kimataifa ili kujikinga na vihatarishi vya kifedha osipokuwa kwa mikataba yenye miamala ya fedha za kigeni n.k.

Zaidi ya hayo, Bajeti ya serikali ya Tanzania inaandaliwa kwa mfumo wa fedha taslimu katika kipindi kinachoanzia Tarehe 1 Julai hadi Tarehe 30 Juni, hata hivyo mrejesho wa taarifa ya matumizi unaandaliwa kwa mfumo wa viwango vya kimataifa vya uandaji wa hesabu za umma kwa mfumo usio wa fedha taslimu- IPSASs.

Sura hii inatoa mrejesho wa mapendekezo ya Bajeti ya Serikali iliyoidhinishwa na Bunge ikiwa ni makadirio ya mapato kupitia vyanzo mbalimbali, ugawaji na matumizi ya rasilimali fedha kwa shughuli za kawaida na maendeleo ikilinganishwa na makadirio na mwenendo wa

mapato yaliyokusanywa katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2018.

Katika mwaka wa Fedha 2017/18, Serikali ilipanga kukusanya na kutumia kiasi cha Sh. bilioni 31,711.99 ikiwa ni ongezeko la kiasi cha Sh bilioni 2,172.39 sawa na asilimia 7.35 ikilinganishwa na kiasi cha makadirio ya Sh. bilioni 29,539.60 kilichopangwa kwa mwaka wa fedha 2016/17.

Jedwali hapa chini linaonesha makadirio ya makusanyo ya Serikali kwa vyanzo vilivyotambuliwa pamoja na asilimia ya kuchangia bajeti;

Jedwali Na. 11: Mchanganuo wa Bajeti ya Makusanyo

Chanzo cha Mapato	Makadirio katika Sh.	Asilimia ya makadirio kwa kila chanzo
Kodi	17,106.34	53.94
Makusanyo yasiyotokana na Kodi	2,870.67 ⁶	9.05
Mikopo ya Ndani⁷	6,168.90	19.45
Mikopo ya Nje na misaada ya Wahisani⁸	5,566.09	17.55
Jumla Kuu	31,711.99	100.00

Chanzo: Hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango, 2017/18

Kutokana na Hotuba ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/18 kiasi cha Sh. billion 19,712.39 kilitengwa kwa matumizi ya kawaida na Sh. bilioni 11,999.59⁹ kwa matumizi ya maendeleo, hata hivyo kutokana na kibali cha marejeo ya bajeti Na.1 cha 2017/18 iliyopitishwa katika vikao vya Bunge ilipitisha marekenisho ya bajeti Sh. bilioni 20,278.99 kwa matumizi ya kawaida na Sh. bilioni 11,432.99¹⁰ Kwa matumizi ya maendeleo, ikiwa ni ongezeko la asilimia 12.13% kwa bajeti ya matumizi ya kawaida na punguzo la asilimia 0.26% kwa bajeti ya maendeleo ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha uliopita Sh.

⁶ Makusanyo yasiyotokana na Kodi; Sh. bilioni 2,183.36 zitakusanywa na Wizara/Idara na Sh. bilioni 687.31 zitakusanywa na Mamlaka za serikali za Mtaa (LGAs)

⁷ Mikopo ya ndani inajumuisha; Sh. bilioni 1,220.67 na Sh. billioni 4,948.23 mikopo ya ndani inayoendelea “rollover financing”


⁸ Mikopo ya Nje na misaada ya Wahisani inajumuisha; Mikopo na misaada nafuu Sh. bilioni 941.26, Mikopo na misaada nafuu kwa miradi ya maendeleo Sh. bilioni 2,473.77, Misaada na mikopo nafuu ya kiskakta Sh. bilioni 556.08, Mikopo ya nje Sh. bilioni 1,594.99

⁹ Kiasi hichi kimetoholewa kwenye Hotuba ya Waziri wa Fedha ya Mwaka 2017/18

¹⁰ Kiasi hichi kinatokana na marejeo ya Bajeti Kibali Na.1 cha mwaka 2017/18 (Marejeo hayo yamesababisha punguzo la Sh. bilioni 566.6 kwa bajeti ya maendeleo iliyopitishwa awali)

bilioni 18,084.56 matumizi ya kawaida na Sh. bilioni 11,462.28 Matumizi ya maendeleo. Kielelezo kifuatacho kinaonyesha mgawanyo wa bajeti ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo.

Kielelezo Na. 8: Mgawanyo wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo.



4.4 Muhtasari wa makadirio na Makusanyo ya Fedha

Makusanyo halisi yaliyokusanywa kutoka katika vyanzo vinavyotambuliwa yalifikia Sh bilioni 27,695.96 hivyo kushindwa kufikia lengo lililokusudiwa kwa kiasi cha Sh. billioni 4,016 sawa na asilimia 12.66 ya makadirio.

a) Makusanyo Yanayotokana na kodi

Makusanyiko ya kodi yalikuwa Sh. bilioni 15,149.47 sawa na asilimia 89 ya makadirio ya Sh. bilioni 17,106.34 hivyo kutifikisha lengo kwa kiasi cha Sh. bilioni 1,957 sawa na asilimia 11, Ikilinganishwa na makusanyo halisi kutokana na kodi yaliyoripotiwa katika mwaka wa fedha 2016/17, Kumekuwa na ongezeko la Sh. bilioni 878.17 sawa na asilimia 6.15 mwenendo huu wa ongezeko unaonyesha matokeo chanya katika ukusanyaji wa kodi.

b) Makusanyo ya Mapato yasiyotokana na Kodi

Makusanyo yasiyotokana na kodi yalikuwa Sh. bilioni 1,589.87¹¹ sawa na asilimia 55.38 ya makadirio ya Sh. bilioni 2,870.67 hivyo kutofikia lengo kwa kiasi cha Sh. billion 1,280.80 sawa na asilimia 44.62, kumekuwa na makusanyo pungufu ya Sh. billion 483 sawa na asilimia 23.30 ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka wa fedha 2016/17. Upungufu huu unawea kumaanisha kupungua kwa jitihada za ukusanyaji wa mapato yasiyotokana na kodi katika Wizara, Idara, na Sekretarieti za Mkoa.

c) Mikopo ya Ndani

Mikopo ya Ndani yenye lengo la kugharamia bajeti pamoja na mikopo inayoendelea Sh. bilioni 5,704.50, kiasi cha mikopo ya Sh. bilioni 464.40 sawa na asilimia 7.53 hakikupokelewa ikilinganishwa na makadirio yaliyopitishwa na Bunge. Mikopo ya ndani imepungua kwa Sh. bilioni 211.35 sawa na asilimia 3.57 ikilinganishwa na mikopo ya ndani iliyopokelewa na kuripotiwa kwa mwaka wa fedha 2016/17.

d) Misaada

Misaada iliyopokelewa katika mwaka wa Fedha 2017/18 ni kiasi cha Sh. bilioni 1,293.64 sawa na asilimia 88 ikilinganishwa na makadirio yaliyopitishwa na Bunge ya Sh. 1,477.40 billion, hivyo kiasi cha Sh. bilioni 183.77 sawa na asilimia 12 ya makadirio hakikupokelewa.

e) Mikopo nyenye Masharti Nafuu

Mikopo yenye Masharti Nafuu iliyopokelewa kwa mwaka wa fedha 2017/18 ni kiasi cha Sh. bilioni 2,214.15 sawa na asilimia 89 ya makadirio waliyopitishwa na Bunge ya Sh. bilioni 2,493.70 billion. Hivyo kiasi cha Sh. bilioni 279.55 sawa na asilimia 11 ya makadirio hakikupokelewa.

f) Mikopo isiyo na Masharti Nafuu

Mikopo isiyo na Masharti Nafuu iliyopokelewa ni Sh. bilioni 1,744.34 sawa na ongezeko la Sh. billioni 149.34 ikiwa ni sawa na asilimia 9

¹¹ Kiasi hiki kimetolewa kwenye taarifa ya Mfuko mkuu wa Hazina

ikilinganishwa na makadirio yaliyopitishwa na Bunge ya Sh bilioni 1,595.


Kwa ujumla, makusanyo kutoka kwenye Misaada, na Mikopo ya nje yenye mashari nafuu na isiyo na masharti nafuu ni Sh. bilioni 5,252.12 sawa na asilimia 94 ya makadirio yaliyopitishwa na Bunge ya Sh. 5,566.1, Hata hivyo kati ya Sh bilioni 5,252.12 zilizopokelewa, Sh. bilioni 1,557.06 billioni zilipokelewa moja kwa moja kwa watekelezaji wa Miradi ya maendeleo bila kupitia mfuko mkuu wa Hazina.

Ni mapendekezo yangu kwa Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha kwamba usuluhisho wa fedha zote zilizopokelewa na vifungu mbalimbali kutoka Hazina au kutoka kwa wafadhili wa miradi ya maendeleo unafanyika, ili kuwezesha awajibikaji wa fedha zilizotolewa.


Maelezo zaidi kuhusu mikopo ya Ndani na Nje pamoja na misaada ya wahisani imeelezwa katika sura ya tano ya ripoti hii.

Ukizingatia mwenendo wa makadirio ya Bajeti na makusanyo ya kodi, makusanyo yasiyotokana na kodi, Mikopo ya ndani, Mikopo ya Nje, Misaada ya Wahisani na Misaada ya Washirika wa Maendeleo kwa miaka mitato mfululizo imeonyeshwa katika kielelezo hapo chini;


Kielelezo Na. 9: Makadirio ya Bajeti pamoja na Makusanyo kutoka katika vyanzo vilivyotambulika kwa Mwaka wa fedha 2017/18 (Kiasi katika Sh. Bilioni)




Kielelezo Na. 10: Mwenendo wa Makadirio ya Serikali kwa Miaka Mitano (Kiasi katika Sh Bilioni)



Kielelezo Na. 11: Mwenendo wa Makusanyo ya Serikali kwa Miaka Mitano (Kiasi katika Sh Bilioni)



Kielelezo Na. 12: Mwenendo wa Makadirio na Makusanyo ya Serikali kwa Miaka Mitano



Kutokana na taarifa iliyotolewa kwenye vielelezo vya michoro hapo juu, hali inaonyesha kwamba kumekuwa na ongezeko la Makadirio na Makusanyo ya serikali kwa mfululizo katika kipindi cha miaka mitano, ongezeko la makusanyo limekuwa likikuwa kwa wastani wa asilimia 11.18%¹². Hata hivyo makusanyo yamekuwa yakiripotiwa chini ya makadirio yaliyopitishwa na Bunge isipokuwa kwa wa fedha mwaka 2015/16.

Mwenendo wa ongezeko la makusanyo na matumizi kwa miaka mitano unamaanisha mwenendo chanya katika kuboresha huduma za jamii, miundombinu na miradi ya Maendeleo.

4.5 Uchanganuzi wa Makadirio ya Mapato Kutoka Kwenye Makusanyo ya Ndani na Mikopo ili Kugharamia matumizi

Katika mwaka huu wa ukaguzi sehemu ya bajeti iliyopangwa kutumia makusanyo ya ndani; mapato ya kodi na yasiyotokana na kodi ni Sh. bilioni 19,977.01 sawa na asilimia 63 ya bajeti ya 31,711.99 iliyopitishwa na Bunge, ikiwa ni ongezeko la Sh bilioni 1,513.51 sawa na asilimia 8.2 ikilinganishwa na sehemu ya bajeti ilipitishwa kwa mwaka 2016/17.

¹² $\frac{\text{Makusanyo halisi ya mwaka 2017/18}}{\text{Makusanyo halisi ya mwaka 2013/14}} - 1 \times 100$


Makusanyo halisi kutoka kwenye kodi na makusanyo yasiyotokana na kodi yalifikia kiasi cha Sh. bilioni 16,739 sawa na asilimia 60 ya makusanyo yote, ikiwa ni ongezeko la Sh. bilioni 395 sawa na asilimia 2.41 ikilinganishwa na makusanyo yaliyoripotiwa katika mwaka wa fedha 2016/7.

Uchambuzi unaonyesha kwamba bila Mikopo na misaada kutoka kwa wahisani wa maendeleo, makusanyo ya ndani yangeweza kugharamia matumizi ya Serikali kwa asilimia 60.

Katika mwaka wa Fedha 2017/18 Bajeti ya serikali ilipanga kutumia kiasi cha Sh bilioni 11,734.99 sawa na asilimia 37 ya makaridio yaliyoidhinishwa kutoka katika vyanzo vya mikopo ya Ndani na Nje, Misaada ya Wahisani na Washirika wa Maendeleo. Kiasi halisi kilichopatikana kutokana na chanzo hiki ni Sh. bilioni 10,957 sawa na asilimia 40 ya makusanyo yote, hili ni sawa na ongezeko la Sh bilioni 1,993 ikiwa ni (22%) ya mikopo iliyotolewa mwaka wa fedha 2016/17.

Uchambuzi wa mikopo unaonyesha ongezeko la utegemezi wa mikopo na misaada ya wahisani kwa mfululizo wa miaka mitano isipokuwa kwa mwaka wa fedha 2013/14 na 2015/16¹³ kama navyoonyeshwa katika kielelezo;

¹³ Kwa mwaka wa Fedha 2013/14; kumekuwa na kupungua 2% kulinganisha na 2012/13, Kwa mwaka wa Fedha 2014/15; kumekuwa na ongezeko la 19% kulinganisha na 2013/14, Kwa mwaka wa fedha 2015/16; kumekuwa na kupungua kwa 7% kulinganisha na 2014/15, Kwa mwaka wa fedha 2016/17; kumekuwa na ongezeko la 27% kulinganisha 2015/16 na 2017/18 kumekuwa na ongezeko la 22% kulinganisha na 2016/17

Kielelezo Na. 13: Mwenendo wa Makusanyo ya ndani na Mikopo kwa mfululizo wa miaka mitano

Kwa ujumla, Mwenendo wa makusanyo ya ndani na mikopo inaonyesha uwiano sambamba na ongezeko la bajeti. Hata hivyo, utegemezi wa Mikopo ya ndani na nje huleta changamoto ya riba ambazo huathiri uchumi wa taifa.

4.6 Uchambuzi wa Fedha zilizopokelewa Mfuko Mkuu wa Serikali na Fedha zilizotolewa kwa Mafungu

Kiasi cha Fedha kilichotoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa matumizi ya kawaida na maendeleo katika Mwaka wa Fedha ni Sh. bilioni 26,947.41 kulinganisha na Sh. bilioni 26,531.56 zilizopokelewa mfuko mkuu, hivyo kufanya upungufu wa Sh. bilioni 415.84 hadi kufikia Tarehe 30 Juni, 2018.

Jedwali linalofuatia linaonyesha Makusanyo kutoka vyanzo mbalimbali kama yalivyopokelewa Mfuko Mkuu wa Serikali aidha, Maelezo zaidi kuhusu Makusanyo na Matumizi ya Fedha zilizopokelewa Mfuko mkuu yamezungumziwa katika Sura ya Tano ya ripoti hii.

Jedwali Na. 12: Makusanyo yaliyopokelewa Mfuko Mkuu

Vyanzo vya Makusanyo	Kiasi katika Sh bilioni
Mkusanyo ya Kodi	15,542.13 ¹⁴
Makusanyo yasiyotokana na Kodi	1,589.87
Mikopo ya Ndani	5,704.50

¹⁴ Kiasi hichi kinajumuisha Sh bilioni 15,149.47 kilichokusanywa kulingana na Bajeti husika na makusanyo mengine yasiyohusiana na Bajeti husika

Vyanzo vya Makusanyo	Kiasi katika Sh bilioni
Misaada, na Mikopo ya ndani yenye mashari nafuu na isiyo na masharti nafuu	3,695.06 ¹⁵
Jumla	26,531.56

Chanzo; Taarifa ya Mapato na Matumizi Mfuko mkuu

Kati ya Sh. bilioni 26,947.41¹⁶ zilizotolewa mfuko Mkuu, kiasi cha Sh. bilioni 22,627.28 kilitolewa kwa Serikali kuu ikiwa ni Wizara, Idara pamoja na Sekretarieti za Mikoa katika uwiano wa Sh bilioni 15,408.03 (68%) kwa matumizi ya Kawaida na kulipa madeni na Sh bilioni 7,219.26 (32%) kwa matumizi ya Maendeleo, Sh bilioni 4,320.13 zilitolewa kwa Serikali za Mitaa.

Ikiinganishwa taarifa ya kutoa Fedha (Exchequer issue report) na taarifa ya Fedha zilizopokelewa na kuripotiwa katika taarifa za fedha za Mafungu husika pamoja na barua za kukiri mapokezi ya fedha kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, nimebaini utofauti wa taarifa zilizo ripotiwa kama ilivyoonyesha kwenye Jedwali hapa chini;

Jedwali Na. 13: Tofauti zilizoonekana kati ya Taarifa za kutoa Fedha na Taarifa za fedha zilizoandaliwa na wizara.

Fungu	Wizara/Idara	Tarehe ya mapokezi	Aina ya Matumizi	Namba ya rejeo	Kiasi	Maoni
56	Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa	30-Jun-18	Fedha za Maendeleo	RW1413/2017/2018	21,428,196,476.30	Taarifa zilizotolewa na Hazina na hazikuripotiwa
39	Jeshi la Kujenga Taifa	30-Oct-17	Fedha za	EB/AG/159/17/0498	172,513,200.00	katika taarifa za fedha za wizara
		22-Mar-18	matumizi ya	EB/AG/159/17/1263	78,711,000.00	
40	Mahakama	15-Sep-17	Fedha za Maendeleo	947373795.7	947,573,795.65	Fedha zilizotolewa moja kwa moja katika miradi na hazikuripotiwa katika Taarifa ya fedha Hazina
		20-Dec-17		1091702112	4,453,128,800	
		08-Dec-17		1121707908	5,551,114,000	
		09-May-18		1051831133	6,754,396,200	

Vyanzo; Taarifa ya kutoa fedha na Taarifa za fedha za wizara zilizokaguliwa.

¹⁵ Kiasi hiki hakijumuishi; Misaada ya Sh bilioni 1,293.64, mikopo ya nje yenye masharti nafuu na mmasharti nafuu Sh bilioni 2,401.57, na kutojuisha Sh bilioni 1,557.06 za mikopo ya nje yenye masharti nafuu na isiyo na masharti nafuu kilichopelekwa moja kwa moja kwenye Miradi.

¹⁶ Kiasi hiki nimetolewa katika taarifa ya makusanyo na matumizi Mfuko mkuu, pamoja na taarifa ya fedha ya Mfuko mkuu iliyokagukiwa.

Tofauti inayoonekana imesababishwa na kutokuwapo kwa mifumo thabiti ya usuluisho kati ya fedha zilizotolewa na hazina na fedha zilizotolewa na wahisani wa maendeleo moja kwa moja kwenye miradi ya maendeleo katika Wizara.

Ni mapendekezo yangu kwa Menejimenti ya Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha inafanya usuluishi sahihi wa taarifa za fedha zilizotolewa kwa wizara mbalimbali na fedha zilizopokelewa moja kwa moja na wahisani wa maendeleo katika miradi, ili kuwezesha utoaji wa taarifa sahihi za mapokezi na matumizi ya fedha.

4.6.1 Uwiano wa Fedha zilizotolewa kwa Matumizi ya Kawaida ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa

Makadirio ya matumizi ya kawaida yaliyoidhinishwa katika mwaka huu wa ukaguzi katika Wizara, Idara za Serikali na Sekretariati za Mikoa yalikuwa Sh bilioni 15,725.16 hili ni ongezeko la Sh bilioni 1,843.12 sawa na asilimia 13.28% ikilinganishwa na bajeti ya 2016/17 ya Sh bilioni 13,882.04.

Mapitio ya taarifa za fedha kwa Wizara, Idara za Serikali na Sekretariati za Mikoa yalibainisha kuwa Sh. bilioni 15,408.03 zilitolewa kama matumizi ya kawaida sawa na asilimia 97.98 ya makadirio yaliyopitishwa na Bunge, hivyo Sh. bilioni 317.13 sawa na asilimia 2.02 ya makadirio hazikutolewa. Ikilinganishwa na fedha zilizotolewa kwa mwaka wa fedha 2016/17 kumekuwa na ongezeko la kiasi cha Sh 2,248.28 sawa na asilimia 17.08.

Kutokana na uchambuzi uliofanywa hapo juu, kuwapo kwa bajeti pungufu ya matumizi ya kawaida kunamaanisha kwamba utekelezaji hafifu au kutotekelezwa kabisa kwa shughulu za kawaida zilizokusudiwa.

4.6.2 Uwiano wa Fedha za Matumizi ya Kawaida zilizotolewa kulinganisha na Matumizi halisi

Kuna ongezeko la matumizi ya fedha za kawaida kwa kiasi cha Sh. bilioni 1,914.98 sawa na asilimia 14.28 ikilinganishwa na matumizi yaliyoripotiwa katika mwaka wa fedha 2016/17.


Matumizi halisi kwa mwaka fedha 2017/18 yalikuwa kiasi cha Sh. bilioni 15,328.66 ikilinganishwa na fedha zilizotolewa kiasi cha Sh. bilioni 15,408.03, hivyo Kiasi cha Sh. bilioni 79.36 kati ya fedha zilizotolewa hakikutumika, uwepo wa bakaa ya fedha zisizotumika kunamaanisha kutotekelezwa au utekelezaji hafifu wa shughuli zilizokusudiwa awali, ucheleweshwaji katika kutolewa kwa fedha, au uwezo hafifu wa Taasisi katika kutumia pesa zilizotolewa kwa wakati.

Maelezo zaidi ya makadirio ya fedha za matumizi, fedha zilizoidhinishwa na kutolewa, pamoja na matumizi halisi yaliyofanyika kwa kila taasisi iliyokaguliwa zimeonyeshwa katika Kiambatisho Na. 8.

Jedwali Na. 14: Makadirio, Fedha zilizotolewa na Matumizi Halisi ya ya Fedha za matumizi ya kawaida kwa miaka Mitano (Kiasi katika Sh billioni)

Mwaka wa Fedha	Makadirio	Fedha zilizotolewa	Matumizi halisi
2013/14	9,959.81	9,559.56	9,551.29
2014/15	11,646.20	11,190.11	11,156.43
2015/16	12,904.75	12,065.22	12,045.94
2016/17	13,882.04	13,159.74	13,413.69
2017/18	15,725.16	15,408.03	15,328.66
Tofauti (2017/18-2016/17)	1,843.12	2,248.28	1,914.98
Asilimia ya (punguzo)/ongezeko	13.28	17.08	14.28

Kielelezo Na. 14: Makadirio, Fedha zilizotolewa na Matumizi Halisi ya ya Fedha za mKielelezo Na. 15: atumizi ya kawaida kwa miaka Mitano (Kiasi katika Sh billioni)



Vyanzo; Taarifa za Fedha zilizokaguliwa kutoka kwenye Wizara, Idara na Sekretariati za Mikoa

4.6.3 Uwiano wa Fedha zilizotolewa kwa shughuli za Maendeleo zikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa

Makadirio yaliyoidhinishwa kwa shughuli za Maendeleo katika Mwaka huu wa Ukaguzi ni Sh. bilioni 10,142.72 ikiwa ni pungufu ya Sh. 92.69 sawa na asilimia 0.91 ikilinganishwa na Sh. bilioni 10,235.41 za bajeti ya mwaka wa fedha 2016/17.

Mapitio ya taarifa za fedha za Wizara, Idara za Serikali na Sekretariati za Mikoa yalibaini kuwa kiasi cha Sh. bilioni 7,219.26 zilitolewa kwa shughuli za maendeleo sawa na asilimia 71 ya makadirio, hivyo kiasi cha Sh. bilioni 2,923 sawa na asilimia 28.82 ya makadirio hakikutolewa. Hata hivyo kunaongezeka la Sh. billioni 280.26 sawa na asilimia 4.04 ikilinganishwa na Sh. bilioni 6,939.00 zilizotolewa katika mwaka wa fedha 2016/17. Ongezeko hili linamaanisha chanya katika maendeleo ya miradi Taifa.

Utolewaji hafifu wa fedha katika shughuli za maendeleo kunamaanisha kutotekelezwa au utekelezwaji hafifu wa miradi ya

maendeleo iliyopangwa, hivyo kuzuia maendeleo endelevu ya miradi ya maendeleo.

4.6.4 Uwiano wa Fedha za Matumizi ya Maendeleo zilizotolewa kulinganisha na Matumizi halisi

Kuna ongezeko la matumizi ya fedha za Maendeleo katika Mwaka wa fedha 2017/18 kwa kiasi cha Sh. 1,054.61 sawa na ongezeko la asilimia 17.44 ikilinganishwa na matumizi yaliyoripotiwa katika mwaka wa fedha 2016/17.

Matumizi ya fedha za maendeleo katika mwaka huu wa ukaguzi 2017/18 ni kiasi cha Sh. bilioni 7,100.42 ikilinganishwa na Sh. bilioni 7,219.26 ya fedha za maendeleo zilizotolewa, hivyo kiasi cha Sh. bilioni 118.83 sawa na asilimia 2 ya fedha zilizotolewa hazikutumika.

Kutotumika kwa fedha za maendeleo zilizotolewa kunamaanisha utekelezaji hafifu au kutotekelezwa kwa miradi ya maendeleo iliyopangwa, mazingira haya yanaweza kuchangiwa na ucheleweshwaji katika kutoa fedha zilizokusudiwa ama uwezo hafifu wa taasisi husika katika kutumia fedha zilizototewa katika kipindi kusudiwa.

Pia katika kupitia taarifa ya fedha zilizotolewa kutoka mfuko mkuu nimebaini kuwa kiasi cha Sh. bilioni 140.53¹⁷ ya fedha za maendeleo sawa na asilimia 2 ya fedha zote za maendeleo zilizotolewa, ziligawanywa kwa wizara mbalimbali katika kipindi cha robo ya mwisho ya mwaka wa fedha 2017/18, sababu hii inaweza kuchangia kuwapo kwa bakaa ya fedha za maendeleo ambazo hazikutumika hadi kufikia tarehe 30 mwezi Juni, 2018.


Maelezo zaidi ya makadirio ya fedha za maendeleo, fedha zilizoidhinishwa na kutolewa, pamoja na matumizi halisi ya fedha za maendeleo yaliyofanyika kwa kila taasisi iliyokaguliwa zimeonyeshwa katika Kiambatisho Na. 9.

¹⁷ Kiasi hiki kimetoka katika ripoti ya fedha (Exchequer Issue report- Development exchequer Issue-Loan/Grant) mwezi Aprili 2018 hadi Juni, 2018

Jedwali Na. 15: Makadirio, Fedha zilizotolewa na Matumizi Halisi ya Fedha za maendeleo kwa miaka Mitano (Kiasi katika Sh. bilioni)

Mwaka wa serikali	Makadirio	Fedha zilizotolewa	Matumizi halisi
2013/14	5,035.94	3,147.04	3,145.08
2014/15	4,389.02	2,954.20	2,916.18
2015/16	4,968.86	3,768.59	3,729.72
2016/17	10,235.41	6,939.00	6,045.81
2017/18	10,142.72	7,219.26	7,100.42
Tofauti (2017/18-2016/17)	(92.69)	280.26	1,054.61
Asilimia ya (punguzo)/ongezeko	(0.91)	4.04	17.44

Kielelezo Na. 1: Makadirio, Fedha zilizotolewa na Matumizi Halisi ya Fedha za maendeleo kwa miaka Mitano (Kiasi katika Sh. bilioni)




Vyanzo; Taarifa za Fedha zilizokaguliwa kutoka kwenye Wizara, Idara na Sekretariati za Mikoa

Kutokana na Aya zilizotangulia hapo juu, kati ya Sh. bilioni 22,627.28 zilizotolewa kwa matumizi ya Serikali Kuu, Sh. bilioni 22,429.09¹⁸ sawa na asilimia 99 zilitumika kwa matumizi ya kawaida, matumizi ya maendeleo pamoja na kupunguza madeni. Kiasi cha Sh. bilioni 198.20 sawa na asilimia 1 hakikutumika hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2018.

¹⁸ Matumizi ya Kawaida Sh. bilioni 15,328.66; Matumizi ya Kawaida Sh. bilioni 7,100.42

Kielelezo kifuatacho kinaonyesha mgawanyo wa fedha kama zilivyotumika katika matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo.

Kielelezo Na. 16: Matumizi halisi ya Kawaida na Maendeleo



4.6.5 Uwiano wa Makadirio pamoja na Makusanyo ya Mapato yasiyotokana na Kodi.

Kutokana na Bajeti iliyopitishwa Kiasi cha Sh. bilioni 2,183.35 kilipangwa kukusanywa na Wizara, Idara za serikali pamoja na ofisi za balozi kutoka katika makusanyo yasiyo tokana na kodi. Hata hivyo, mgawanyo wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/18 kwa Wizara/idara ulikuwa Sh. bilioni 2,158.59¹⁹, Sekretarieti za Mikoa Sh bilioni 9.58 na Balozi Sh. bilioni 25.41.

Makusanyo halisi yalikuwa Sh. bilioni 1,421.81 kutoka Wizara/idara, Sh bilioni 6.71 kutoka Sekretarieti za Mikoa na Sh. bilioni 31.06 kutoka ofisi za Balozi.

Wizara ilikusanya pungufu ya Sh. bilioni 736.78 sawa na asilimia 34.13 ya bajeti husika, Sekretarieti za mikoa zilikusanya pungufu ya Sh. bilioni 2.87 sawa na asilimia 29.9 ya makusanyo ya bajeti husika, Balozi zilikusanya zaidi kwa Sh. bilioni 5.65 sawa na asilimia 22 ya bajeti husika.

¹⁹ Kiasi hichi hakijumuishi bajeti ya Fungu 34 Wizara ya mambo ya nje na ushirikiano wa Afrika Mashariki, mwenendo wa makusanyo kwa fungu hili unaonekana katika makusanyo ya Balozi Kiambatisho Na. 11.


Vielelezo vifuatavyo vinaonyesha makusanyo ya mapato yasiyotokana na kodi kutoka kwenye Wizara/Idara, Sekretarieti za Mikoa na Balozi kwa miaka minne mfululizo;

Jedwali Na. 16: Mwenendo wa makusanyo yasiyotokana na kodi kwa miaka mitano Mfululizo (Kiasi katika Sh)

Mwaka wa Fedha	Maelezo	Makadirio	Makusanyo halisi	Makusanyo zaidi/(pungufu)
2017/18	Wizara/Idara za Serikali	2,158.59	1,421.81	(736.78)
	Sekretarieti za Mikoa	9.59	6.71	(2.87)
	Balozi	25.41	31.06	5.65
2016/17	Wizara/Idara za Serikali	0.00	0.00	(0.00)
	Sekretarieti za Mikoa	0.09	0.08	(0.01)
	Balozi	0.00	(0.00)	(0.00)
2015/16	Wizara/Idara za Serikali	691.58	727.12	35.54
	Sekretarieti za Mikoa	26.01	0.05	(25.96)
	Balozi	18.06	22.02	3.97
2014/15	Wizara/Idara za Serikali	701.56	597.61	(103.95)
	Sekretarieti za Mikoa	39.67	89.13	49.46
	Balozi	15.51	19.03	3.52

Vyanzo: Taarifa za Fedha zilizokaguliwa kutoka katika Wizara, Idara za serikali na Balozi

Kielelezo Na. 17: Makusanyo yasiyotokana na Kodi kutoka katika Wizara na Idara za serikali



Chanzo: Taarifa za fedha zilizokaguliwa kutoka katika Wizara na Idara za serikali

Makadirio na Makusanyo ya mapato yasiyotokana na kodi kutoka katika Wizara/Idara yamekuwa yakiongezeka kwa miaka minne


mfululizo isipokuwa kwa makusanyo yaliyoripotiwa mwaka 2016/17. Licha ya makusanyo pungufu yanayoonekana katika jedwali, kumekuwa na ongezeko la makusanyo la Sh. bilioni 948.55 kulinganisha na makusanyo ya ya Sh. bilioni 473.27 yaliyoripotiwa katika Mwaka wa fedha 2016/17.

Maelezo ya kina katika **Kiambatisho Na. 10.** ya naonyesha Wizara/idara 20 zimeripoti makusanyo ya ziada, wakati 22 zimeripoti makusanyo pungufu.

Hata hivyo, katika kupitia taarifa za hesabu na kitabu cha makadirio ya makusanyo kilichopitishwa na Bunge kutoka Tarehe 1 Julai, 2017 hadi tarehe 30 June, 2018 nimeona tofauti ya kati ya Sh. bilioni 358.97 kati ya Makadirio yaliyoripotiwa katika vitabu vya Hesabu - "Taarifa ya Bajeti dhidi ya makusanyo halisi" na Makadirio ya makusanyo yaliyopitishwa na Bunge kwa baadho ya vifungu.²⁰

Ni ushauri wangu kwa Wizara na Idara zote kuwa, makadirio ya makusanyo katika fungu husika yanapaswa kutokana na makadirio ya makusanyo katika vifungu kama ilivyopitishwa na bunge na sio vinginevyo ili kutoa taswira halisi ya makusanyo katika fungu husika, pia naendelea kushauri wizara na idara kuongeza juhudi katika ukusanyaji wa mapato yasiyotokana na kodi ili kuchangia Bajeti ya Taifa.

Kielelezo Na. 18: Makusanyo yasiyotokana na kodi katika sekretarieti za Mikoa



Vyanzo; Taarifa za Fedha zilizokaguliwa kutoka sekretarieti za Mikoa


²⁰ Vifungu 46, 62,99,52,37,56,35,39,68 na 16.

Licha ya makusanyo pungufu yanayoonekana katika vielelezo hapo juu, kumekuwa na ongezeko la makusanyo ya Sh. billioni 6.64 Katika Sekretarieti za Mikoa sawa na ongezeko la zaidi ya asilimia 100 ukilinganisha na makusanyo ya Sh. bilioni 0.08 yaliyoripotiwa katika mwaka wa fedha 2016/17.

Maelezo ya kina katika Jedwali yanaonyesha Sekretarieti za Mikoa 5 zimekusanya zaidi, 6 zimekusanya pungufu, 1 imekusanya sawa sawa na makadiria na Sekretarieti zilizobaki hazikukusanya chochote. Hata hivyo Sekretarieti 3 ziliweza kukusanya mapato japo hazikuwa na makadirio yoyote ya ukusanyaji wa mapato yasiyotokana na kodi. Kama ilivyoelezwa katika **Kiambatisho Na. 10**.

Ni ushauri wangu kwa Ofisi zote za Sekretarieti za Mikoa kuandaa makadirio ya makusanyo ya mapato yasiyotokana na kodi, pia kuweka juhudi zaidi katika ukusanyaji wa mapato.

Kielelezo Na. 19: Makusanyo yasiyotokana na Kodi katika Balozi



Vyanzo: Taarifa za Fedha zilizokaguliwa kutoka katika Balozi

Makusanyo ya mapato kutoka katika Balozi yamekuwa yakionyesha ongezeko chanya kwa miaka Minne mfululizo, karibu Balozi zote zilizokaguliwa zimekusanya zaidi ya makadirio yaliyokuwa yamewekwa awali, kumekuwa na ongezeko la Sh. bilioni 3.21 sawa na asilimia 11.53 kulinganisha na makusanyo yaliyoripotiwa mwaka

2016/17. Balozi 11 zimekusanya chini ya makadirio, 26 zimekusanya zaidi, 2 haziyakusanya chochote kama ilivyoonyeshwa katika Kiambatisho Na. 11.

4.6.6 Mapato yasiyotokana na Kodi ambayo hayakuwasilishwa Mfuko Mkuu Sh. 2,537,773,463.50

Kifungu cha 11 cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha ya mwaka 2001, “kinataka maduhuli au fedha nyingine zozote zinazokusanywa au kupokelewa kwa ajili ya Serikali zipelekwe katika Mfuko Mkuu isipokuwa pale tu ambapo fedha zilizokusanywa zinapelekwa katika mifuko mingine iliyoanzishwa kisheria kwa madhumuni maalumu au kubakizwa katika mamlaka iliyokusanya kwa ajili ya kulipia gharama za mamlaka hiyo kama inavyotakiwa na Sheria maalumu”.

Pia, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kupitia barua yenye kumbukumbu Na. DA 68/226/02/83 ya tarehe 19 Juni, 2018 ilitoa maelekezo kuwa makusanyo yote kutoka katika balozi mbalimbali yasiyotokana na kodi yanapaswa kuwasilishwa Mfuko mkuu wa ofisi za Hazina kabla ya tarehe 20 June, 2018

Kinyume na agizo lililopo kwenye Kifungu cha sheria pamoja na maelekezo yaliyotolewa na Wizara, Ukaguzi ulibaini kuwa kiasi cha Sh. bilioni 2,537,773,463.50 kilichokusanywa na balozi 7 katika mwaka wa fedha 2017/18 hakikuwasilishwa Mfuko mkuu wa Hazina, badala yake kiasi hicho cha fedha kilibakizwa katika akaunti za fedha za Balozi husika, Hata hivyo rekodi hii inaonyesha punguzo la asilimia 82.5 ukilinganisha na balozi 21 zilizo ripotiwa kutokuwasilisha kiasi cha Sh. bilioni 14,546,473,044.63 katika mwaka wa fedha 2016/17. Mwenendo huu unaonyesha ongezeko la kuzingatia wa sheria katika kuwasilisha Makusanyo mfuko mkuu.

Maelezo zaidi ya kiwango cha fedha na Balozi husika zimeonyeshwa katika Jedwali lililoonyeshwa hapa chini;

**Jedwali Na. 17: Makusanyo yasiyotokana na Kodi ambayo
hayakuwasilishwa Mfuko Mkuu**

Na.	Kufungu kidogo	Jina la Balozi	Kiasi (Sh)
1	2005	Ubalozi wa Tanzania Abuja	295,240,405.57

Na.	Kufungu kidogo	Jina la Balozi	Kiasi (Sh)
2	2001	Ubalози wa Tanzania Addis Ababa, Ethiopia	259,358,948.85
3	2024	Ubalози wa Tanzania Riyadh, Saudi Arabia	58,580,000.00
4	2016	Ubalози wa Tanzania Stockholm	828,362,785.00
5	2035	Ubalози wa Tanzania Kuwait	218, 224,307.91
6	2007	Ubalози wa Tanzania Tanzania - Lusaka	93,280,322.12
7	2018	Ubalози wa Tanzania Washington, D.C.	784,726,694.05
Jumla Kuu			2,537,773,463.50

Chanzo: Hesabu za Balozi zilizokaguliwa

Ni maoni yangu wangu kwamba, kwa kutopeleka makusanyo yasiyotokana na kodi katika mfuko mkuu wa Hazina kiasi cha Sh. bilioni 2,537,773,463.50 kama ilivyoelezwa katika Sheria ya Fedha na miongozo iliyotolewa, kunainyima fursa serikali kutumia kiasi cha fedha kilichokusanywa katika shughuli nyingine za kimaendeleo, pia kunaongeza hatari ya kutumia fedha hizo zilizokusanywa katika matumizi yasiyokusudiwa.

Ninashauri kwa menejimenti ya Wizara ya Mambo ya nje na ushirikiano wa Afrika mashariki kuhakikisha kwamba kiasi chote cha Fedha kilichokusanywa kinawasilishwa katika mfuko mkuu wa Hazina kama ilivyo elezwa katika Sheria ya Fedha ya mwaka 2001, ili kupunguza hatari ya matumizi yasiyokusudiwa.

4.6.7 Uandaaji wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti isiyo na usahihi

Kifungu cha 55 kifungu kidogo cha 3 cha Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015, kama ilivyo fanyiwa marekebisho katika kanuni ya 29 kifungu kidogo cha 4 cha kanuni za Bajeti, kinamtaka “Kamishina wa Bajeti akishirikiana na Kamishina wa Mipango kuandaa na kutoa taarifa ya robo mwaka ya utekelezaji wa Bajeti katika kila mwisho wa robo mwaka. Taarifa hiyo inalenga kutoa mrejesho wa utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha robo mwaka na mwaka mzima.

Katika ukaguzi wa Mapato yaliyokusanywa na Wizara ya Fedha na mipango kwa kipindi cha robo ya mwisho wa mwaka wa fedha unaoishia 2017/18, nimebaini kuwapo kwa tofauti kati ya kiasi cha fedha kilichoropotwa katika taarifa ya fedha ya robo mwaka na taarifa ya fedha katika wizara/ idara za Wizara ya Fedha na mipango zilizokusanywa kwa kipindi kimoja.

Jedwali linalofuata hapa chini linaonyesha Makusanyo ya mapato na mikopo iliyopokelewa hadi Tarehe 30 Juni, 2018 kama ilivyoripotiwa katika Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti na Wizara.

Jedwali Na. 18: Utofauti ulioonekana katika Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti na Taarifa ya fedha katika wizara

Vyanzo vya Makusanyo	Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti	Taarifa ilivyoripotiwa katika Fungu 21	Taarifa kutoka Fungu 22	Tfauti iliyoonekana
	Makusanyo halisi katika Sh.	Makusanyo halisi katika Sh.	Makusanyo halisi katika Sh.	Tofauti katika Sh.
Kodi	15,191,000,000,000	15,123,000,000,000		68,000,000,000
Misaada (A)	930,400,000,000	1,238,449,701,518		(308,049,701,518)
Mikopo ya masharti nafuu (B)	1,535,400,000,000	1,056,269,918,423		479,130,081,577
Mikopo ya nje isiyo na masharti nafuu (C)	1,474,300,000,000	-	1,807,752,875,530	(333,452,875,530)
Mikopo ya Ndani	5,704,400,000,000		5,704,400,000,000	-

Kumbuka: Usahihi wa Taarifa umeonekana kwenye mikopo ya ndani pekee

Hata hivyo katika kupata maelezo ya kina, nimebaini kwamba utofauti wa taarifa unaonekana umesababushwa na kuwapo kwa nyakati tofauti za uandaaji wa Taarifa. Taarifa ya utekelezaji wa bajeti inaandaliwa mwezi mmoja baada ya kufunga mwaka wa fedha wa serikali wakati Taarifa ya fedha inaandaliwa miezi mitatu baada ya kufunga mwaka wa fedha wa serikali, Kwa mantiki hiyo taarifa ya utekelezaji wa bajeti huandaliwa kwa kutumia taarifa ambazo hazijakamilika.

Ni maoni yangu kwamba, Taarifa ya utekelezaji wa bajeti ni taarifa muhimu kwa serikali inayolenga kutoa mrejesho wa utekelezaji wa bajeti kwa wadau mbalimbali ikiwemo Bunge, Wanataauma, Wadau wa maendeleo, Mkaguzi na mdhibiti wa hesabu za Serikali na wananchi kwa ujumla. Hivyo kutokuandaliwa kwa usahii kunaweza kupotosha umma na kuathiri mwenendo wa tathmini ya Bajeti.

Ni ushauri wangu kwa Menejimenti ya Wizara ya Fedha na idara inayohusika kuongeza usahihi katika uandaaji wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti, ama kwa kubadili kipindi cha kuwasilisha taarifa husika kama kilivyoelezwa katika Bajeti, au kufanya mabadiliko ya kisheria ili kuruhusu uwasilishwaji wa taarifa iliyo fanyiwa marekebisha pia kuboresha njia za ukusanyaji wa taarifa katika kuandaa ripoti

Sura ya Tano

Mamlaka ya Mapato Tanzania

5.1.1 Utangulizi

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria Na.11 ya mwaka 1995 na ilianza kutekeleza majukumu yake tarehe 01 Julai 1996, ikiwa na majukumu ya kusimamia na kukusanya mapato ya kodi kwa niaba ya Serikali.

Mamlaka inatayarisha aina mbili za Taarifa za Fedha, Taarifa za Mapato na Taarifa za Matumizi. Taarifa zote mbili za Fedha zinaandaliwa kwa kutumia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma visivyo vya misingi ya fedha taslimu (IPSAS Accrual basis of accounting). Taarifa za mapato hufafanua masuala yahasuyo makusanyo ya kodi mbalimbali, na ile taarifa ya matumizi hufafanua kuhusu jinsi fedha zilizotolewa na serikali na vyanzo vingine zilivyotumiwa na kutekeleza majukumu ya Mamlaka.

5.1.2 Mwelekeo wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Miaka Iliyopita

Katika taarifa ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu ya mwaka wa fedha uliopita (2016/17) mapendekezo hamsini (50) yalitolewa kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2017; na mapendekezo mia moja hamsini na saba (157) yalisalia yakisubiri kufanyiwa kazi toka mwaka wa fedha 2001/2002 mpaka 2015/2016, hivyo kufanya jumla ya mapendekezo 207 yanayohitaji kutekelezwa.

Nimepitia hatua zilizochukuliwa katika utekelezaji wa jumla ya mapendekezo mia mbili na saba (207). Kati ya hayo, mapendekezo 92 (asilimia 44) yanahusiana na Idara ya Forodha na Ushuru wa bidhaa, mapendekezo 53 (asilimia 26) yanahusiana na Idara ya Walipakodi Wakubwa, mapendekezo 10 (asilimia 5) yanahusiana na Idara ya Uchunguzi wa Kodi na mapendekezo 52 (asilimia 25) yanahusiana na Idara ya Mapato ya Ndani kama ilivyoainishwa kwenye jedwali hapo chini.

Jedwali Na. 19: Idadi ya mapendekezo yaliyotolewa kwa miaka iliyopita kwa kila Idara

Na	Mwaka	Idara ya Forodha na Ushuru wa bidhaa	Idara ya Walipa kodi wakubwa	Idara ya uchunguzi wa kodi	Idara ya Mapato ya Ndani	Jumla
1	2001/2002	1	-	-	-	1
2	2002/2003	-	-	-	-	-
3	2003/2004	-	-	-	-	-
4	2004/2005	2	-	-	-	2
5	2005/2006	4	-	-	-	4
6	2006/2007	3	-	-	-	3
7	2007/2008	5	1	-	1	7
8	2008/2009	1	2	-	2	5
9	2009/2010	2	2	-	2	6
10	2010/2011	1	4	-	1	6
11	2011/2012	3	5	-	-	8
12	2012/2013	2	6	-	2	10
13	2013/2014	7	6	-	4	17
14	2014/2015	20	13	-	6	49
15	2015/2016	22	7	6	14	39
	Jumla ndogo	73	46	6	32	157
16	2016/2017	19	7	4	20	50
	Jumla	92	53	10	52	207

Kati ya mapendekezo 207, mapendekezo arobaini na tano (45) sawa na asilimia 22 yalitekelezwa na mapendekezo miamoja sitini na mbili (162) sawa na asilimia 78 yalikuwa kwenye hatua za utekelezaji. Muhtasari wa mwelekeo wa utekelezwaji wa mapendekezo yote umeoneshwa katika Jedwali hapo chini;

Jedwali Na. 20: Mwelekeo wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyopita

Mwelekeo wa Utekelezaji	Kipaumbele cha juu	Kipaumbele cha kati	Kipaumbele cha chini	Jumla	
	(idadi)	(idadi)	(idadi)	(idadi)	%
Yaliyotekelezwa	45	-	-	45	22
Yapo kwenye hatua za utekelezwaji	162	-	-	162	78
Hayajatekelezwa	-	-	-	-	-
Jumla	207	-	-	207	100

Jumla ya mapendekezo yaliyo kwenye hatua za utekelezaji ni mia moja sitini na mbili (162) sawa na asilimia 78. Baada ya kupitia zaidi utekelezaji wa mapendekezo yaliyosalia nilibaini kuwa, jumla ya mapendekezo kumi na tisa (19) sawa na asilimia 12 yanahitaji maamuzi ya Taasisi nyingine nje ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kama vile Bodi za Rufani za Kodi, Baraza la Rufani za Kodi, Mahakama ya Rufaa ya Tanzania na Bunge kwa kodi zilizo katika mapingamizi na madeni ya kodi yaliyopendekezwa na Mamlaka ya Mapato kupitia Hazina kwa ajili ya kufutwa. Maamuzi ya kesi hizo na kufutwa kwa madeni kusubiriwa kwa muda mrefu tangu mwaka wa fedha

2001/2002. Mapendekezo mia moja arobaini na tatu (143) yaliyobaki, sawa na asilimia 88, yanashughulikiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Kwa ujumla, kulingana na uhalisia wa mapendekezo yaliyosalia, mwelekeo wa utekelezaji hauridhishi, hivyo uongozi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania unashauriwa kuongeza jitihada katika utekelezaji wa mapendekezo ili kukomboa mapato yaliyokwama kutokana na mapungufu yaliyoainishwa. Hatua hii itaongeza zaidi ukusanyaji wa mapato.

5.1.3 Mwelekeo wa Mapato nchini Tanzania

Kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018 Mamlaka ya Mapato ilikusanya jumla ya Shilingi 15,386,495,236,448 dhidi ya malengo yaliyowekwa ya Shilingi 17,315,767,525,241. Hii inaonesha makusanyo yalikuwa pungufu kwa Shilingi 1,929,272,288,793 ambazo ni sawa na asilimia 11 ya malengo. Jumla hii ya makusanyo haihusishi Shilingi 18,945,791,406 za vocha ya misamaha ya kodi kutoka hazina, pamoja na fedha za marejesho ya kodi. Mapato halisi ya mwaka wa fedha 2017/2018 ni Shilingi 15,405,441,027,854. Jedwali hapo chini linaonesha jumla ya makisio na makusanyo ya mapato toka Tanzania bara na Zanzibar.

Jedwali Na. 21: Jumla ya makusanyo kwa mwaka 2017/18 kwa idara (Shilingi kwa mamilioni)


Idara	Lengo - Tanzania bara na Zanzibar	Makusanyo halisi Tanzania bara na Zanzibar	Makusanyo Pungufu	Makusanyo Pungufu kwa asilimia
Mapato ya ndani	3,645,429	2,956,346	(689,083.00)	(18.90%)
Walipa kodi wakubwa	6,712,717	6,243,877	(468,840.00)	(6.98%)
Forodha na Ushuru wa bidhaa	7,174,950	6,229,210	(945,740.00)	(13.18%)
Marejesho ya kodi	(217,329)	(42,938)	174,391.00	(80.24%)
Jumla ndogo	17,315,767	15,386,495	(1,929,272.00)	(11.14%)
Vocha za misamaha ya kodi	49,285	18,946	(30,339.00)	(61.56%)
Jumla kuu	17,365,052	15,405,441	(1,959,611.00)	(11.28%)

Chanzo: Taarifa za mapato zilizokaguliwa za mwaka 2017/18

Kwa ujumla, idara zote tatu za mapato zilishindwa kufikia malengo kwa mwaka huu wa fedha 2017/18. Kielelezo cha hapo chini kinaonesha kwamba Idara ya walipa kodi wakubwa ilikusanya asilimia

41 ya makusanyo yote ambayo ndiyo sehemu kubwa kuliko idara zote; ikifuatiwa na Idara ya Forodha yenye asilimia 40 na idara ya kodi za ndani yenye asilimia 19 ambayo ndiyo ya mwisho kwa mwaka wa fedha 2017/2018, makusanyo haya hayahusishi vocha ya misamaha ya kodi kutoka Hazina.

Kielelezo Na. 20: Uwiano wa Makusanyo halisi Kwa Idara kwa mwaka 2017/18



Kutokana na mchanganuo huo, ni dhahiri kuwa mchango wa makusanyo kutoka Idara ya Mapato ya Ndani umekuwa nyuma ikilinganishwa na idara nyingine. Kwa maoni yangu, kuna mambo mengi ambayo mamlaka ikiyafanya yanaweza kuongeza mapato katika idara ya mapato ya ndani, nashauri ufanisi na makusanyo katika idara hii uongezwe kwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwemo ufatiliaji wa karibu kwenye kukusanya madeni ya kodi na kutumia taratibu za kisheria ili kuhakikisha kodi zinalipwa, kushughulikia mapingamizi ya kodi kwa wakati, kuimarisha ukaguzi na ukadiriaji wa kodi, kuisitiza matumizi ya mashine na risiti za kielekroniki (EFD) na jitihada nyingine ili kuhakikisha kuwa kila mfanyabiasha na raia analipa kodi.

5.1.4 Mwelekeo wa Makusanyo ya Mapato

Mwelekeo wa makusanyo ya mapato kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita kwa wastani, ulikuwa chini ya makadirio yaliyoidhinishwa,

isipokuwa kwa mwaka wa fedha 2015/16 ambapo makusanyo halisi yalikuwa juu ya makadirio kwa asilimia 0.13. Hata hivyo, ufanisi katika ukusanyaji mapato kwa mwaka huu wa fedha haukuwa mzuri kwani uwiano wa kodi dhidi ya pato la ndani la taifa umepungua (kodi kwa pato la taifa) mpaka kufikia asilimia 12.8 ikilinganishwa na asilimia 13.2 kwa mwaka 2016/17. Hivyo Mamlaka imeshindwa kutimiza lengo na mkakati wa kufikia uwiano wa asilimia 19.9 wa kodi dhidi ya pato la ndani la taifa, lengo ambalo Mamlaka ilijiwekea ili lifikiwe kwa kipindi cha hadi kufikia mwaka 2018. Hivyo, nashauri serikali iongeze jitihada katika ukusanyaji wa mapato.

Jedwali hapo chini linaonesha mwelekeo wa makusanyo na uwiano wa kodi dhidi ya pato la ndani la taifa kwa kipindi cha miaka mitano kwa Tanzania na nchi nyingine za Afrika Mashariki

Jedwali Na. 22: Mwelekeo wa makusanyo ya mapato kwa Tanzania na nchi za Afrika Mashariki, 2013/14 - 2017/18 (Shilingi kwa milioni)

Maelezo	Mwaka wa Fedha [Shilingi kwa milioni]				
	2013/14	2014/15	2015/16	2016/17	2017/18
Lengo	10,957,001	12,078,015	13,220,252	15,293,899	17,365,052
Makusanyo halisi	10,026,659	10,743,765	13,238,045	14,271,382	15,405,441
Tofauti kati ya Lengo na Makusanyo	-930,342	-1,334,250	17,793	-1,022,517	1,959,611
Tofauti kati ya Lengo na Makusanyo kwa asilimia	-8	-11	0.13	-6.69	-11.28
Uwiano wa kodi dhidi ya pato la jumla la ndani (Kodi/pato la jumla la ndani):					
Tanzania	12.50%	11.60%	12.90%	13.20%	12.80%
Uganda	11.30%	12.30%	12.80%	14.00%	14.20%
Kenya	19.10%	18.70%	18.80%	19.30%	18.50%
Rwanda	14.90%	15.10%	16.10%	15.20%	15.80%
Burundi	13.60%	13.70%	13.00%	13.40%	13.00%

Chanzo: Takwimu za Mamlaka ya Mapato Tanzania, 2014 -2018

Mchanganuo linganifu wa ufanisi wa kodi kwa nchi za Afrika Mashariki unaonesha kwamba, Tanzania iko nafasi ya mwisho kwa mwaka huu wa fedha. Kwa kuzingatia mwelekeo linganifu wa nchi za Afrika Mashariki, nashauri kuwa Serikali iongeze ufanisi katika ukusanyaji wa kodi ili kufikia malengo yake, kwani bado kuna maeneo ya kuboresha zaidi kwenye ukusanyaji wa mapato, ikiwemo kuongeza wigo wa vyanzo vya kodi, kudhibiti mianya ya upotevu wa kodi na kuongeza

ulipaji kodi kwa hiari. Kwa ujumla, hatua hizi na nyingine zitasaidia kupunguza kiwango cha utegemezi wa bajeti.

5.1.5 Changamoto katika ukusanyaji wa mapato na mapendekezo

Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita Mamlaka ya Mapato Tanzania haikuweza kufikia malengo ya ukusanyaji wa kodi, isipokuwa kwa mwaka wa fedha 2015/16 na mwelekeo wa ukusanyaji wa mapato umekuwa chini ya makadirio yaliyoidhinishwa kwa wastani wa asilimia 7.3 katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Kuna changamoto ambazo zinatakiwa kufanyiwa kazi na Serikali ili kuongeza ukusanyaji wa mapato ambazo ni pamoja hizi zifuatazo;

a) Kuwapo kwa kesi za kodi za muda mrefu

katika Bodi ya Rufaa za Kodi (TRAB), Baraza la Rufaa za Kodi (TRAT) na Mahakama ya Rufaa Tanzania imekuwa ni kikwazo kikubwa katika juhudi za ukusanyaji wa mapato. Mahojiano yangu na Uongozi wa Bodi ya Rufaa za Kodi na Baraza la Rufaa za Kodi juu ya ufanisi usioridhisha kwenye kusikiliza na kukamilisha kesi za kodi, nilifahamu kwamba Taasisi hizi zinatakiwa wakati wote ziwe na uwiano sawa wa Mwenyekiti, Makamu Wenyeviti na Wajumbe ili ziweze kufanya vikao vingi na kwa wakati. Kadhalika, taasisi hizi zimekuwa na tatizo la ufinyu wa bajeti, hivyo kuathiri kufanyika kwa vikao vya kutosha vya kusikiliza kesi kama inavyotakiwa na sheria. Mapungufu haya yamesababisha wafanyabiashara wasio waaminifu kutumia mwanya huu kuchelewesha malipo ya kodi kwa kupeleka kesi zao kwenye taasisi hizi wakijua zitachukua muda mrefu kusikilizwa. Jambo hili linazuia ukusanyaji wa mapato makubwa ya Serikali, kwani kesi hizi zinakuwa na kodi nyingi sana. Ni vema Serikali ikahakikisha Taasisi hizi zinakuwa na idadi kamili ya Wenyeviti, Makamu Wenyeviti na wajumbe, pia zipewe bajeti ya kutosha ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi

Naishauri Serikali iziboreshe na kuziongezea uwezo Bodi ya Rufaa za Kodi na Baraza la Rufaa za Kodi kwa kuteua wenyeviti, makamu wenyeviti na wajumbe wa kutosha ili kuziwezesha Taasisi hizi kufanya vikao vya kusikiliza na kuhitimisha kesi za kodi zaidi ya kimoja kwa wakati mmoja. Kadhalika, naishauri Serikali iongeze

bajeti na kutoa pesa za kutosha kwa ajili ya kuziwezesha Taasisi hizi kufanya shughuli zao kwa wakati na kwa ufanisi. Hatua hizi zitasaidia kupunguza mlundikano wa kesi za kodi zilizokaa muda mrefu bila kuhitimishwa.

b) Mapungufu katika ufuatiliaji wa madeni ya kodi na makadirio ya kodi yaliyotolewa kwa walipa kodi.

Mamlaka ya mapato ina kiasi kikubwa cha kodi ambacho hakijakusanywa kwa muda mrefu kutoka kwa walipa kodi mbalimbali. Mapitio yangu yalibaini kuwa kiasi hiki hakijakusanywa kutokana na ufuatiliaji hafifu wa Mamlaka kwa walipa kodi, kukosa taarifa za kutosha kuhusu biashara za walipa kodi, mamlaka kushindwa kutumia nguvu yake ya kisheria iliyopewa kupitia kifungu na.61 (1-3) cha sheria ya usimamizi wa kodi ya mwaka 2015, ambacho kimempa mamlaka Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kuchukua mali za mlipa kodi ili kukomboa kiasi cha kodi ambacho mlipa kodi anadaiwa. Kwa maoni yangu, iwapo jitihada za kutosha na hatua madhubuti zingechukuliwa na Mamlaka kwa wakati, malimbikizo haya ya kodi yangekusanywa na kuongeza mapato ya mwaka huu wa fedha.

Naishauri Serikali iongeze jitihada katika ukusanyaji wa kodi ambazo hazijalipwa na walipa kodi. Jambo hili linaweza kufanikiwa kwa kuboresha na kukiongezea uwezo kitengo cha ukusanyaji wa madeni na mikakati ya kuhakikisha kuwa kodi zote zinakusanywa kwa wakati baada ya kufanyiwa makadirio au uthamini hivyo kuzuia ulimbikizaji wa kodi.

c) Mapungufu katika ukaguzi wa kodi na ukadiriaji kodi.

Mapitio yangu katika ukaguzi wa kodi na ukadiriaji wa kodi nilibaini maeneo mbali mbali ambayo kodi ilikusanywa pungufu au haikusanywa kabisa kwasababu ya kukosekana kwa ufanisi wakati wa kupitia taarifa za hesabu na nyaraka nyingine za walipa kodi ili kupata uhakika iwapo taarifa hizo zinatoa na kuonesha uhalisia wa biashara na kipato cha walipa kodi husika. Hali hii ilichangiwa na uchambuzi hafifu wa taarifa za fedha zilizowasilishwa na walipakodi hivyo kupelekea makadirio ya biashara kuwa madogo. Swala hili

limechangiwa na uwezo mdogo kwa baadhi ya wafanyakazi wa Mamlaka wakati wanatekeleza majukumu yao ya ukaguzi na ukadiriaji wa kodi.

Naishauri Serikali iwaongeze uwezo na ujuzi wafanyakazi wote wanaohusika na ukaguzi wa kodi na ukadiriaji wa kodi kupitia mafunzo mbalimbali yatakayowawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na hivyo kuongeza mapato ya Serikali.

d) Ufanisi mdogo katika ukusanyaji wa mapato ya serikali.

Katika ukaguzi wangu niliangalia pia ufanisi na jitihada za Mamlaka ya Mapato katika kuhakikisha kuwa kodi kutoka vyanzo vyote na mapato ya serikali inakusanywa, nilibaini upungufu katika ukusanyaji wa mapato, ambapo baadhi ya mapato ya serikali yaliachwa bila kukusanywa. Moja kati ya vyanzo vya mapato ambavyo nilibaini kuna upungufu mkubwa kwenye makusanyo ni tozo za viwanja vya ndege na bandari zinazokusanywa na mashirika ya ndege na vyombo vya baharini kutoka kwa abiria wanaosafiri. Mapitio yangu yalibaini kuwa Mamlaka ya Mapato haikuwa na taarifa za kutosha na zilizokamilika kutoka kwa mashirika ya ndege na vyombo vya majini ambazo ni za muhimu kwa ajili ya kujua kiasi cha kodi (tozo) kinachotakiwa kukusanywa kutoka kwa mashirika ya ndege na vyombo vya baharini.

Naishauri Serikali iongeze na kuimarisha udhibiti katika ukusanyaji wa mapato ya tozo za viwanja vya ndege na bandari na kuhakikisha mapato hayo yanakusanywa, kuzuia na kudhibiti mianya yote inayoweza kusababisha upotevu wa mapato ya Serikali.

e) Uhakiki na usimamizi usioridhisha wa udhibiti wa mifumo ya uagizaji na uingizwaji wa bidhaa na mafuta yaliyonunuliwa kutoka nchi nyingine, na bidhaa zinazopita nchini kwa ajili ya kusafirishwa kwenda nchi nyingine, pia imekuwa ni sababu ambayo inapelekea upotevu wa mapato ya Serikali.

Naishauri serikali kuendelea kuimarisha ukaguzi na udhibiti wa bidhaa katika ukusanyaji wa kodi na ushughulikiaji wa bidhaa zinazoingizwa nchini kutoka nchi nyingine kwa ajili kutumika hapa

nchini na kuzuia bidhaa zinazopaswa kusafirishwa kwenda nje ya nchi zisitumike nchini bila kulipia kodi stahiki.

f) Usimamizi usioridhisha wa bidhaa zilizokaa katika maghala ya kulipiwa ushuru wa forodha na bandari kavu.

Nilibaini kuwa bidhaa zinazoingizwa nchini kutoka nchi nyingine zinakaa kwa muda mrefu katika maghala ya forodha na bandari kavu bila kulipiwa kodi, swala ambalo ni kinyume na sheria. Pia mapungufu ya mfumo wa kulipia kodi wa TANCIS yamepelekea Mamlaka kushindwa kukusanya kodi, hii imetokea kwa bidhaa zinazoingizwa nchini kupitia mipakani kutoka bandari ya Mombasa kwenda kwenye maghala ya forodha ambazo zilisafirishwa na malori ya kigeni ambayo yalikuwa hayajasajiliwa katika mfumo wa TANCIS. Hivyo bidhaa hizi hazikuweza kuingizwa kwenye mfumo wa TANCIS kwa ajili ya kukadiriwa na kukusanya kodi.

Nashauri Serikali kurekebisha mapungufu kwa kukusanya kodi zote katika bidhaa zilizo katika maghala ya ushuru wa forodha na bandari kavu na kurekebisha kasoro zilizobainika katika mfumo wa TANCIS ili uweze kufanya ukadiriaji wa kodi zote za bidhaa zinazoingizwa kwenye maghala ya forodha na bandari kavu na kuhakikisha kuwa mapato yote ya Serikali yanakusanywa kwa wakati.

5.1.6 Masuala maalum yaliyoonekana katika ukaguzi wa mwaka 2017/18

Sehemu hii inatoa taarifa ya maeneo makuu manne ambayo yanahitaji usimamizi na uangalifu wa karibu ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato. Maeneo hayo ni: Usimamizi wa mapingamizi ya Kodi, Usimamizi wa Misamaha ya Kodi, Usimamizi wa Makusanyo ya Kodi, na Tozo na ada zinazokusanywa na Mamlaka kwa niaba ya taasisi nyingine.

5.1.6.1 Usimamizi wa Mappingamizi ya kodi.

a) Kodi zilizoshikiliwa katika kesi za muda mrefu kwenye Mamlaka Za Rufaa za Kodi

Katika ukaguzi wangu wa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2018, nilibaini kwamba, Mamlaka ya Mapato ina kesi zilizo katika Bodi ya Rufaa za Kodi, Baraza la Rufaa za Kodi na Mahakama ya Rufaa kwa muda mrefu zenye jumla ya kodi ya Shilingi trilioni 382.6 ambapo, kiasi cha Shilingi trilioni 382 (asilimia 99.84) kimekwama katika Bodi ya Rufaa za Kodi, Shilingi bilioni 65.995 (asilimia 0.02) kimekwama katika Baraza la Rufaa za Kodi, na kiasi kilichobaki cha Shilingi bilioni 548.31 (asilimia 0.14) kinasubiri maamuzi katika Mahakama ya Rufaa Tanzania.

Ongezeko hili kubwa la kesi za kodi limetokana na uelewa zaidi wa walipakodi na jamii kwa ujumla kuhusu uwepo wa mamlaka za rufaa za kodi na mabadiliko ya taratibu za Bodi ya Rufaa za Kodi ya mwaka 2018 ambazo zimerahisisha namna ya kushughulikia mappingamizi ya kodi. Aidha, kati ya jumla ya kesi za kodi zilizopo katika Bodi ya Rufaa ya Kodi ya shilingi trilioni 382, kuna kesi nne zenye jumla ya kodi ya shilingi trilioni 374.7 sawa na asilimia 98.08 zinahusu kampuni ya uchimbaji madini ya ACACIA. Ikilinganishwa na mwaka wa fedha uliopita (2016/17), mapato yaliyokwama katika Mamlaka za Rufaa za Kodi yameongezeka kwa Shilingi trilioni 378.2 (sawa na asilimia 85) kutoka kesi 709 zenye kodi yenye thamani ya Shilingi trilioni 4.4 kwa mwaka 2016/17 hadi kufikia kesi 817 zenye kodi yenye thamani ya Shilingi trilioni 382.6 kwa mwaka 2017/18.

Uchambuzi wangu umeonesha kuwa mapato yaliyokwama katika Mamlaka za Rufaa za Kodi ni asilimia 1,206 ya bajeti ya mwaka 2017/2018 na ni asilimia 317.9 ya pato la ndani la Taifa (GDP) kwa mwaka 2017/2018, kiwango ambacho ni cha juu sana.

Naishauri Serikali iboreshe na kuimarisha utendaji wa mfumo mzima wa mamlaka za rufaa za kodi katika kuendesha kesi za rufaa za kodi kwa kuhakikisha kuwa inatenga na kutoa fedha za kutosha, na wakati wote mamlaka hizi zinakua na viongozi na wajumbe wa kutosha ili

ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi hivyo kusikiliza na kuhitimisha kesi za kodi kwa wakati.

b) Mapungufu katika kushughulikia mapingamizi ya kodi

Katika ukaguzi wangu wa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2017/18, nilibaini kuwa jumla ya mapingamizi ya kodi mia moja arobaini na nne (144) kutoka kwa walipa kodi yenye thamani ya Shilingi 77,857,964,376.52 yaliyowasilishwa katika Idara ya Walipakodi Wakubwa na Idara ya Kodi za Ndani yalikuwa hayajashughulikiwa kwa muda mrefu. Swala huli ni kinyume na taratibu za Mamlaka za utoaji huduma ambazo zinahitaji mapingamizi madogo (yasio na utata) kumalizwa ndani ya miezi mitatu na mapingamizi makubwa (yenye utata) kumalizwa ndani ya miezi 6. Mapingamizi haya yalikuwa hayajashughulikiwa na kumalizwa kwa kipindi kati ya miezi 5 hadi miezi 89 tangu tarehe ya kupokelewa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka. Ucheleweshwaji wa kushughulikia mapingamizi ya kodi una madhara katika kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato ya serikali kwani mapingamizi haya yanashikilia kiasi kikubwa cha kodi.

Kadhalika, nilibaini kuwa Mamlaka ilipokea mapingamizi ya kodi yasiyokidhi vigezo vya kisheria kuhusu mapingamizi hayo. Nilibaini mapingamizi ya kodi yenye kodi ya jumla ya shilingi 863,565,515.07 ambayo yaliwasilishwa na kupokelewa katika mkoa wa kikodi wa Arusha wakati muda wa kuwasilisha mapingamizi hayo ulikuwa umekwishapita, na hakukuwa na kibali kutoka kwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka cha kuongezewa muda wa kuwasilisha mapingamizi hayo.

Kuwapo kwa mapingamizi mengi ya kodi ambayo hayashughulikiwi kwa wakati na kutolewa maamuzi, kunachangiwa na uwezo na ufanisi hafifu wa kitengo cha ukaguzi wa kodi na kitengo cha ufundi katika Mamlaka ya Mapato. Pia swala hili limesababishwa na upungufu wa wafanyakazi kwa ajili ya kushughulikia mapingamizi ya kodi wakati idadi ya mapingamizi yanayoletwa na walipa kodi ni kubwa.

Ninaishauri Serikali:

- a) Kuongeza ufanisi katika kushughulikia kesi za mapingamizi ya kodi yanayoletwa na walipa kodi ili kuyamaliza mapingamizi*

yaliyokaa kwa muda mrefu. Hili linawezekana kwa kuongeza idadi ya watumishi wenye uzoefu na ujuzi pamoja na kuwaongezea mafunzo watumishi wote walio katika kitengo cha Huduma za Kiufundi na Kitengo cha Ukaguzi wa Kodi ili kuboresha utoaji wa tathmini za kodi.

- b) *Kuhakikisha kuwa Mamlaka ya Mapato inafanya uhakiki wa kutosha wa mapingamizi ya kodi yanayowasilishwa na walipa kodi ili kujiridhisha iwapo yanakidhi vigezo vya sheria ya usimamizi wa kodi (Tax Administration Act) kabla ya kuyashughulikia. Sheria hii inataka pamoja na mambo mengine, mapingamizi yote ya kodi yawasilishwe kwa Kamishna wa Mamlaka ndani ya siku thelathini tangu tarehe ambayo maamuzi ya kodi yalifanyika.*

5.1.6.2 Usimamizi na ufuatiliaji usioridhisha wa makusanyo ya madeni ya kodi

Mapitio ya rejista zinazohifadhi taarifa za kodi ambazo hazijalipwa, majedwali ya madeni ya kodi, taarifa za uchunguzi wa kodi zilizokamilika, ritani za kodi za VAT, majalada ya makosa ya walipa kodi pamoja na nyaraka mbalimbali, nimebaini kuwa kodi ya Shilingi 119,604,133,635 haikukusanywa kutoka kwa walipa kodi. Katika kiasi hicho, jumla ya Shilingi 37,764,033,242.06 kinahusiana na Idara ya Walipakodi Wakubwa na kiasi cha Shilingi 81,840,100,393.10 kinahusiana na Idara ya Kodi za Ndani, kama ifuatavyo;

- a) **Kodi ya Ongezeko la thamani (VAT) ambayo haikulipwa Sh.4,417,426,199.94**

Nilipitia walipa kodi 15 waliosajiliwa katika kodi ya ongezeko la thamani (VAT) katika Idara ya Walipakodi wakubwa waliwasilisha ritani zao kwa Kamishna wa Mamlaka ili kujiridhisha iwapo walilipa kodi stahiki. Hata hivyo, nilibaini kuwa walipa kodi wanne (4) hawakulipa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) ya jumla shilingi 4,417,426,199.94 wakati wa kuwasilisha ritani zao kwa Kamishna wa Mamlaka. Jambo hili ni kinyume na kifungu na. (67) (3) cha sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya mwaka 2014 ambayo inataka tofauti

chanya ya Kodi ya Ongezeko la thamani kulipwa wakati wa kuwasilisha ritani za VAT.

b) Madeni ya kodi ya muda mrefu ambayo hayajakusanywa Sh.114,463,396,095.22

Mapitio yangu katika taarifa za madeni ya kodi, majalada ya walipa kodi na majedwali ya madeni ya walipa kodi nilibaini kuwa kodi ya shilingi Sh.114,463,396,095.22 haikukusanywa na mamlaka kutoka kwa walipa kodi. Kati ya kiasi hicho, jumla ya Shilingi.33,346,607,042.12 kinahusiana na Idara ya Walipa kodi Wakubwa na Kiasi cha Shilingi 81,116,789,053.10 kinahusiana na Idara ya Kodi za Ndani. Baadhi ya kodi hizi hazijakusanywa tangu mwaka 2007.

c) Tozo za adhabu kutokana na makosa ya walipa kodi ambazo hazikukusanywa Sh.723,311,340

Baada ya kupitia rejista na majalada ya makosa ya walipa kodi na taarifa za malipo ya kodi za wateja nilibaini tozo za jumla ya shilingi 948,771,000 ambazo mamlaka iliwatoza walipa kodi mbalimbali kutokana na kutotumia mashine na risiti za kielektroniki (EFD). Hata hivyo, mamlaka iliweza kukusanya kiasi cha Shilingi 208,959,660, hivyo kiasi kilichosalia cha Shilingi 723,311,340 hakikukusanywa.

Naishauri Serikali iongeze jitihada na kuboresha mikakati katika usimamizi, ufuatiliaji na ukusanyaji wa madeni na kuhakikisha kuwa kodi zote na tozo zinakusanywa kwa wakati. Pamoja na mambo mengine, serikali inaweza kufanya makubaliano na walipa kodi ili malipo yafanyike kwa awamu na kutumia vizuri msamaha uliotolewa na Serikali kuhusu riba na adhabu za kodi. Maboresho haya yataepusha malimbikizo ya kodi zilizokaa muda mrefu bila kukusanywa.

5.1.6.3 Mapungufu katika ukaguzi wa kodi na ukadiriaji wa kodi

Baada ya kupitia majalada ya ukaguzi wa taarifa za walipa kodi, taarifa za hesabu za walipa kodi, uchambuzi wa ritani za VAT, taarifa za ukaguzi wa kodi, ritani za mapato na taarifa nyingine za walipa kodi, nilibaini makusanyo pungufu ya kodi ya jumla ya shilingi

46,548,934,370.70. Makusanyo haya pungufu yalisababishwa na mawasilisho pungufu ya kodi ya makampuni na kodi ya ongezeko la thamani (VAT) na kodi ya zuio ambayo haikukusanywa, ambazo zilikuwa na jumla ya shilingi TZS. 8,560,828,433.98 kutoka makampuni manne yaliyo chini ya Idara ya Walipakodi Wakubwa, na mawasilisho pungufu ya mapato ya jumla ya shilingi Sh.37,988,105,936.72 katika ritani zilizowasilishwa na walipa kodi katika idara ya kodi za ndani. Ukusanyaji huu pungufu ulichangiwa na kukosekana kwa ufanisi katika ukaguzi wa taarifa za hesabu za walipa kodi, ritani za mapato na taarifa nyingine zilizowasilishwa na walipa kodi ili kujiridhisha iwapo taarifa hizo zinaonyesha uhalisia wa biashara na kipato cha walipa kodi.

Kadhalika, nilipitia taarifa za walipa kodi 71 katika mfumo wa kodi wa ITAX katika idara ya walipa kodi wakubwa na kubaini kuwa kodi ya mapato (PAYE) na tozo ya maendeleo ya ujuzi (SDL) ya walipa kodi 30 haikuwasilishwa Mamlaka ya Mapato kwa kipindi cha jumla ya miezi 149. Pia kodi ya mapato (PAYE), tozo ya maendeleo ya ujuzi (SDL) na kodi ya zuio yenye jumla ya shilingi 1,951,215,244.93 haikuwasilishwa Mamlaka ya Mapato na walipa kodi wa Idara ya Kodi za Ndani. Mapungufu haya yalisababishwa na ufanisi mdogo katika ukaguzi wa taarifa za walipa kodi na kukosekana kwa ufuatiliaji wa malipo ya kodi za mapato, tozo za maendeleo ya huduma na kodi ya zuio kutoka kwa walipa kodi, ambao umeathiri malengo ya kukusanya kodi na unaweza kusababisha upotevu wa mapato ya Serikali.

Naishauri serikali

- a) *Kuongeza ufanisi katika ukaguzi na uhakiki wa taarifa za hesabu za walipa kodi, uchambuzi wa ritani za VAT, ritani za mapato na taarifa nyingine za walipa kodi ili kupata hali halisi ya biashara na kipato cha walipa kodi. Pia, hatua stahiki za kisheria zichukuliwe dhidi ya walipa kodi wanaowasilisha taarifa za udanganyifu ili kukwepa kodi.*
- b) *Kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara kwa walipa kodi ili kuhakikisha kwamba kodi ya mapato (PAYE), tozo ya maendeleo ya ujuzi (SDL) na kodi ya zuio (withholding tax) inawasilishwa Mamlaka ya Mapato kwa wakati.*

5.1.6.4 Ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya serikali

Nilifanya ukaguzi katika ukusanyaji wa mapato yanayotokana na tozo za viwanja vya ndege na bandari zinazokusanywa na mashirika ya ndege na vyombo vya baharini kutoka kwa abiria wanaosafiri na kubaini mapato ya kiasi cha jumla ya shilingi 1,845,250,227 na Dola za Kimarekani 2,747,249 hayakuwasilishwa Mamlaka ya Mapato kutoka mashirika ya ndege 19, Mamlaka ya Viwanja vya ndege (Arusha) na Kampuni ya huduma za meli. Kutokukusanywa kwa mapato haya kulisababishwa na baadhi ya walipa kodi kutoa taarifa pungufu na wengine kutokutoa taarifa kabisa kuhusu tozo za jumla ya shilingi TZS.1,093,132,705 na Dola za Kimarekani 2,746,634 kutoka mashirika ya ndege, makusanyo pungufu ya shilingi 719,534,022 kutoka Mamlaka ya Viwanja vya ndege na makusanyo ambayo hayakuwasilishwa na Kampuni ya huduma za meli ya shilingi 32,583,500 na Dola za Kimarekani 615. Ukaguzi wangu ulibaini kuwa hali hii ilisababishwa na Mamlaka ya Mapato kukosa taarifa zilizokamilika na sahihi kuhusu idadi ya abiria waliosafiri kutoka kila kiwanja cha ndege na bandari, na kwa kila kampuni; na hakukuwa na ulinganifu wa taarifa za abiria kati ya Mamlaka ya Viwanja vya ndege, kampuni za huduma za meli na Mamlaka ya Mapato (TRA).

Kadhalika, nilibaini kuwa nyaraka za msingi ili kuthibisha malipo ya tozo za viwanja vya ndege yenye jumla ya Dola za Kimarekani 21,048,320 na Sh.19,600,000 zilikosekana, hivyo sikuweza kuthibitisha na kujiridhisha kuhusu usahihi na ukamilifu wa mapato yaliyopelekwa Mamlaka ya Mapato kutoka makampuni ya ndege na kampuni ya huduma za meli. Kwa upande mwingine nilibaini tofauti ya taarifa za mapato kati ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) na makampuni ya ndege.

Pia, nilibaini kukosekana kwa taarifa za abiria wanaosafiri kutoka viwanja vinavyomilikiwa na makampuni binafsi. Kwa mfano, nilibaini viwanja vya ndege nane (8) vyenye umiliki binafsi katika hifadhi ya wanyamapori ya Serengeti, hata hivyo, hakukuwa na taarifa zozote zilizowasilishwa Mamlaka ya Mapato na wamiliki wa viwanja hivyo kuhusu ukusanyaji wa tozo za huduma ya viwanja vya ndege. Pia, katika mkoa wa Kagera, nilibaini jumla ya abiria 56,379 walisafiri

kutoka bandari za Bukoba na Kemondo bila kulipa tozo. Vile vile kulikuwa na bandari na vyombo kadhaa vya usafiri wa majini vilivyosajiliwa na vilikuwa vikifanya safari zake ndani ya ziwa Victoria bila kukusanya tozo hizi.

Naishauri Serikali

- a) *Kuimarisha uhibititi katika taratibu za tozo za huduma za viwanja vya ndege na huduma za bandari kwa abiria wanaosafiri ili kuhakikisha kuwa taarifa sahihi zinapatikana, na mapato yanayowasilishwa yanaambatanishwa na idadi sahihi ya abiria waliosafiri ili kuzuia uwasilishwaji wa makusanyo pungufu kutoka kwa walipa kodi.*
- b) *Kuhakikisha kuwa usuluhishi na ulinganifu wa taarifa za abiria na mapato kulingana na taarifa za Mamlaka ya Viwanja vya ndege (TAA) na Mamlaka ya Bandari, dhidi ya taarifa za mapato zilizowasilishwa Mamlaka ya Mapato na kampuni za ndege na kampuni za meli.*
- c) *Kuhakikisha kuwa makampuni ya ndege na meli wanawasilisha ritani za mapato katika Mamlaka ya Mapato, zikionyesha idadi na taarifa za abiria waliosafiri na makampuni hayo kutoka viwanja vya ndege, viwanja vyenye umiliki binafsi na bandari zote.*
- d) *Ipitie na kufanya uhakiki maalumu katika eneo hili la tozo za huduma za viwanja vya ndege na bandari ili kubaini na kudhibititi viashiria hasi vinavyoweza kuathiri ukusanyaji wa mapato.*

5.1.6.5 Ufuatiliaji na usimamizi usioridhisha wa Misamaha ya Kodi

Serikali, kwa kupitia Mamlaka ya Mapato, ilitoa misamaha ya kodi kwa ajili ya shughuli maalum zilizoainishwa katika sheria za kodi mbalimbali kama vile uwekezaji katika bidhaa za mtaji kwa kipindi maalum ili kuvutia uwekezaji kutoka nje ya nchi. Vilevile na kukuza sera maalum za kiuchumi kama vile kuhamasisha uwekezaji katika sekta maalum, kuendeleza uhusiano na mataifa mengine kwa kutoa

misamaha kwa shughuli za kidiplomasia na kwa sababu za kibinadamu.

Taarifa za Fedha za Mamlaka ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2017/18 zinaonesha misamaha ya kodi yenye jumla ya Shilingi bilioni 1,215.6 ikiwa ni ongezeko la Shilingi bilioni 178 (asilimia 17.2) ikilinganishwa na misamaha ya kodi iliyotolewa mwaka 2016/17 ambayo ilikuwa na thamani ya Shilingi bilioni 1,037.6. Ongezeko hili ni kubwa kwani ni asilimia moja (1) ya pato la ndani la taifa (GDP) kwa mwaka 2017/18 ikilinganishwa na malengo ya Serikali ya kupunguza misamaha ya kodi kuwa chini ya asilimia moja ya pato la ndani la taifa (GDP). Mwenendo wa misamaha ya kodi iliyotolewa kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita imeoneshwa katika jedwali hapo chini.

Jedwali Na. 23: Mwenendo wa Misamaha ya Kodi kuanzia mwaka 2013/14-2017/18 (Shilingi kwa mamilioni)

Mwaka wa Fedha	Pato la taifa la Mwaka (TZS)	Jumla ya misamaha ya kodi (TZS)	Asilimia ya misamaha ya kodi ikilinganishwa na pato la ndani la Taifa
2013/14	55,619,077	1,834,097	3.3
2014/15	84,279,922	1,627,012	1.9
2015/16	97,304,216	1,100,337	1.1
2016/17	106,866,941	1,037,643	1
2017/18	120,355,007	1,215,576	1

Chanzo: Taarifa za Mapato za Mamlaka ya Mapato, takwimu na uchambuzi wa wakaguzi, 2013/14-2017/18

Kutokana na mchanganuo wa hapo juu, kwa wastani misamaha ya kodi kwa asilimia ya Pato la Ndani la Taifa (GDP) kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita ni asilimia 1.7 ya Pato la Ndani la Taifa, kiwango hicho ni kikubwa kikilinganishwa na lengo la chini ya asilimia moja (1) ya pato la Ndani la Taifa (Rejea bajeti kuu ya Serikali ya mwaka 2013/14).

Ninashauri serikali kuendelea kuboresha udhibiti na kuwa na mikakati na juhudi za makusudi zitakazoweza kupunguza misamaha ya kodi hadi kufikia chini ya asilimia moja ya pato la ndani la taifa hivyo kuongeza ukusanyaji wa mapato ya serikali.

5.1.6.6 Magari yenye msamaha wa kodi yaliyouzwa na wanufaika bila kulipia kodi Sh. 114,524,502

Nilipitia taarifa za mfumo wa TANCIS na majalada ya walipakodi katika ofisi za forodha za mkoa wa Arusha kuhusu miamala ya ulipaji kodi za magari yenye msamaha wa kodi ambayo umiliki wake umehamishwa kwenda kwa watu wengine wasiowanufaika na misamaha ya kodi. Ukaguzi wangu ulibaini kodi ya shilingi 114,524,502 ambayo haikukusanywa katika magari 29 yenye msamaha wa kodi yaliyouzwa na wanufaika. Jambo hili ni kinyume na kifungu na 119 (1) cha sheria ya forodha ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004 kinachotaka bidhaa zote zilizoingizwa nchini kwa msamaha wa kodi, zilipiwe ushuru wa forodha iwapo umiliki wake utabadilishwa au bidhaa kuuzwa kwa mtu mwingine asiye mnufaika. Aidha, nilibaini kuwa baadhi ya magari haya yalianza kumilikiwa na watu wasio wanufaika wakati kodi ya magari hayo ilikuwa bado haijalipwa kwa Mamlaka ya Mapato kwa zaidi ya miaka miwili.

Kadhalika, ukaguzi wa nyaraka katika majalada, uliojumuisha mikataba ya mauziano baina ya wanufaika wa misamaha na wanunuzi wa magari yenye msamaha wa kodi, nilibaini kuwa magari 36 yenye jumla ya ushuru wa forodha wa shilingi 229,934,730 yalikabidhiwa kwa wanunuzi baada ya malipo kwa muuzaji, lakini kabla ya malipo ya ushuru wa forodha kwa Mamlaka ya Mapato. Wanunuzi waliendelea kutumia magari hayo ya msamaha wa kodi kwa muda mrefu bila kulipia kodi kwa wakati, badala yake walikaa muda mrefu ndipo wakaenda Mamlaka ya Mapato kwa muda wao kufanyiwa ukadiriaji na kulipa kodi husika.

Nashauri

- a) Serikali iboreshe udhibiti, usimamizi na ufuatiliaji wa karibu wa misamaha ya kodi kwenye magari ili kuzuia matumizi mabaya ya misamaha hiyo ikiwemo uuzaji wa magari hayo bila kulipia kodi stahiki na kwa wakati.
- b) Serikali ikusanye kodi ya jumla ya shilingi 114,524,502 kutoka kwenye magari ya misamaha yaliyouzwa na wanufaika, pamoja

na tozo za adhabu na riba kwa kushindwa kuzingatia sheria ya forodha ya Afrika Mashariki.

5.1.6.7 Tathmini ya mifumo ya udhibiti wa misamaha ya kodi za mafuta yaliyonunuliwa kutoka nje ya nchi kwa ajili ya matumizi ya uchimbaji wa madini

Katika uchambuzi wangu wa nyaraka za matumizi ya mafuta yaliyopewa misamaha ya kodi katika kampuni za uchimbaji wa madini ya dhahabu za Buzwagi, North Mara na Geita niligundua mafuta ya dezeli yenye jumla ya lita katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2017 hadi Juni 2018 yalikuwa yametolewa kwenda kwa wakandarasi na watu wengine ambao sio wanufaika wa misamaha ya kodi. Jumla ya thamani ya mafuta yaliyopewa misamaha ya kodi kwa wakandarasi na watu ambao sio wanufaika ilikuwa ni Shilingi 401,332,896. Utolewaji wa mafuta kwenda kwa wakandarasi na watu ambao hawastahili kunufaika na misamaha ya kodi ni kinyume na matakwa ya Agizo la Serikali Namba 190 na 191 (GN) la mwaka 2011 ambalo linazuia kutolewa kwa mafuta yenye msamaha wa kodi kwenda kwa makampuni na watu ambao hawastahili kunufaika na msamaha huo.

Nashauri Serikali;

- a) *Ihakikishe inakusanya kodi yenye jumla ya Shilingi 401,332,896 kwenye mafuta ya msamaha wa kodi ambayo yalitolewa kwenda kwa makampuni na watu wengine ambao sio wanufaika wa msamaha wa kodi.*
- b) *Kufanya Ukaguzi na uchunguzi wa kila mara kwa wanufaika wa misamaha ya kodi ili kuhakikisha kuwa wanufaika na makampuni yanatii sheria na kanuni za misahama ya kodi; hivyo kuepuka hasara inayoweza kutokea kwa kutumia vibaya misahama hii ya kodi*

5.1.6.8 Tathmini ya mifumo ya udhibiti wa misamaha ya kodi kwenye mafuta yaliyotumiwa na wawekezaji

Katika ukaguzi wangu wa mafuta yenye msamaha wa kodi kwa ajili ya matumizi ya wawekezaji nchini, nilibaini kuwa kiasi cha lita 1,713,526 za mafuta yenye kodi ya jumla ya shilingi TZS.1,041,823,808

kilichopokelewa na kutumika katika makampuni ya BAM International Ltd na Kilombero Plantation Ltd kilikosa udhibiti na usimamizi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Hali hii ilitokea wakati Mamlaka ya Mapato ilikuwa ikisitisha kufanya udhibiti na usimamizi wa mafuta kipindi ambacho Matangazo ya Serikali (GN) yalikuwa yameisha muda wake, hivyo Mamlaka haikuwa na taarifa wala nyaraka zozote zilizohusu mafuta ya msamaha ambayo yalipelekwa na kutumika kwa wawekezaji baada ya Tangazo la Serikali kuisha muda wake. Hata hivyo, serikali ilitoa matangazo mengine mapya (GN) ambayo yalijumuisha kipindi cha nyuma siku ambayo matangazo yaliyopita yaliisha lakini kabla ya kutolewa matangazo mapya (retrospectively). Hivyo, maombi ya kurejeshewa kodi ya mafuta ya msamaha kutoka kwa wawekezaji yalijumuisha mafuta yaliyonunuliwa na kutumiwa katika kipindi ambacho Mamlaka ya Mapato ilisitisha kufanya udhibiti na usimamizi wa mafuta.

Kadhalika, nilibaini kuwa Kampuni ya Kilombero Plantation Limited (KPL) ilipewa msamaha wa kodi kwenye mafuta bila kuwa na tangazo la Serikali (GN). Katika ukaguzi wangu nilibaini kuwa kampuni hiyo ilipewa kibali cha muda kupitia barua yenye kumbukumbu na.CAB.286/547/01 ya 13 Novemba 2015 kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kununua na kutumia kiasi cha lita 1,065,989 za mafuta ya dizeli wakati wakisubiri Tangazo la Serikali (GN) ambalo lingetolewa na Waziri wa Fedha na Mipango. Hata hivyo, hadi kipindi cha msamaha wa kodi kinakwisha tarehe 23 Septemba 2017, Tangazo hilo la Serikali lilikuwa halijatolewa na kampuni hiyo ilikuwa imeshatumia kiwango chote cha mafuta ya msamaha cha lita 1,065,989 na kuwasilisha madai ya marejesho ya kodi ya shilingi 648,121,312 katika Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Aidha, nilibaini kuwa hakukuwa na ushahidi wa nyaraka kuthibitisha matumizi ya mafuta yaliyotumika kudai marejesho ya kodi ya jumla ya shilingi 7,446,592,735 kutoka kampuni ya Kagera Sugar Limited kwa kipindi cha Januari 2013 hadi Juni 2017, wakati taarifa na nyaraka za mafuta yaliyotumika katika kampuni kwa kipindi cha mwaka 2012 na kipindi cha Januari hadi Februari 2018 hazikuwepo Mamlaka ya Mapato wala kwa Kampuni husika. Kampuni haikuonesha

namna ambavyo kiasi cha marejesho kilivyokokotolewa na kufikiwa kwani hakukuwa na taarifa za masaa/umbali na uwezo wa kutumia mafuta yaliyotumika wa kila mashine ili kuthibitisha kiwango cha mafuta yaliyotumika kwenye mashine hizo.

Pia, nyaraka na taarifa za mafuta yaliyotumika katika kampuni ya Kagera Sugar Limited hazikutofautisha kati ya kazi za upanuzi wa mradi na shughuli nyingine za kawaida. Swala hili ni kinyume na matakwa ya Tangazo la Serikali (GN) ambalo lilitaka mafuta ya msamaha yatumike tu kwenye shughuli za upanuzi wa mradi na sio kwenye shughuli nyingine za kawaida. Hivyo, hatukuweza kuthibitisha iwapo mafuta hayo yalitumika kwenye shughuli zilizokusudiwa au la.

Vile vile, nilibaini madai ya marejesho zaidi ya kiwango kilichopaswa kurejeshwa ya jumla ya shilingi 122,109,804.4 katika lira 214,982 za mafuta ambazo hazikutumika na makampuni mawili, yaani kampuni ya Kagera Sugar lira 63,022 zenye kodi ya Sh.35,796,496 na kampuni ya Mount Meru Millers Limited lira 151,960 zenye kodi ya Sh.86,313,308.4. Hali hii ilisababishwa na uhakiki dhaifu wa nyaraka za madai ya marejesho ya kodi zilizowasilishwa na makampuni haya ambayo yapo kwenye kundi la makampuni ya wawekezaji.

Nashauri;

- a) Serikali ihakikishe kuwa Matangazo ya Serikali yanatolewa kwa wakati ili kuzuia makampuni kutumia mafuta yenye misamaha ya kodi bila kuwa na kibali cha Tangazo la Serikali.
- b) Serikali ihakikishe kuwa utolewaji wa matangazo mapya ya serikali (renewals) kwa ajili ya msamaha wa kodi za mafuta yanayotumika na wawekezaji unafanyika kwa wakati ili kuepuka kukosekana kwa udhibiti kunakoweza kusababisha upotevu wa mapato ya serikali.
- c) Serikali ifanye uhakiki wa kutosha ili kujiridhisha na usahihi wa kiwango cha mafuta kinachowasilishwa na makampuni kwa ajili ya madai ya marejesho ya kodi kwa kuhakiki na kukokota kiwango cha mafuta kilichotumika kwa kuzingatia masaa yaliyotumika na uwezo wa kila mashine katika kutumia mafuta, kabla ya kufanya malipo.

- d) Serikali ifanye uhakiki wa kutosha katika misamaha ya kodi kwenye mafuta yanayotumika na wawekezaji na kuhakikisha kuwa ushahidi wa nyaraka unatunzwa kabla ya kutoa kibali cha malipo ya madai ya marejesho ya kodi
- e) Serikali ikomboe kiasi cha shilingi 122,109,804.40 cha marejesho ya kodi kilichorejeshwa kimakosa na Mamlaka ya Mapato kwa kampuni ya Kagera Sugar Limited na Mount Meru Millers Limited.

5.1.6.9 Udhibiti na usimamizi usioridhisha wa bidhaa zilizo kwenye maghala ya kulipiwa ushuru wa forodha na bidhaa zilizoruhusiwa kuingia ndani ya nchi kwa muda maalum

Ukaguzi na uhakiki uliofanyika katika maghala ya forodha ya Makao makuu ya Mamlaka, ofisi za forodha za mikoa na ofisi za forodha za mipakani ulibaini kuwa, bidhaa mbalimbali 1,129 katika maghala hayo zilikaa zaidi ya muda wa kisheria, ambapo baadhi ya bidhaa zilikaa kwenye maghala kwa zaidi ya miaka sita (6) zikisubiri taratibu na hatua za utoaji bidhaa zinazotakiwa kulipiwa ushuru wa forodha. Pia, nilibaini bidhaa 337 zenye kodi ya Shilingi 5,535,199,201.60 (ambazo kwa sehemu kubwa zilikuwa magari) katika maghala binafsi 99 ambazo zilikaa kwa kipindi cha zaidi ya miezi sita (6). Swala hili ni kinyume na kifungu namba 42(1) na namba 57(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya forodha ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004 ambavyo vinataka bidhaa zilizokaa kwenye maghala ya forodha ya Mamlaka (customs warehouses) wa zaidi ya siku 60 na zilizokaa kwenye maghala ya forodha ya binafsi (bonded warehouses) kwa zaidi ya miezi sita ziuzwe kwa njia ya mnada wa wazi au kwa njia yoyote ambayo Kamishna ataona inafaa.

Kuchelewa kufanya minada kwa bidhaa zilizokaa muda mrefu kunaweza kusababisha upotevu wa mapato ya Serikali kutokana na bidhaa hizo kuchakaa au kuharibika.

Kadhalika, nilibaini bidhaa zilizoingizwa nchini kwa ajili ya kwenda kwenye maghala ya forodha ya binafsi zenye Kodi ya Ongezeko la Thamani ya shilingi 5,517,966,092 ambazo hazikuingizwa kwenye

mfumo wa TANCIS na hivyo kushindwa kuzifanyia tathmini na ukadiriaji wa kodi katika ghala la forodha la A To Z textile mills, na hivyo kushindwa kukusanya kodi katika bidhaa hizo. Hali hii ilisababishwa na bidhaa zilizokuwa zinazoingizwa nchini kupitia mipakani kutoka bandari ya Mombasa kwenda kwenye ghala binafsi la forodha la kampuni ya A To Z textile mills ya Arusha kwa kutumia malori ya kigeni ambayo yalikuwa hayajasajiliwa katika mfumo wa TANCIS. Ni vema hatua za haraka zichukuliwe kurekebisha kasoro na mapungufu ya mfumo wa TANCIS ili kuhakikisha kuwa kodi za serikali zinakusanywa na mizigo hiyo inaondolewa katika maghala ya forodha.

Katika mapitio zaidi ya taarifa kutoka mfumo wa kodi za forodha wa Mamlaka (TANCIS) na rejista zinazohifadhi taarifa za magari (C32/C49) kutoka nje ya nchi na kuruhusiwa kuingia nchini kwa muda maalum katika mipaka kumi na moja (11), nilibaini magari 2,305 yaliyoingizwa kuanzia Julai 2017 hadi Juni 2018 lakini yalika Tanzania zaidi ya miezi mitatu bila kutoka nje ya Tanzania, na hapakuwa na kibali cha kuongezewa muda wa magari hayo kuendelea kukaa nchini. Mchanganuo wa magari hayo umeoneshwa kwenye jedwali hapa chini.

Jedwali Na. 24: Magari yaliyoingia nchini kwa muda maalum lakini hayakutoka nje ya Tanzania

Kwa mtazamo wangu, utaratibu wa kuwapo kwa bidhaa zilizokaa zaidi katika maghala ya kuhifadhi bidhaa zikisubiri kulipiwa ushuru wa forodha na magari yaliyokaa nchini zaidi ya muda ulioruhusiwa kunasababishwa na usimamizi usioridhisha wa bidhaa katika maghala ya forodha na magari yaliyoruhusiwa kuingia ndani ya nchi kwa muda maalum. Mapungufu haya ni kinyume na kanuni na. 137 za Sheria ya Usimamizi wa Kodi za forodha ya Afrika Mashariki ya mwaka 2006 ambazo zinataka magari yaliyoingizwa nchini kwa muda maalumu, kuondoka nchini ndani ya kipindi cha miezi mitatu, au kupata kibali maalumu kutoka Kamishna wa Mamkala kitakachoruhusu muda zaidi wa magari hayo kuendelea kubaki nchini. Mapungufu haya yanatoa mianya ya kukwepa kodi kwa wafanyabiasha wasio waaminifu kutumia vibaya utaratibu wa kuweka bidhaa kwenye maghala ya kulipia ushuru

na kuingiza magari kwa kipindi maalum, hivyo Serikali kushindwa kukukusanya kodi stahiki.

Naishauri Serikali:

- a) *Kuimarisha udhibiti katika bidhaa zinazowekwa kwenye maghala ya forodha ya Mamlaka na maghala ya forodha ya binafsi kwa kuhakikisha kuwa hatua stahiki zinachukuliwa kwa wakati, ikiwemo kufanya minada au kutoa misaada ili kuiondoa mizigo hiyo kwenye maghala ili kuzuia isiharibike na kupelekea kupoteza mapato ya serikali.*
- b) *Kuimarisha udhibiti na kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara kwenye magari yanayoingizwa nchini kwa muda maalumu, na kufanya uchunguzi kwenye swala hili ili kujiridhisha na kubaini iwapo magari haya yaliingizwa kwa matumizi ya ndani ya nchi bila kulipia kodi.*
- c) *Kufanya maboresho katika mfumo wa TANCIS ili uweze kufanya tathmini na ukadiriaji wa kodi kwa bidhaa zinazosafirishwa na magari yenye usajili wa nchi nyingine ili kurahisisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali.*

5.1.6.10 Udhibiti hafifu katika ukusanyaji wa kodi na usimamizi wa bidhaa zilizo katika bandari kavu (ICDs)

Baada ya kupitia taarifa za ukadiriaji kodi uliofanywa kupitia mfumo wa kodi za forodha wa TANCIS katika bandari kavu mbalimbali kwa bidhaa zilizoingizwa nchini kwa kipindi cha kuanzia Januari 2017 hadi Machi 2018, nilibaini makadirio ya kodi ya shilingi 4,734,719,220.80 yaliyofanywa na waingizaji wa bidhaa ambayo yalikuwa hayajalipwa kwa muda mrefu wa kati ya miezi 3 hadi 12. Kutokusanywa kwa kodi hizi kulichangiwa na ufuatiliaji dhaifu kwa waingizaji wa mizigo na mawakala kwa makadirio ya kodi ambayo yamekaa muda mrefu bila kulipwa.

Kadhalika, uhakiki wa mizigo iliyowekwa kwenye bandari kavu 13 na bandari kuu (TICTS na Mamlaka ya Bandari) nilibaini bidhaa katika makontena zaidi ya 286 zilizoharibika hivyo kutofaa kwa matumizi ya binadamu kwa mujibu wa vigezo vya Mamlaka ya Chakula na Dawa

(TFDA) na Shirika la Viwango Tanzania (TBS). Baadhi ya bidhaa hizi zilikuwa zimekaa kwenye bandari hizi tangu mwaka 2002.

Mahojiano yangu na uongozi wa bandari hizi ulibaini sababu mbalimbali zilizocheleweshwa kufanyika minada na bidhaa kushindwa kupata soko, hivyo kusababisha upotevu wa mapato ya Serikali; kati ya sababu hizo ni kushindwa kuchukua hatua kwa wakati na kutambua kwa wakati mizigo inayokaa bandarini kwa zaidi ya muda wa kisheria, kuchelewa kutoa idhini ya kuuza mizigo kwenye minada na upangaji wa bei kubwa kuliko hali halisi ya mizigo husika. Mchanganuo wa bidhaa zilizoharibika katika makontena umeoneshwa kwenye jedwali hapa chini.

Jedwali Na. 25: Makontena (makasha) yenye bidhaa zilizoharibika

Na	Bandari/ Bandari kavu	Idadi ya makontena
1	TICTS Terminal	29
2	ZAMBIA CARGO - ICD	9
3	UBUNGO- ICD	76
4	TRH -ICD	50
5	AMI -ICD	91
6	DICD	31
	Jumla	286

Chanzo: uchambuzi wa kikaguzi

Aidha, nilifanya uhakiki katika bandari kavu mbalimbali na kubaini kuwa zaidi ya makontena 2,537, magari 708 na mizigo mingine 450 ilikuwa haijaondolewa na waingizaji kwenye bandari hizo na kodi husika zilikuwa hazijalipwa tangu mwaka 2001 hadi wakati nafanya ukaguzi huu mwezi Mei 2018.

Jedwali Na. 26: Bidhaa/mizigo iliyokaa muda mrefu katika bandari, na bandari kavu bila kodi kukusanywa

Na	Bandari/ bandari kavu	Idadi ya makontena	Idadi ya magari	Mizigo mingine
1	TICTS	630		
2	ZAMBIA CARGO ICD	120	2	450 pcs of timber logs
3	AMI -ICD	331		
4	TPA	668	673	
5	DICD	270	11	
6	SSB	149	3	
7	PMM	38	3	
8	AFRICAN ICD	30		
9	JIEFANG	18		
10	ETC	2		
11	AMI-ICD	280	15	
12	AL HUSHOOM ICD	1	1	
	Jumla	2,537	708	450

Chanzo: uchambuzi wa kikaguzi

Nashauri serikali

- a) Ifanye ufuatiliaji kwa wakati kwa waagizaji au mawakala wa forodha ili kuhakikisha kuwa makadirio yote ya kodi yanalipwa kwa wakati, ikiwa ni pamoja na kukusanya kiasi cha shilingi 4,734,719,220.80 pamoja na tozo za adhabu au riba kwa mujibu wa matakwa ya kifungu na.249 cha Sheria ya forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004 (EACCM, 2004).
- b) Kuimarisha udhibiti katika bidhaa/mizigo inayowekwa kwenye maghala ya bandari kavu na bandari kuu kwa kuhakikisha kuwa hatua stahiki zinachukuliwa kwa wakati kuondoa mizigo hiyo kwa mujibu wa matakwa ya sheria.
- c) Kufanya minada kwa wakati na kwa bei zenye uhalisia ili kuuza mizigo yote iliyokaa muda mrefu bandarini na kwenye bandari kavu, na kuchukua hatua nyingine kwa mujibu wa sheria zitakazo wezesha kuondoa mizigo iliyokaa kwa muda mrefu kwenye maghala ya bandari hizi.

5.1.6.11 Mifumo isiyoridhisha ya udhibiti wa bidhaa zinazosafirishwa kwenda nchi nyingine na bidhaa zinazouzwa nje ya Tanzania.

a) Bidhaa ngumu na mafuta yanayopita nchini kwenda nchi nyingine (dry cargo and fuel)

Nilifanya ukaguzi katika bidhaa zinazoingizwa nchini kwa ajili ya kusafirishwa kwenda nchi nyingine kupitia katika mipaka ya Kabanga, Rusumo, Mutukula, Tunduma, Kasumulu, Namanga, Kilambo na Horohoro kuanzia mwezi julai 2017 hadi June 2018. Mizigo hii ilikuwa ikisafirishwa kutoka bandari ya Dar es Salaam na mipaka mingine ya Tanzania. Hata hivyo nilibaini kuwa mizigo yenye kodi ya jumla ya shilingi haikuondoka nchini kwenda nchi zilizokusudiwa. Wakati wa uhakiki wangu sikupata ushahidi wowote kwenye vitabu (registers) na mfumo wa TANCIS kuthibitisha kuwa bidhaa hizi zilitoka kwenda nchi zilizokusudiwa kupitia mipaka hiyo.

Kadhalika, ukaguzi wangu ulibaini upungufu wa udhibiti na usimamizi katika mizigo inayopita nchini kwenda nchi nyingine. Baadhi ya mapungufu niliyobaini ni pamoja na mizigo iliyokuwa inasafirishwa

kutoka bandari ya Dar es salaam na maeneo mengine ambayo mizigo iliingilia, kwenda mipakani bila kufuata taratibu za kiforodha. Kwa mfano; nilibaini miamala 286 ya mizigo ambayo ilisafirishwa kwenda mipakani bila kukamilisha taratibu za kuruhusiwa kutoka katika bandari ya Dar es salaam. Pia nilibaini mizigo 53 ambayo iliwekewa ving'amuzi vya kielektroniki vya kufuatilia mizigo lakini ving'amuzi hivyo vilikuwa havifanyi kazi. Ving'amuzi hivyo havikufanya kazi kwa sababu havikuwashwa wakati mizigo inaondoka katika bandari ya Dar es Salaam.

Pia, nilibaini kuwa miamala 1,871 ya mizigo na mafuta ilikamilishwa na mizigo na mafuta kusafirishwa kwenda nchi nyingine bila kuwa na amana au ilikuwa na amana pungufu kinyume na matakwa ya kanuni na.104 (3) za sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki za mwaka 2010. Kiasi kikubwa cha mizigo na mafuta hayo hayakuwa na uthibitisho kutoka mipakani kwamba ilivuka kwenda nchi husika, hivyo kuna uwezekano kuwa mizigo na mafuta hayo yailiuzwa nchini bila kulipiwa kodi stahiki.

b) Bidhaa ambazo zimeuzwa nje ya nchi (Export goods)

Taratibu za forodha zinataka bidhaa au mizigo isiondolewe kwenye eneo la forodha iwapo taratibu za kiforodha hazijakamilika na kodi husika hazijalipwa.

Nilipitia taarifa za mizigo inayosafirishwa kutoka nchini kwenda nchi nyingine katika mfumo wa kodi za forodha wa TANCIS katika mipaka ya Mtambaswala, Horohoro, Bandari za Mtwara na Tanga, na kubaini miamala 99 ya mizigo kwa kuanzia Julai 2017 hadi Juni 2018 yenye kodi ya ongezeko la thamani (VAT) ya shilingi 649,451,067.85 ambayo iliruhusiwa kwenda nje ya nchi bila kukamilisha taratibu za kiforodha. Jedwali hapo chini linaonyesha mchanganuo huo;

Jedwali Na. 27: Bidhaa ambazo zimeuzwa nje ya nchi (Export goods)

Na.	Mpaka	Mkoa	Aina ya Muamala	Idadi ya Miamala	Thamani ya kiforodha ya Mizigo (Shilingi)	Kodi ya ongezeko la thamani (VAT) (Shilingi)
1	Mtambaswala	Mtwara	EX1	7	31,053,049.05	5,589,548.83
2	Bandari ya Mtwara	Mtwara	EX1	16	647,036,460.16	116,466,562.83
3	Horohoro	Tanga	EX1	45	1,639,970,219.33	295,194,639.48

Na.	Mpaka	Mkoa	Aina ya Muamala	Idadi ya Miamala	Thamani ya kiforodha ya Mizigo (Shilingi)	Kodi ya ongezeko la thamani (VAT) (Shilingi)
4	Bandari ya Tanga	Tanga	EX1	31	1,290,001,759.50	232,200,316.71
			Jumla	99	3,608,061,488.04	649,451,067.85

Chanzo: uchambuzi wa kikaguzi

Kutokamilika kwa taratibu za kiforodha na kukosekana kwa mizigo hiyo wakati wa uhakiki katika mipaka husika kunaashiria kwamba huenda mizigo hiyo haikusafirishwa kwenda nje ya nchi, bali ilitumika nchini bila kulipa kodi ya ongezeko la thamani (VAT)

Nashauri;

- a) *Serikali iboreshe udhibiti wa mizigo inayosafirishwa kwenda nje ya nchi kwa kuhakikisha kuwa inazingatia taratibu za kiforodha za usafirishaji wa mizigo hiyo ili kuzuia isibaki kwa ajili ya matumizi ya ndani bila kulipia kodi.*
- b) *Serikali ikomboe kodi ya shilingi 57,748,315,692.68 kutoka kwenye bidhaa ambazo hazikusafirishwa kwenda nje ya nchi.*
- c) *Serikali ikomboe kodi ya ongezeko la thamani (VAT) ya shilingi 649,451,067.85 kutoka kwenye mizigo ambayo haikusafirishwa kwenda nje ya nchi, na kuboresha udhibiti wa mizigo inayotoka nchini kwenye nchi nyingine kwa kuhakikisha kuwa inazingatia taratibu zote za kiforodha.*

5.1.6.12 Udhibiti usioridhisha katika ukusanyaji wa kodi kwenye mafuta yaliyoingizwa kutoka nchini nyingine kwa ajili ya matumizi ya ndani ya nchi

Nilifanya ukaguzi wa taarifa za mafuta yaliyoingizwa kutoka nchi nyingine kwa ajili ya matumizi ya ndani ya nchi. Katika ukaguzi huo nilibaini mafuta yenye kodi ya jumla ya shilingi 4,772,815,004.75 yaliyoingizwa nchini na makampuni ya mafuta 20, ila yaliruhusiwa na Mamlaka ya Mapato kuchukuliwa na makampuni hayo kabla ya kukamilisha taratibu za kiforodha, na hakukuwa na ushahidi wa kuthibitisha kuwa kodi husika zilikusanywa. Miamala ya mafuta haya ilikuwa katika hatua mbalimbali za taratibu za kiforodha (kama vile, uhakiki wa nyaraka, ukaguzi wa mizigo, ulinganifu wa nyaraka za

kuingizia na kutolea mzigo). Aidha miamala mingine ilioneshwa kufutwa kwenye mfumo bila kuwepo sababu za kufuta miamala hiyo au kuwepo miamala mbadala iliyotumika kulipia kodi za mafuta hayo.

Kadhalika, katika ukaguzi huu nilibaini lita 1,898,502.18 za mafuta yenye kodi ya shilingi 2,519,765,899.69 yaliyoingizwa kwa ajili ya matumizi ya ndani, na yale yaliyobaki nchini kutoka kwenye mafuta yaliyokuwa yakisafirishwa kwenda nchi nyingine. Mafuta hayo yaliagizwa na makampuni matatu (3) ya mafuta (kupitia nyaraka 4 za kuagizia mizigo nje ya nchi) lakini hayakuingizwa kwenye mfumo wa TANCIS kwa ajili ya kukadiriwa na kulipia kodi. Kutoingiza mafuta kwenye mfumo wa TANCIS ni kinyume na matakwa ya taratibu za Mamlaka na inaashiria kuwa mafuta hayo hayakulipiwa kodi hivyo kusababisha upotevu wa mapato ya Serikali.

Pia, nilifanya ulinganisho kati ya kiasi cha kodi kilichokadiriwa na kiasi cha kodi kilicholipwa kutoka kwenye mafuta yaliyoingizwa nchini kwa mwaka wa fedha wa 2017/18 na kubaini malipo pungufu ya kodi ya jumla ya shilingi 1,167,107,857 kutoka makampuni tisa (9) ya mafuta.

Vile vile, nilibaini ada ya bandari (wharfage fees) yenye jumla ya shilingi 1,286,992,434.00 haikukusanywa katika miamala 17 ya mafuta yaliyoingizwa nchini na makampuni mbalimbali ya mafuta.

Nashauri;

- a) *Serikali ifanye uchunguzi wa mapungufu yaliyojitokeza ili kujua sababu za mafuta yenye kodi ya shilingi 7,292,580,904.44 kutofuata taratibu za kodi na yaliruhusiwa kuchukuliwa na makampuni husika kabla ya kukamilisha taratibu za kodi za forodha; na ihakikishe kuwa kodi zote pamoja riba (kama ipo) zinakusanywa kutoka kwa makampuni husika.*
- b) *Serikali iendeele kuboresha udhibiti katika mafuta yanayoingizwa nchini kwa kufanya usuluhishi wa mara kwa mara wa nyaraka zinazotumika kuingiza mafuta nchini na nyaraka zilizoingizwa kwenye mfumo wa TANCIS kwa ajili kukadiriwa na kulipiwa kodi ili kuzuia kujirudia kwa matatizo kama haya siku za mbeleni.*

- c) *Serikali iboreshe udhibiti katika ukadiriaji na ukusanyaji wa kodi kwenye mafuta ili kuhakikisha kuwa kodi zote zilizokadiriwa zinakusanywa.*
- d) *Serikali ikomboe malipo ya kodi pungufu ya shilingi 1,167,107,857 na ada ya bandari (wharfages fees) ya shilingi 1,286,992,434 ambayo haikulipwa.*

5.1.6.13 Mifumo isiyoridhisha ya udhibiti katika ukadiriaji na ukusanyaji wa kodi kwenye mizigo inayoingizwa nchini kutoka nchi nyingine

Nilipitia taarifa kutoka katika mfumo wa kodi za forodha wa TANCIS kwa mizigo iliyoingizwa nchini kutoka nchi nyingine kupitia mipaka ya Kagera, Kilimanjaro, Arusha, Mara, Mwanza, Mtwara, Pwani na Tanga. Baada ya kupitia nilibaini kuwa miamala 1,095 ya mizigo yenye kodi ya jumla shilingi 35,223,221,808.42 haikukamilisha taratibu za forodha katika mfumo wa TANCIS, mizigo hiyo haikuwepo katika maghala ya ofisi hizo za forodha wakati wa uhakiki, na hapakuwa na ushahidi wa nyaraka zinazothibitisha kuwa kodi ilikusanywa kwenye mizigo hiyo. Kitendo hiki kinaashiria kwamba kuna uwezekano kuwa mizigo hiyo iliyoingizwa nchini iliruhusiwa na kuchukuliwa na waagizaji bila kodi husika kulipwa.

Kadhalika, ukaguzi wangu katika uingizwaji wa mizigo kwa ajili ya matumizi ya ndani kupitia mipaka ya Holili na Sirari nilibaini kuwa ada kwa ajili ya taratibu za kiforodha (customs processing fees) ya shilingi 318,920,914.38 haikukusanywa katika mizigo iliyoingizwa kutoka nchi zisizo Wanachama wa Jumuiya na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Nashauri

- a) *Serikali ifanye uchunguzi wa sababu zilizopelekea kuruhusu mizigo iliyoingizwa nchini kuchukuliwa na waagizaji kabla ya kukamilisha taratibu za forodha na ikomboe kodi ya jumla ya shilingi 35,223,221,808.42 kutoka kwenye mizigo hiyo.*
- b) *Serikali ihakikishe kuwa ada kwa ajili ya taratibu za forodha inakusanywa kwa mizigo yote inayoingizwa nchini kutoka nchi*

zisizo Wanachama wa Jumuiya na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

5.1.6.14 Bidhaa zinazoingizwa nchini bila kukaguliwa na Mamlaka nyingine za Serikali za kudhibiti ubora na viwango.

Nilihakiki sampuli ya bidhaa zilizoingizwa nchini kupitia mipaka ya forodha ya bandari ya Bukoba, Murongo, Mtambaswala, Kilambo na Horohoro na kubaini kuwa bidhaa zilizoruhusiwa kuingia na Mamlaka nchini kati ya mwezi July 2017 na Juni 2018 hazikukaguliwa na Shirika la Viwango Nchini (TBS) ili kubaini iwapo bidhaa hizo zinakidhi vigezo na viwango vinavyostahili kutumika nchini kwa mujibu wa sheria ya viwango ya mwaka 2009.

Kadhalika, hakukuwa na ushahidi wa ukaguzi uliofanywa na Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) kwenye vipodozi vilivyoingia nchini kupitia bandari ya Bukoba. Kitendo hiki ni kinyume na kifungu na.86 cha sheria ya Mamlaka ya Chakula na Dawa ya mwaka 2003 ambacho kinazuia uingizaji wa vipodozi ambavyo haviendani na matakwa ya sheria hii.

Katika mazingira haya kuna uwezekano bidhaa zilizoingizwa nchini hazikukidhi vigezo vya ubora na viwango vinavyofaa kutumika nchini, na kukosekana kwa ukaguzi wa bidhaa zinazoingia nchini kunaweza kusababisha uingizwaji wa bidhaa zenye ubora hafifu na zenye madhara kwa matumizi ya binadamu. Pia, serikali inakosa mapato ambayo yangekusanywa kutokana na tozo za ukaguzi wa bidhaa hizo.

Nashauri Serikali;

Ihakikishe kuwa, kabla ya kukusanya kodi kwenye bidhaa zinazoingizwa na waagizaji mbalimbali, ufanyike ukaguzi kwenye bidhaa hizo na kupewa vibali vya kukidhi vigezo vya ubora na viwango kutoka mamlaka za Serikali zinazohusika.

Ihakikishe kuwa mamlaka zinazohusiaka na ubora na viwango vya bidhaa kama vile TBS na TFDA zinapeleka maafisa wake katika mipaka ambayo inatumika kuingiza bidhaa kutoka nchi za nje.

5.1.6.15 Mapato yaliyokusanywa na Mamlaka kwa niaba ya Taasisi nyingine ambayo hayakuwasilishwa kwenye Taasisi husika

Ukaguzi wa ada, tozo na mapato mengine yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato kwa niaba ya taasisi nyingine kama vile Bodi ya Mfuko wa Barabara, Mamlaka ya Bandari na tozo ya maendeleo ya reli kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2018; ulibaini kuwa Shilingi 678,472,140,726.58 zilizokusanywa na Mamlaka ya Mapato lakini hazikuhamishwa kwenda kwenye taasisi husika, badala yake zililihamishwa kwenda kwa Mlipaji mkuu wa serikali.

Katika mahojiano yangu na Uongozi wa Mamlaka, nilifahamishwa kwamba tozo na mapato hayo yaliingizwa kwenye akaunti za kawaida za makusanyo badala ya akaunti maalumu za amana, na iwapo tozo na mapato zimeingizwa kwenye akaunti za kawaida za makusanyo Mamlaka haina ruhusa ya kuhamisha tozo na mapato hayo kwenda kwa taasisi husika. Makusanyo hayo yaliyoingizwa kwenye akaunti za kawaida za makusanyo yanahusu tozo ya maendeleo ya reli, ada ya bandari, tozo za korosho na tozo kwenye ngozi ambazo kwa ujumla ni shilingi ambayo ni asilimia 99.8 ya makusanyo ambayo hayakuhamishwa kwenda kwenye Taasisi husika (Shilingi 678,472,140,726.58). Wizara ya Fedha na Mipango, kupitia Hazina ndio ina wajibu wa kuhamisha fedha hizi kwenda kwa Taasisi husika baada ya kukusanywa na Mamlaka ya Mapato.

Ucheleweshwaji wa tozo na mapato haya kwenda kwenye Taasisi lengwa kunaathiri utoaji wa huduma na utekelezwaji wa mipango mbalimbali ya Taasisi hizo. Mapungufu haya yakiachwa yaendeleo yataharibu nia nzuri ya uanzishwaji wa utaratibu huu wa makusanyo ya tozo na mapato haya. Aidha, sio tu yatazuia utekelezwaji wa mipango ya Taasisi husika, bali pia kwa ujumla yataathiri upatikanaji wa huduma zilizotarajiwa kwa jamii. Muhtasari wa makusanyo hayo umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 13

Mapendekezo

- a) *Serikali ihakikishe kuwa tozo na mapato yaliyokusanywa na Mamlaka kupitia akaunti maalum za amana kwa niaba ya*

Taasisi nyingine yanahamishwa kwa wakati kwenda kwenye Taasisi husika ili kuziwezesha kutekeleza malengo na mipango iliyokusudiwa.

- b) Serikali ihakikishe kuwa tozo ya maendeleo ya reli, ada ya bandari, tozo za korosho na tozo kwenye ngozi zilizokusanywa na Mamlaka kwa niaba ya Wizara ya Uchukuzi na Usafirishaji, Mamlaka ya Bandari, Wizara ya Kilimo na mifugo na kuwekwa kwenye akaunti za kawaida za makusanyo zilizo chini ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) zinahamishwa kwenda taasi husika bila kuchelewa.*

5.2 Hesabu za Taifa

Deni la Serikali

5.2.1 Utangulizi


Deni la Serikali linajumuisha madeni inayodaiwa Serikali Kuu na Taasisi zake kama inavyoelezwa katika Sheria ya Madeni, Dhamana na Misaada ya Serikali ya mwaka 1974 (iliyorekebisha mwaka 2004). Kulingana na vifungu namba 3 na 6 vya Sheria ya Madeni, Dhamana na Misaada ya Serikali, ya mwaka 1974, Waziri wa Fedha ndiye mwenye dhamana ya kukopa na kutoa dhamana kwa niaba ya Serikali.

5.2.2 Mchanganuo wa Deni la serikali

Deni la Serikali kufikia tarehe 30 Juni, 2018 lilikuwa Sh. bilioni 50,926.51 ambapo deni la ndani lilikuwa Sh. bilioni 14,732.45 na deni la nje Sh. bilioni 36,194.06 ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 4,845.08 sawa na asilimia 10.5 ikilinganishwa na deni la Sh. bilioni 46,081.43 lililoripotiwa tarehe 30 Juni 2017.

Deni la serikali limekuwa likiendelea kukua kila mwaka kutokana na kuwapo kwa nakisi ya mapato ya serikali dhidi ya matumizi, ubadilishwaji wa hati fungani, ukopaji kwa ajili ya shughuli za maendeleo na hasara katika kubadilisha fedha za kigeni ikisababishwa na kushuka kwa thamani ya shilingi dhidi ya fedha nyingine za kigeni ambazo ni imara. Kielelezo Na. 21 hapo chini kinaonesha mwenendo wa ukuaji wa deni kwa miaka mitano iliyopita:

Kielelezo Na. 21: Mwenendo wa Ukuaji wa Deni la serikali kwa Miaka Mitano, 2013/14 hadi 2017/18



5.2.3 Sababu za kuongezeka kwa Deni la Serikali

Kuongezeka kwa deni la serikali kwa kiasi kikubwa kunasababishwa na mikopo halisi (mikopo halisi hapa inajumuisha mapokezi ya fedha za mikopo, ulipaji wa mtaji, malipo ya riba za dhamana za Serikali za muda mfupi na misamaha ya madeni). Kwa miaka mitatu iliyopita, sababu hii imekuwa ikichangia ukuaji wa deni kwa zaidi ya asilimia 70, ambapo mwaka 2016/17 ilikuwa juu zaidi na kufikia asilimia 88.


Uchambuzi wa kina ulibainisha kuwa, kushuka kwa thamani ya sarafu/fedha ya Tanzania kumechangia ongezeko la deni la taifa kwa asilimia 20 kwa mwaka 2017/18 (ongezeko kubwa ikilinganishwa na asilimia 9 ya mwaka 2016/17). Ni wazi kuwa kushuka kwa thamani ya sarafu ya Tanzania kunaathiri vibaya ongezeko la deni, jambo ambalo linatoa wito kwa watunga sera kubuni mikakati itakayopunguza athari hizo. Malimbikizo ya riba yanatokana na nchi tano (Iraq, India, Romania, Angola na Iran) za kundi lisilo la wanachama wa Paris, ambazo hazijatoa misamaha ya madeni kulingana na makubaliano. Rejea Jedwali Na. 28 na Kielelezo Na. 22

Jedwali Na. 28: Ukuaji wa Deni kwa miaka mitatu 2015/16 hadi 2017/18

	2017/18		2016/17		2015/16	
	Sh. Bilioni	%	Sh. Bilioni	%	Sh. Bilioni	%
A Salio anzia (Deni)	46,081.43		41,039.39		33,539.59	
B Mikopo Halisi	3,722.08	76	4,429	88	5,363	71
C Malimbikizo ya riba	178.04	4	161.64	3	221.92	3
D Kushuka kwa thamani ya Shilingi	944.96	20	451.53	9	1,914.88	26
E Jumla ya ongezeko = B+C+D	4,845.08	10.5	5,042.04	12	7,499.80	22
F Salio ishia (Deni) = A+E	50,926.51		46,081.43		41,039.39	

Chanzo: Hesabu za fedha fungu 22-deni la serikali kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2018, 2017 na 2016.

Kielelezo Na. 22: Ukuaji wa Deni kwa miaka mitatu 2015/16 hadi 2017/18



Chanzo: Hesabu za Fedha-2016-2018

5.2.4 Mwenendo wa Deni la Ndani kwa mwaka 2017/18

Deni la ndani linajumuisha hati fungani, Hisa za serikali, dhamana za serikali za muda mfupi na deni lisilokuwa dhamana za serikali. Hadi kufikia 30 Juni 2018, Deni la ndani lilifikia Sh. 14,732.45 bilioni (2017:Sh. 13,335.65 billion). Deni la ndani limeongezeka kwa shilingi bilioni 1,396.79, sawa na asilimia 10 ya deni la ndani lililorekodiwa mwaka jana.

Kwa kipindi cha mwaka 2017/18 serikali ilikopa fedha zenye thamani ya Sh. 6,664 bilioni (2017: Sh. 7,303.46 bilioni) toka soko la ndani ambazo zilijumuisha Sh. bilioni 1,828.94 (2017: Sh. bilioni 2,687.83) kwa ajili ya kusaidia Bajeti na Sh. 4,835.20 bilioni (2017: Sh. 4,615.63 bilioni) kwa ajili ya kulipia dhamana za serikali zilizoiva. Malipo ya dhamana za serikali zilizoiva na riba yalifikia Sh. bilioni 6,152.75 kwa kipindi hicho.

Ijapokuwa deni la ndani haliathiriwi na kushuka kwa thamani ya shilingi lakini linakuwa. Deni la ndani linaathiri ukopeshaji kwa sekta binafsi, na ni mzigo kwa serikali kwa siku zijazo. Uchambuzi unaonesha kuwa, jumla ya Sh. billion 5,704 zilizokopwa ndani

hazikuweza kulipa deni na riba za mwaka husika zilizofikia Sh Billion 6,152.75. Hivyo serikali ilitumia Sh. billion 448.75 toka vyanzo vingine vya mapato ili kuhudumia deni la ndani. Kwa hiyo, deni la ndani halikuchangia miradi ya maendeleo.


Kiwango cha kuhudumia deni la ndani kilifikia asilimia 108 ya fedha zilizopatikana toka mikopo ya ndani. Kwa maoni yangu, hii ni sehemu kubwa; na kuna uwezekano wa kuwa na madhara kwa uchumi isipotafutiwa ufumbuzi. Kwa hiyo, ni muhimu kwa watunga sera kubuni mbinu zitakazozuia ukuaji usio na tija wa deni la ndani kwa mtazamo wa kugeuza mwenendo wa matumizi ya fedha zinazopatikana kwa kukopa ndani.

Mbinu hizo, pamoja na mambo mengine, zinaweza kuhusisha ulipaji wa deni la ndani kwa kutumia fedha za bajeti badala ya kukopa kwa ajili ya kulipa

5.2.5 Mwenendo wa Deni la Nje kwa mwaka 2017/18

Deni la nje linahusisha mikopo kutoka Taasisi za Kimataifa, nchi marafiki, Mabenki ya kuuza na kununua nje, na wakopeshaji wa kibiashara. Hadi tarehe 30 Juni 2018, Deni la nje lilikuwa Sh. bilioni 36,194.06, sawa na asilimia 71 ya deni la Serikali. Deni hili liliongezeka kwa shilingi bilioni 3,448.28, sawa na asilimia 10.5 ya deni la nje la shilingi bilioni 32,745.78 lililoripotiwa mwaka 2016/17. Kama inavyooneshwa kwenye Kielelezo Na. 23 na Jedwali Na. 29 hapa chini, Taasisi za Kimataifa ndio wakopeshaji wakubwa zaidi wakiwa na 58% [56% kwa 2017] ya deni lote la nje. Nchi marafiki zinashikilia sehemu ndogo zaidi zikiwa na 11% [13% kwa 2017] hii inahusiana na ukweli kuwa nchi nyingi marafiki zimeanza kutumia mabenki yao ya kuwezesha biashara ya forodha ili kutoa mikopo hiyo.

Kielelezo Na. 23: Vyanzo vya Deni la nje hadi 30 Juni 2018




Uchambuzi wa madeni ya nje kwa makundi ya wakopeshaji hadi kufikia 30 Juni 2018 ni kama inavyoonesha kwenye Jedwali Na. 29 hapa chini:

Jedwali Na. 29: Vyanzo vya Deni la nje hadi 30 Juni 2018

Kundi la wakopeshaji	Kiasi cha Deni	
	Asilimia	Shilingi bilioni
Mashirika ya Kimataifa	58	20,843.00
Nchi Marafiki	11	4,144.95
Benki za kuwezesha biashara ya Forodha	17	6,055.55
Wakopeshaji wa kibiashara	14	5,150.56
Jumla	100	36,194.06

Kama ilivyooneshwa kwenye Kielelezo Na. 24, tathmini ilibainisha kuwa kupanda kwa deni la nje kulitokana na mikopo mipya.


Kielelezo Na. 24: Sababu za kuongezeka kwa deni la nje, 2015/16 hadi 2017/18



Kielelezo Na. 25 kinaonesha Vyanzo vya Deni la nje kwa mwaka 2017/2018. Uchambuzi wa Kiasi cha ukopeshaji kwa kila chanzo umeoneshwa katika **Jedwali Na. 30** na **Kiambatisho Na. 15** viinaonesha Miradi muhimu iliyopokea fedha za deni la nje kwa mwaka 2017/18. **Kiambatisho Na. 14** kinaonesha mchanganuo wa miradi iliyowezeshwa na mikopo mipya iliyotolewa kwa Serikali kwa mwaka 2017/18.

Kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 25, mashirika ya Kimataifa ndiyoyalikuwa wakopeshaji wakubwa zaidi yakiwa na 50%, yakifuatiwa na wakopeshaji wa kibiashara 34%. Nchi marafiki zilikopesha fedha kidogo zaidi 3%. Hii inahusiana na ukweli kuwa nchi nyingi marafiki zimeanza kutumia mabanki yao ya kuwezesha biashara ya forodha 13% ili kutoa mikopo hiyo.

Kielelezo Na. 25: Vyanzo vya Deni la nje kwa mwaka 2017/2018



Uchambuzi wa Kiasi cha ukopeshaji kwa kila kundi kwa mwaka 2017/18 umeoneshwa katika Jedwali Na. 30

Jedwali Na. 30: Vyanzo vya Deni la nje kwa mwaka 2017/2018

Kundi la wakopeshaji	Mikopo kwa 2017/18	
	Asilimia	Shilingi Bilioni
Mashirika ya Kimataifa	50	1,985.87
Nchi Marafiki	3	125.44
Benki za kuwezesha biashara ya Forodha	13	492.93
Wakopeshaji wa kibiashara	34	1,354.25
Jumla	100	3,958.49

5.2.5.1 Mwenendo wa deni la nje kwa miaka mitano

Tathmini yangu ya deni la nje katika mwaka 2017/18 ilibainisha kuwa mikopo ya kibiashara kutoka vyanzo vya nje ilifikia shilingi bilioni 1,354.3. Hili ni ongezeko la shilingi bilioni 376, sawa na asilimia 38 ikilinganishwa na shilingi bilioni 978 zilizokopwa kibiashara mwaka 2016 / 17. Mikopo ya kibiashara inaongeza gharama za kuhudumia madeni kwa kuwa na vipindi vifupi vya neema, riba kubwa na muda mfupi wa kuiva. Kwa hiyo, ni muhimu kwa watunga sera kuwa na busara wakati wa kuchagua miradi ya kupewa fedha za mikopo ya


kibiashara. Katika hali hii, maamuzi yazingatie uzalishaji wa mradi husika. Vinginevyo shinikizo la gharama za kuhudumia litaikumba bajeti ya fedha. Jedwali Na. 31 na Kielelezo Na. 26 vinaonesha mlinganisho wa Muundo wa deni la nje kwa Unafuu wa masharti

Jedwali Na. 31:Ulinganisho wa Muundo wa deni la nje kwa miaka mitano

Mwaka wa fedha	Masharti ya juu		Masharti nafuu		Jumla Kiasi (Sh bilioni)
	Kiasi (Sh bilioni)	Asilimia (%)	Kiasi (Sh bilioni)	Asilimia (%)	
2013/14	4,746	25	14,597	75	19,343
2014/15	7,835	31	17,715	69	25,550
2015/16	9,155	31	20,691	69	29,846
2016/17	10,125	31	22,621	69	32,746
2017/18	11,206	31	24,988	69	36,194

Mwenendo unaonesha kwamba, sehemu kubwa ya deni la nje bado ni la masharti nafuu; Sh. bilioni 24,988, sawa na asilimia 69 ya deni la nje. Asilimia ya mikopo ya masharti nafuu imebakia kuwa asilimia 69 katika mwaka 2017/18 kama ilivyokuwa mwishoni mwa 2016/17. Hata hivyo, deni la kibiashara mnamo 30 Juni 2018 lilikuwa Sh. bilioni 11,206 [2016/17: shilingi bilioni 10,125] ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 11.

Kielelezo Na. 26: Muundo wa deni la nje kwa Unafuu wa masharti



5.2.6 Shughuli za Ukopaji

5.2.6.1 Uptoshwaji wa mapokezi ya mikopo kutokana na mapungufu ya Udhhibiti wa Ndani katika kurekodi na kutaarifu

Katika mapitio niliyofanya katika sampuli ya miradi 15 (17%) kati ya 87 iliyorekodiwa kupokea fedha kwa Mujibu wa mfumo wa kurekodia taarifa za deni (CS-DRMS), niligundua kwamba mapokezi ya fedha za mikopo yaliingizwa katika kumbumumbu bila kuwa na uthibitisho kutoka kwa waliopokea fedha hizo (benki kuu au watekelezaji wa miradi). Kumbukumbu hizo ziliingizwa kwa kigezo cha taarifa ambazo Fungu Na.22 ilipokea kutoka kwa wakopeshaji. Pia, niligundua kutofautiana kwa taarifa za mapokezi ya fedha baina ya mfumo wa kutunza taarifa (CS-DRMS) na hesabu za fedha kulikosababishwa na mchakato wa kianalojia katika kuchukua taarifa toka CS-DRMS.

Kwa mtazamo wangu, Idara ya Fedha za Nje, ambayo ndiyo yenye wajibu wa kufuatilia kutolewa kwa fedha kwa wakopeshaji na wapokeaji, inapaswa kuwapatia uthibitisho wa maandishi kwa fungu Na. 22 juu ya mapokezi ya fedha za mikopo ili kutunza kumbukumbu stahili na sahihi.

Naishauri Serikali kupata kutoka kwa wanufaika uhakika wa mapokezi ya fedha za mikopo kabla ya kuingiza kumbukumbu hizo katika mfumo wa kutunza kumbukumbu za madeni. Pia kuzingatia kubuni vidhibiti ambavyo vitawezesha usahihi wa taarifa za fedha kuchukuliwa kutoka CS-DRMS.

5.2.6.2 Kucheleweshwa kulipa madeni ya Benki Kuu, Sh. bilioni 212.7

Uchambuzi wangu wa mwenendo wa gharama za kuhudumia madeni ambayo Serikali inadaiwa na Benki Kuu ulibaini kuwapo kwa jumla ya Sh. bilioni 212.7 ambazo hazikulipwa kwa wakati. Kati ya hizo, Sh. bilioni 199.79 zinatokana na riba ya nakisi ya Serikali, na Shilingi bilioni 12.9 ikiwa ni sehemu ya Serikali ya gharama za kudhibiti ukwasi kuanzia mwaka 2015/16 hadi 2017/18 ambapo zilikuwa hazijalipwa hadi wakati wa ukaguzi mwezi Desemba 2018.

Katika kufanya uchambuzi zaidi, niligundua kuwapo kwa mkataba wa makubaliano (MoU) kati ya Serikali na Benki Kuu ambao unaitaka Serikali kulipa kila robo mwaka sehemu yake ya gaharama ya kudhibiti ukwasi pindi hati ya madai inapotolewa. Suala la ucheleweshaji wa malipo likiendelea litaongeza kuwapo kwa mali za Benki Kuu zisizo na tija; na kwa mtazamo wangu, hii ni dalili ya Serikali kushindwa kutimiza majukumu yake ya kifedha, kinyume na Sehemu ya 3.02 ya mkataba wa makubaliano kati yake na Benki Kuu.

Hivyo, naishauri Serikali: (i) Kulipa sehemu yake ya gharama ya kudhibiti ukwasi pamoja na riba ya nakisi katika akaunti yake kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 2006 na mkataba wa makubaliano (MoU) baina yao. Kuwezesha bajeti ya Fungu 22 kuweza kumudu gharama hizo ndio njia sahihi hapo mbeleni; na (ii) Kuzingatia kufanya marekebisho ya Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 2006 ili kuruhusu Benki Kuu kupunguza madeni yake kwa Serikali kutoka katika gawio lake. Juhudi hizi zitapunguza kasi ya ukuaji wa madeni yatokanayo na gaharama ya kudhibiti ukwasi pamoja na riba ya nakisi ya Serikali.

5.2.6.3 Kutokuwapo kwa usuluhisho wa taarifa za mfumo wa malipo (Epicor) na mfumo wa kutunza taarifa za deni la taifa (CS-DRMS)

Katika ukaguzi wangu wa hesabu za Fungu Na. 22 za mwaka 2017/18 na taarifa za mfumo wa kutunza taarifa za deni la taifa (CS- DRMS), nilibaini kuwapo kwa tofauti baina ya taarifa hizo kulikotokana na kutokuwapo kwa uwiano wa taarifa za mfumo wa malipo (Epicor) na mfumo wa kutunza taarifa za deni la taifa (CS-DRMS) kabla na wakati wa kuandaa taarifa za fedha hesabu za Fungu 22. Ijapokuwa menejimenti ilirekebisha hesabu zilizotofautiana, lakini kiini cha tatizo hakijaondolewa.

Kwa mtazamo wangu, taarifa za fedha hazikuwianishwa na vyanzo vyake, hivyo kuhatarisha uadilifu wa taarifa zilizowasilishwa.

Napendekeza Serikali iimarisha mifumo ya ndani ili kuhakikisha hesabu zinapitiwa kwa umakini kabla ya kuwasilishwa kwa ukaguzi

5.2.7 Huduma za Jumla

5.2.7.1 Kushindwa kutambua madeni yatokanayo na malimbikizo ya michango ya pensheni

Serikali imekuwa ikiyalipa mashirika ya pensheni malimbikizo ya michango ya pensheni na adhabu zake kwa miaka kadhaa. Malimbikizo hayo, kwa kawaida, husababishwa na makosa yanayofanywa wakati wa kuingiza taarifa za watumishi kwenye mfumo wa Lawson na michango mingine iliyolimbikizwa kabla ya kuwapo kwa mfumo wa Lawson. Malimbikizo hugunduliwa na mifuko ya pensheni pindi mtumishi anapodai stahiki zake za kustaafu, hivyo kusababisha usumbufu usiotarajiwa kwa wastaafu na Mifuko ya pensheni.

Serikali kupitia fungu Na. 22 ina wajibu wa kulipa sehemu ya mwajiri kwa watumishi wote wa serikali na sehemu ya mwajiriwa hulipwa na afisa masuuli husika. Malipo hufanyika kutoka fungu 22 baada ya sehemu ya malipo inayomhusu Afisa Masuuli kuthibitika. Utaratibu huu ni mzuri sana katika kuzuia malipo yaliyozidi kwenda mifuko ya pensheni. Hata hivyo, husababisha malimbikizo ya michango ya pensheni; na malimbikizo hayo hayarekodiwi fungu 22 kama madeni/madai kutokana na fungu hili kutokuwa na uwezo wa kupata taarifa hizo kutoka kwenye mfumo ya kulipia mishahara.

Mhasibu Mkuu (Fungu Na. 22) hulipa malimbikizo hayo kulingana na hati ya madai kutoka mifuko ya pensheni bila kuthibitisha kutoka mifumo ya serikali na yenye taarifa hizo (Lawson au GSPP). Kwa maoni yangu, haikupaswa kuwa hivyo.

Tathimini ya taarifa za Ukaguzi kwa miaka iliyopita ilibainisha kuwapo kwa malipo ya malimbikizo kila mwaka kwa miaka mitano iliyopita kama inavooneshwa kwenye Jedwali Na. 32 hapa chini.

Jedwali Na. 32 : Sampuli ya malimbikizo yaliyolipwa kwa mifuko ya Pensheni

No	Mwaka wa fedha	Malimbikizo yaliyolipwa Shilingi ²¹
1	2013/14	299,978,036

21 Tarakimu hizi ni kwa sampuli tu, Malipo halisi yaweza kuwa Zaidi ya hapo.

No	Mwaka wa fedha	Malimbikizo yaliyolipwa Shilingi21
2	2014/15	359,386,600,377
3	2015/16	385,301,247
4	2016/17	268,440,612
5	2017/18	591,495,998
	Jumla	360,931,816,270

Ninapendekeza Serikali kuzingatia kutumia programu zake zilizopo, ikiwa ni pamoja na Lawson na GSPP, katika kupata taarifa halisi kwa wakati kuhusu madai ya michango ya kisheria na kulipa kwa wakati huohuo ili kuepuka malimbikizo yasiyokuwa ya lazima kwa serikali na kuripoti madai kwa upungufu.

Pensheni

5.3 Ukaguzi Wa Awali Wa Malipo Ya Mafao Ya Wastaafu

5.3.1 Utangulizi

Ukaguzi wa awali wa malipo ya mafao ya hitimisho la kazi hufanyika kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 (Iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2005) na Kifungu cha 29 cha Sheria ya Ukaguzi No.11 ya mwaka 2008. Kifungu cha 5(a) cha sheria hiyo kinamtaka Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuidhinisha malipo yafanyike kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali baada ya kujiridhisha kwamba, Ibara ya 136 ya Katiba imezingatiwa.

Hivyo, ni muhimu kufanya ukaguzi wa awali kwenye malipo yote ya Serikali ambayo siyo rahisi kuyatabiri na kutengewa fedha.

Ukaguzi wa awali wa malipo ya mafao ya hitimisho la kazi hufanyika kwa kuzingatia sheria za mafao ya hitimisho la kazi ambazo ni pamoja na Sheria ya Hitimisho la Kazi katika Utumishi wa Umma ya mwaka 1999; Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa ya mwaka 2006; Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2002; Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii ya mwaka 1997; Sheria ya Ulinzi wa Taifa ya mwaka 1966 (Iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2002); Sheria ya Utumishi wa Usalama wa Taifa ya mwaka 1996; Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kusimamia Sekta ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2008; Sheria ya Mafao ya Kustaafu ya GEPF ya mwaka 2013 na Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa ya mwaka 1999.

5.3.2 Lengo la kufanya Ukaguzi wa Awali

Lengo la ukaguzi huu ni kuhakiki usahihi wa mafao ya hitimisho la kazi yaliyokokotolewa na waajiri kwa ajili ya kuwalipa wanufaika ili kuwezesha kutambua makosa mapema huku kukiwa na lengo la kuhakikisha kuwa wastaafu wanalipwa kile wanachostahili. Hii pia ni muhimu kwa kuwa, kiasi chochote kitakacholipwa kimakosa ni vigumu kurejeshwa kutoka kwa wastaafu.

Kwa upande mwingine, madhumuni ya uhakiki wa mafao ni kuhakikisha kuwa sheria husika, kanuni za mafao ya hitimisho la kazi,

sera za kazi zinazohusiana na utumishi wa umma, nyaraka mbalimbali, Ikama na muundo wa mishahara vinazingatiwa.

5.3.3 Mawanda ya Ukaguzi

Ukaguzi wa awali wa mafao ya hitimisho la kazi unahusisha Watumishi wa Umma ambao mafao yao hulipwa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali na hauhusishi Watumishi wa umma ambao ulipwaji wa mafao yao unashughulikiwa na Mfuko wa Mafao ya Hitimisho la Kazi katika Utumishi wa Umma (PSPF), Mfuko wa Mafao ya Hitimisho la Kazi kwa Mashirika ya Umma (PPF), Mfuko wa Mafao ya Hitimisho la Kazi kwa Serikali za Mitaa (LAPF), Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na mifuko mingine ya hifadhi ya jamii. Kazi ya ukaguzi wa awali inayofanywa na ofisi yangu ni kwa ajili ya malipo ya mafao ya hitimisho la kazi yanayolipwa moja kwa moja kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali, malipo ambayo yanahusisha:-

- a) Pensheni na kiinua mgongo kwa watumishi wa umma watoa huduma mchanganyiko, wanajeshi na viongozi wengine, walimu na maafisa wa usalama;
- b) Malipo ya kimkataba kwa viongozi wa kisiasa, wageni toka nje, wastaafu waliorejeshwa kwenye utumishi, na raia walioajiriwa wakiwa na umri wa zaidi ya miaka 45;
- c) Kiinua mgongo kwa watumishi wasio kwenye masharti ya pensheni; na
- d) Malipo ya kiinua mgongo kwa askari polisi.

5.3.4 Ufafanuzi wa Hoja za Ukaguzi na Mapendekezo

Sehemu hii ya ripoti inaeleza mambo muhimu yaliyobainika wakati wa ukaguzi wa awali wa malipo ya mafao ya hitimisho la kazi na mapendekezo kwa mwaka wa fedha 2017/18 kama ifuatavyo:

5.3.5 Muhtasari wa matokeo ya ukaguzi

Zoezi la ukaguzi wa awali lilianza na majalada 250 yaliyotokana na ukaguzi wa kipindi cha mwaka 2016/17. Jumla ya majalada ya wastaafu 3,187 yalipokelewa na kufanya jumla ya majalada 3,437 yaliyokuwepo kwa ajili ya ukaguzi wa awali kwa kipindi cha mwaka

2017/18. Kati ya majalada 3,437, ofisi yangu ilikagua majalada 2868; ambapo majalada 2,814 yenye jumla ya Sh. 165,446,698,552.92 yalikaguliwa na kuidhinishwa na ofisi yangu kwa malipo. Majalada hamsini na nne (54) yalihojiwa na kurudishwa kwa Maafisa Masuuli husika kwa ajili ya masahihisho, hivyo kubakiwa na majalada 569 ambayo yalikuwa bado yakiendelea na ukaguzi wakati wa kufunga mwaka wa fedha tarehe 30 Juni, 2018 kama inavyooneshwa katika jedwali Na.1 hapo chini:-

Jedwali Na. 33: Majalada ya wastaafu yaliyokaguliwa 2017/2018

Maelezo	Idadi
Majalada yaliyokuwepo tarehe 1 Julai, 2017	250
Majalada yaliyopokelewa	3,187
Jumla ya majalada yaliyokuwepo kwa ukaguzi	3,437
Majalada yaliyokaguliwa na kuidhinishwa	2,814
Majalada yaliyokaguliwa na kurejeshwa kwa waajiri yakiwa na hoja	54
Majalada yaliyosalia tarehe 30 Juni, 2018	569

5.3.6 Kuzidisha Mafao ya Hitimisho la Kazi Sh.282, 975,824.31

Ukaguzi niliufanya katika nyaraka za malipo ya pensheni kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ulibaini kuwa baadhi ya nyaraka zilizoletwa kwangu kwa ukaguzi wa awali zilionyesha mafao ya hitimisho la kazi yaliyokokotolewa kwa vinakosa.

Kati ya majalada 2,868 yaliyokaguliwa kwa mwaka wa fedha 2017/18, mafao ya wastaafu 295 (10.5%) yalibainika kukokotolewa kimakosa. Kati ya hayo, majalada 172 yamebainika kuwa na ziada ya malipo ya Sh. 577,327,968.39 huku majalada 123 yakiwa na pungufu ya malipo ya Sh. 294,352,144.07 kama inavyoonesha kwenye jedwali Na 2. Hata hivyo, makosa yaliyoainishwa hapo juu yanatia shaka juu ya kutosheleza kwa utaratibu wa uhakiki wa karatasi za mafao, uwezo wa waandaaji na wahakiki katika ustadi na uzoefu wa masuala ya pensheni na sheria husika, na ufungashaji wa majalada ya mafao.

Jedwali Na. 34: Makosa katika ukokotozi wa mafao ya hitimisho la akazi

Na	Maelezo	Mafao Yaliyozidishwa		Mafao Yaliyopunjwa		Jumla Halisi (a-b) (Shilingi)
		(a)		(b)		
		Idadi ya kesi	Kiasi (Shilingi)	Idadi ya kesi	Kiasi (Shilingi)	
1	Kipindi cha utumishi kisicho sahihi.	97	249,343,899.75	74	224,939,285.20	24,404,614.55
2	Mishahara iliyokosewa.	37	214,304,826.32	20	41,534,063.32	172,770,763.01
3	Makosa katika michango ya NSSF.	26	27,120,657.17	26	21,637,642.29	5,483,014.88
4	Mikopo/madeni.	4	40,298,754.00	0	0	40,298,754.00
6	Makosa mbalimbali katika ukokotoaji.	8	46,259,831.15	3	6,241,153.27	40,018,677.88
	JUMLA	172	577,327,968.39	123	294,352,144.07	282,975,824.31

Chanzo: Fomu za malipo ya mafao, 2017/18

Kutokana na uchambuzi wa hapo juu, serikali ingepata hasara ya Sh. 577,327,968.39 kutokana na kuzidishwa kwa mafao. Pia, wastaafu wangeweza kupunjwa mafao yao kwa kiasi cha Sh. 294,352,144.07. Ukokotoaji wa mafao kwa makosa ungesababisha serikali kupata hasara halisi ya Sh. 282, 975,824.31.

Kiasi hicho kilichookolewa ni matokeo ya ufanisi wa ukaguzi wa awali wa mafao yanayolipwa moja kwa moja toka kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali. Zaidi ya hayo, inaonesha jinsi ambavyo kushindwa kwa mifumo ya ndani ya udhibiti na mapungufu ya Maafisa Masuuli yangeweza kuigharimu Serikali na wastaafu kama ukaguzi wa awali usingefanyika.

5.3.7 Ucheleweshwaji wa uandaji wa Mafao

Kanuni ya 89 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 inawataka waajiri na waajiriwa kutunza kumbukumbu za kiutumishi kwa lengo la kufanya marejeo wakati wa ukokotozi wa mafao ya hitimisho la kazi. Kanuni ya 32(2) inaeleza kuwa ni wajibu wa waajiri kupitia taarifa za waajiriwa walioko chini yao ili kuhakikisha kuwa utumishi wa watumishi wa umma unakoma pale wanapofikisha umri wa kustaafu. Pia, Kanuni Na. F.48 ya Kanuni za

Kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 2009 ikisomwa pamoja na Kanuni ya 32(3) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 inamtaka mtumishi wa umma aliye tayari kwa kustaaafu, kutoa taarifa ya maandishi ya kusudio lake hilo kwa mwajiri wake kupitia taratibu za kawaida, kwa uchache miezi sita kabla ya kustaaafu.

Hata hivyo, ukaguzi wa awali wa majalada ya wastaafu 1,501 kati ya majalada 2,868 ulibaini kuwapo kwa waajiri waliochelewa kuandaa na kuwasilisha taarifa za mafao kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa ajili ya ukaguzi wa awali. Ucheleweshwaji huo ulikuwa katika vipindi mbalimbali kama inavyoonesha kwenye jedwali Na 3.

Jedwali Na. 35: Majalada yaliyocheleweshwa

Na	Muda(katika miaka)	Idadi ya majalada
1	Chini ya 1	862
2	1 mpaka 4	443
3	Zaidi ya 4	196
JUMLA		1,501

Chanzo: Fomu za malipo ya mafao 2017/2018

Katika mazingira hayo, ukiukwaji wa taratibu unaofanywa na waajiri umesababisha kucheleweshwa kwa ulipaji wa mafao ya hitimisho la kazi. Ni maoni yangu kuwa, vitendo hivyo visingeweza kutokea kama waajiri wangukuwa makini katika kuandaa mafao na kupelekea ukiukwaji wa matakwa ya sheria na kanuni, suala linaloathiri wanufaika na kusababisha usumbufu usio wa lazima achilia mbali kupungua kwa thamani ya fedha/mafao.

5.3.8 Kiwango cha Malipo ya Hitimisho la Kazi kwa Viongozi wa Kisiasa hakijaainishwa kweye sheria

Kifungu cha 21 (3) cha Sheria ya Mafao ya Hitimisho la Kazi kwa Viongozi wa Kisiasa ya mwaka 1999 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2005) inaelezea kuwa, nanukuu, 'A Member of Parliament shall, in addition to the benefits granted under subsection (1), be granted a winding-up allowance, such other allowances and benefits as may be determined by the appropriate authority pursuant to the provisions of section 24'.

Kwa mujibu wa kifungu cha sheria kilichoanishwa hapo juu, marekebisho yaliyofanywa hayaoneshi kiwango cha kukokotoa posho za hitimisho la kazi kwa Viongozi wa Kisiasa; badala yake, kinaipa nguvu mamlaka husika kutathmini kiwango cha posho hizo.

Kabla ya marekebisho ya kifungu cha 21 (3) cha Sheria ya Mafao ya Hitimisho la Kazi kwa Viongozi wa Kisiasa ya mwaka, 1999, ilikuwa ikisomeka, “The former Member of Parliament shall in addition to the benefits granted under subsection (1) be granted a winding up allowance of a sum equal to twenty per cent of the total sum of the salaries he received in twenty four months”.

Kiwango cha posho kilikuwa kimeainishwa kwenye sheria, hivyo hakukuwa na nafasi kwa mamlaka kutathmini kiwango cha posho hizo.

Kutokuwapo kwa kiwango cha malipo ya hitimisho la kazi kwa viongozi wa kisiasa kwenye sheria kunaweza kusababisha malipo hayo kutolewa kwa matakwa ya mamlaka husika kwa kuwa yataathiriwa na maamuzi ya mamlaka hiyo kwa wakati huo.

5.3.9 Majalada yenye Hoja ambayo hayakurudishwa kwa Ukaguzi wa awali

Pensheni ya Serikali inahusisha hatua kuu tatu (3); uanzishaji na ukokotozi wa Mafao, Uhakiki wa awali unaofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na malipo yanayofanywa na Hazina.

Ukaguzi wa awali wa mafao huanza kwa kupokea majalada ya wastaafu kutoka kwa waajiri husika. Mchakato wa ukaguzi unahusisha vigezo vitatu yaani Uhalali, Ukamilifu wa nyaraka zinazowasilishwa (kama vile barua ya ajira, fomu ya rekodi binafsi, barua za kupandishwa vyeo, barua ya hitimisho la kazi, kiambatisho cha mshahara wa mwisho), na usahihi wa hesabu kulingana na sheria, kanuni na Miongozo inayohusiana na malipo ya mafao. Ikiwa malipo hayo hayajakidhi vigezo, hoja huibuliwa ambayo huhitaji majibu ya haraka kutoka kwa mwajiri.

Wakati wa ukaguzi, nilibaini kuwa majalada sitini na tisa (69) yaliyorudishwa kwa waajiri kwa hoja yalikuwa hayajarudishwa ofisini

kwangu kwa ajili ya kukaguliwa upya mpaka mwisho wa mwaka wa fedha 2017/2018 ikiwa imepita muda wa miezi 3 hadi miezi 53 (miaka 4). Ucheleweshwaji wa kurudishwa majalada yaliyohojiwa unasababisha kuchelewa kwa malipo ya hitimisho la kazi kwa wastaafu au wanufaika.

5.3.10 Hitimisho

Kutokana na mchanganuo wa hapo juu, kuna umuhimu mkubwa kwa waajiri kuwa na udhibiti na utaratibu wa uhakiki katika kuandaa karatasi za mafao ya wastaafu. Kukosekana kwa mfumo wa udhibiti wa ndani na udhaifu kwa Afisa Masuuli kunatoa mwanya kwa watumishi wasio waaminifu kuharibu utaratibu wa ulipaji wa mafao kwa ukokotozi usio sahihi, kitu ambacho kingeiharimu serikali na wastaafu kama tu ukaguzi wa awali usingewezesha kubaini. Ucheleweshaji wa uandaaji wa mafao ya hitimisho la kazi kwa wastaafu wa utumishi wa umma unachangia pia kuwapo kwa makosa ambayo ukaguzi unayabaini. Usumbufu huu usio wa lazima ungeweza kuepukika kama umakini ungezingatiwa katika uandaaji wa mafao na uwasilishaji wa karatasi za mafao kwa ajili ya ukaguzi wa awali.

Zaidi ya hayo, kutokuwapo kwa kiwango cha malipo ya hitimisho la kazi kwa viongozi wa kisiasa kwenye sheria kunaweza kusababisha malipo hayo kutolewa kwa matakwa ya mamlaka husika kwa kuwa yanaathiriwa na maamuzi ya mamlaka hiyo.

Mapendekezo

Serikali, kupitia kwa Maafisa Masuuli, iimarisha udhibiti na utaratibu wa kufanya mapitio ya uandaaji wa mafao. Hii itahakikisha kuwa waandaaji wa mafao ya kiinua mgongo na pensheni wanafuata kanuni na vigezo vya ukokotoaji na sheria kabla ya kuwasilisha kwa ukaguzi wa awali na malipo, na kuepuka kucheleweshwa kwa mafao ya hitimisho la kazi na hasara kwa serikali.

Serikali ihakikishe kuwa Maafisa Masuuli wote wanaandaa na kuwasilisha karatasi za mafao ya wastaafu zikiwa na nyaraka muhimu zimeambatishwa kwa ukaguzi wa awali miezi sita kabla ya tarehe halisi ya kustaafu ili kuepuka ucheleweshwaji wa malipo ya mafao.

Serikali ihakikishe Maafisa Masuuli wote wanawajengea uwezo maafisa wanaohusika kuandaa karatasi za mafao ili kuleta uelewa, hususani katika uandaaji wa mafao, taratibu na sheria za mafao. Pia, ihimize uendeshwaji wa mara kwa mara wa mipango ya mafunzo ya waandaaji wa pensheni ili kuboresha uelewa wa pamoja juu ya sheria, kanuni na taratibu.

Serikali, kupitia Mamlaka husika, ifanyie marekebisho kifungu cha 21(3) cha Sheria ya Mafao ya Hitimisho la Kazi kwa Viongozi wa Kiasia ya mwaka 1999 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2005) kwa kuainisha kiwango cha malipo ya posho la hitimisho la kazi.

Hesabu Jumuifu

5.4 Ukaguzi Wa Hesabu Za Taifa-Hesabu Jumuifu

5.4.1 Utangulizi

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilirasimisha matumizi ya Kanuni za Uhasibu za Kimataifa katika Sekta ya Umma (IPSAS accrual basis of accounting) kuanzia tarehe 1 Julai, 2012. Hivyo Serikali iliandaa hesabu jumuifu kwa mara ya kwanza mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2013 kwa kuzingatia matakwa ya IPSAS 35. Pamoja na nia ya dhati ya serikali katika kuboresha uwazi na uwajibikaji, ujumuishwaji wa taasisi za umma kwenye Taarifa za Hesabu za Majumuisho umeendelea kukumbwa na changamoto kadha wa kadha katika utekelezaji katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018. Changamoto hizo ni pamoja na:

5.4.2 Ufafanuzi Usiofaa na Upimaji wa Uwekezaji wa Mitaji (Equity investments Held for Trading)

Aya ya 10 ya IPSAS 30 inahitaji taasisi kufafanua taarifa ambazo zitamsaidia msomaji wa hesabu kutathmini umuhimu wa mitaji ya kifedha (financial instruments) katika mizania na taarifa ya utendaji. Pia, Aya ya 48 ya IPSAS 29 inazitaka taasisi baada ya kutambua thamani ya uwekezaji wa awali kutambua mali za kifedha (financial assets) na kuthaminisha kwa bei ya soko la wakati husika bila kuondoa gharama za miamala inayoweza kuhusika wakati wa kuuza au kuiondoa kwenye umiliki mali hiyo.

Mapitio yangu ya hesabu za taasisi 10 zenye Uwekezaji wa Mitaji ('equity investments held for trading') zenye thamani ya Sh. 473,320,623,180 yalibaini kuwa, uwekezaji hauna maelezo ya kina juu ya bei ya soko la hisa na mbinu zilizotumika kuthaminisha bei za hisa husika. Pia, taasisi 9 kati ya 10 hazikuwa na taarifa za kina juu ya idadi ya hisa zinazomilikiwa isipokuwa kwa PPF pekee; hii ni kinyume na Aya ya 10 ya IPSAS 30 (rejea Jedwali Na. 36 hapo chini).

Jedwali Na. 36: wekezaji wa Mitaji uliokosa Ufafanuzi wa Kina

Na.	Taasisi	Salio Anzia Julai 2017	Bakaa Juni 2018
		Sh.	Sh.
1	Mfuko wa Pansheni Mashirika ya Umma (PPF)	308,036,749,000	358,994,932,000
2	Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa (LGLB)	146,400,000	146,400,000
3	Manispaa ya Kigoma Ujiji	1,605,000	1,605,000
4	Halmashauri ya Wilaya Kyela	550,000	550,000
5	Shirika la Bima la Taifa	21,420,795,000	21,488,896,500
6	Mfuko wa Uwekezaji - Miradi (UTT Projects)	90,000,000	81,059,000
7	Mfuko wa Uwekezaji (UTT - AMIS)	15,704,330,000	21,425,813,000
8	Mfuko wa Pansheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF)	75,631,398,000	69,965,653,000
9	Chuo Kikuu Dar es Salaam (UDSM)	8,000,000	8,000,000
10	Manispaa ya Kigamboni	-	1,207,714,680
	Jumla	421,039,827,000	473,320,623,180

Mapitio zaidi yalibainisha kuwa, Uwekezaji wa Mitaji yenye thamani ya Sh. 18,477,500,000 (rejea Jedwali Na. 37 hapo chini) yaliripoti uwekezaji ambao ulibakia sawa na kipindi kilichopita. Kutokana na hali hiyo, sikuweza kuthibitisha usahihi wa uwekezaji wa Sh. 1,030,589,862,000 zilizoripitiwa katika hesabu jumuifu kama uwekezaji wa mitaji kama matakwa ya Aya 48 ya IPSAS 29.

Jedwali Na. 37: Uwekezaji ambao thamani yake imebaki ile ya mwaka uliopita

Na.	Taasisi/mwekezaji	Mwekezaji	Salio Anzia Julai 2017	Bakaa Juni 2018
			Sh.	Sh.
1	Mfuko wa Pansheni Mashirika ya Umma (PPF)	Benki NMB	13,290,945,000	13,290,945,000
2	Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa (LGLB)	Benki CRDB	146,400,000	146,400,000
3	Manispaa ya Kigoma Ujiji	Kiwanda cha sementi Tanga	1,605,000	1,605,000
4	Halmashauri ya Wilaya Kyela	Kampuni ya Bia Tanzania	550,000	550,000
5	Mfuko wa Uwekezaji (UTT - AMIS)	Swala	30,000,000	30,000,000
6	Mfuko wa Pansheni Watumishi wa Umma (PSPF)	Benki ya Biashara Mwalimu	5,000,000,000	5,000,000,000
7	Chuo Kikuu Dar (UDSM)	Tanzania Oxygen Ltd	8,000,000	8,000,000
	Jumla		18,477,500,000	18,477,500,000

Licha ya jambo hili kushauriwa katika taarifa yangu ya jumla ya mwaka 2016/2017 kupitia Aya Na. 5.4.6, mapendekezo yangu hayakufanyiwa kazi ipasavyo.

Narejea tena mapendekezo yangu ya mwaka uliopita kwamba, Serikali ipime uwekezaji wa mitaji ya biashara kwa thamani halisi (fair value) na kuonesha taarifa muhimu za hisa zilizozituliwa.

5.4.3 Mali za Kibaiolojia zimeainishwa kwenye hesabu Jumuifu pasipo kuainishwa kwenye hesabu za taasisi husika Sh.100.9 Bilioni

Aya ya 39 ya IPSAS 27 inahitaji taasisi kutoa maelezo kuhusu mali za kibaiolojia zinazotofautisha baina ya zinazotumika na kwisha (Consumable) na zinazozaa na zilizopo kwa ajili ya kuuza au kusambazwa bila malipo au kwa malipo pungufu ya thamani yake. Ibara ya 42 ya IPSAS 27 inasema kwamba, katika kufanya ufafanuzi kwa mujibu wa Aya ya 39, taasisi inahimizwa pia kutofautisha kati ya mali zilizokomaa na changa/zisizokomaa, kama inafaavyo. Pia, taasisi inapaswa kufafanua msingi wa kutofautisha/kuainisha huko.

Nilibaini kuwa katika mapitio yangu ya taasisi 15 za serikali kati ya taasisi 17 ambazo mali za kibaiolojia zilioneshwa katika hesabu jumuifu za kitaifa kwa kiasi cha Sh. 100,937,953,540 hazikutofautisha mali hizo kwa makundi ya yaliyoainishwa hapo juu katika hesabu za taasisi husika. Hii ni kinyume na matakwa ya Aya 39 ya IPSAS 27 na ufafanuzi wa hesabu jumuifu (rejea Jedwali Na. 35 hapo chini). Licha ya jambo hili kushauriwa katika taarifa yangu ya Jumla ya 2014/15, bado serikali hakutekeleza ushauri wangu.

Jedwali Na. 38: Taasisi zilizotoa ufananuzi wa Mali za Kibaiolojia

Fungu Na.	Taasisi	KiasiSh"000"	Maelezo
Fungu Na. 29	MoHA	36,855,477.00	Haikuoneshwa kwa usahihi
Missenyi DC	PO-RALG	25,424,110.00	Haikuoneshwa kwa usahihi
Fungu Na. 43	MoAFSC	13,560,048.06	Haikuoneshwa kwa usahihi
Fungu Na. 99	MoLDF-F	4,791,450.83	Haikuoneshwa kwa usahihi
H/W ya Ludewa	PO-RALG	2,975,329.80	Haikuoneshwa kwa usahihi
H/W ya Makete	PO-RALG	2,920,500.00	Haikuoneshwa kwa usahihi
NARCO	MoAFSC	2,728,907.00	Haikuoneshwa kwa usahihi
H/M wa Mbinga	PO-RALG	1,998,165.00	Haikuoneshwa kwa usahihi
SUMA	MoDNS	1,506,600.00	Haikuoneshwa kwa usahihi
Makambako TC	PO-RALG	1,431,717.44	Haikuoneshwa kwa usahihi
H/M ya Kinondoni	PO-RALG	1,000,000.00	Haikuoneshwa kwa usahihi
LITA	MoAFSC	960,889.00	Haikuoneshwa kwa usahihi
TVLA	MoAFSC	366,054.00	Haikuoneshwa kwa usahihi
Fungu Na. 64	MoLDF-L	28,179.00	Haikuoneshwa kwa usahihi
H/J la Arusha	PO-RALG	1,400.00	Haikuoneshwa kwa usahihi
H/W ya Mufindi	PO-RALG	2,294,193.40	Haikuoneshwa kwa usahihi
H/W ya Muleba	PO-RALG	2,094,933.00	Haikuoneshwa kwa usahihi
Kiasi kilichofanyiwa uhunguzi		100,937,953.54	
Kiasi chote katika fungu hili		125,143,831.92	
Asilimia (%)		80	

Chanzo: Taarifa za Taasisi moja kwa moja kwa mwaka 2017/18

Narejea mapendekezo yangu ya awali kwamba Serikali ihakikishe mali za kibiolojia zinatofautishwa kuanzia kwenye hesabu za fedha za taasisi ili kuendana na matakwa ya Aya ya 39 ya IPSAS 27 na kusaidia uthibitisho wa mawasilisho ya Hesabu Jumuifu.

5.4.4 Mpangilio wa vipengele usio sawa baina ya hesabu jumuifu na hesabu za taasisi hivyo kusababisha uwasilishwaji usio sahihi Sh. 251.7 Bilioni

Aya ya 88 ya IPSAS 1 inatoa orodha ya vitu ambavyo vina utofauti wa kutosha kiasili au matumizi (nature and function) kusababisha uwasilishaji wa kujitegemea katika taarifa ya mizania. Zaidi ya hayo, aya ya 90 (a & b) ya IPSAS inahitaji vitu kujumuishwa kulingana na ukubwa, asili, au matumizi au mkusanyiko wa vitu vinavyofanana. Hii ni muhimu kwa uelewa wa taarifa ya hali ya kifedha ya taasisi; na mkusanyiko wa vitu vinavyofanana utafanyiwa marekebisho kwa mujibu wa hali ya tasisi na miamala yake.

Kinyume na matakwa ya IPSAS hapo juu, tathmini yangu ya hesabu jumuifu (CFS) ilibainisha kuwa, mizania jumuifu iliunganisha takwimu zisizoendana toka mizania za hesabu za taasisi (rejea **Kiambatisho Na. 16**). Mapitio zaidi yalibaini kuwa, orodha ya makundi ya taarifa kwenye mizania jumuifu haikuwa sawa na ile ya mizania za taasisi, kwa sababu hiyo baadhi ya takwimu zilizoonekana kwenye mizania Jumuifu hazikuwepo kwenye hesabu za taasisi kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 17** na **Kiambatisho Na. 18**.

Ninapendekeza Serikali kuanzisha mikakati ya kiuhasibu kuhakikisha orodha ya makundi ya taarifa kwenye mizania jumuifu ni sawa na ile ya mizania za taasisi ili kuwako kwa urahisi katika kuwasilisha hesabu zinazoonesha ukweli na haki wa mizania jumuifu na pia kuendana na matakwa ya aya ya 88 ya IPSAS 1.

5.4.5 Taarifa kwenye hesabu jumuifu bila kusainiwa/kuidhinishwa na Afisa Masuuli au Bodi ya Wakurugenzi

Kanuni 11(3) (a) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001 (iliyorekebishwa mwaka 2004) inamtaka Afisa Masuuli kusaini taarifa za hesabu, biashara na taarifa zingine alizokasimiwa chini ya masharti ya Sheria au Kanuni za fedha; na kwa kufanya hivyo, huwajibika binafsi kwa

usahihi kama ilivyoelekezwa na sheria au na Mhasibu Mkuu wa Serikali.

Mapitio ya hesabu za taasisi 376 zinazodhibitiwa na Serikali yaliyojumuishwa katika hesabu yalibaini taasisi 126, ikiwa ni sawa na asilimia 34, ambazo hesabu zake hazikusainiwa na mhusika Afisa Masuuli au Bodi ya Wakurugenzi ili kukidhi vigezo vya wajibu wa usahihi, ukamilifu na muonekano stahiki (Rejea Kiambatisho Na. 19).

Katika mapendekezo yangu kwa Serikali kupitia taarifa yangu ya jumla ya kipindi cha mwaka 2016/2017, nilisisitiza suala hili katika Aya Na. 5.4.4. Hivyo, bado nina shaka kwa taarifa zilizounganishwa, kutokana na ukosefu wa umiliki wa Afisa Masuuli au Bodi ya Wakurugenzi.

Narejea tena mapendekezo yangu ya mwaka uliopita, Serikali ifanye majumuisho ya hesabu ya taasisi zinazodhibitiwa ambazo zimesainiwa na Maafisa Masuuli husika na wenyeviti wa Bodi za Wakurugenzi.

5.4.6 Hesabu zilizojumuishwa zikiwa na tarehe tofauti na hesabu Jumuiifu Bila Kufanyiwa Marekebisho

Ukaguzi wangu wa Hesabu jumuiifu za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ulibaini kuwapo kwa hesabu za taasisi nne (4) za serikali zilizojumuishwa wakati zikiwa zimefunga hesabu zake tarehe tofauti na tarehe ya hesabu ya taasisi inayozidhibiti (rejea Jedwali Na. 39 hapo chini). Hii ni kinyume na Aya ya 46 ya IPSAS 35 na Waraka wa Hazina Na.12 uliotolewa tarehe 9 Januari 2015 ambao unataka taarifa za fedha za Taasisi inayodhibiti na zinazodhibitiwa kuwa na tarehe sawa za ufungaji wa hesabu pamoja. Ikiwa tarehe zinatofautiana, kunatakiwa kuandaliwa taarifa za hesabu za nyongeza zenye tarehe zinanzofanana na Taasisi inayodhibiti.

Pia, nilibaini kuwa hakuna marekebisho yaliyofanyika katika hesabu za Taasisi zinazodhibitiwa ili kuzioanisha na tarehe ya hesabu ya taasisi inayodhibiti. Pia, hakuna marekebisho ya madhara ya miamala muhimu au matukio yanayotokea kati ya tarehe hiyo na tarehe ya taarifa za kifedha za taasisi inayodhibiti.

Jedwali Na. 39: Mashirika yanayodhibitiwa yenye tarehe tofauti za kutoa taarifa

Na.	Jina la Taasisi	Tarehe ya Taasisi inayodhibitiwa	Tarehe ya Taasisi inayodhibiti
1	Benki ya Rasimali (TIB - Corporate Bank)	31 Desemba, 2017	30 Juni, 2018
2	Benki ya Rasimali (TIB) - Development Bank)	31 Desemba, 2017	30 Juni, 2018
3	Benki ya Posta (TPB)	31 Desemba, 2017	30 Juni, 2018
4	Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB)	31 Desemba, 2017	30 Juni, 2018

Chanzo: Hesabu za taasisi inayodhibiti na zianzodhibitiwa 2017/2018 na 2017.

Napendekeza Serikali ihakikishe kuwa Taasisi zake zinaandaa taarifa za ziada. Aidha, ihakikishe marekebisho ya taarifa za kifedha yanafanyika kwa usahihi ili kuendana na mahitaji ya IPSAS 35 na Waraka wa Hazina Na. 12 wa tarehe 9 Januari 2015.

5.4.7 Uondoshwaji Usio sahihi wa miamala katika Hesabu Jumuiifu za Kitaifa

Aya ya 40 (a) hadi (c) ya IPSAS 35 inataka taasisi zinazoandaa taarifa Jumuii kuunganisha mali, madeni, mapato na matumizi ya taasisi zinazodhibiti na zile za taasisi zinazodhibitiwa. Pia, inaitaka taasisi inayodhibiti kuondoa mali, madeni, mali halisi, mtaji, mapato, matumizi na mtiririko wa fedha ambazo zinazohusiana na miamala baina ya taasisi zinazojumuishwa. Lengo la utaratibu huu ni kuondoa kuhesabu mara mbili na kuboresha uhalisia wa matukio yaliyoripotiwa katika hesabu za taifa.

Mapitio yangu ya hesabu jumuiifu za kitaifa pamoja na hesabu za taasisi za kipindi cha mwaka unaoishia 30 Juni 2018 yalibaini mapungufu yafuatayo:

- a) Utofauti wa kiasi kilichoondolewa kwenye ruzuku zilizoenda kwenye taasisi za serikali na ruzuku zilizotoka taasisi za serikali kwa kiasi cha Shilingi 2,323 Bilioni**

Ruzuku kwa taasisi za serikali zenye thamani ya shilingi 11,829,185,997,000 ziliondolewa dhidi ya ruzuku zilizopokelewa na taasisi za serikali zenye thamani ya shilingi 9,506,212,051,000 kwenye taarifa ya mahesabu ya mapato na matumizi. Hii imesababisha kuondolewa zaidi kwa ruzuku zilizoenda kwa taasisi za serikali kwa

kiasi cha Sh. 2,322,973,946,000. Hivyo kiasi cha matumizi kilichooneshwa kwenye taarifa ya mapato na matumizi kwenye hesabu za majumuisho kimepunguzwa kwa kiasi hicho.

b) Uwasilishwaji usio sahihi wa madeni uliotokana na uondoshwaji zaidi/pungufu Sh. 291Bilioni

Uwasilishwaji wa madeni kwa kiasi cha Shilingi 291,840,344,994 haukuwa sahihi kutokana na uondoshwaji wa Shilingi 901,247,049 ambazo sio miamala ya kitaasisi inayooana (miamala ilihusisha taasisi binafsi) pamoja na kutoondolewa kwa kiasi cha Shilingi 290,939,097,945 ambazo ni miamala ya taasisi zinazohusiana (miamala ya taasisi za kiserikali) (Rejea Kiambatisho Na. 20).

5.4.8 1Takwimu zisizo sahihi kuhusu ziada / nakisi ya uwekezaji katika Washirika na Ubia

Aya ya 36 (a na b) ya IPSAS 36 inazitaka taasisi kutumia taarifa za karibuni za kifedha za washirika au ubia katika kutumia njia ya usawa (equity method). Zaidi ya hayo, iwapo tarehe ya kufunga hesabu za taasisi ni tofauti na ya washirika au wabia, taasisi yaweza kupata taarifa za ziada za fedha za washirika na wabia kwa tarehe ya kufunga hesabu ya taasisi. Au huweza kurekebisha taarifa za fedha za karibuni zaidi za washirika au wabia ili kuepuka madhara ya shughuli muhimu au matukio yanayotokea kati ya tarehe ya kufunga hesabu za taasisi na ile ya washirika au wabia.

Katika ukaguzi wangu wa hesabu jumuiifu ikihusiana na uwekezaji katika mashirika ya ubia na katika hesabu za taasisi nilibaini kuwa:

- i) Kati ya taarifa za fedha 30 za washirika (associates) na ubia (Joint venture) zilizojumuishwa katika hesabu jumuiifu za kitaifa, 27 zilikuwa na tarehe tofauti na tarehe ya hesabu jumuiifu (rejea Kiambatisho Na. 21).
- ii) Kati ya taarifa za fedha 30 za washirika na ubia zilizojumuishwa katika hesabu jumuiifu za kitaifa, taarifa 23 ziliwasilishwa na kujumuishwa pia katika taarifa za fedha jumuiifu, hivyo kuacha taarifa za fedha 7 ambazo hazikujumuishwa. Hii inafanya kiasi cha Sh. 1,691,052,208,000 kilichoripotiwa kama uwekezaji

katika washirika na ubia kutokuwa na uhalisia katika uwasilishwaji (rejea Jedwali Na. 40 hapo chini)

Jedwali Na. 40: Taasisi za Washirika na Ubia zisizoshirikishwa katika hesabu Jumuifu

NO	WASHIRIKA/UBIA	ASILIMIA YA UMILIKI
1	Celtel Tanzania Ltd (now Airtel (T) Limited	40
2	Datel Tanzania Limited	35
3	Friendship Textile Co.	49
4	Kiwira Coal Mines	30
5	Mwananchi Engineering and Construction Company (MECCO)	25
6	Tanscan Timber Company Limited	49
7	Tanzania Development Finance Ltd (TDFL)	32.1

Kwa hali hiyo, sikuweza kuthibitisha uthabiti ‘reliability’, usahihi na ukamilifu wa kiasi cha mali halisi na mgawanyo wa ziada / nakisi (share of surplus/deficit) zilizoripotiwa katika hesabu jumuifu za kitaifa.

Naishauri Serikali kutekeleza matakwa ya Aya ya 36 a & b ya IPSAS 36 na kuhakikisha kuwa, hesabu zote za mashirika ya fedha za Washirika na Ubia ambazo hazikujumuishwa zinapatikana na kujumuishwa kwa ukamilifu.

5.4.9 Bakaa Hasi ya Mfuko wa Fedha za Walipakodi Shilingi Bilioni 10,860

Waraka Namba 2 wa Hazina wa mwaka wa fedha 2018/2019 wenye kumbukumbu Na.EG.3/102/03/01 uliotolewa na Katibu Mkuu Hazina tarehe 7 Novemba, 2018 uliwaelekeza Maafisa Masuuli wote namna sahihi ya kuonesha Mfuko wa walipa kodi (taxpayers fund) na kutambua mapato yatokanayo na matumizi ya fedha za mtaji. Kifungu cha 4.1 (i) cha waraka huo kinafafanua kuwa, mfuko wa walipakodi kuwa fedha za umma zinazojumuisha rasilimali zote zilizokusanywa na kutumiwa na serikali katika miundombinu mbalimbali kama vile shule, hospitali na miradi mingine ya kimkakati kwa manufaa ya wananchi.

Mfuko wa walipakodi unahusishwa na mtaji wa Serikali ambao husaidia kuanza kwa shughuli mbalimbali. Kipengee hiki kinaripotiwa kama moja ya vipengee vya mali (equity) za serikali, na kufuatilia jinsi inavyoripotiwa katika taarifa za taasisi mojammoja na Hesabu Jumuiifu, mfuko wa walipakodi unatarajiwa kuwa na bakaa chanya.

Mapitio yangu katika taarifa za Hesabu yalibaini kuwa, mfuko wa walipakodi una taarifa hasi ya shilingi 10,860,403,131,100. Mapitio zaidi ya usuluhishi wa hesabu kuanzia Julai 2016 yalibainisha kuwa taarifa hasi ilisababishwa na bakaa ya kuanzia mwaka shilingi 36,251,977,396,000 na taarifa za mfuko wa walipakodi ya matumizi hasi shilingi 48,009,104,628,000. Hivyo, nilishindwa kuhakiki nini kinachofanya matumizi ya mfuko wa walipa kodi kuwa na matumizi hasi kwa mwaka 2016-17 ya shilingi 11,757,127,232,000. Hii ni kutokana na kuzingatia ukweli kwamba, hakuna taasisi ambayo ipo kwenye hesabu jumuiifu ambayo imeripoti matumizi ya mfuko wa walipakodi.

Ninapendekeza Serikali kuchunguza kipengele kilichoingizwa katika Hesabu Jumuiifu kuhusiana na mfuko wa walipakodi kwa mwaka 2016-17 ambayo imesababisha taarifa hasi na kufanya marekebisho ya taarifa ya mfuko wa walipakodi kwa miaka inayofuata.

Sura ya Sita

Tathmini ya Mifumo Ya Udhhibiti wa Ndani na Utawala Bora

6.1 Utangulizi

Uthibiti wa ndani ni mchakato unaofanywa kwa uimara na ufanisi ili kufikisha malengo ya taasisi kwa kutegemea ripoti za fedha, kuzingatia sheria, kanuni na sera. Udhibiti wa mfumo wa ndani ni kigezo muhimu katika uimarishaji na ufanisi wa menejimenti.

Hujumuisha mfumo mzima wa fedha na usio wa kifedha katika menejimenti, na husaidia wakaguzi kuweza kufikia malengo waliyojipangia. Udhibiti wa mfumo wa ndani hushughulikia ukaguzi na udhibiti ili kuhakikisha ukuaji wa uchumi bora.

Utawala bora unahusisha michakato ya kiutawala kupitia sheria, desturi na mamlaka ya jamii.

Sura hii inatoa matokea ya tathmini ya uthibiti wa mfumo wa ndani uliojitokeza katika Wizara, Idara na Wakala katika mwaka wa fedha 2017/2018. Mapungufu yaliyojitokeza katika tathmini ya udhibiti wa ndani ni pamoja na utekelezaji wa usimamizi wa mali zilizonyang'anywa, tathmini ya mifumo ya udhibiti wa ndani, utawala bora, mfumo wa teknolojia na habari, kamati za ukaguzi, kazi za ukaguzi wa ndani, tathmini za udanganyifu na vihatarishi.

Matokeo na mapendekezo ya ukaguzi wa mfumo wa udhibiti wa ndani yanaonesha kwamba njia za udhibiti na uendeshaji lazima ziwekwe sawa ili kuongeza utoshelevu, ufanisi na umakini katika kudhibiti vihatarishi vinavyobainika. Mambo yaliyopewa kipaumbele zaidi ni Utendaji wa Kamati za Ukaguzi, na Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, Udhibiti Mkuu wa TEHAMA, taratibu za tathmini ya vihatarishi, uendeshaji wa ulaghai na udhibiti pamoja na masuala ya utawala. Mapungufu yafuatayo yalibainika:

6.2 Utawala Bora

Utawala bora ni hatua ya kufanya maamuzi ambayo yanatekelezwa au hayatekelezwi. Utawala bora ni muunganiko wa hatua za muundo wa taasisi ambao unatekelezwa na Bodi ya Wakurugenzi kutaarifu,

kutoa muongozo, kusimamia na kufuatilia rasilimali za taasisi, mkakati na sera katika kufanikisha malengo ya taasisi.

Muundo wa utawala bora hufafanua kwa umakini uangalizi wa mamlaka, kuchukua hatua za maamuzi juu ya uwajibikaji na mawasiliano na usambazaji wa habari ili kufikia malengo ya taasisi. Kupitia ufanisi wa utawala bora, malengo hubainika, rasilimali zinasimamiwa, na maslahi ya wadau yanalindwa na kufanyiwa maamuzi sahihi.

Nilitathmini kuwapo kwa utendaji wa Bodi za Uongozi katika taasisi za Serikali nilizochagua na kukuta mapungufu katika maeneo yafuatayo:

6.2.1 Kutoteuliwa kwa Mkurugenzi wa NGOs

Kifungu cha 4 (1) (b) ya Sheria ya NGO kinahitaji uteuzi wa Mkurugenzi wa kufanya Sheria iweze kutekelezwa ili kuhakikisha utekelezaji sahihi wa Sheria hiyo. Sheria ambayo haijatekelezwa ipaswavyo imesababishwa na Mkurugenzi wa NGO kutochaguliwa tangu kuanzishwa kwa NGO mwaka wa 2002 hadi 2018; na usimamizi wa uendeshaji wa NGO bado unasimamiwa na Idara ya NGO Wizara ya Afya ya Maendeleo ya Jamii, Wazee na Watoto.

Menejimenti ilikubali ushauri na iliahidi kufanyia kazi kwa umakini kwa ajili ya uboreshaji wa shughuli za NGOs na sekta kwa ujumla.

Kutokuteuliwa kwa Mkurugenzi wa NGO kumesababisha kushindwa kutekeleza malengo yaliyoanzishwa kwa kufuata Sheria ya NGO ya 24 ya 2002 kama ilivyorekebisha mwaka 2005.

Ninapendekeza, Mkurugenzi na Bodi kuteuliwa na wanapaswa kujitegemea kutoka Wizara kwa kutekeleza mamlaka kama ilivyoelezwa katika Sheria ya NGOs ya 24 ya 2002 iliyorekebisha na vifungu vya 4 - 11 vya Sehemu ya IV ya Sheria ya Marekebisho No 11 ya 2005 na kanuni zinazohusiana na usimamizi sahihi wa shughuli za NGOs.

6.2.2 Ukosekanaji wa Bodi ya Ushauri

Kifungu cha Sheria ya Wakala ya mwaka 1997 (G. N. 83 ya 2003) kinamuhitaji Waziri anayehusika na Wakala kuanzisha Bodi ya

Ushauri. Kutokana na Sheria ya Wakala (yenye marekebisho) ya mwaka 2009, kila Wakala anatakiwa kuwa na Bodi ya Ushauri, na kuwa na Mwenyekiti na wanachama wengine wasio zaidi ya tano.

Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri wa Waziri atateuliwa kutoka nje ya Wizara ambayo Wakala huyo ameanzishwa. Waziri atawateua Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi ya Ushauri kati ya watu ambao wanafahamu vizuri kazi za Wakala au mambo yaendayo na hayo.

Katika mwaka huu wa ukaguzi nilibaini kuwa taasisi tatu zilizooneshwa katika jedwali Na. 6.1 hapo chini hazina Bodi za Ushauri kwa kipindi cha miaka miwili (2) hadi mitatu (3), kinyume na mamlaka ya uanzilishi. Jumla ya taasisi tatu (3) zina mapungufu makubwa ikilinganishwa na mwaka uliopita ambapo kulikuwa na taasisi nne (4); hivyo kusababisha kupungua kwa taasisi mmoja (1), ambayo ni sawa na asilimia 25. Hii inaonesha kuwa kuna maboresho mwaka huu.

Jedwali Na. 41: Wakala wasiokuwa na Bodi za ushauri

Na	Jina la Wakala	Muda wa Mwisho wa Bodi	Kipindi bila Bodi ya ushauri
1	Wakala wa Elimu ya Uvuvi na Mafunzo (FETA)	Mei 2015	Miaka mitatu(3)
2	Wakala wa Nyumba na Utafiti wa Majengo Tanzania	Machi 2017	Miaka miwili(2)
3	Wakala wa Barabara Vijijini na Mjini Tanzania	Mei 2017	Miaka miwili(2)

Chanzo: Barua ya mapungufu

Kifungu cha 7 cha Sheria ya Wakala wa Serikali ya 1997 (G.N. Nambari ya 83 ya mwaka 2003), inaelezea kazi ya Bodi ya Ushauri ni kumshauri Waziri kuhusu yafuatayo: (a) malengo ya taasisi; (b) vipaumbele na mikakati ya kufikia malengo ya kila mwaka ya taasisi; (c) ripoti ya kila mwaka ya taasisi na akaunti na; (d) tathmini ya utendaji wa taasisi. Hii inaonesha kazi zote zilizotajwa hazikufanyika kwa kiwango kinachotakiwa na kuwa na vikwazo vya kupunguza uamuzi na utendaji wa taasisi husika.

Ukosefu wa Bodi ya Ushauri unazorotesha utendaji wa shughuli za Serikali, hasa katika sera zilizoidhinishwa, miongozo na mipango ya kimkakati.

Ninapendekeza mawaziri husika kuanzisha Bodi ya Ushauri wa Waziri kulingana na mahitaji ya Sheria, kwa ufanisi wa usimamizi wa menejimenti katika ili malengo yao.

6.2.3 Kutokuteuliwa kwa Bodi ya Wadhamini

Kifungu cha tano (5) cha sheria ya Taasisi ya Mafunzo ya Serikali za Mitaa (LGTI) ya mwaka 2002 kinahitaji taasisi hiyo kuwa na Bodi ya Wadhamini. Sehemu ya 17 ya sheria hiyo inahitaji Bodi ya mdhamini kuwasilisha taarifa za kifedha zilizokaguliwa kwa waziri.

Ukaguzi huu umebaini kuwa, muda stahiki wa Bodi ya Wadhamini uliopo umekamilika tarehe 30 Aprili 2018. Kwa hiyo, Bodi ya Wadhamini iliacha kufanya kazi tarehe 30 Aprili 2018. Mpaka 29 Januari 2019 (ambayo ni karibu miezi tisa) Bodi ya wadhamini ikiwa bado haija anzishwa. Aidha, Taasisi zinaendeshwa bila kusaini mkataba wa utendaji na Msajili wa Hazina kama ilivyooanishwa na kifungu cha 10 cha Sheria ya Msajili wa Hazina ya mwaka 2002

Menejimenti ilijibu kuwa, tangu Bodi ya Wadhamini muda wake ulipokwisha mnamo tarehe 30 Aprili 2018, wamekuwa wakifuatilia kwa karibu kwa mamlaka husika (OR - TAMISEMI) ili kuhakikisha kuwa Bodi ya Wadhamini imeanzishwa kama inavyotakiwa na sheria. Kwa upande wake, mamlaka husika imewapa Mamlaka ya kufanya kazi kwa niaba ya Bodi ya wadhamini mpaka kuanzishwa kwa Bodi mpya.

Kutokuanzishwa kwa Bodi ya Wadhamini kunakiuka mahitaji ya kifungu cha tano (5) cha Sheria ya Taasisi ya Mafunzo ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2002.

Ninapendekeza kwa menejimenti ya LGTI kushirikiana na Waziri anayehusika na OR - TAMISEMI ili kuhakikisha kuwa Bodi ya Wadhamini inaanzishwa kama inavyohitajika kisheria

6.2.4 Changamoto zinazoikabili ofisi ya NPS katika utekelezaji wa sheria za kutaifisha na kuokoa mali

Utaifishaji ni upotevu wa moja kwa moja wa umiliki wa haki kwa mali binafsi au mali isiyohamishika kwa kutofuata sharia, au kama mahakama iliamuru fidia kwa kupoteza au uharibifu kwa mdai. Ukaguzi wangu umebaini yafuatayo katika utaifishaji mali:

- i) Ukaguzi wetu umegundua kuwa hakuna ufanisi wa usimamizi wa uuzaji wa mali zilizoshikiliwa na kunyanganywa kutoka kwa baadhi ya wadau waliohusika ambao hawafanani na hakuna sheria inayosimamia utaifishaji wa mali.
- ii) Ukosefu wa mfumo ulio wazi kwa kuwa hakuna mfumo dhabiti uliowekwa wa kufuatilia mali iliyoshikiliwa na kutathminiwa thamani yake katika kuwajibika na harakati za uuzaji
- iii) Ukaguzi umebaini kuwa, hakuna utunzaji wa kumbukumbu sahihi katika uuzaji; na ikitokea kuna mauzo, thamani ya mauzo haijulikani na haiwekwi benki. Kila mdau anawajibika bila kuwa na mawasiliano na wengine.
- iv) Ukosefu wa mfumo mmoja wa kisheria wa kusimamia mali zilizoshikiliwa na kunyang'anywa ikiwamo mamlaka ya kisheria ya kuhifadhi na kusimamia mali hizo.
- v) Pia, tumegundua kuwa rasilimali hazitoshi katika kushughulikia nyanja zote za usimamizi wa mali.
- vi) Uwezekano wa ukosefu wa utaalamu katika kusimamia mali zilizotaifishwa

Kuwapo kwa sheria nyingi zinazosimamia masuala ya kurejesha mali na kutaifisha; kila sheria inaunda usimamizi wake na taratibu za kuondoa.

Kwa sasa, urejeshaji wa mali umewekwa katika kanuni kadhaa zifuatazo:

Sheria ya Wanyamapori na Uhifadhi, Sheria Nambari ya 5 ya 2009 - Sehemu ya 111 (1) (a) na (b), Sheria ya Udhhibiti wa Dawa na Utekelezaji, Nambari ya 5 ya 2015 - Sehemu ya 49 (1), 56 na 57, Sheria

ya Misitu 2002 - Sehemu ya 97 (1) (b) na Kanuni za Misitu GN No.153 ya 2004 - Kanuni ya 57, Sheria ya Uvuvi, Na. 22 ya 2003 - Sehemu ya 38 (1) na (39).

Kila sheria ina usimamizi wake na utaratibu wa kuuza. Kwa mfano, Sheria ya Udhhibiti wa Dawa na Utekelezaji wa Sheria, Sheria ya Nambari ya 5 ya mwaka 2015 inatoa wajibu wa usimamizi na uondoaji wa mali ya mtuhumiwa aliyehukumiwa na madawa ya kulevya. Hii ilitungwa na Serikali chini ya Kamishna Mkuu wa Udhhibiti wa Dawa na Usimamizi. Kifungu cha 57 (2) cha Sheria kinaelezea mapato yanayotokana na kuuza mali zilizotaifishwa chini ya Sheria hii yanaweza kutumika kukidhi gharama zilizotumika katika hatua zilizochukuliwa kupambana na uuzaji haramu au kudhibiti matumizi mabaya ya madawa ya kulevya.

Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, kwa upande mwingine, huweka usimamizi na uondoaji wa mali zilizotaifishwa kwa Serikali chini ya Sheria hiyo kwa Mkurugenzi wa Wanyamapori. Kifungu cha 111 (3) cha Sheria husema kwamba, mali yoyote ambayo imetaifishwa na Serikali inapelekwa kwa Mkurugenzi wa Wanyamapori.

Kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 91 (3) (b) cha Sheria hiyo juu ya utoaji wa mali zilizotaifishwa, asilimia 25 ya mapato ya uuzaji wa mali zilizotaifishwa chini ya Sheria zinawekwa katika Mfuko wa Ulinzi wa Wanyamapori Tanzania. Fedha zilizowekwa katika Mfuko huu zinaweza kutumika kwa mujibu wa kifungu cha 91 (2) cha Sheria ili kuunga mkono vitu vingine vya kupambana na kuhamasisha utekelezaji wa sheria na uhifadhi wa wanyamapori.

Sharia nyingi zinazolenga suala la kurejesha mali zinaleta ugumu kutathmini mali zilizopatikana kutoka kwa wahalifu na kusimamia mali zilizopatikana. Pia, huwa na changamoto za kuandaa taarifa za uhasibu. Mchakato wa kufufua mali unaweza kuwa wazi na ufanisi zaidi kama masharti ya kutaifisha mali yataingizwa katika sheria moja ya uhalifu au masharti ya kurejesha yanafanywa kwa kuzingatia sheria nyingine za kunyang'anya.

Ninashauri Serikali kuunganisha taasisi za serikali / mashirika ya uchunguzi kwa mtazamo wa kuanzisha sheria moja inayotambuliwa

na Sheria ya Uhalifu (Cap. 256 R.E.2002) ambayo inahusika na kurejesha kwa Mali na mchakato wa kutaifisha.

6.3 Tathmini ya Ukaguzi wa Ndani

Ukaguzi wa ndani ni shughuli inayojitegema na inayojiwekea malengo iliyoundwa ili kuongeza thamani na kuboresha shughuli za taasisi. Inasaidia taasisi kutekeleza malengo yake kujiwekea utaratibu makini ili kutathmini na kuboresha ufanisi wa usimamizi wa vihatarishi, udhibiti na utaratibu wa utawala. Kila taasisi, bila kujali ukubwa wake, inapaswa kuwa na mfumo wa udhibiti wa ndani.

Kutokana na Kanuni ya 28(1) ya Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001, kila Afisa Masuuli anatakiwa kuanzisha Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani ili kutoa maoni iwapo mifumo ya ndani ya taasisi inafanya kazi ipasavyo.

Tathmini yangu kuhusu ukaguzi wa ndani kwenye sampuli ya Wizara, Idara na Taasisi pamoja na Sekretarieti za Mikoa ilibaini kuwa, Taasisi 33 zikiwamo Wizara na Idara 10, Mawakala 3, Sekretarieti za Mikoa 15 na Taasisi nyingine 5, zilionekana na mapungufu yakiwemo: kutokuanzishwa kwa vitengo vya ukaguzi wa ndani, vitendea kazi hafifu na mipango ya ukaguzi wa ndani kutoidhinishwa na Kamati ya Ukaguzi, upungufu wa wafanyakazi, kuwa na eneo dogo la kufanyia kazi na kutopata mafunzo kwa wafanyakazi. Orodha ya Taasisi zenye mapungufu kwenye kitengo cha Ukaguzi wa Ndani zimeoneshwa kwenye Kiambatisho Na. 22

Jedwali Na. 42: Mlinganisho wa Tathmini ya Udhhibiti wa Ndani


Mwaka wa fedha \ Taasisi	Idadi ya Wizara	Idadi Sekretarieti za Mikoa	Idadi ya Taasisi Nyingine	Idadi ya Wakala	Jumla ya Taasisi
2016/2017	3	15	0	0	18
2017/ 2018	10	15	5	3	33
Tofauti	7	0	5	3	15
Tofauti ya Asilimia					83.33

Jedwali Na. 42 hapo juu linaonesha kuongezeka kwa idadi ya mapungufu katika kitengo cha ukaguzi wa ndani. Jumla ya mapungufu yaliyojitokeza kwa mwaka huu ni taasisi 33 ikilinganishwa na mwaka

uliopita ambapo kulikuwa na taasisi 18. Hivyo, kuleta tofauti ya taasisi 15, ambazo ni sawa na 83.33%. Hii inaonesha kuwa hapakuwa na maboresho katika eneo hili.

Chati ya hapo chini inaonesha ulinganisho wa miaka miwili ya fedha kati ya 2016/2017 na 2017/2018 yenye mapungufu ya ukaguzi wa ndani.

Kielelezo Na. 27: Tathmini ya Ukaguzi wa Ndani



Kutokana na kutokuwapo kwa Ukaguzi wa ndani, taasisi inakosa kipengele muhimu cha utawala bora. Mara nyingi hukosa ufahamu kamili wa lengo katika ufanisi wa usimamizi wa vihatarishi, udhibiti wa ndani na utaratibu wa utawala, pamoja na tathmini na kuboresha.

Ninapendekeza kuwa, Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani inapaswa kuwa huru na kupewa zana sahihi za ukaguzi. Wafanyakazi wanapaswa kuwa wenye sifa na kulipwa vizuri. Menejimenti inapaswa kuonyesha kujitolea kuimarisha kitengo cha ukaguzi wa ndani katika kutekeleza wajibu wake. Menejimenti inapaswa kutoa msaada na kutoa rasilimali za kutosha kwa ukaguzi wa ndani, na kukubali wakaguzi walete maboresho katika taasisi. Pia, wakaguzi wanatakiwa kupatiwa mafunzo endelevu.

6.4 Tathmini ya Kamati ya Ukaguzi

Kamati ya ukaguzi ina jukumu muhimu katika kusaidia taasisi kutekeleza majukumu yake ya uangalizi katika maeneo kama ripoti za kifedha, mifumo ya udhibiti wa ndani, mifumo ya usimamizi wa vihatarishi na kazi za ukaguzi wa ndani na nje.

Kanuni ya 30 ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 inahitaji kila Wizara au Mikoa kuwa na Kamati ya Ukaguzi. Uanachama wake (kuwa na mhasibu wa kitaaluma) na kazi zake zimeelezwa kwenye Kanuni ya 31 na 32 ya Kanuni za Fedha za Umma. Kamati ya Ukaguzi itaundwa na wajumbe wa Wizara, Wakala au Idara. Pia, inawezekana, kuteuliwa na Afisa Masuuli husika na angalau mwanachama mmoja atakayeteuliwa na Katibu Mkuu kutoka kwenye vyanzo vya nje

Jumla ya wananachama wa Kamati ya Ukaguzi wanatakiwa isizidi tano au chini ya tatu; na angalau mmoja ya mwanachama anatakiwa kuwa na uzoefu wa majukumu ya uhasibu na ukaguzi. Pia, majukumu ya kamati ya ukaguzi ni pamoja kufanya mikutano ya robo mwaka, kuidhinisha mipango na mikakati ya ukaguzi ya kila mwaka ya Wizara, Wakala au Idara; kupitia upya ripoti zote za ukaguzi wa ndani na nje, kutoa ushauri kwa Afisa Masuuli juu ya hatua zitazochukuliwa juu ya masuala yaliyotolewa katika ripoti ya mkaguzi wa ndani au katika ripoti ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, na kuandaa ripoti ya kila mwaka juu ya kazi zake.

Katika tathmini ya Kamati ya Ukaguzi, tumeona mapungufu yafuatayo: Kamati ya Ukaguzi haikuandaa ripoti ya kila mwaka juu ya kazi zake. Kamati haijawahi kukutana na wakaguzi wa nje angalau mara moja bila ya mtendaji wa wajumbe kutoka katika taasisi iliyopo ili kuhakikisha kuwa hakuna suala ambalo halijatatuliwa. Ukosefu wa utaratibu wa Kamati ya Ukaguzi inayohusika kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo, na kushindwa kufanya tathmini ya maendeleo ya Kamati ya Ukaguzi.

Hata hivyo, tathmini ya ukaguzi katika utendaji wa Kamati za Ukaguzi katika Wizara, Idara, Sekretari za Mikoa ilibaini Taasisi 30 zikijumuisha Wizara na Idara 12, Sekretarieti za Mikoa 11, Mawakala 3, na Taasisi Nyingine 4 zilipatikana na mapungufu mbalimbali.

Orodha ya Taasisi zenye mapungufu kwenye Kamati za Ukaguzi zimeonyeshwa kwenye **Kiambatisho Na. 23**


Jedwali Na. 43: Tathmini ya Kamati ya Ukaguzi

Mwaka wa Fedha \ Taasisi	Idadi ya Wizara	Idadi ya Sekretarieti za Mikoa	Idadi ya Wakala	Idadi ya Taasisi Nyingine	Jumla ya Taasisi
2016/2017	6	18	3	0	27
2017/2018	12	11	3	4	30
Tofauti	6	(7)	0	4	3
Tofauti ya Asilimia					11.11

Jedwali la hapo juu linaonesha kuwa, kuna ongezeko la idadi ya taasisi zenye mapungufu katika Kamati ya Ukaguzi. Jumla ya taasisi zenye mapungufu mkubwa katika mwaka huu ni 30 ikilinganishwa na taasisi 27 za mwaka uliopita na kusababisha kuongezeka kwa taasisi 3, sawa na 11.11%. Hii inaonyesha kuwa hakuna maboresho katika mwaka huu.

Chati ya hapo chini inaonesha ulinganisho wa tofauti ya miaka miwili ya fedha kati ya 2016/2017 na 2017/2018 zenye mapungufu katika kamati ya ukaguzi.

Kielelezo Na. 28: Tathmini ya Kamati ya Ukaguzi



Kutokuwapo kwa ufanisi wa Kamati ya Ukaguzi kunaweza kupunguza ufanisi katika mazingira kwa jumla, na udhibiti wa utawala bora ndani ya Taasisi. Ni vigumu kuelewa kama Kamati ya Ukaguzi na wanachama wake hufanya kazi zake kwa usahihi. Hii ni kwa sababu hakuna njia ya kupima utendaji wao

Ninapendekeza Maafisa Masuuli kuimarisha Kamati ya Ukaguzi kwa kuboresha masuala ya utawala bora na udhibiti wa mazingira ya ndani ya taasisi na kuhakiki mwongozo wa Kamati ya Ukaguzi kwa kuweka sheria kwenye Kamati husika ili iweze kuwajibika. Ikiwa itashindwa kutekeleza majukumu yake na kutathmini utendaji wa kamati ya Ukaguzi angalau mara moja kwa mwaka.

6.5 Tathmini ya Usimamizi wa Vihatarishi

Tathmini ya vihatarishi ni jitihada za pamoja za kutambua na kuchambua matukio ya baadaye ambayo yanaweza kuathiri vibaya watu, mali, na mazingira na kufanya uamuzi "juu ya vihatarishi vinavyovumilika kutokana na uchambuzi wa vihatarishi" wakati unazingatia visababishi wakati wa kutathmini vihatarishi.

Tathmini ya vihatarishi inachambua kitu gani kinaweza kwenda vibaya, kiwezekanavyo kutokea, jinsi gani kinaweza kuvumilika, na ni sehemu ya hatua ya matokeo ya kuelezea vihatarishi katika mtindo wa kiasi au ubora.

Tathmini ya vihatarishi ni sehemu ya asili ya mkakati wa jumla wa usimamizi wa vihatarishi, ambao unajaribu, baada ya tathmini ya vihatarishi, "kuanzisha hatua za udhibiti ili kuondoa au kupunguza" matokeo yoyote yanayohusiana na vihatarishi.

Mwaka huu, tathmini ya Usimamizi wa vihatarishi kwenye sampuli za Wizara, Mikoa, Wakala na Taasisi nyingine, nilibaini kuwa taasisi 8 zilikuwa na mapungufu kwenye usimamizi wa vihatarishi. Nazo ni wizara 2, Sekretarieti ya Mikoa 3, Taasisi Nyingine 1 na Wakala 2. Taasisi hizi zina mapungufu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutokuwa na Rejista ya vihatarishi, kutokuwa na sera ya kudhibiti vihatarishi, kuwa na Rejista isiyoenda na wakati, pamoja na kukosekana kwa mpango wa kukabiliana na majanga.

Maelezo ya Taasisi pamoja na mapungufu ni kama inavyoonekana katika Jedwali hapo chini:


Jedwali Na. 44: Tathmini katika usimamizi wa vihatarishi

Taasisi Mwaka wa fedha	Idadi ya Wizara	Idadi ya Sekretarieti za Mikoa	Idadi ya Wakala	Idadi ya Taasisi Nyingine	Idadi ya Balozi	Jumla ya Taasisi
2016/2017	4	11	0	0	1	16
2017/2018	2	3	2	1	0	8
Tofauti	(2)	(8)	2	1	(1)	(8)
Tofauti ya asilimia						(50)

Jedwali hapo juu linaonyesha kwamba kuna kupungua kwa idadi ya taasisi zenye upungufu wa kusimamia vihatarishi. Jumla ya taasisi zenye upungufu katika mwaka huu ni 8 ikilinganishwa na mwaka uliopita ambapo zilikuwa 16 na kusababisha kupungua kwa taasisi 8, sawa na asilimia 50. Hii inaonesha kwamba kuna maboresho kwa mwaka huu wa fedha

Chati ya hapo chini pia inaonyesha picha ya tofauti ya miaka miwili ya fedha kati ya 2016/2017 na 2017/2018 zenye mapungufu katika tathmini ya usimamizi wa vihatarishi

Kielelezo Na. 29: Tathmini ya usimamizi wa vihatarishi



Kutokuwapo kwa sera ya usimamizi wa vihatarishi huhatarisha malengo ya taasisi na uwajibikaji wa wadau wote juu ya usimamizi wa vihatarishi ambavyo havijulikani; hatimaye huathiri utambuaaji na upunguzaji wa vihatarishi.

Ninashauri Maafisa Masuuli kuimarisha michakato ya usimamizi wa vihatarishi kwa kuhakikisha kuwa kuna tathmini ya vihatarishi, majibu ya vihatarishi, usimamizi wa vihatarishi na upatikanaji na utekelezaji wa mpango mkakati ulioidhinishwa ili kuwezesha taasisi katika kufafanua dira nzima ya kufikia malengo yake ndani ya kazi zake na mamlaka.

6.6 Kupitia Mifumo ya TEHAMA

TEHAMA ni dhana zinazozalisha bidhaa ambazo zitahifadhi, kupata, kuendesha, kutumikia, au kupokea taarifa za elektroniki kwa fomu ya kidigital kama vile; kompyuta binafsi, televisheni, barua pepe, au roboti.

Udhhibiti wa TEHAMA ni utaratibu au sera ambazo hutoa uhakika kwamba teknolojia ya habari inayotumiwa na taasisi inafanya kazi kama inavyotarajiwa; na kwamba, data ni za uhakika na taasisi inafuata sheria na kanuni zilizopo

Katika tathmini ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na udhhibiti wa mazingira katika Wizara, Idara, Wakala, Balozi, Sekretarieti ya Mikoa na Taasisi nyingine, nilibaini kuwa baadhi ya taasisi hazikuwa na sera ya TEHAMA, Mpango wa Mkakati wa TEHAMA, na hakuna mwendelezo wa kibiashara na mpango wa kuzuia majanga.


Matokeo ya ukaguzi yalionesha kwamba, katika sampuli ya taasisi 40 zilizopatikana na mapungufu ya TEHAMA, ni wizara 10, Sekretarieti ya Mikoa 11, Mawakala 8, Taasisi Nyingine 6 na Balozi 5 zilibainika na mapungufu makubwa katika TEHAMA. Baadhi ya mapungufu hayo ni kutokuandaa mpango na sera wa teknolojia ya habari na vifaa vya kuzuia majanga kama ilivyoonyeshwa katika Kiambatisho Na. 25

Jedwali Na. 6.5: Kulinganisha Tathmini ya mazingira ya Habari na Teknolojia ya Mawasiliano (TEHAMA)

Taasisi	Idadi ya Wizara	Idadi ya Sekretarieti	Idadi ya Mawakala	Idadi ya Taasisi Nyingine	Idadi ya balozi	Jumla ya Taasisi
Mwaka wa fedha						
2016/2017	5	13	0	0	13	31
2017/2018	10	11	8	6	5	40
Tofauti	5	-2	8	6	-8	9
Tofauti ya asilimia						29

Jendwali Na. 6.5 hapo juu linaonesha kuwa kuna ongezeko la idadi ya Taasisi zenye mapungufu ya TEHAMA. Jumla ya taasisi zenye mapungufu katika mazingira ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika mwaka huu ni 40 zikilinganishwa na 31 za mwaka uliopita. Hii inaonesha ongezeko la Taasisi 9 sawa na asilimia 29. Hii inaonyesha kuwa hakuna maboresho katika mwaka huu.

Chati ya hapo chini inaonesha ulinganisho wa tofauti ya miaka miwili ya fedha kati ya 2016/2017 na 2017/2018 zenye mapungufu katika TEHAMA.



Ukosefu wa mifumo ya habari ya upatikanaji wa kudhibiti unaweza kusababisha hatari ya kuwa na watumiaji ambao hawana ruhusa kupata mifumo ambayo inaweza kuathiri usiri wa mfumo, uaminifu na upatikanaji wa mifumo ya TEHAMA.

Ninapendekeza kwa Maafisa Masuuli wa taasisi husika kuhakikisha kwamba, mfumo una usimamizi sahihi. Serikali inapaswa kuwa na muundo mzuri wa mipango ya kukabiliana na majanga na mikakati ya

kuhakikisha kuwa vifaa vya kompyuta na programu vinatunzwa ili kuweza kukabiliana na majanga pale yanapotokea.

6.7 Tathmini ya Kutambua na Kuzuia Ubadhirifu

Ubadhirifu ni udanganyifu au uhalifu uliopangwa kutokea kwa matokeo ya kifedha au mataakwa ya kibinafsi.

Tathmini ya vihatarishi vya ubadhirifu ni chombo kinachotumiwa na menejimenti ili kutambua na kuelewa vihatarishi vya ubadhirifu kwa taasisi. Mara vihatarishi vikiwa vimetambuliwa, mpango unaweza ukaundwa ili kupunguza vihatarishi hivyo kwa kuanzisha udhibiti au taratibu na kuwaagiza watu kufuatilia na kutekeleza mpango wa kupunguza.

Kutokuwapo kwa tathmini ya vihatarishi vya ubadhirifu na taratibu zinazozuia uharibifu huvunja kanuni ya 35 (2) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 inayosema kwamba, 'kuzuia, kugundua na uchunguzi wa ubadhirifu wa ndani ni wajibu wa menejimenti, ingawa katika kufanya kazi za ukaguzi, mkaguzi wa ndani atakuwa mwanagarifu wa fursa, kama vile kudhibiti udhaifu ambao unaweza kuruhusu ubadhirifu na akihisi kuwepo kwa ubadhirifu ataijuza mamlaka husika ndani ya idara.

Katika mwaka huu, tathmini ya ubadhirifu katika taasisi nilizofanyia sampuli (Wizara, Sekretarieti ya Mkoa, Wakala, Taasisi nyingine na Balozi), nilibaini Sekretarieti 7 zilikutwa na mapungufu katika tathmini ya ubadhirifu. Ikulinganishwa na mwaka uliopita, balozi moja tu ilikuwa na mapungufu ya kudhibiti ubadhirifu. Mapungufu hayo yameoneshwa katika Kiambatisho Na. 26.

Uelewa mdogo wa sera za usimamizi wa ubadhirifu kati ya wafanyakazi wa idara unaweza kupunguza ufanisi na utekelezaji wa mafanikio yaliyofanywa. Hivyo, matokeo yaliyotarajiwa hayawezi kufikiwa; na udhibiti wa taasisi unaweza kuharibika na hatari kwa taasisi inaweza kuwa kubwa.

Ninapendekeza kuwa, tathmini inapaswa kufanywa na menejimenti na viongozi wanaohusika na kila idara muhimu au eneo ndani ya taasisi, kisha kushirikiana na menejimenti ya juu. Kwa pamoja, pande

zote zinaweza kutekeleza katika shughuli za kuzuia ubadhirifu ili kupunguza vihatarishi vilivyotambuliwa, na kuhakikisha kuwa kuna udhibiti.

6.8 Hitimisho

Nashauri Serikali kuendelea kufuatilia na kuboresha mifumo ya udhibiti wa ndani kwa kuwa na mifumo ya udhibiti ambayo inasaidia ufanisi katika kupunguza makosa ambayo hujitokeza katika taasisi. Pia, nashauri Wizara na menejimenti za Sekretarieti za Mikoa ziwekewe udhibiti wa ufanisi wa kuchunguza makosa haya katika mifumo ya udhibiti wa ndani na kuhakikisha kuwa tatizo hilo limetatuliwa.

Sura ya Saba

Ukaguzi wa Rasilimali Watu na Mishahara

7.1 Utangulizi

Sehemu hii inahusiana na kuonesha matokeo ya Ukaguzi wa rasilimali watu na mishahara kama ilivyokaguliwa katika Wizara, Sekretarieti za Mikoza na Balozzi. Katika Mwaka huu wa Fedha, nimebaini kupungua kwa changamoto mbali mbali ingawa bado kuna maeneo yanahitaji udhibiti zaidi. Miongoni mwa maeneo hayo yanaelezwa kwa kina katika aya zinazofuata kama yalivyoonekana katika Taasisi zilizokaguliwa.

7.2 Watumishi Wanaokaimu Nafasi za Ukuu wa Idara Kwa Zaidi ya Miezi sita.

Ukaguzi uliofanyika umebaini kwamba kuna watumishi wa umma 57 ambao wanakaimu nafasi zao kwa Zaidi ya kipindi cha miezi 6 kama ilivyonekana katika Taasisi 20, hii ni kinyume na matakwa ya kanuni namba D.24 (3) ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa umma ya Mwaka 2009 ambayo inataka watumishi kutokaimu kwa Zaidi ya miezi sita na mamlaka za uteuzi zinatakiwa kuteua ili kuziba nafasi zilizowazi ndani ya kipindi cha miezi hiyo sita. Orodha ya Taasisi zenye watumishi wanaokaimu zaidi ya kipindi cha miezi 6 ni kama ilivyooneshwa katika **Kiambatisho Na. 27**

Kushindwa kuwathibitisha watumishi katika nafasi wanazokaimu kwa zaidi ya miezi sita kunaweza kuathiri uwezo wao juu ya ufanyaji maamuzi na kuwaondolea morali ya kazi hivyo kuathiri utoaji Huduma katika Taasisi husika.

Ukilinganisha na taarifa yangu iliyopita, Mwaka huu inaonesha kukua kwa tatizo hili kwani kuna kuongezeka kwa Taasisi toka 15 za Mwaka uliopita hadi 20 kwa Mwaka huu wakati huo huo watumishi wanaokaimu kufikia 57 mwaka huu ukilinganisha na 50 wa Mwaka uliopita.

Nawashauri Maafisa Masuuli wote kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi Umma na Utawala Bora, kuwathibitisha

watumishi wanaokaimu nafasi zao kwa zaidi ya miezi sita na pia kwa nafasi zinazofahamika kuwa zitakuja kuwa wazi ziwekewe mpango wa kuzibwa kabla hazijatokea.

7.3 Upungufu wa Watumishi

Katika Mwaka huu wa Fedha pia nimeangalia kwa mara ingine tena tatizo la upungufu wa watumishi katika Taasisi mbali mbali kwani tatizo hili lina athari kubwa katika utoaji wa huduma na ufanisi wa Taasisi.

Mapitio niliyofanya katika ikama za Wizara, Wakala, Sekretarieti za Mikoa na Balozzi 62 inaonesha kwamba watumishi waliopo ni 9,714 ukilinganisha na mahitaji ya watumishi 19,469 ambayo inapelekea upungufu wa watumishi 9,755 sawa na asilimia 50.1 ya mahitaji, Kiambatisho Na. 28 kinaonesha kwa kina upungufu huu. Kuendelea kwa tatizo hili linahatarisha utendaji kazi wa Taasisi ikiwemo utoaji wa huduma hafifu kutokana na mlundikano wa kazi na kuchoka kwa watumishi waliopo.

Ukilinganisha na taarifa yangu ya Ukaguzi uliopita, upungufu wa watumishi unaonekana kushuka kutoka watumishi 34,081 katika Taasisi 52 kwa Ukaguzi uliopita hadi kufikia watumishi 9,755 katika Taasisi 62 katika Mwaka huu wa Ukaguzi, hii ina maana ya kuwa nafasi zilizowazi bado zinaendelea kujazwa.

Nawashauri Maafisa Masuuli wote kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi Umma na Utawala Bora kujaza nafasi zilizowazi au kufanya upya mapitio ya uhitaji wa watumishi ukilinganisha kwa watumishi waliopo na huduma zinazotakiwa kutolewa.

7.4 Kutozingatia mafunzo kwa watumishi

Kanuni namba G.1 (7) ya kanuni za Kudumu za Watumishi wa Umma ya Mwaka 2009 inasema kuwa, Taasisi zote zinatakiwa kuandaa mafunzo maalum kwa watumishi waliopo kazini kwa kuzingatia mahitaji ya mafunzo yaliotambulika wakati wa utendaji kazi zao. Kila Taasisi itatakiwa kutenga bajeti katika Mwaka wa fedha kwa ajili ya mafunzo.

Nilipopitia nyaraka katika Taasisi mbali mbali niligundua kuwa kuna Taasisi 5 (tano) hazikufanya tathimini ya mahitaji ya mafunzo wala kuwepo kwa mpango wa mafunzo kwa watumishi waliopo kazini kama ilivyooneshwa katika Jedwali Na. 45

Jedwali Na. 45: Orodha ya Taasisi ambazo hazikuwa na Mpango wa Uhitaji wa Mafunzo na Mafunzo kwa Watumishi.

Na	Fungu	Taasisi
1	16	Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali
2	91	Mamlaka ya Kuzuia Madawa ya Kulevya.
3	41	Wizara ya Katiba na Sheria
4	27	Msajili wa Vyama vya Siasa
5	92	Tume ya Kudhibiti Ukimwi

Chanzo: Taarifa za Mapungufu Kwa Menejimenti za Taasisi Husika kwa Mwaka 2017/18

Kukosekana kwa tathimini ya mahitaji ya mafunzo na kutofanya mafunzo kwa watumishi unahatarisha ufanisi wa Taasisi husika kwani watumishi watahondwa kujiendeleza katika utendaji wao wa kazi kuendana na uhitaji wa wakati huo kama vile maboresho ya taratibu mbali mbali, kutumia vifaa vipya vilivyoanzishwa na Taasisi na mabadiliko ya sheria, yote haya yanaweza yasifungamane na kazi za kila siku za watumishi. Hivyo, itasababisha ufanisi wa Taasisi usiendane na taratibu, sheria na matokeo yanaotarajiwa.

Hivyo ninawashauri Maafisa Masuuli wote kufanya tathimini ya uhitaji wa mafunzo kwa watumishi, kuandaa mpango wa mafunzo kwa watumishi wake kulingana na udhaifu ulioonekana kwa watumishi hao wakati wa utendaji wao wa kazi, kuandaa bajeti na kutekeleza mpango wao wa mafunzo kwa ajili ya uhai wa utoaji huduma katika Taasisi.

7.5 Makato Yaliozidi Ukomo katika Mishahara ya Watumishi

Kifungu namba 3 cha Sheria ya kurejesha Madeni ya mwaka 1970 inasema “ikitokea Afisa yeyote anadaiwa, pasipo kuwa na upendeleo wowote ule mamlaka inayohusika na Afisa huyo inaweza , kutafuta njia ya kurejesha deni hilo kwa kuruhusu Afisa huyo akatwe kidogo kidogo katika mshahara wake kila mwezi kwa kiasi kisichozidi robo moja ya mshahara wake na makato hayo kupelekwa katika mamlaka

inayohusika na ikitokea Afisa huyo ana madeni zaidi ya moja basi kiasi kinachoruhusiwa kukatwa kila mwezi kisizidi theluthi mbili ya mshahara wa mwezi”.

Halikadhalika, Waraka wa Serikali wenye kumbukumbu namba C/CE.45/271/01/1/87 wa tarehe 19 mwezi wa tatu 2009 uliotolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora ukiwaelekeza Maafisa Masuuli wote kuhakikisha kuwa, makato yote ya mishahara ya watumishi kwa ajili ya marejesho ya madeni katika mwezi yasizidi theluthi mbili ya mshahara wa mtumishi kwa mwezi.

Kinyume na matakwa ya sheria na Waraka nilioutaja hapo juu nimebaini mishahara ya watumishi 229 imekatwa juu ya theluthi moja, Makato haya yameshuhudiwa katika Taasisi 7 zilizokaguliwa kama zivyoonekana katika Jedwali Na. 46

Jedwali Na. 46: Orodha ya Baadhi ya Taasisi zilizokata Makato makubwa katika mishahara

Na.	Fungu	Taasisi	Idadi ya Wafanyakazi
1	50	Wizara ya Fedha na Mipango	21
2	63	Sekretarieti ya Mkoa-Geita	30
3	81	Sekretarieti ya Mkoa- Mwanza	18
4	86	Sekretarieti ya Mkoa -Tanga	39
5	78	Sekretarieti ya Mkoa -Mbeya	21
6	36	Sekretarieti ya Mkoa -Katavi	16
7	75	Sekretarieti ya Mkoa- Kilimanjaro	84
Jumla			229

Chanzo: Barua ya Ukaguzi kwa Menejimenti

Katika hali hii, watumishi ambao wanapokea kipato kidogo tofauti na matarajio wataanza kutafuta njia mbadala za kuongeza kipato ikiwemo ubadhirifu wa muda ama mali za Taasisi na kupoteza uwezo katika kujikita na kazi zao hivyo, kupelekea kutotekeleza majukumu yao kama inavyotakiwa.

Kama ilivyokuwa katika taarifa yangu iliyopita Mwaka huu pia kuna muendelezo wa kutozingatia sheria hii.

Ulinganisho niliufanya katika taarifa hii na ile iliyopita inaonesha kuwa uhibititi katika kuzuia watumishi wasikope zaidi unaendelea

kushuka kwani Mwaka wa fedha 2016/2017 kulikuwa na Taasisi 12 zenye watumishi 278 wakati Mwaka huu Taasisi zilizopitiwa 7 zina watumishi 229 wanakatwa kiwango kikubwa kutokana na mikopo iliyokopwa katika Taasisi mbali mbali na hivyo kupelekea kupokea mshahara chini ya theluthi mbili kwa mwezi.

Katika hali hii bado naendelea kusisitiza katika ushauri nilioutoa kuwa Maafisa Masuuli kuongeza udhibiti kwa watumishi kutokuwa na mikopo mingi na mikubwa kwa kutokopa hadi itakapo pitiwa na kuthibitishwa kuwa mkopo wa awali umeisha au hautavuka kiwango cha juu cha makato,

Pia kuwasiliana na wakopeshaji ili wasitoe mikopo kwa watumishi ambao Makato yatasababisha kupokea mshahara chini ya theluthi moja ya mshahara wa mwezi na ikitokea wamekopa pasipo Taasisi kujua basi inashauriwa wakopeshaji hao wasilipwe kupitia mshahara halikadhalika mfumo wa LAWSON utumike kama njia ya kudhibiti ukopaji holela.

7.6 Usimamizi Usiofaa kwa malipo mbali mbali yanayohusu watumishi TZS 1,372,897,958.5

Ukaguzi niliofanya katika usimamizi wa rasilimali watu na mishahara katika Taasisi 8 za Serikali Kuu nimebaini kuwa kuna muendelezo wa matukio niliyokwisha yatolea taarifa ikiwemo malipo ya watumishi ambao hayajalipwa kwa wakati, malipo ya mishahara na Makato ambayo wapokeaji wake hawajakiri kupokea, mishahara isiyolipwa ambayo haikurudishwa Hazina na malipo ya kazi za ziada ambazo hazikuoneshwa katika nyaraka na malipo kwa watumishi wasio hudhuria kazini. Mambo yote haya yanaelezewa kwa kina kwenye hapo chini na kwenye kiambatisho Kiambatisho Na. 29.

7.6.1 Stahili za Watumishi Ambazo Hazijalipwa kwa Muda Mrefu kiasi cha TZS 591,662,727

Katika Ukaguzi huu nimebaini kuwa kuna malimbikizo ya madai ya watumishi kuanzia Mwaka 2011 kiasi cha TZS 591,662,727 yakijumisha mishahara itokanayo na kupanda vyeo, ajira mpya na posho ya kukaimu. Hili nimeliona kwa kupitia sampuli ya Taasisi mbili ambazo

ni Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano yenye madai ya TZS 204,161,612 na Sekretarieti ya Mkoa wa Rukwa TZS 387,501,115.

Kuchelewesha kulipa stahili za watumishi kunaweza kushusha motisha kwa watumishi katika utoaji huduma kwa Wananchi.

Ninawashauri Maafisa Masuuli wote kupunguza kuzalisha madeni mapya kwa kuandaa mpango na kuutumia kabla kuajiri, kupandisha vyeo na kuhamisha watumishi wakati huo huo Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora waajiri, kupandisha vyeo na kuhamisha watumishi kulingana na mpango wa Taasisi husika.

Pia, kwa madai yanayoendelea ninawashauri Maafisa Masuuli washirikiane na Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha wanalipa madai ya watumishi kufuatana na muda deni lilipozaliwa kwa wakati.

7.6.2 Marejesho ya Mishahara Isiyochukuliwa na Makato Ambayo Wapokeaji Wake Hawajakiri Kupokea TZS 230,092,901.96

Kutokana na sampuli ya Taasisi tatu nilizofuatilia nimebaini kuwa kuna malipo ya TZS 19,793,675 yamelipwa na Idara ya Zima Moto na Uokoaji kwenda Hazina ikiwa ni mishahara isiyochukuliwa malipo haya hayajaonekana kufika, TZS 113,157,780 iliyolipwa na Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza, fedha hii haijaonekana kufika PSPF na TZS 97,141,446.96 ilihusu malipo ya Makato kwenda Taasisi mbali mbali yaliofanywa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto nayo pia hayajaonekana kufika.

Kukosekana kwa nyaraka za kukiri mapokezi kunaweza kupelekea kumlipa asiestahili na hivyo kuzalisha deni upya.

Hivyo, naendelea kuwakumbusha Maafisa Masuuli wote kuwa ni jukumu lao kuhakikisha malipo yote wanayofanya yawe yana nyaraka za kukiri mapokezi kwa kiasi cha fedha kilicholipwa.

7.6.3 Mishahara Isiyochukuliwa na Makato ya Mishahara Ambayo Hayajapelekwa katika Taasisi husika TZS 227,883,921.55

Wizara ya Fedha na Mipango kupitia barua yake yenye namba za kumbukumbu EB/AG/485/01/Vol. V/32 ya tarehe 3 Juni 2016 (na kufutwa na ingine iliyotoka mnamo 31 agosti 2007) inawaelekeza

Maafisa Masuuli wote kurejesha fedha za mishahara ambayo haikuchukuliwa wanatakiwa kuituma Hazina katika akaunti iliyofunguliwa Benki Kuu lakini mapitio niliyofanya katika Taasisi 3 nilizozionesha katika jedwali namba 7.4 zinaonesha kuwa kuna kiasi cha fedha cha TZS 51,825,065.10 ikiwa ni mishahara isiyochukuliwa katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi fedha hizi hazikurudishwa Hazina, pia kuna kiasi cha TZS 176,058,856.45 yakiwa ni Makato ambayo hayakuwasilishwa katika Mamlaka mbali mbali katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi TZS 4,943,022, Wizara ya Maliasili na Utalii kuna TZS 168,268,834.45, na mwisho ni TZS 2,847,000 katika Sekretarieti ya Mkoa wa Iringa.

Kushindwa kupeleka mishahara isiyochukuliwa Hazina na kutopeleka Makato katika mishahara kwa mamlaka husika kunaweza kusababisha Taasisi kuzitumia fedha hizo katika matumizi yasiyo husika na kuzalisha madeni yasiyoweza kulipika.

Hivyo, ninawashauri Maafisa Masuuli kuhakikisha kuwa mishahara isiyochukuliwa inawasilishwa Hazina kwa wakati kama ilivyoelekezwa na Makato yote yawasilishwe kwa mamlaka husika ndani ya mwezi mmoja baada ya kukatwa katika mishahara wa mwezi.

7.6.4 Malipo ya kazi za ziada ambazo hazikuthibitishwa kiasi cha Sh 315,317,407.99

Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 2009, Kifungu namba L.24 (c) kinataka kulipwa kwa kazi za ziada ambazo zilisimamiwa na kuonesha kazi hizo zilifanywa nje ya muda wa kawaida wa kazi lakini mapitio niliyofanya katika Taasisi mbili niligundua kuwa kuna malipo ya kazi za ziada ambazo hazikuainishwa katika maombi ya madai, hazikusimamiwa wala kubainisha wahusika kama walifanya kazi nje ya muda wa kawaida wa kazi, hili limeonekana katika Wizara ya Mambo ya Ndani ambapo kiasi cha Sh 306,645,407.99 kililipwa na Tume ya Mipango ya Matumizi bora ya Ardhi ambayo ililipa kiasi cha kiasi cha Sh 8,672,000. Angalia kwa maelezo ya kina.

Kushindwa kudhibiti malipo ya kazi za ziada kunaweza kuvutia Watumishi kutumia muda wa kawaida wa kazi kufanya shughili zao

binafsi na zile za Taasisi kufanywa muda wa ziada ili kujipatia kipato, hii inaweza kupelekea kazi za Taasisi kuharibika kutokana makosa ya kibidamu yanayosababishwa na uchovu hivyo kuathiri utoaji huduma wa Taasisi.

Hivyo, ninawashauri Maafisa Masuuli kufuatalia malipo ya kazi za ziada kwa kuwapa Watumishi wito maalum kuendelea na kazi muda wa ziada na watumishi hao lazima wawepo katika kazi husika ambayo itakuwa na usimamizi.

7.6.5 Malipo kwa Watumishi Ambao Wamestaafu Kazi kiasi cha Sh 7,941,000

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imewalipa watumishi 2 waliomaliza muda wao wa utumishi kiasi cha TZS 7,941,000 ikiwa ni mishahara ya miezi 3 ambapo hadi tunamalizia Ukaguzi huu hakuna fedha iliyoonekana kurejeshwa. Kiambatisho Na. 29 inaonesha kwa kina.

Ulipwaji wa mishahara ya aina hii umeonekana kuendelea kushuka katika Mwaka huu kwani hatua zilizochukuliwa zimezaa matunda kwa kupunguza Idadi ya malipo kwa watumishi wasiokuwepo kazini.

Bado ninawashauri Maafisa Masuuli kuendelea kuwatoa katika orodha ya malipo ya mishahara Watumishi wote ambao hawakuhudhuria kazini na wale waliolipwa kimakosa wagunduliwe mapema na fedha zilizolipwa ziweze kurudishwa ili kuepuka hasara kwa Serikali.

7.7 Hitimisho

Ukiachilia mbali hatua madhubuti za makusudi zinazochukuliwa na Serikali kupitia kwa Maafisa Masuuli katika kuongeza udhibiti wa ndani katika usimamizi wa rasilimali watu na mishahara nimebaini kuwa bado kuna maboresho zaidi yanahitajika kwa hoja ambazo zinajirudia rudia kama vile watumishi wanao kaimu kwa Muda Mrefu, upungufu wa watumishi, Kukosekana kwa mafunzo kwa watumishi, makato Yaliozidi Ukomo Katika Mishahara ya Watumishi na Stahili za watumishi ambazo zinacheleweshwa kulipwa kwa wakati.

Uanzishwaji wa udhibiti wa ndani ambao matatizo yaliobainishwa yanaweza kuleta matokeo hasi katika uzalishaji wa huduma za

Taasisi, kwani hatua nyingi za utoaji huduma zinahitaji rasilimali watu hivyo tatizo lolote katika eneo hili linahitaji utatuzi wa kipekee ili kuepuka uvunjwaji wamaadili katika kulinda maslahi ya Taasisi.

Hivyo ninashauri Maafisa Masuuli kutoa taarifa mapema kwa mamlaka zinazohusika na uteuzi pindi inapotokea nafasi zilizo wazi huku pakiwepo na mpango kwa nafasi zinazotarajiwa kuwa wazi ili kuepuka kukaimu nafasi za kazi kwa muda mrefu, kufanya utathimini upya wa shughuli za Taasisi kulingana na mahitaji ya watumishi na kujazwa nafasi zilizowazi. Watumishi waliopo kazini wanatakiwa kupewa mafunzo kulingana na hitajiko na mpango wa mafunzo ulilopatikana wakati wa utendaji kazi zao za kila siku,

Mengine ni pamoja na mikopo kwa watumishi iwe inafatiliwa kwa kina kiasi ambacho hakuna mkopo utakao tolewa kama mtumishi atavuka Ukomo wa marejesho kupitia mshahara, stahiki za watumishi zilipwe ndani ya kipindi cha mwaka wa fedha kwa kuwa na mpango uliondaliwa kupitia visababishi vinavyoleta madeni hayo na kuratibiwa kwa mujibu wa kisababishi.

Sura ya Nane

Ukaguzi wa Wakala za Serikali na Taasisi Nyingine

8.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea matokeo ya ukaguzi wa Wakala wa Serikali 33²², Mifuko Maalumu ya Fedha 17²³, Taasisi Nyingine za Serikali 41²⁴, na Mabonde ya maji 14²⁵. Sura hii inaonesha masuala mahususi na mtambuka yanayohitaji kushughulikiwa na Serikali, Bunge, Bodi ya Ushauri ya Wizara na Menejimenti za Taasisi husika ili kuhakikisha ufanisi katika utendaji wa shughuli za taasisi hizo.

8.2 Matokeo ya Ukaguzi wa Wakala za Serikali

Yafuatayo ni matokeo ya ukaguzi wa Wakala wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018:

8.2.1 Utegemezi wa Ruzuku ya Serikali

Kifungu. Na. 12 (2) (a) cha Sheria ya Wakala wa Serikali Na 30 ya mwaka 1997, kinataka Wakala wote kufanya kazi zao kwa mujibu wa kanuni za biashara; na kuhakikisha kuwa, mapato yao yanatosha kulipia matumizi ya Wakala husika. Kifungu Na. 12 (3) kinataka sehemu ya mapato ya Wakala kutumika ndani ya Wakala hao na sehemu nyingine ipelekwe Mfuko Mkuu wa Fedha za Serikali.

Ifuatayo ni taarifa ya ukaguzi juu ya utegemezi wa Wakala kwa Serikali katika Ufadhili wa bajeti ya Matumizi ya Kawaida na bajeti ya Maendeleo: -

22 Kaguzi ya TARURA imeingizwa kwa mara ya kwanza kwenye taarifa hii. Hii imetokana na wakala kuanza kazi Mei 2017. NFRA na ADEM hazijaingizwa kwenye hii taarifa. Hii imetokana na ukaguzi kuwa unaendelea kipindi cha kutayarisha taarifa hii

23 Ukaguzi wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana haujaingizwa kwenye hii taarifa. Hii inatokana na kaguzi kuwa unaendelea kipindi cha kutayarisha taarifa hii.

24 Taasisi 3 zilijumuishwa kwenye taarifa hii lakini hazikuwa kwenye taarifa ya mwaka uliopita, nazo ni Bodi ya Usajili wa Mpango Mji, Taasisi ya Mafunzo ya Misitua na Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu.

25 Ukaguzi ya Bodi ya Bonde la Maji la Ziwa Tanganyika umejumuishwa kwenye taarifa hii ambapo kwenye taarifa ya mwaka uliopita haikujumuishwa.

Kumbuka: Maelezo ya hapo juu yanabainisha tofauti kati ya taasisi ambazo kaguzi zake zimejumuishwa kwenye taarifa hii na zilizojumuishwa kwenye taarifa ya mwaka 2016/2017 ambazo ni Wakala wa Serikali 33, Mifuko Maalumu ya Fedha 17, Taasisi Nyingine za Serikali 38 na Mabonde ya maji 14.

8.2.2 Uwezo wa Wakala wa Kujiendesha kwa kutumia mapato ya ndani kugharamia Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo

Kwa mwaka 2017/2018 mapato ya ndani yana uwezo wa kutekeleza bajeti kwa asilimia 16 tu ikilinganishwa na asilimia 18 ya mwaka wa fedha 2016/17. Tazama Jedwali la hapo chini

Jedwali Na. 47: Ulinganifu wa Bajeti kuu na makusanyo ya fedha kutoka vyanzo vya ndani

Mwaka	Jumla Kuu ya Bajeti (Shilingi)	Mapato ya ndani (Shilingi)	Asilimia ya mapato ya ndani katika bajeti kuu
2017/2018	2,486,084,953,29526	393,434,851,146	16
2016/2017	2,369,119,704,458	426,061,768,231	18
2015/2016	1,050,130,006,901	472,090,811,427	45

Chanzo: Taarifa ya fedha za Wakala za mwaka 2017/2018

Jedwali la hapo juu linaonesha kuwa, kwa ujumla wake Wakala wa Serikali hawawezi kujiendesha kwa kutumia mapato yao ya ndani kwa asilimia 84.

Mchanganuo wa kina wa ukusanyaji wa mapato ya Wakala za Serikali, unaonyesha kuwa, ni Wakala 16 (48%) tu ambao wana uwezo wa kutekeleza bajeti zao kwa asilimia 100; na zaidi, kwa kutumia mapato ya ndani. Wakala nyingine 17 (52%) hazina uwezo wa kutekeleza bajeti zao kwa kutumia mapato ya ndani, hivyo kutegemea ufadhili wa Serikali kujiendesha.

Mchanganuo wa makusanyo ya mapato ya Wakala wa serikali na ulinganifu wa uwezo wa kufadhili bajeti zao za matumizi umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 30

Nazishauri Menejimenti za Wakala 17 kuongeza mapato ya ndani kwa kubuni vyanzo vipya vya mapato, kuendesha shughuli zao kwa

26

Maelezo	Kiasi Sh.
Bajeti ya fedha za Maendeleo	1,439,929,313,468
Bajeti ya fedha za matumizi ya kawaida	1,046,155,639,827
Majumuisho ya Bajeti	2,486,084,953,295

kutumia mbinu za kisasa za kibiashara, pamoja na kupitia upya viwango vya tozo wanazotumia.

Pia, nazishauri Menejimenti za Wakala wote wa Serikali kuja na njia itakayoongeza kiwango cha makusanyo; na makusanyo yote ya ziada ya iwekwa katika mfuko mkuu wa fedha za serikali kama ilivyoelekezwa na Sheria ya Wakala za Serikali Na. 30 ya 1997.

8.2.3 Ulinganifu wa fedha iliyoidhinishwa na fedha iliyotolewa na Serikali

8.2.3.1 Fedha iliyoidhinishwa na serikali kwa matumizi ya kawaida haikutolewa Sh. 192,536,196,607

Kwa mwaka huu wa fedha 2017/2018, nimebaini kuwa Serikali haikutoa kiasi cha Sh. 192,536,196,607 (18%) ikilinganishwa na makisio ya Sh. 1,046,155,639,827. Kwa mwaka huu, fedha za matumizi ya kawaida zilizopokelewa na Wakala wa Serikali ni Sh. 853,619,443,220 ilikinganishwa na kiasi cha Shilingi 597,132,649,284 kilichopokelewa mwaka jana.

Fedha za matumizi ya kawaida zinazotolewa na Serikali kwenda kwa Wakala zimeongezeka kwa asilimia 43%²⁷ ikilinganishwa na mwaka jana. Tazama Jedwali la hapo chini

Jedwali Na. 48: Ulinganifu wa Fedha za matumizi ya kawaida zilizoidhinishwa na fedha iliyotolewa

Mwaka wa Fedha	Jumla Kuu ya Makisio (shilingi)	Fedha iliyotolewa (Shilingi)	Fedha ambayo haijatolewa (Shilingi)	Asilimia ya fedha ambayo haijatolewa
2017/2018	1,046,155,639,827	853,619,443,220	(192,536,196,607)	18
2016/2017	863,713,444,873	597,132,649,284	(266,580,795,590)	18
2015/2016	617,624,835,456	588,776,834,907	(28,848,000,549)	5

Chanzo: Taarifa ya fedha za Wakala za mwaka 2017/2018

27 Fedha iliyotolewa kwa matumizi ya kawaida kwa mwaka 2017-18 - Sh. 853,619,443,220
 Kutoa: Fedha iliyotolewa kwa matumizi ya kawaida kwa mwaka 2016-17 - Sh. 597,132,649,284
 Ongezeko la fedha zilizotolewa Sh. 256,486,793,936 (43%)

Jedwali la hapo juu linaonesha kuwa, shughuli za Wakala wa Serikali hazikufanikiwa kwa kiwango kinachokusudiwa kutokana na upungufu wa fedha Sh. 192,536,196,607, sawa na asilimia 18.

Mchanganuo wa fedha za matumizi ya kawaida zilizoidhinishwa na fedha halisi zilizopokelewa na Wakala umeoneshwa kwenye Kiambatisho Na. 31 Kiambatisho Na. 30

Sheria ya Wakala wa Serikali inawataka Wakala wote wa Serikali kujiendesha kwa kutumia mapato yao ya ndani. Kulingana na upungufu huo wa Fedha zilitolewa na Serikali, nawashauri Wakala wote wa Serikali kuboresha ukusanyaji wa mapato yao ya ndani ili waweze kujiendesha kulingana na sheria ya uanzishwaji wa Wakala.

8.2.3.2 Fedha ya Maendeleo kutolewa zaidi ya iliyoidhinishwa Sh. 272,874,426,737

Katika mwaka wa Fedha 2017/2018, kiasi cha Sh. 1,712,803,740,205 kilitolewa kwa ajili ya shughuli za maendeleo ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa ya maendeleo ya Sh. 1,439,929,313,468. Hii inasababisha kiasi cha Sh. 272,874,426,737, sawa na asilimia 119, kutolewa zaidi ya bajeti kama ilivyooneshwa kwenye jedwali. Wakala wa Barabara pekee alipokea jumla ya Sh. 1,228,696,742,000 dhidi ya bajeti iliyoidhinishwa ya Sh. 725,880,580,000; hivyo kuwapo kwa fedha iliyotolewa zaidi ya bajeti jumla ya Sh. 502,816,162,000.

Hata hivyo, kwenye mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali ilipeleka fedha za maendeleo zaidi ya Mwaka wa fedha uliopita kwa asilimia 163%²⁸. Angalia jedwali hapo chini:

28 Fedha za maendeleo zilizopelekwa kwa mwaka 2017-18 -	Sh. 1,712,803,740,205
Toa: Fedha za maendeleo zilizopelekwa kwa mwaka 2016-17 -	Sh. 651,350,345,808
Ongezeko la fedha za maendeleo	Sh. 1,061,453,394,397
Asilimia ya ongezeko	163%

Jedwali Na. 49: Ulinganifu wa Fedha za Maendeleo zilizoidhinishwa na fedha iliyotolewa

Mwaka wa Fedha	Jumla Kuu ya Makisio (Shilingi)	Fedha iliyotolewa (Shilingi)	Fedha ambayo haijatolewa (Shilingi)	Asilimia ya fedha ambayo haijatolewa /Kutolewa zaid
2017/2018	1,439,929,313,468	1,712,803,740,205	272,874,426,737	19
2016/2017	1,505,406,259,577	651,350,345,808	(854,055,913,769)	(57)
2015/2016	432,505,171,445	822,491,065,815	389,985,894,370	90

Chanzo: Taarifa ya fedha za Wakala za mwaka 2017/2018

Mchanganuo wa fedha za maendeleo zilizoidhinishwa na fedha halisi zilizotolewa umeonyeshwa kwenye Kiambatisho Na. 32.

Hii inadhihirisha kuwa, bila ya bajeti za ziada kupata idhini stahiki, kiasi cha ziada cha fedha kilichotolewa kinaweza kutumika kwa matumizi yasiyokuwa ya lazima.

Nazishauri menejimenti za Wizara ya Fedha na Mpango, kutoa fedha kuendana na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge, na kama kuna hitaji zaidi ya bajeti, inashauriwa kuomba idhini ya kutumia fedha zaidi ya bajeti kutoka Bungeni.

8.2.3.3 Makusanyo ya Mapato kutoka vyanzo vya ndani kupungua kwa asilimia 8

Katika ukaguzi wa ukusanyaji wa maduhuli ya Wakala wa Serikali, nimebaini kuwa makusanyo ya mwaka 2017/2018 yamepungua kwa asilimia 8%²⁹ ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka 2016/2017.

Wakala wa Serikali 33 waliweza kukusanya kiasi cha Sh. 393,434,851,146 ikilinganishwa na bajeti ya Sh. 420,229,790,256 na hivyo kuwa na makusanyo pungufu ya Sh. 26,794,939,110 (6%). Angalia jedwali hapo chini:

29 Kiasi kilichokusanywa kwa mwaka 2017-18 -	Shs	393,434,851,146
Toa: Kiasi kilichokusanywa kwa mwaka 2016-17 -	Sh.	426,061,768,231
Anguko la makusanyo	Sh.	(32,626,917,085)
Asilimia la anguko		8%

Jedwali Na. 50: Ukusanyaji wa Maduhuli kutumia vyanzo vya ndani

Mwaka wa fedha	Makisio ya Maduhuli (Shilingi)	Makusanyo ya Maduhuli (Shilingi)	Kiasi (pungufu)/Zaidi kulinganisha na makisio	Asilimia ya makusanyo na ulinganisho wa makadilio
2017/2018	420,229,790,256	393,434,851,146	(26,794,939,110)	(6)
2016/2017	465,832,080,527	426,061,768,231	(39,770,312,297)	(9)
2015/2016	456,839,140,654	472,090,811,427	15,251,670,773	3

Chanzo: taarifa za fedha za Wakala kwa mwaka 2017/2018

Ukaguzi wa ukusanyaji wa Wakala mmoja mmoja umebainisha kuwa, Wakala 19 (58%) wamekusanya chini ya makisio yao. Wakala nyingine 14 (42%) wamefanikiwa kukusanya zaidi ya makisio yao. Tazama Kiambatisho Na. 32.

8.2.3.4 Ukaguzi wa Makusanyo yaliyotumwa kwenda Mfuko Mkuu wa Hazina

Kifungu. 11 (3) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa mwaka 2016) inawataka Wakala, Mashirika ya Umma, Mamlaka za Umma au Taasisi za Umma ambazo zinatoza na kukusanya ada za huduma zilizotolewa, mwishoni mwa kila robo ya mwaka wa fedha, kupeleka kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina asilimia kumi na tano (15) ya mapato kwa ujumla.

Katika ukaguzi wa mwaka huu, nilipitia Taasisi nane (8) na nikabaini Taasisi nne (4) zilitakiwa kuhamisha kiasi cha Sh. 15,452,199,835 kwenda Mfuko Mkuu wa Hazina, lakini ni kiasi cha Sh. 6,184,151,134 tu ndizo zilizohamishwa kinyume na Sheria tajwa hapo juu.

Taasisi tatu (3) zilihamisha kiasi cha Sh. 29,640,756,954 ambapo ni zaidi ya kiasi kilichohitajika cha Shilingi 20,808,053,039 kinyume na matakwa ya sheria. Hii inasababisha upotoshaji kwenye Taarifa za Kifedha za Taasisi husika pamoja na ukiukwaji wa Sheria.

BRELA iliamisha kiasi cha Sh. 1,012,818,000, sawa na asilimia 15 ya makusanyo ya Sh. 6,752,120,000 kama inavyotakiwa kisheria, kama ilivyoonyeshwa kwenye Kiambatisho Na. 33.

Pia, nilibaini kuwa Taasisi tatu (3) zilizohamisha fedha hazikuwa kwenye orodha ya Taasisi zinazotakiwa kupeleka fedha Mfuko Mkuu

wa Hazina kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Kifungu 11 (2) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebisha mwaka 2016);

Jedwali Na. 51: Taasisi ambazo hazikutakiwa kuhamisha Fedha kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina

Na	Taasisi
1.	Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori
2.	Wakala wa Usalama na Afya Kazini (OSHA)
3.	Mfuko wa Misitu Tanzania

Chanzo: Jedwali la Sheria ya Fedha za Umma, 2001

Serikali imeelekeza fedha zake za makusanyo ya ndani katika kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo ili kufikia uchumi wa ushindani unaoweza kuzalisha ukuaji endelevu na faida za pamoja. Kwa hiyo, nahimiza Taasisi tajwa kuhamisha asilimia 15 ya makusanyo ya jumla kwenda Mfuko Mkuu wa Hazina kama Sheria inavyotaka.

8.2.4 Mapugufu Yaliyoonekana Kwenye Ukaguzi Wa Wakala

8.2.4.1 Malipo ya ziada (riba) yanayodaiwa na wakandarasi kutokana na kuchelewesha malipo ya kazi walizofanya Sh. 57,094,951,223.34

Katika ukaguzi wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) nimebaini kuwepo kwa deni la Wakandarasi la kiasi cha Sh. 833,000,944,462.02, ambapo ndani yake kuna riba ya Sh. 57,094,951,223.34 iliyotokana na ucheleweshaji wa malipo hayo. Makubaliano ya kimkataba yaliyoingiwa na wakandarasi yanamtaka Wakala wa Barabara kumlipa Mkandarasi au Mshauri malipo ya ziada kama malipo yake yatachelewesha ndani ya muda uliotajwa kwenye Mikataba. Tazama Kiambatisho Na. 34

Menejimenti ilitoa maelezo kwamba upungufu na ucheleweshaji wa fedha za maendeleo kutoka Hazina ndio sababu kuu ya kutowalipa Wakandarasi na Washauri kwa muda sahihi.

Ni mtazamo wangu kuwa malipo haya ya ziada yanaweza kuepukika na fedha zikaelekezwa kwenye miradi mingine ya maendeleo.

Naishauri serikali kutoa fedha za utekelezaji wa miradi ya barabara kwa wakati kama ilivyoidhinishwa na Bunge ili kuepuka malipo ya ziada yanayotakana na riba.

8.2.4.2 Kutorudishwa kwa Fedha zilizokopwa kutekeleza miradi ambayo haikuidhinishwa Sh. 9,578,473,554

Katika ukaguzi wa Wakala wa Serikali nimebaini fedha kiasi cha Sh. 9,578,473,554 zilihamishwa kwenye matumizi yake yaliyoidhinishwa na kupelekwa kutekeleza miradi mingine. Mpaka mwisho wa mwaka 2017/2018 fedha hizo hazikurejeshwa kwenye miradi husika. Lengo lilikuwa ni kurejesha fedha pale tu Wakala atakapopata Fedha za Maendeleo kutoka Hazina na makusanyo ya madeni. Tazama Kiambatisho Na. 35.

Menejimenti ya Wakala ilitoa maelezo kwamba, ucheleweshaji wa fedha kutoka Hazina na Taasisi nyingine ndiyo sababu ya kukopa fedha kutoka kwenye vyanzo vingine.

Nina mashaka na urejeshwaji wa fedha zilizokopwa na kutumika kwenye shughuli ambazo hazikuwa na bajeti kama vile; sherehe za uzinduzi wa barabara. Pia makusanyo ya ndani kutumika kugharamia miradi ya wateja huweza kuathiri utendaji wa Wakala kutekeleza kazi zake zilizoidhinishwa.

Nashauri usimamizi wa Wakala wa Barabara Tanzania na Wakala wa Majengo Tanzania kurejesha kiasi kilichokopwa ili kufanikisha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

8.2.4.3 Kuchelewa kwa utekelezaji wa miradi inayosimamiwa na Wakala wa Majengo (TBA)

a) Kutokamilika kwa Ujenzi wa Miradi iliyopewa na Taasisi za Serikali Sh. 24,068,482,278

Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) aliingia mikataba na taasisi nyingine za Serikali kujenga majengo mapya katika mikoa mbalimbali.

Katika ukaguzi wa mwaka 2017/2018, nimebaini kulikuwa na ucheleweshaji katika utekelezaji na ukamilishaji wa miradi yenye thamani ya Sh. 24,068,482,278 kutokana na udhaifu mbalimbali kama ilivyoielezwa kwenye Kiambatisho Na. 36.

Aidha, kufuatia ziara nilizofanya kwenye miradi nilibaini udhaifu katika usimamizi wa vifaa vya ujenzi, mashine na wafanyakazi wenye ujuzi kama ilivyoelezwa hapo chini:

- i) Vifaa vya ujenzi vilivyotolewa na kutumiwa havikuwa na kiambatisho cha karatasi ya kipimo kutoka kwa Mhandisi wa Mradi ili kuthibitisha uhalisi wa matumizi hayo kuendana na bili ya vipimo (BoQ). Hii inamaanisha kwamba, ni vigumu kupima thamani ya kazi iliyofanyika na kuhalalisha kiasi kinachodaiwa katika Hati za Muda za Malipo (IPC).
 - ii) Vifaa vya ujenzi viliamishwa kutoka kwenye mradi uliokusudiwa kwenda katika miradi mingine. Hii ilisababisha uhaba wa vifaa kwenye maeneo ya ujenzi; hivyo kuchangia kazi kutokamilika kwa muda uliopangwa.
 - iii) Uhaba wa wafanyakazi wenye ujuzi na upungufu wa mashine za kutosha. Ilionekana kuwa miradi miwili ilikuwa inasimamiwa na Mratibu mmoja wa Mradi, na Vifaa kwa ajili ya mradi mmoja vilitumika kwenye miradi tofauti. Hii ilisababisha kasi ndogo katika utekelezaji wa miradi.
- b) Kuchelewa kukamilika kwa Ujenzi wa Nyumba za Magomeni na Nyumba za Makazi ya Gereza la Ukonga.**

Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) alipata maelekezo ya kujenga Nyumba za Magomeni na Nyumba za Makazi ya Gereza la Ukonga kutoka kwa Serikali. Taarifa za ujenzi ni kama ilivyooneshwa kwenye jedwali:

Jedwali Na. 52: Miradi inayoendelea

Na	Jina la Mradi	Tarehe ya Kuanza	Tarehe ya Kumaliza	Gharama ya Mradi (Sh.)
1	Ujenzi wa Nyumba za Magomeni	1 Octoba 2016	15 Februari 2018	20,000,000,000
2	Ujenzi wa Nyumba za Makazi ya Gereza la Ukonga	Machi 2017	5 Juni 2018	10,000,000,000

Chanzo: Taarifa ya Upungufu wa Menijimenti

Nilifanya ziara tofauti kwenye miradi tajwa hapo Januari 2019 na nilibaini mapungufu yafuatayo:

- i) Ujenzi wa nyumba za Magomeni ulikuwa katika hatua ya kufungwa kwa sakafu katika ghorofa ya nne. Pia, Ujenzi wa nyumba za makazi Gereza la Ukonga ulikuwa kwenye hatua ya kufunga sakafu katika ghorofa ya kwanza. Hata hivyo, ilibainika kuwa muda wa ujenzi ulikuwa umeisha kama inavyoonekana kwenye jedwali hapo juu.
- ii) Kutokuwapo kwa vifaa vya ujenzi kwenye eneo la Ujenzi
- iii) Ucheleweshaji wa utoaji wa fedha za ziada na Serikali ili kuwezesha kukamilika kwa miradi hii.

Udhibiti wa ndani usio na uwezo mzuri wa usimamizi wa mikataba, fedha za ujenzi kutolewa kwa kiwango cha chini na wateja na upungufu wa vifaa vya ujenzi ndio sababu kuu ya kasi ndogo katika kutekeleza miradi.

Maoni yangu kwamba, kuchelewa kukamilisha miradi kunainyima jamii haki ya kutumia huduma kwa wakati. Hii pia inaweza kusababisha hatari ya gharama za ziada kwenye miradi

Nashauri menejimenti ya Wakala wa Majengo (TBA) kuhakikisha kuna usimamizi wa kutosha katika miradi yote ili ikamilike ndani ya muda uliokubaliwa. Pia, ninahimiza uboreshwaji wa udhibiti wa ndani juu ya usimamizi wa fedha, vifaa vya ujenzi, mashine na wataalamu wa ujenzi ili kuharakisha kazi za ujenzi

8.2.4.4 Uwekezaji usio na tija wa Nyumba za Makazi huko Bunju, Dar es Salaam - Sh. 145,338,500,000

Katika mwaka wa 2012, Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) alianzisha uwekezaji wa ujenzi wa nyumba za makazi huko Bunju, Dar es Salaam. Mradi ulikuwa na makadirio ya ujenzi wa nyumba 851 zitakazozalisha mapato ya Sh 145,338,500,000 baada ya mradi kukamilika kama ilivyoielezwa katika jedwali hapo chini:

Jedwali Na. 53: Uwekezaji wa Nyumba usio na tija, Bunju

Aina ya Jengo	Makadirio ya Idadi	Idadi zilizokamilika	Bei kwa kitengo (Sh.)	Jumla ya Mapato Iliyopangwa (Sh.)
	144	0	220,000,000	31,680,000,000
	280	0	200,000,000	56,000,000,000
	96	0	180,000,000	17,280,000,000
	144	0	150,000,000	21,600,000,000
2-Storey (Villa)	29	34	280,000,000	8,120,000,000
Bungalow	10	18	175,000,000	1,750,000,000
Detached Low cost	23	18	49,500,000	1,138,500,000
Semi Detached Low Cost	26	24	38,000,000	988,000,000
Detached Medium	25	55	70,000,000	1,750,000,000
Semidetached Medium	74	70	68,000,000	5,032,000,000
Jumla	851	219		145,338,500,000

Chanzo: Taarifa ya mapungufu ya menejimenti

Mnamo tarehe 24 Juni na 3 Septemba 2015, Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) alifanikiwa kupata mkopo kutoka CRDB Bank Plc na PSPF wenye thamani ya Sh.19,500,000,000 na Sh. 3,500,000,000 ili kufadhili mradi husika. Mkopo huo uliambatana na makubaliano ya marejesho kutoka kwenye mapato ya mauzo ya nyumba hizo. Hata hivyo, tathmini yangu juu ya uwekezaji huo ilibainisha mapungufu yafuatayo:

- i) Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) alirejesha mkopo wenye thamani ya Sh. 21,059,668,320 wakati mapato yaliyopatikana kutoka kwenye mauzo ya nyumba ni Sh. 5,559,970,214 tu, kiasi cha ziada cha Sh. 15,499,698,106 kililipwa kutoka kwenye makusanyo ya ndani, kinyume na makubaliano yaliyotajwa hapo awali. Hii inamaanisha kwamba, shughuli zilizoidhinishwa kutekelezwa na makusanyo ya ndani hazikufanyika.
- ii) Mpaka sasa, ni nyumba 219 tu zilizokamilika kutoka kwenye matarajio ya ujenzi wa nyumba 851; hivyo nyumba 632 bado hazijakamilika. Katika nyumba ambazo hazijakamilika,

nyumba 60 ziko katika hatua mbalimbali huku ujenzi wake ukiwa umesimama tangu Machi 2018. Nyumba zilizobakia 572 ujenzi wake haujaanza mpaka kipindi cha ukaguzi Desemba, 2018

iii) Idadi ya nyumba 164 kati ya nyumba 219 zilizokamilika ziliuzwa na kuzalisha mapato ya Sh. 5,559,970,214. Menejimenti ilinitaarifu kwamba, kasi ndogo ya uuzaji wa nyumba zilizokamilika inatokana na uamuzi wa Serikali kuhamia Dodoma. Hii ni kwa sababu baadhi ya watumishi wa umma waliolipa malipo ya awali waliamua kuondoa maombi yao na kurejeshewa kiasi cha Sh. 426,132,800 (pitia taarifa ya kifedha ya Wakala)

Nashauri yafuatayo kwa Menejimenti ya Wakala wa Majengo (TBA):
(a) Kubadilisha mkakati wake wa masoko, ikiwa ni pamoja na kutafuta ushauri kutoka Wizara mama ili kuwezesha nyumba zilizokamilika kuuzwa kwenye umma kwa ujumla badala ya Watumishi wa Serikali; na (b) kuelekeza rasilimali zake kwenye Mji wa Dodoma badala ya Dar es Salaam, ambapo mahitaji ya nyumba kwa wafanyakazi yameshuka tangu kutolewa kwa agizo la kuhamia Dodoma.

8.2.4.5 Kutohamishwa kwa Fedha zenye thamani ya Sh. 6,655,417,488.24 na Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGA) kwenda kwa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA)

Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) alianzishwa kupitia Gazeti la Taifa na GN 211 ya 12 Mei 2017 kwa lengo la kutoa matengenezo endelevu na gharama nafuu za mtandao wa barabara za Vijijini na Mijini ili kusaidia maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini Tanzania. Wakala alianzishwa kutekeleza miradi ya barabara iliyokuwa inasimamiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Kifungu namba 17 cha Sheria ya Wakala ya mwaka 1997 (GN nambari 83 ya 2003) kinazitaka mali zote zinazohamishika na zisizohamishika, zinazohusiana na kuanzishwa kwa Wakala, tangia kipindi linachapishwa tangazo la kuanzishwa kwenye Gazeti, kuhamishiwa

maslahi yote, madeni, mashtaka, majukumu na muamana unaoathiri mali hizo.

Wakati wa ukaguzi nilibaini kwamba, jumla ya Sh. 6,655,417,488.24 hazikuhamishwa kutoka kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGA) kwenda kwa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) baada ya uanzishwaji wake. Fedha hizo zilijumuisha fedha za zuio la kazi (retention money), tozo ya ucheleweshaji kazi (liquidated damage) na fedha nyingine zilizokopwa kutoka kwenye akaunti za miradi ya matengenezo ya barabara. Angalia jedwali hapo chini:

Jedwali Na. 54: Fedha ambazo hazikupelekwa TARURA

Kipengele	Kiasi kilichotakiwa Kuhamishwa (Sh)	Kiasi kilichohamishwa (Sh)	Kiasi hakikuamishwa (Sh)
	A	B	[A-B]
Fedha za zuio la kazi (Retention money)	7,509,391,547.74	1,880,176,359.37	5,629,215,188.37
Tozo ya ucheleweshaji kazi (Liquidated damage)	336,551,627.05	12,701,368.35	230,576,773.76
fedha zilizokopwa	1,089,460,033.14	293,834,507.03	795,625,526.11
Jumla	8,935,403,207.93	2,186,712,234.75	6,655,417,488.24

Chanzo: Taarifa ya Mapungufu kwa Menejimenti

Nilibaini zaidi kuwa, Mamlaka za Serikali za Mtaa saba (7)30 bado hazikusaini Mkataba wa Maelewano na Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA), ikiwa ni kinyume na barua ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) yenye namba ya Kumb Na. AE.35/488/01/104 ya tarehe 5/10/2017 iliyowaelekeza Wakurugenzi wa Halmashauri kuhamisha kazi zote za barabara na majukumu pamoja na rasilimali zote muhimu kwa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA).

Uchunguzi wangu unaonesha kwamba, Serikali za Mitaa 84 hazikuhamisha fedha zinazohusiana na zuio la kazi, Mamlaka za Serikali za Mitaa 18 hazikuhamisha fedha zinazohusiana na tozo ya ucheleweshaji kazi; na Serikali za Mitaa 13 hazikuhamisha fedha zilizokopwa kutoka kwenye Akaunti za Mfuko wa Barabara, kama ilivyoonyeshwa kwenye Kiambatisho Na. 37 (A-C)

30 Bukombe DC, Chato DC, Geita DC, Tanga CC, Mwanga DC, Kilosa DC and Temeke MC

Kutohamishwa kwa fedha hizo kunaweza kuathiri uendeshaji wa Wakala wakati wa kulipa madeni ya nyuma. Kwa hiyo, nazihimiza Halmashauri tajwa kuhamisha mali na madeni yote yanayohusiana na miradi ya barabara kwa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) na; Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) inapaswa kufuatilia utekelezaji.

8.2.4.6 Tozo ya ucheleweshaji kazi (Liquidated damage) ya Sh. 689,842,606 haikukusanywa kutoka kwa wakandarasi

Kifungu namba 112 (1) cha Kanuni za Manunuzi ya Umma 2013 (iliyorekebishwa mwaka 2016) kinasema kwamba taasisi ya manunuzi itatoza tozo ya ucheleweshaji wa kazi, huduma, bidhaa au vifaa.

Masharti ya Kanuni za Mikataba yanamtaka mwajiri kutoza tozo ya ucheleweshaji kazi kwa kiwango maalum kilichooneshwa kwenye mkataba, ikiwa mkandarasi hawezi kufanya kazi ndani ya muda ulioelezwa.

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa, Wakala wa Serikali wawili (2) hawakutoza tozo ya ucheleweshaji kazi (liquidated damages) yenye thamani ya Sh. 689,842,606 kwa wakandarasi waliochelewesha kazi zaidi ya muda uliokubalika kwenye mikataba, kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini;

Jedwali Na. 55: Fedha za ucheleweshaji wa kazi ambazo hazijakusanywa

Na	Wakala	Kiasi	Maelezo
1	Wakala wa Vipimo (WMA)	510,086,299	Ujenzi wa Jengo la Ofisi - mkoa wa Kilimanjaro
2	Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA)	179,756,307	Miradi mbalimbali ya ukarabati wa Barabara
	Jumla	689,842,606	

Chanzo: Taarifa ya mapungufu kwa Menejimenti

Ni maoni yangu kuwa, kushindwa kuwatoza wakandarasi tozo ya ucheleweshaji kazi kutafanya gharama zilizoongezeka baada ya ucheleweshaji wa kazi kulipwa na mwajiri badala ya Mkandarasi. Hivyo basi, nashauri menejimenti ya Wakala; (a) kutoza kiasi cha Sh.

689,842,606 kwa wakandarasi waliochelewesha kazi na; (b) kufuata kikamilifu masharti ya mkataba kwa ufanisi wa usimamizi wa miradi

8.2.4.7 Ukaguzi wa Wakala wa Mabasi yaendayo Haraka (DART)

Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) ni mfumo wa Usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka unaunganisha sehemu mbalimbali za Dar es Salaam na sehemu ya biashara katikati ya Mji. Nilipitia shughuli za Wakala ya Mabasi Yaendayo Haraka na nilibaini udhaifu ufuatao:

a) Kukosekana kwa Mtoa Huduma na Mabasi ya kutosha

Nimepitia utendaji wa Wakala kuendana na mpango wa kimkakati wa mwaka 2009/10 mpaka 2014/15 ambapo tathmini ya hali halisi ya utekelezaji wa mpango huo ilifanyika na kuoneshwa kwenye mpango wa sasa ulioanzia 2016/17 mpaka 2020/21. Nibaini ya kwamba, kuna mtoa huduma mmoja tu tofauti na mpango uliowekwa wa kuwa na watoa huduma wawili kuanzia mwezi Juni 2015.

Pia nilibaini kuwa, Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) alitarajia kuwa na jumla ya mabasi 305 kuanzia Juni 2015. Hata hivyo, ni mabasi 140 tu ndiyo yanafanya kazi huku kukiwa na ongezeko la abiria linalokadiriwa kutoka 77,000 mwezi Mei 2016 hadi 200,000 mwezi Juni 2017. Kukosekana kwa mtoa huduma na mabasi ya kutosha kunasababisha mabasi yaliyopo kujaa zaidi ya uwezo; hivyo kuchangia uchakafu, kuharibika kwa mabasi pamoja na usumbufu katika utoaji huduma.

b) Upotefu wa Sh. 54,362,000 uliotokana na kutotumika kwa ardhi iliyokodiwa

Mnamo tarehe 30 Machi 2011, ulisainiwa Mkataba wa Makubaliano kati ya Tanzania Friendship Textile Co LTD na Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART). Sehemu hizo mbili zilikubaliana juu ya uanzishwaji na matumizi ya eneo la Urafiki kati ya China na Tanzania kwenye barabara ya Morogoro katika Wilaya ya Kinondoni, ili kuwezesha kazi ya mradi wa Usafiri wa haraka wa Mabasi Dar es Salaam (BRT). Eneo lilikodishwa kwa kipindi cha miaka 40 yaani mpaka 30 Machi 2051.

Nilibaini kwamba, kiasi cha Sh. 271,810,000 zililipwa kwa ujumla na Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) tangu mwaka 2011 kwa

kukodi mita za mraba 2,471 kwa Sh. 110,000 kwa mita kwa muda wa miaka 40. Hata hivyo, eneo lilokodishwa halikutumika kwa miaka 8 mpaka kufikia kipindi cha ukaguzi Desemba 2018. Hii ilichangia Wakala kupata hasara ya Sh. 54,362,000 (Sh 6,795,250 kodi ya mwaka mara miaka 8) kwa kutotumia ardhi kwa miaka hiyo minane (8).

Menejimenti ilitoa maelezo kwamba, nia ya DART ya kutumia eneo haikubarikiwa na wanahisa wa kiwanda cha Urafiki kati ya Serikali ya Tanzania na China licha ya kwamba DART alikuwa amelipia tayari eneo na kukabidhiwa. Inavyooneka, DART ataendelea kupoteza pesa nyingi kama jitihada za haraka hazitafanyika kutatua hali hiyo.

Nashauri yafuatayo kwa menejimenti ya DART; (a) kutafuta suluhisho mbadala ili kukabiliana na changamoto zilizopo kwenye huduma za BRT; (b) kudai fidia ya Sh. 54,362,000 kutoka Tanzania Friendship Textile Co Ltd; na (c) Kuendeleza ardhi iliyokodishwa bila kuchelewa zaidi.

8.2.4.8 Kutokuwepo na mikataba kwa wapangaji wa majengo ya Wakala wa Ugavi na Huduma za Manunuzi (GPSA)

Wakati wa ukaguzi nilipitia mikataba mbalimbali kati ya Wakala wa Ugavi na Huduma za Manunuzi (GPSA) (Mmiliki) na Wapangaji waliopangishiwa majengo ya Wakala nikabaini kwamba wapangaji 19 hawakuwa na mikataba. Pia, wakala alishindwa kukusanya jumla ya Sh. 587,706,543.60 kutoka kwa wapangaji hao kama ilivyoneshwa kwenye Kiambatisho Na. 38

Nina mashaka na usimamizi wa majengo hayo pamoja na mapato yanayotokana na majengo yaliyokodishwa. Hivyo, naikumbusha Menejimenti ya GPSA kuhakikisha wapangaji wote wana mikataba inayotambulika kisheria.

8.3 Ukaguzi Wa Taasisi Nyingine Za Serikali

8.3.1 Ukaguzi wa Uwekezaji, Viwanda, Miradi na uendeshaji wa Makampuni yanayosimamiwa na Jeshi la Ulinzi.

Katika ukaguzi wa mwaka 2017/2018, nimekagua shughuli za uzalishaji mali na uwekezaji zinazofanywa na SUMA-mradi wa matrekta, SUMA-Kampuni ya Ulinzi na SUMA-Kampuni ya Ujenzi. Pia, nimekagua kampuni ya uzalishaji mali ya Jeshi la Magereza, na Shirika la Nyumbu.

Yafuatayo ni matokeo ya Ukaguzi wa mashirika haya yanayoendeshwa na majeshi:

8.3.1.1 Matokeo ya Ukaguzi wa uwekezaji wa SUMA JKT.

SUMA JKT ni Taasisi ya kujitegemea iliyoanzishwa kisheria chini ya Sheria ya Uwezeshaji (Sura ya 23) ya 1974 (Sura ya 119 Iliyorejewa 2009) kwa amri ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1982. Kampuni hii inajihusisha na uwekezaji na uendeshaji wa miradi katika maeneo ya uhandisi na ujenzi, Kilimo na ufugaji, huduma za usalama, utengenezaji wa samani na uuzaji wa Matrekta na Vifaa vya Kilimo.

Yafuatayo ni matokeo ya Ukaguzi na Mapendekezo:

a) **Mkataba wa ubia usiyo na tija baina ya SUMA JKT na Equator Automech Company Ltd (EACL)**

Mnamo tarehe 13 Novemba 2009, SUMA JKT iliingia mkataba wa pamoja wa Ubia na Equator Automech Company Ltd (EACL) wa kuunda kampuni iitwayo EQUATOR-SUMA JKT Limited. Lengo la ubia lilikuwa kufanya uunganishi wa magari mazito, vipuri na masuala mengine. Mkataba huo ulibadilishwa tarehe 19 Agosti, 2015 kwa kurekebisha sehemu ya hisa, ambapo asilimia 70 ya hisa alipewa EACL na 30% kwa SUMA JKT.

Nilipitia nyaraka mbalimbali zinazohusiana na ubia na kubaini kwamba SUMA iko kwenye mchakato wa kujiondoa kwenye ubia kwa mujibu wa Ibara ya 14.10 ya Mkataba. Hii ni kutokana na mapungufu yafuatayo:

Shughuli za ubia hazikufanyika tangu kuundwa kwa kampuni na kusababisha kutopatikana kwa mapato kwa kipindi cha miaka 8. Hii ina maanisha kwamba, kampuni iliyotengenezwa nje ya ubia ni ya kidanganyifu kulingana na Kifungu Na. 400 (1) cha Sheria ya Makampuni No.12 ya mwaka 2002.

Mshirika wa Mradi wa Ubia, kampuni ya Equator Automech Company Ltd (EACL), alishindwa kutoa mtaji wa awali wa kiasi cha dola 2,133,000 kama alivyotakiwa na Ibara ya 6.1 ya Mkataba huo.

Haukufanyika upembuzi wa kina kabla ya kuingia ubia; pia, Mwanasheria Mkuu wa Serikali hakuhusika katika kuanzishwa kwa ubia huo.

Ni maoni yangu kwamba kutofanyika kwa upembuzi wa kina kabla ya kuingia kwenye makubaliano ndiyo sababu ya kuingia kwenye ubia usio na manufaa.

Nashauri yafuatayo menejimenti ya SUMA JKT; (a) kufanya upembuzi wa kina kabla ya kuingia katika ubia ili kupunguza hatari ya kuingiza rasilimali zake kwenye uwekezaji usio na faida; (b) kuchukua tahadhari zote ili kulinda maslahi ya kitaifa mpaka kukamilika kwa mchakato wa kujiondoa kwenye ubia.

b) Usimamizi na uendeshaji usioridhisha wa Mikataba ya Ubia kati SUMA JKT na Kampuni nyingine - Makao makuu ya SUMA

Sheria ya uanzishwaji wa SUMA inaitaka shirika hili kujihusisha na shughuli za uzalishaji mali, Ujenzi, Kilimo, Viwanda na nyinginezo. Kutokana na gharama na teknolojia kuwa kubwa, SUMA limejikuta likilazimika kuingia ubia na mashirika mengine ili kuwezesha kufanikisha shughuli zake. Nimekagua kuangalia ufanisi wa mikataba ya ubia na kugundua mapungufu kadhaa, kama yanavyooneshwa katika jedwali la hapo chini;

Jedwali Na. 56: Mapungufu katika Makubaliano ya Ubia

Makubaliano ya Ubia	Aina ya Shughuli	% za Hisa	
		40%	60%
SUMA JKT na Maoming Sino-Tanzania Great Wall Industrial & Trading Development	Sekta ya mavazi pamoja na shughuli zingine zinazohusiana		

Makubaliano ya Ubia	Aina ya Shughuli	% za Hisa	
Ltd			
SUMA JKT na ANIT ASFALT INS.TES.TAAH.SAN.TIC.AS (ANIT ASFALT) Formed Joint venture Company- SUMAJKT ANIT ASFALT	Kujiunga katika uzalishaji wa kokoto, na kuuza lami	30%	70%

Chanzo: Barua ya Ukaguzi kwa Menejimenti

Katika ukaguzi wangu wa nyaraka kuhusiana na makubaliano ya ubia nimebaini mapungufu yafuatayo:

- i) Kampuni zilizoanzishwa kwa ubia kukosa miundo ya uendeshaji wa siku hadi siku, mpango wa kazi, miundo ilyoandikwa ya Kampuni pamoja na Muundo wa timu ya usimamizi kutoka pande zote mbili. Hii inapelekea kutolindwa vizuri kwa kusudio na madhumuni ya SUMA JKT.
- ii) Umiliki wa Hisa usio na uhalisi. Nilibaini hisa za SUMA JKT katika ubia ni chini ya wastani wa udhibiti wa asilimia hamsini (50%). SUMA huchangia ardhi katika ubia, ambapo kwenye uwekezaji ni rasilimali muhimu sana. Hata hivyo, ardhi inayotolewa thamani yake haikuthaminiwa kuendana na uhalisia wa soko wa wakati huo. Hii inasababisha SUMA kupewa gawio dogo zaidi la hisa kuliko inavyostahili.

Kutofanyika kwa upembuzi wa kina na kutathimini thamani ya ardhi kabla ya kuingia kwenye makubaliano ndiyo sababu ya kupata gawio dogo la hisa.

Kwa kuwa Tanzania inakua kuelekea Uchumi wa Viwanda, nashauri menejimenti ya SUMA-Makao Makuu: (a) Kuhakikisha kuwa shughuli za uendeshaji wa kampuni zilizoanzishwa kwa ubia zimeelezwa vizuri kwenye nyaraka ili kuongeza ufanisi kwenye usimamizi na; (b) Mali zote zikadiriwe kwa thamani ya bei ya soko kabla ya kuingia ubia ili kupata gawio zuri la Hisa.

Katika ukaguzi huu, nimebaini kuwa katika makubaliano yote ya ubia hapo juu, hakuna taarifa yoyote ya faida, mapato au gawio iliyopatikana kwa SUMA JKT kutokana na ubia hizo.

8.3.2 Ukaguzi wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)

Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) ilianzishwa kama ilivyochapishwa katika Gazeti la Serikali, GN No.122, mwaka 2012, ikiwa inalenga kutoa Kadi za Vitambulisho vya Taifa kwa wananchi wa Tanzania, wakazi wa kisheria na wakimbizi ili kuimarisha amani na usalama wa Taifa na kuhifadhi maelezo ya msingi kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Katika mwaka huu wa ukaguzi nilipitia mkataba na uzalishaji wa vitambulisho na kubaini mapungufu yafuatayo:

8.3.2.1 Kasi ndogo ya Uzalishaji wa Vitambulisho vya Taifa

NIDA iliingia mkataba wa makubaliano wa miaka mitano na IRIS Corporation Berhad ya Malaysia (Mkandarasi) mnamo 21 Aprili 2011 kwa kiasi cha Dola za Kimarekani 149,956,303 kwa Manunuzi na ugavi wa vifaa na utekelezaji wa mfumo wa vitambulisho vya Taifa kulingana na Teknolojia ya 'Smartcard'. Muda wa mkataba ulianza 14 Septemba 2011 hadi Septemba 2016; na baadaye ukaongezwa hadi 14 Machi 2018.

Wakati wa ukaguzi (Januari 2019) nilibaini kuwa, uzalishaji wa Kadi za Vitambulisho umesimamishwa na mkandarasi kutokana na changamoto zifuatazo:

- i) Kutotolewa kwa fedha na Serikali kwa ajili ya kulipa deni la mkandarasi lenye thamani ya Dola 30,175,107,60 sawa na Sh. 69,983,747,348.10.
- ii) Kutoongezwa kwa muda wa mkataba kwa kipindi cha miezi kumi (10) tangu kuisha kwa kipindi cha mkataba, tarehe 14 Machi 2018.

Nilifanya tathmini kwenye uzalishaji wa vitambulisho na kubaini kwamba, Mamlaka ilikuwa ina mpango wa kusajili watu 22,268,463 ili ni watu 19,662,105 tu waliosajiliwa mpaka sasa ikiwa sawa na asilimia 88. Pia, nilibaini kuwa, kati ya watu 19,662,105 walioandikishwa, ni kadi 4,511,809 tu za vitambulisho ndizo zilizotengenezwa, sawa na asilimia 23 tu ya idadi ya watu walioandikishwa. Jedwali la hapo chini linaelezea takwimu hizi;

Jedwali Na. 57: Kasi ya chini ya Uzalishaji wa vitambulisho vya Taifa

Aina	Matarajio	Idadi ya waliosajiliwa	Vitambulisho vilivyotengenezwa
Wananchi	22,000,000	19,638,857	4,494,790
Wahamihaji halali	59,207	17,017	17,017
Wakimbizi	209,256	6,231	2
Jumla	22,268,463	19,662,105	4,511,809

Chanzo: Taarifa ya mapungufu kwa menejimenti

Nina mtazamo kwamba, lengo la NIDA halitofikiwa kama inavyotarajiwa bila ya Serikali kuingilia kati kwenye masuala ya fedha, ufuatiliaji na kutafuta ufumbuzi wa migogoro ya mkataba.

Kwa hiyo, nashauri Serikali: (a) kumlipa Mkandarasi madai yake bila kuchelewesha zaidi; (b) kutathmini utendaji kazi wa Mkandarasi na kuamua kama kumuongezea muda wa mkataba au kuingia kwenye Mkataba na Mkandarasi mpya.

8.3.3 Ukaguzi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA)

Katika ukaguzi wa Wakala wa umeme vijijini, nilikagua Mikataba na miradi ya Ujenzi wa Miundombinu ya Umeme inayotekelezwa na Wakala. Katika ukaguzi huu nilitembelea utekelezaji wa Mradi wa uenezaji wa umeme, ujenzi wa umeme mkubwa pamoja na Mpango wa Umeme Vijijini na kubaini yafuatayo;

8.3.3.1 Usimamiaji usioridhisha wa umeme katika Mkoa wa Kagera (REA Phase II)

Mnamo 18 Februari 2014, REA iliingia mkataba na M/s Urban and Rural Engineering Services kwa Mradi na Usambazaji wa Transfoma, nyaya za umeme wa kawaida na mdogo na Kuunganisha Umeme kwa Wateja katika maeneo ya Vijijini visivyo na umeme katika Wilaya za Biharamulo & Ngara, Karagwe, Wilaya za Kyerwa, Misenyi, Bukoba Vijijini na Muleba katika Mkoa wa Kagera kwenye sehemu (lots) 2, 3, 4, 5 & 6. Mkataba ulikuwa na thamani ya kiasi cha Sh. 110,792,506,113.18 (iliyorekebishwa kutoka Shilingi 98,373,054,560.75 kwa Mkataba wa Nyongeza uliosainiwa tarehe 28 Aprili 2016), huku muda wa kukamilika wa tarehe 27 Agosti 2015

ulisogezwa mbele hadi tarehe 30 Juni 2016. Hitilafu zifuatazo zilibainishwa kwenye ziara ya kufuatilia utekelezaji wa miradi:

- i) Vijiji 65 kutoka kipande (lot) cha 3, 4, 5 na 6 bado havijaunganishwa na huduma ya umeme kama ilivyoonekana kwenye ziara Oktoba 2018 (Angalia Taarifa ya Ukaguzi ya REA).
- ii) Vijiji 50 vilivyounganishwa na huduma ya umeme havikuwamo kwenye makubaliano ya mkataba; na mabadiliko hayo hayakuidhinishwa na Wakala. Hii ni kinyume na Kanuni 110 (3 - 4) ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 (Angalia Taarifa ya Ukaguzi ya REA).
- iii) Kuwapo kwa wateja waliolipia gharama za umeme ila bado hawajaunganishwa. Wakati wa kikao na Menejimenti, nilipatiwa idadi ya wateja kadhaa ambao wanasubiria kuunganishwa na huduma ya umeme zaidi ya mwaka mmoja, kama inavyoonekana katika Jedwali la hapo chini;

Jedwali Na. 58: Idadi ya wateja wanaosubiria huduma ya umeme

Na.	Wilaya	Kipande (Lot)	Mita
1	Karagwe	3	933
2	Kyerwa	4	252
3	Missenyi	5	64
4	Muleba	6	68
Idadi			1,317

Chanzo: Taarifa ya mapungufu

8.3.3.2 REA Awamu I na II: Kutokamilika kwa Utekelezaji wa Miradi kwa Wakati

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa, Miradi 37 ya Awamu ya I na II imechelewa kukamilika kwa kipindi cha miaka 2. Ucheleweshaji huu wa mradi unawanyima walengwa kupata huduma ya umeme, pia gharama za mradi zinaendelea kuongezeka.

Pia, nilibaini kuwa REA (kupitia TANESCO) haikutoa vyeti vya kukamilika kwa miradi 80 ya umeme ambayo ilikuwa imekamili kati ya mwaka 2008 na 2017. Hii inaashiria kuwa, ukaguzi wa ubora wa kazi haukufanyika; hivyo baada ya muda zile kasoro ambazo zitaweza kugundulika wakati wa ukaguzi zitasababisha uchakafu wa vifaa

ambao utagharimiwa na Mwajiri badala Mkandarasi. Maelezo ya miradi iliyochelewa ya Awamu I na II imeoneshwa katika jedwali hapo chini.

Jedwali Na. 59: Miradi ya REA iliyochelewa ya Awamu ya I na II

Mwaka Fedha	Idadi ya mradi ambayo haijapokea vyeti kukamilika vya	Idadi ya Miradi inayoendelea	Idadi ya miaka miradi iliyochelewa
2008/09	2	-	Cheti cha kukamilika kwa mradi hakijatolewa kwa miaka 7
2010/11	5	-	Cheti cha kukamilika kwa mradi hakijatolewa kwa miaka 5
2011/12	7	-	Cheti cha kukamilika kwa mradi hakijatolewa kwa miaka 4
2012/13	12	-	Cheti cha kukamilika kwa mradi hakijatolewa kwa miaka 3
2013/14	18	9	Cheti cha kukamilika kwa mradi hakijatolewa; na kazi ya wakandarasi 9 bado zinaendelea huku zikichelewa kukamilika kwa zaidi ya miaka 2.
2014/15	25	20	Cheti cha kukamilika kwa mradi hakijatolewa; na kazi ya wakandarasi 20 bado zinaendelea huku zikichelewa kukamilika kwa Zaidi ya mwaka 1.
2015/16	11	8	Cheti cha kukamilika kwa mradi hakijatolewa na kazi ya wakandarasi 8 bado zinaendelea huku zikichelewa kukamilika kwa Zaidi ya mwaka 1.
Jumla	80	37	

Chanzo: Taarifa ya Mapungufu

Usimamizi usioridhisha wa mkataba ni sababu kuu iliyochelewesha kukamilika kwa miradi hiyo. Hivyo basi, ninahimiza Menejimenti ya Wakala wa Nishati Vijijini (REA), kusimamia kwa ufanisi na kuhakikisha kwamba miradi yote inayotekelezwa inakamilika ndani ya muda uliowekwa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Pia, ninawahimiza wasimamizi wa Miradi kufanya ukaguzi wa pamoja juu ya ubora wa kazi zilizofanyika kwa wakati na kutoa vyeti kwa kazi zilizokamilika.

8.4 Ukaguzi Wa Bodi Za Mabonde Ya Maji

Bodi za Mabonde ya Maji zilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Udhhibiti wa Maji Na. 42 ya mwaka 1974 na marekebisho yake ya baadaye Sheria hii imechukuliwa na Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali Na. 11 ya mwaka 2009.

Katika ukaguzi huu, nimekagua Bodi za Mabonde ya maji 14 yafuatayo ni matokeo ya Ukaguzi huo:

Kutolewa Fedha pungufu katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo Sekta ya Maji Sh. 31,257,980,080

Bodi za Mabonde ya Maji zinapokea fedha za maendeleo kupitia Mradi wa Maendeleo sekta ya Maji. Nimepitia utoaji wa fedha za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na kubaini upungufu wa kiasi cha Sh. 31,257,980,080 (81%) kutoka katika bajeti iliyoidhinishwa ya Sh. 38,436,203,320.

Kwa ujumla, Mabonde haya yalipokea jumla ya Sh. 7,178,223,240 sawa na asilimia 19 ya bajeti nzima ya Maendeleo. Utoaji pungufu wa fedha umeathiri utendaji wa Bodi za Mabonde ya Maji. Tazama Jedwali na 8.12 hapo chini:

Jedwali Na. 60: Fedha pungufu zilizotolewa kwa Miradi ya Maji

Na	Jina la Taasisi	Makisio ya fedha za maendeleo (Sh.)	Fedha za maendeleo zilizopokolewa (Sh.)	Upungufu/(zaidi) (Sh.)	%
1	Bodi ya bonde la Maji la Ziwa Nyasa	1,050,000,000	241,709,409	808,290,591	77
2	Bodi ya bonde la Maji Ziwa Rukwa (LRBWB)	3,820,453,671	36,128,491	3,784,325,180	99
3	Bodi ya bonde la Maji Ziwa Tanganyika	1,148,500,000	-	1,148,500,000	100
4	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Handeni (HTMWSSA)	2,660,000,000	740,822,767	1,919,177,233	72
5	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Wanging'ombe (WANGIWASA)	-	-	-	-
6	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Makonde Plateu	3,199,692,000	955,651,802	2,244,040,198	70
7	Bodi ya Bonde la Maji la Ruvuma na Pwani ya kusini	2,440,500,000	1,916,127,933	524,372,067	21
8	Bodi ya Bonde la Maji la Rufiji	5,445,541,800	25,000,000	5,420,541,800	100
9	Bodi ya Bonde la Maji la ndani	3,000,000,000	954,854,544	2,045,145,456	68
10	Bodi ya Bonde la Maji la Pangani	250,000,000	44,618,000	205,382,000	82
11	Bodi ya Bonde la Maji la Wami-Ruvu	12,648,040,000	-	12,648,040,000	100
12	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mugango-kiabakari	324,000,000	445,662,000	-121,662,000	-38
13	Bodi ya Bonde la Maji la Ziwa Victoria	1,200,000,000	1,143,499,819	56,500,181	5
14	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Maswa	1,249,475,849	674,148,474	575,327,375	46
	Jumla	38,436,203,320	7,178,223,240	31,257,980,080	81

Chanzo: Barua ya Ukaguzi kwa Menejimenti kwa mwaka 2017/2018

Jedwali la hapo juu linaonesha kuwa Bodi hizi za Mabonde ya Maji zinahitaji fedha kwa ajili ya kutoa huduma ya maji kwa jamii.

Naishauri Wizara ya Maji, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha kutoa fedha za uendeshaji wa Bodi hizi za Maji kama ilivyo dhinishwa katika bajeti zao.

Fedha za Mradi wa Maendeleo ya Maji (WSDP) zilizotumika kwenye matumizi ya kawaida Sh. 88,378,660

Katika ukaguzi wa taarifa za fedha za Bodi za Mabonde ya Maji, nimebaini kuwa kati ya Bodi hizi 14, kuna Bodi 4 (28%) zimetumia kiasi cha Sh. 88,378,660 za fedha za maendeleo kwenye matumizi ya kawaida. Lengo lilikuwa kurudisha kiasi cha fedha pale tu watakapokusanya makusanyo ya ndani. Hata hivyo, hadi mwisho wa ukaguzi Desemba, 2018 kiasi kilichokopwa kilikuwa hakijarejeshwa kama inavyooneshwa kwenye jedwali lifuatalo:

Jedwali Na. 61: Fedha za maendeleo zilizotumika kwenye matumizi ya kawaida

a	Jina la Taasisi	Kiasi Sh.
1	Bodi ya Bonde la Maji la Ziwa Nyasa	10,200,000
2	Bodi ya Bonde la Maji la Pangani	35,354,360
3	Bodi ya Bonde la Maji Ziwa Tanganyika	28,664,300
4	Bodi ya Bonde la Maji la ndani	14,160,000
	Jumla (Tshs)	88,378,660

Chanzo: Barua ya Ukaguzi kwa Menejimenti kwa mwaka 2017/2018

Nilibaini kuwa sababu kuu ni makusanyo hafifu ya mapato ya ndani yanayosababisha kutumia fedha za maendeleo. Nashauri mamlaka za bodi za maji kuhakikisha fedha zote zilizokopwa zinarudishwa ili zitumike katika miradi ya maendeleo.

8.5 Ukaguzi Wa Mifuko Maalumu Ya Serikali

Udhibiti wa Mikopo inayotolewa na Mifuko Maalumu

8.5.1 Mfuko wa Udhamini wa pembejeo za kilimo (AGITF) - Kukosekana kwa Hati Miliki ya pamoja kwa Trekta zilizokopeshwa

Mfuko wa Udhamini wa Pembejeo za Kilimo (AGITF) ni mfuko unaojiendesha ulio chini ya usimamizi wa Bodi ya Wadhamini. Mfuko huo ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Bunge Na. 9 ya mwaka 1994 kwa lengo la kuunga mkono ununuzi na usambazaji wa pembejeo za

kilimo kupitia utoaji wa mikopo kwa wasambazaji wa pembejeo za kilimo.

Sehemu ya 3.3.5 (ix) ya Sera ya Mikopo ya AGITF (Mashine za Kilimo) inahitaji mashine iliyokopwa kuandikishwa kwa pamoja kati ya AGITF na Wakopaji mpaka ulipaji wa mkopo kukamilika

Wakati wa ukaguzi wa Mfuko wa Udhadini wa pembejeo za kilimo (AGITF) nilibaini Matrekta yaliyokopeshwa hayakuandikishwa kwa pamoja kati ya AGITF na mkopaji, kadi za usajili zilizopitia katika kaguzi zilionesha kwamba Matrekta yamesajiliwa kwa jina la mkopaji tu ikiwa ni kinyume na sera ya mikopo kama ilivyotajwa hapo juu. Baadhi ya Kadi zilizopitiwa zimeonyeshwa kwenye jedwali la hapo chini;

Jedwali Na. 62: Trekta ambazo hazina umiliki wa pamoja

Na	Kadi Na.	Aina	Mwaka wa kutengenezwa	Jina la mmiliki
1	T866 AQQ	Dong Feng Hong	2006	Alhaj Shaweji Abdallah
2	T515 ALQ	Fiat	1985	Ezekiel Malambo
3	T673 CNU	Tiger	2013	John Kabeya Joseph
4	T714 CFD	Sonalika	2011	Mwishehe Seif Kulita
5	T776 AYZ	Massey Ferguson	2007	Nemburis Samwel Kimbele
6	T840 AQA	Massey Ferguson	2006	Losierian Meiseye Loisujaki

Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi wa Mfuko kwa mwaka 2017/2018

Sababu kuu ni usimamizi usioridhisha wa mfuko kwenye kuhakikisha sera za mkopo zinafuatwa. Hii inaweza kuchangia mkopaji akauza trekta bila ya mfuko kutambua hivyo kusababisha mkopo kukosa dhamana na hasara kama atashindwa kurudisha mkopo. Hivyo basi, nashauri menejimenti ya AGITF kuhakikisha kwamba, matrekta yaliyokopwa yanasajiliwa kwa pamoja na yanasimamiwa vizuri na wakopaji ili kulinda thamani yake.

Masuala mengine ya kiukaguzi yaliyobainika katika ukaguzi wa Mifuko ya Serikali

8.5.2 Ukaguzi wa Mfuko wa Barabara kwa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

Fedha za Mfuko zilizokopeshwa kwenda Halmashauri hazijarudishwa Sh. 4,233,290,403

Kiasi cha Sh. 4,233,290,403 kililipwa kutoka Mfuko wa Barabara kwa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwenda Halmashauri ya Manispaa ya Ilala na Kinondoni ili kukidhi madai mbalimbali ya fidia. Hata hivyo, hadi mwishoni mwa ukaguzi, Desemba 2018, kiasi hicho cha fedha bado hakikuwa kimerejeshwa. Fedha hizo zilikopwa kutoka Mradi wa Maendeleo ya Mjini Dar es Salaam (DMDP), kama inavyoneshwa kwenye Jedwali la hapo chini;

Jedwali Na. 63: Fedha ambazo hazijarudishwa

Tarehe	Halmashauri	Kiasi (Sh)	Dhumuni
28/08/2017	Ilala Manispaa	1,274,030,103	Kulipia fidia kata ya Gongolamboto, Kiwalani and Ukongo
10/10/2017	Ilala Manispaa	436,102,400	Kulipia fidia Majichumvi-Kilungule
10/10/2017	Kinondoni Manispaa	2,523,157,900	Kulipia fidia Kilimani - Manzese
	Jumla	4,233,290,403	

Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti kwa mwaka 2017/2018

Hii inaonesha kwamba, shughuli zilizoidhinishwa hazikutekelezwa kama ilivyopangwa kutokana na upungufu wa fedha. Hivyo basi, ninahimiza Halmashauri husika kurejesha kiasi cha mkopo kwa Mfuko wa Barabara-OR TAMISEMI ili kufanikisha utekelezaji wa shughuli zilizoidhinishwa.

8.5.3 Ukaguzi wa Mfuko wa Taifa wa Uwekezaji katika Sekta ya Maji (NWIF)

Kuondolewa kimakosa na TRA kiasi cha Sh. 1,108,783,664 kwenye Akaunti ya Benki ya NWIF

Mnamo tarehe 19 Desemba 2017, Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA) ilitoa kiasi cha Sh. 1,108,783,664 kutoka akaunti ya benki ya NWIF kwa nia ya kufidia deni la muda mrefu la Kodi kwa Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

Menejimenti ilinitaarifu kwamba, fedha hizo ziliondolewa bila idhini yao na bila kuheshimu kwamba NWIF ni Taasisi, iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Usambazaji wa Maji Safi na Taka ya mwaka 2009. Kitendo hicho kilichangia kuathirika kwa utekelezaji wa shughuli zilizoidhinishwa.

Nashauri menejimenti ya Uwekezaji katika Sekta ya Maji (NWIF), kwa ushirikiano na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, kufuatilia na kuiomba Mamlaka ya Mapato ya Tanzania kurudisha kiasi tajwa kwenye Akaunti ya Benki ya Mfuko wa Taifa wa Uwekezaji katika Sekta ya Maji (NWIF).

8.5.4 Ukaguzi wa Bodi ya Maabara ya Binafsi ya Afya (PHLB)

Fedha kiasi cha Sh. 152,061,526.60 zilizokopwa na Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Wazee na Jinsia Hazijarudishwa

Katika ukaguzi wa shughuli za Bodi ya Maabara ya Binafsi ya Afya (PHLB) nilibaini kuwa, jumla ya Sh. 152,061,526.60 ilikopwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Wazee na Jinsia kwa miaka minne kuanzia fedha 2013/2014 hadi 2017/2018. Hata hivyo, kiasi hicho cha fedha hakikurejeshwa hadi mwisho wa ukaguzi huu Desemba 2018 kama inavyooneshwa kwenye jedwali;

Jedwali Na. 64: Fedha ambazo hazijarejeshwa na Wizara ya Afya

Mwaka wa	Maelezo	Kiasi (Sh.)
2017/18	Fedha alizokopa Wizara ya Afya	18,848,602
2015/16	Fedha alizokopa Wizara ya Afya	39,963,124
2014/15	Fedha alizokopa Wizara ya Afya	86,155,901
2013/14	Fedha alizokopa Wizara ya Afya	7,093,899.60
Jumla		152,061,526.60

Menejimenti ilinitaarifu kwamba, walishafanya mawasiliano mbalimbali na Wizara lakini bado hakuna kiasi kilichorudishwa. Hii inaonesha kwamba, Wizara ina desturi ya kukopa fedha kutoka kwenye Bodi hii mara kwa mara bila kurudisha, kitendo kinachoweza kuathiri shughuli zake.

Nashauri Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Wazee na Jinsia kurejesha kiasi walichokopa kutoka Bodi ya Maabara ya Binafsi ya Afya (PHLB) ili kufanikisha utekelezaji wa shughuli zilizoidhinishwa.

8.6 Mambo Mtambuka Yaliobainika Katika Ukaguzi wa Wakala, Mifuko Maalumu ya Fedha, Bodi za Mabonde ya Maji na Taasisi Nyingine za Serikali

8.6.1 Madeni ya Muda Mrefu Sh. 1,104,081,922,807

Katika mwaka wa fedha 2017/2018, nilibaini Madeni katika Wakala 33 wa Serikali, Taasisi 24 za Serikali, na Bodi 11 za Mabonde ya Maji yalikuwa yenye thamani ya Sh. 1,104,081,922,807.

Katika madeni yote ya Serikali, nimebaini kuwa kiasi cha Sh. 965,971,392,954 sawa na asilimia 87 ni madeni yaliyozidi miezi 12; na kiasi cha Sh.138,110,529,854 sawa na asilimia 13 ni madeni yaliojitokeza ndani ya miezi 12. Tazama Jedwali hapo chini:

Pia, nilibaini kuwa madeni yamepungua kwa kiasi cha Sh. 208,901,325,706 (16%)³¹ ikilinganishwa na madeni ya mwaka wa fedha uliopita 2016/2017 ya Sh. 1,312,983,248,513.

Jedwali Na. 65: Madeni yasiolipika

Kipindi	Mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2018	
	Kiasi (Sh.)	Asilimia
Ndani ya miezi 12	138,110,529,854	13
Zaidi ya miezi 12	965,971,392,954	87
Jedwali	1,104,081,922,807	100

Chanzo: Barua ya Ukaguzi kwa Menejimenti

Mchanganuo wa kina wa madeni haya umeonyeshwa katika Kiambatisho Na. 39

Sababu kuu ya kutokulipwa kwa madeni haya ya muda mrefu ni upungufu wa fedha zinazotolewa na Serikali wakati wa utekelezaji wa shughuli za Serikali. Kushindwa kulipa madeni kwa muda muafaka kunaathiri sifa za Taasisi za Serikali kwa Watoa huduma na Makandarasi.

Nashauri Taasisi za Serikali kulipa madeni yao kwa muda muafaka kwa kuongozwa na uchambuzi wa miaka ya madeni na kuunda mikakati ya

31 Madeni ya Mwaka 2017/18 - Sh 1,104,081,922,807
 Toa: Madeni ya Mwaka 2016/17 - Sh 1,312,983,248,513
 Kiasi kilichopungua cha deni Sh (208,901,325,706)
 Asilimia 16%

kulipa madai yao kwa muda ili kuepuka uwezekano wa kulipa adhabu kutokana na madeni hayo. Pia, udhibiti wa kutosha, sera na taratibu zinapaswa kuanzishwa na Menejimenti ili kuhakikisha kuwa Taasisi zinawajibika kwa mikataba wanayoingia bila kuwa na fedha.

8.6.2 Madai ya serikali yasiyokusanywa Sh. 558,144,649,635

Katika mwaka wa fedha 2017/2018, nilibaini kuwa jumla kuu ya madai ya Serikali kutoka kwa Wakala wa Serikali 33, Taasisi za Serikali 33, na Bodi za Mabonde ya Maji 13 ni Sh. 558,144,649,635.

Katika jumla kuu ya madai ya Serikali nimebaini kuwa kiasi cha Sh. 422,867,433,636 (76%) ni madai yaliyokaa zaidi ya miezi 12 na kiasi cha Sh. 135,277,215,999 (24%) ni madai mapya yalio chini ya miezi 12

Pia nilibaini kuwa madai yamepungua kwa kiasi cha Sh. 99,848,196,880 (15%)³² kulinganishwa na madai ya mwaka wa fedha uliopita 2016/2017 ya Sh. 657,992,846,515.

Kutokusanya madeni kwa muda muafaka kunapunguza rasilimali za Taasisi hizi katika kujiendesha, hivyo kushindwa kutimiza malengo yao. Tazama Jedwali la hapo chini:

Jedwali Na. 66: Madai yasiokusanywa

Kipindi	Mwaka wa fedha unaishia tarehe 30 Juni 2018	
	Kiasi (Sh.)	Asilimia
Ndani ya miezi 12	135,277,215,999	24
Zaidi ya miezi 12	422,867,433,636	76
Jedwali	558,144,649,635	100

Chanzo: Barua ya Ukaguzi kwa Menejimenti

Mchanganuo wa Madai haya ya Serikali yamechanganuliwa katika Kiambatisho Na. 40.

Naishauri Serikali kufuatilia kwa ukaribu madai yake yote kwa Wadaiwa wake na kuweza kukusanya madeni hayo pale muda wa kukusanya unapofika.

32 Madai kwa mwaka wa fedha 2017/18 - 558,144,649,635
 Toa: Madai kwa mwaka wa fedha 2016/17 - 657,992,846,515
 Kiasi kilichopungua (99,848,196,880)
 Asilimia 15%

8.6.3 Mapungufu yaliyojitokeza katika Ukaguzi wa Matumizi ya Taasisi za Serikali.

Wakati wa ukaguzi wa Wakala wa Serikali, Bodi za Bonde la Maji, Mifuko ya Fedha Maalum za Serikali na Taasisi nyingine za Serikali, nilibaini mapungufu mtambuka kwenye usimamizi wa matumizi ambayo yanahitaji kushughulikiwa na Menejimenti.

Mapungufu yote niliyoyabaini mwaka huu nilishayatolea taarifa katika taarifa zangu za miaka iliyopita. Hii ina maana kuwa utekelezaji wa mapendekezo yangu kwa Taasisi za Serikali ni mdogo.

Katika ukaguzi wangu wa mwaka wa fedha 2017/2018 nilibaini kuwa kuna: (i) Matumizi yenye nyaraka pungufu ya Sh. 1,347,912,012.83 (ii) Masurufu yasiyorejeshwa ya Sh. 380,947,840.76; na (iii) Malipo ya Sh. 88,356,439.84 yaliyofanywa bila kukata kodi za zuio.

Kwa kuwa mapungufu haya yote ya matumizi ya fedha za Serikali nilishayatolea taarifa kipindi cha nyuma, hivyo narudia kuisitiza kwa Menejimenti zote: (i) Kutengeneza mifumo imara ya uthibiti wa ndani ili kusaidia kutunza nyaraka zote za matumizi, (ii) Kurejesha masurufu yote ya kazi ambazo zimekamilika na (iii) Kuhakikisha Taasisi hizi zinaisaidia Serikali kukusanya Mapato kwa kukata Kodi ya zuio pale Taasisi hizi zinapokuwa zinafanya malipo ya huduma.

Katika ukaguzi wa ugavi na menejimenti ya mikataba, nimebaini kuwa kuna ukiukwaji wa Sheria ya Manunuzi. Nilibaini kuwa: (i) Kuna malipo ya Sh. 935,358,546.88 yaliyofanyika bila ya kukagua mali zilizonunuliwa; na (ii) Manunuzi ya Sh. 2,976,003,845.95 yaliyofanyika bila kupata idhini ya Bodi ya Zabuni.

Katika suala la utekelezaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma, ninazishauri menejimenti: (i) Kuhakikisha kuwa Vifaa vyote vinavyonunuliwa vinakaguliwa na Kamati Maalum ya Ukaguzi kabla ya malipo kufanyika; na (ii) Zabuni zote zipitishwe kwenye Bodi ya Zabuni kuweza kupata idhini ya Bodi.

Pia, nilibaini kuwa kuna malipo yaliyofanyika bila kufuata utaratibu wa kibajeti. Katika suala hili nilibaini kuwa: (i) Kuna malipo ya Sh. 232,512,534 yaliyofanyika nje ya bajeti iliyopitishwa; na (ii) Malipo

ya Sh. 235,697,497.24 yaliyofanyika nje ya Makubaliano ya Mkataba baina ya Serikali na Bodi ya Mfuko wa Barabara. Hii sio tu inapotosha taarifa ya utekelezaji wa bajeti lakini pia Taarifa za fedha kutokua sahihi.

Kuhusu suala la matumizi yaliyofanyika zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa, ninashauri menejimenti kufuata Kanuni ya 46 (3) ya Kanuni za Fedha za Umma ya 2001 (Marekebisho ya mwaka 2004) na kuboresha udhibiti wa ndani katika kuhakikisha matumizi yanaendana na bajeti.

Kwa ujumla, mapungufu yaliyoorodheshwa hapo juu yanatokana na ukiukwaji wa Sheria ya Fedha ya Umma ya mwaka 2001 (iliyoboreshwa mwaka 2004), Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013, na Sheria ya Kodi ya mwaka 2008 ni Sh. 6,334,596,141.50. Mchanganuo wa Taasisi zilizopatikana na mapaungufu hayo katika matumizi ya fedha zinaonekana katika Kiambatisho Na. 41

8.6.4 Malipo yaliyofanywa na Serikali bila mikataba & Zabuni za ushindani Sh. 3,709,380,004.68

Katika kipindi cha ukaguzi, nilibaini kuwa Taasisi moja (1) ya Serikali ilifanya manunuzi ya bidhaa na huduma zenye thamani ya Sh. 258,189,948 kutoka kwa Wauzaji bila ya kuwa na mikataba; wakati Taasisi nne (4) zilifanya manunuzi yenye thamani ya Sh. 3,451,190,056.68 bila kuingia kwenye ushindanishi wa Zabuni kama ilivyooneshwa kwenye jedwali la hapo chini:

Jedwali Na. 67: Wakala waliofanya malipo bila Mkataba na Zabuni

Na	Taasisi	Kiasi(Sh.)	Maelezo
1	Wakala wa Uchimbaji	1,017,766,535.00	Ushindani wa zabuni haukuwepo
2	Kampuni ya Mzinga	258,189,948	Hakuna mkataba
3	Idara ya ujenzi wa Kitaifa - SUMA JKT	1,659,613,000.00	Ushindani wa zabuni haukuwepo
4	Idara ya Kilimo na Viwanda - SUMA JKT	681,852,432.00	Ushindani wa zabuni haukuwepo
5	Baraza la Famasia	91,958,089.68	Ushindani wa zabuni haukuwepo
	Jumla	3,709,380,004.68	

Kwa maoni yangu, kukosekana kwa ushindani wakati wa Zabuni humanisha kuwapo kwa hatari ya kukosekana kwa uwazi na uaminifu

wa mchakato mzima wa manunuzi. Pia, ukosefu wa mikataba unaweza kusababisha migogoro ambayo haiko kisheria.

Nashauri menejimenti ya Taasisi za Serikali: (a) kuhakikisha shughuli yoyote ya manunuzi inakuwa na mikataba ya makubaliano; (b) kuhakikisha ushindani katika mchakato wa utoaji wa zabuni kama Kifungu. 163 & 164 cha Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013. Aidha, nashauri Wanasheria katika Taasisi za serikali husika kushauri vizuri jinsi ya kuboresha uhibitaji juu ya usimamizi wa mkataba.

8.6.5 Ukosekanaji wa Hati Miliki za Ardhi zinazomilikiwa na Taasisi za Serikali

Katika mapendekezo yangu ya ukaguzi wa mwaka 2016/2017 nilipendekeza Taasisi zote za Serikali kuwa na Hati zinazoonesha umiliki wa Ardhi zao. Katika ukaguzi wa mwaka huu wa 2017/2018 nilibaini kuwa Taasisi kumi na mbili (12) hazina Hati ya Umiliki wa Ardhi. Tazama Jedwali la hapo chini

Jedwali Na. 68: Taasisi za Serikali zisizokuwa na hati Miliki ya Ardhi

Na.	Jina la Taasisi
1	Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa (DDCA)
2	Wakala wa Maabara za Mifugo (TVLA)
3	Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA)
4	Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA)
5	Mamlaka ya Maji safi na Maji taka Mugango-Kiabakari
6	Mamlaka ya Maji safi na Maji taka Maswa
7	Bodi ya Bonde la Maji la Ruvuma na Pwani ya Kusini
8	Taasisi ya Maji
9	Bodi ya Bonde la Maji Rufiji
10	Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)
11	Bodi ya Bonde la Maji Pangani
12	Chuo cha Utumishi wa Umma

Chanzo: Barua ya Ukaguzi kwa Menejimenti

Kukosekana kwa hatimiliki ya Ardhi katika Taasisi za Serikali ni kinyume na maelekezo yaliyotolewa na Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maendeleo ya Makazi kupitia barua yake yenye Kumb Na. AB 225/305/01 ya tarehe 7 Septemba 2016. Barua hii iliwataka Wakuu wote wa Taasisi kuzitambua Ardhi zao, kuzithaminisha na kuomba kupatiwa Hati za umiliki za Ardhi hizo.

Ninazishauri Menejimenti za Taasisi za Serikali ambazo hazina Hati miliki za viwanja vyao kufuata maagizo yalioletolewa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuthaminisha Ardhi zao, na kuomba kupatiwa hati hizi na Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maendeleo ya Makazi.

8.6.6 Malipo yaliyofanyika bila kudai Risiti za Kielektroniki (EFD) - Sh. 7,956,320,106.61

Sheria ya Usimamizi wa kodi ya Mwaka 2017 Kifungu Na. 36 inamtaka kila mtu anayetoa huduma yoyote ile kutoa Stakabadhi kwa kutumia kifaa cha kielektroniki.

Katika mwaka huu wa fedha 2017/2018, Taasisi za Serikali 14 zilifanya malipo ya kiasi cha Sh. 7,956,320,106.61 bila Taasisi hizo kudai stakabadhi za kielektroniki kinyume na Kanuni Na. 28(1) ya Kanuni za Sheria ya Kodi ya Mapato (Mashine za Stakabadhi za Kielektroniki) ya mwaka 2012.

Mwaka 2016/2017 niliripoti kiasi cha malipo ya Shilingi 42,407,098,471 kutoka katika Wakala, Bodi za Mabonde ya Maji, na Taasisi nyingine za serikali yaliyofanyika bila kudai risiti za kielektroniki (EFD).

Kwa mwaka huu wa 2017/2018 tatizo hili la kutokudai risiti limepungua kwa kiasi kikubwa katika Taasisi za Umma na kufikia kiasi cha Sh. 7,956,320,106.61, sawa na asilimia 81 ikilinganishwa na kiasi cha Sh. 42,407,098,471 mwaka uliopita. Tazama Jedwali hapo chini


Jedwali Na. 69: Malipo yasiyokuwa na risiti za kielektroniki-EFD

Na	Jina la Taasisi	Kiasi (Shs)
1	Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA)	131,965,866
2	Wakala wa Umeme Vijijini (REA)	6,578,636,440
3	Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi	181,042,753
4	Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART)	48,384,400
5	Prisons Corporation Sole	90,113,356
6	SUMA Agriculture and industrial segment	531,852,850
7	Taasisi ya UONGOZI Institute	17,695,520
8	Mfuko wa Taifa wa Uwekezaji katika Sekta ya Maji (NWIF)	24,591,366
9	Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA)	71,183,915
10	Mamlaka ya Maji safi na Maji taka Makonde Plateu	3,287,700
11	Bodi ya bonde la Maji Rufiji	17,872,929
12	Wakala wa Ugavi na Huduma za Manunuzi (GPSA)	22,956,732
13	Chuo cha Uhasibu (TIA)	40,027,281
14	Bodi ya bonde la Maji Pangani	196,709,000
	Jumla	7,956,320,107

Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti kwa mwaka 2017/2018

Mwenendo wa kutokuchukua EFD kwa Wakala wa Serikali kwa miaka miwili unaoneshwa katika chati ya hapo chini.

Kielelezo Na. 2: Malipo yasiyokuwa na Stakabadhi za Kielektroniki



Kwa mujibu wa kielelezo cha hapo juu, Taasisi zisizochukua Stakabadhi za Kielektroniki zimefungua kwa asilimia 26, wakati kiasi cha malipo kisichokuwa na stakabadhi za kielektroniki kimefungua kwa asilimia 81 ikilinganishwa na kiasi cha mwaka jana.

Nashauri Serikali iendelee kutoa elimu juu ya utekelezaji wa hiari wa Kanuni na Sheria ya Kodi ya Mapato za mwaka 2012 kuhusu matumizi ya hiari ya mashine za EFD zitakazochangia kwa kiasi kikubwa kuongeza mapato ya Serikali kama kila Manunuzi ya Serikali yataambatana na Stakabadhi za Kielektroniki.

8.7 Mapungufu yaliyobainika kwenye Usimamizi wa Mikataba ya Miradi ya Barabara

8.7.1 Usimamizi Usiojitosheleza wa Mikataba ya Ushauri na Ujenzi kwenye Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Kisesa-Usagara kwa Kiwango cha Lami

Tarehe 26 Machi 2013, Wakala wa Barabara (TANROADS) iliingia mkataba na kandarasi M/S Nyanza road Works Limited kujenga Barabara ya Usagara-Kisesa (km 16) kwa kiwango cha lami kwa gharama ya Sh.17,898,375,742.50 (kiasi hicho kilifanyiwa mapitio na

kuwa Sh. 20,328,392,742.50). Mkataba ulianza tarehe 2 Mei 2013 na ulikuwa unatakiwa kukamilika tarehe 01 Agosti, 2014, ila marekebisho yalifanywa mpaka tarehe 31 Machi, 2018.

Wakati wa ukaguzi wa kiufundi Oktoba 2018 nilibaini kuwa, gharama ya mkataba iliongezeka kwa kiasi cha Sh. 2,430,017,000. Ongezeko hili kutoka Sh. 17,898,375,742.50 hadi Sh. 20,328,392,742.50 ambayo ni sawa na asilimia 13.5. Ongezeko hili la gharama lilisababishwa na ucheleweshwaji wa malipo ya fidia ya mali zilizokuwa ndani ya eneo la barabara. Hii inapingana na Kanuni Na. 5(2) (c) cha Kanuni ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 kilichotolewa kwa mujibu wa tangazo la Serikali Na. 446 la mwaka 2013 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2016) inayowataka watumishi wa umma na wajumbe wa bodi za zabuni wakati wa utekelezaji au uidhinishaji wa manunuzi, kuhakikisha bidhaa zinawasilishwa, huduma zinatolewa au utekelezaji wa kazi za ujenzi zinakamilishwa kwa wakati kwa mujibu wa vipaumbele vya tasisi inayofanya manunuzi hayo.

Pia nilibaini, kutokana na kutolipwa kwa fidia, mkandarasi alikabidhiwa eneo la kazi kwa utaratibu ambao sio rasmi na hivyo kusababisha kuchelewa kuanza kazi kwa kipindi cha kuanzia siku 270 hadi 3,338 (rejea Ripoti ya Ukaguzi wa Kiufundi). Hii, inapingana na Kipengele kidogo Na. 9 cha Masharti Maalum ya Mkataba (SCC) na Kipengele 23.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba (GCC) inayomtaka mwajiri kukabidhi eneo la kazi kwa kandarasi kwa tarehe iliyotajwa. Endapo mwajiri atashindwa kukabidhi eneo la kazi kwa muda uliokubaliwa, itasababisha kwa kiasi kikubwa kuchelewa na kuongezeka kwa gharama za mradi.

Kwenye, Mkataba wa Huduma za Ushauri kwenye ujenzi wa Barabara ya Usagara-Kisesa (Km 16) kwa kiwango cha Lami ambao ulioingwa na AARVEE Associates Architects Engineers & Consultants PVT Ltd (India) kwa gharama ya Sh. 1,123,000,000 kwa muda unaomalizika tarehe 05 Februari 2015. Nilibaini pia, kulikuwa na ongezeko la gharama kutoka Sh. 1,123,000,000 hadi Sh. 3,483,509,927. Ongezeko hili la gharama lilisababishwa na uchelewaji wa malipo ya mkandarasi mshauri wakati wa kipindi cha utekelezaji, na kuongezeka kwa muda wa usimamizi ulioongezwa kutoka tarehe 24 Januari 2016 hadi tarehe

31 Januari 2018. Hii pia, inapingana na Kanuni Na. 75 (1) ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma, tangazo la serikali namba 446 la mwaka 2013 (kama lilivyorekebisha mwaka 2016) ambayo inazitaka tasisi zinazofanya manunuzi kuhakikisha fedha imetengwa kabla ya kuanza michakato ya manunuzi.

Kushindwa kuhakikisha upatikanaji wa fedha za kutosha kumeathiri mwenendo wa mradi iliyosababisha kuchelewa kukamilika na ongezeko la gharama kwa mkandarasi na mshauri kwa 13.5% na 210% kwa mtiririko huo (kwa mhandisi mshauri gharama iliongezeka zaidi ya mara tatu ya gharama za awali za mkataba).

Naushauri uongozi wa Wakala wa Barabara Tanzania, kuhakikisha upatikanaji wa fedha za miradi iliyoidhinishwa, ili kuzuia upotevu wa fedha za umma zinazotozwa kama riba ya ucheleweshaji wa malipo na makato mengine yanayohusiana na ongezeko la muda.

8.7.2 Usanifu Usiojitosheleza kwenye Ujenzi wa barabara ya Njia Mbili ya Sakina Tengeru (Km14.1) na Kutokidhi kwa Viwango vya Lami kwenye Barabara ya Mchepuko ya Arusha (Km 42.4)

Tarehe 12 Februari 2015, Wakala wa Barabara (TANROADS) iliingia mkataba na Hanil Jiangsu Joint Venture kutekeleza Ujenzi wa Barabara ya Njia mbili Sakina -Tengeru (km 14.1) na Barabara ya Mchepuko ya Arusha (km 42.4) kwa gharama ya Sh. 139,345,512,351 ikafanyiwa mapitio mpaka Sh. 185,241,986,981 ikiwa ni pamoja na Kodi ya Ongezeko la Thamani. Muda wa Mkataba ulikuwa ni miezi 33 mpaka tarehe 29 Machi 2018.

Wakati wa ukaguzi wa kiufundi uliofanyika Oktoba 2018, nilibaini usanifu usiojitosheleza uliotokana na kutozingatiwa kwa shughuli nyingine katika muundo wa awali. Hii ilisababisha, mapitio ya kina ya usanifu kufanyika wakati mkandarasi akiwa eneo la ujenzi na kuongeza gharama za mradi kwa Sh. 45,896,474,630, sawa na asilimia 33. Ongezeko hili la kazi lilijumuisha: kusanifu upya wima na unyoofu wa barabara ili kuepuka kugusa nyaya zinazopitisha mkondo mkubwa wa umeme; ujenzi wa kuta za kuzuia kifusi kinachojazwa kisiondoke wakati wa mvua kwenye daraja la kwanza; miundombinu ya

umwagiliaji kwa maeneo yaliyokatwa ambayo ililazimu kupita chini ya barabara ambayo ni chini zaidi kuliko ilivyokuwa awali; ununuaaji wa ardhi na kuhamisha miundombinu ya umeme na simu kwenye mizunguko miwili ya barabara; na kukata na kuondoa udongo usiofaa uliobainika wakati wa hatua za utekelezaji. Hii ilisababishwa mkandarasi mshauri kutosimamiwa vizuri na Wakala wa Barabara (TANROADS) kwenye hatua za awali za upembuzi yakinifu na usanifu.

Pia ukaguzi ulibaini, mapungufu kwenye ubora wa kazi. Matokeo ya vipimo vya uimara (stability value), uwezo wa kutiririka (flow value) na viunganishi (binder content) katika kipande cha barabara ya mchepuko kuanzia umbali wa kilomita (chainage) 35+90 hadi 42+373 havikukidhi kipimo cha viwango vinavyohitajika kwenye shughuli za barabara. Matokeo hayo yalitofautiana na kipimo cha Viwango vya Ujenzi wa Barabara cha Wizara ya Ujenzi cha mwaka 2000, Jedwali 7205/2, kama inavyooneshwa kwenye Jedwali la hapo chini:

Jedwali Na. 70: Mchanganuo wa Sampuli ya Msingi wa Tabaka la Saruji ya Lami.

Kipimo (Test)	Mahitaji kwa kadiri ya SPFRW na PMDM	Matokeo ya vipimo vya maabara wakati wa ukaguzi	Maoni
Binder content (%)	5% (jedwali 420272 la SPFRW na jedwali 10.14 la PMDM) kwa lami inayotumia kokoto za mm 20 (AC20)	Wastani=4.14%	Kiwango pungufu (binder content) lko nje kwa kuwa juu ya kiwango kinachotakiwa kwa 0.56 (kinachotakiwa isitoke nje zaidi ya 0.3)
Core thickness(mm)	50mm (matakwa ya mkataba)	Unene ulianza mm 40.052 hadi mm 50.37	(kati ya sehemu 10) kwenye umbali wa km 35+950 na Km 36+750 zilikuwa chini ya unene wa mm 50
Air voids (%)	3%(kiasi cha chini) - 6% (kiasi cha juu) jedwali 10.13 la PMDM	2.34%-7.53%	Inatoka nje kidogo ya kiasi kinachotakiwa (Fell slightly outside the range)
Stability value (N)	For traffic TLC 20 8000N(min) and max 18000N(max.)	lianzia 700N-4900N	lko chini(low stability value)
Flow value(mm)	2mm(kiasi cha chini) - 4mm(kiasi cha juu) jedwali 10.13 la PMDM	Inanzia mm6.09 - mm 8.89	lko juu (High flow value)

Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi wa Kiufundi wa TANROADS

Uimara mdogo (low stability value) unaweza kupelekea kupungua kwa uimara wa safu ya lami kuhimili mkandamizo wa magari. Udhaifu katika kiwango cha kumiminika (high flow value) cha tabaka la lami

unaweza kupunguza uwezo wa barabara ya lami kubonyea kutokana na magari yanayopita juu yake na kuchakaa haraka.

Hivyo basi, nashauri menejimenti ya Wakala wa Barabara Tanzania: (a) kuhakikisha wahandisi washauri wanaofanya kazi zausanifu wanasimamiwa ipasavyo ili kuhakikisha kuwa utafiti na uchunguzi wa maeneo ya ujenzi vinafanyika kwa kina; (b) kupitia usanifu, michoro, makadirio ya gharama za ujenzi wa miradi ili kuepuka kukosekana kwa baadhi ya vitu muhimu ambayo inaweza kusababisha mabadiliko kwenye mikataba wa awali wakati wa ujenzi; na (c) kuchukua hatua za marekebisho kwa sehemu za barabara ambazo hazijakidhi viwango ili kuepuka hasara itokanayo na uharibifu wa barabara.

8.7.3 Usimamizi usiojitosheleza wa Mkataba wa Ujenzi wa Barabara ya Kabuhoro-Ziwani wa Lami nyepesi ya Tabaka mbili (Double Surface Dressing)

Tarehe 2 Mei 2018, Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA) kwa Mkoa wa Mwanza aliingia Mkataba na Gemen Engineering Company Limited kutekeleza Ujenzi wa Barabara ya Kabuhoro - Ziwani kuwa ya Lami nyepesi yenye Tabaka mbili kwenye Manispaa ya Ilemela kwa gharama ya Sh. 785,011,519.03 (pamoja na Kodi ya Ongezeko la Thamani). Mkataba ulikua na muda unaoishia tarehe 6 Novemba 2018.

Wakati wa ukaguzi wa kiufundi uliofanyika mnamo Oktoba 2018 nilibaini kuwa, TARURA - Ilemela alimlipa mkandarasi kiasi cha Sh. 153,122,000 bila ya kupima thamani za kazi zilizofanywa. Hii, ni kinyume na Kifungu kidogo Na. 19 cha Masharti Maalumu ya Mkataba inayotaka, malipo yote ya kazi zilizofanywa na mkandarasi yaambatane na Taarifa ya Vipimo.

Nilipima thamani ya kazi zilizofanywa na kubaini kuwa, mkandarasi alilipwa kiasi cha Sh. 78,900,000 sawa na asilimia 52 ya Hati ya Malipo ya Muda Namba 1, kwa kazi ambazo zimeainishwa kwenye Bili ya Vipimo lakini bado hazijafanyika, kama inavyonekana kwenye Kiambatisho Na. 42

Ni mtazamo wangu kwamba, kukosekana kwa usimamizi madhubuti kwa mkandarasi kunaweza kusababishia hasara Serikali, pamoja na

ubora duni kwa barabara zetu. Hivyo basi, nashauri menejimenti ya Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini, kufanya ufuatiliaji wa karibu kwa mkandarasi na kuhakikisha malipo yanafanywa kwa kuendana na ubora wa kazi pamoja na muda.

8.7.4 Mapungufu ya Ubora wa kazi za Ujenzi kuendana na Michoro, na Bili ya Vipimo katika Matengenezo ya Muda ya Barabara ya Moshono, Kalimaji na Ujenzi wa Kalavati katika Barabara za Arusha Modern, Seminari na TANESCO

Tarehe 29 January 2018, Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA) kwa Mkoa wa Arusha aliingia Mkataba na WULKAN Engineering wenye Namba. AE/092/2017-18/ACC/W/09, kwaajili ya Matengenezo ya Muda ya Barabara ya Moshono, Kalimaji na Ujenzi wa Kalavati katika Barabara za Arusha Modern, Seminari na TANESCO kwa gharama ya Sh. 114,000,000. Mkataba ulikuwa na muda unaoisha tarehe 11 Juli 2018.

Wakati wa ukaguzi wa kiufundi uliofanywa mnamo Oktoba 2018 nilibaini kuwa, sampuli 9 kati ya 11 zilizojaribiwa ukubwa wa changarawe (gravel thickness) hazikufikia kiwango cha chini cha ushindiliaji wa asilimia 96.3 kama invyotakiwa na Viwango vya Ubora wa Ujenzi wa Barabara Tanzania (Jedwali 7205/1).

Pia nilibaini, matokeo ya kipimo cha kuangalia kiwango cha mshindilio (field density) kwenye changarawe aina ya (G25) ilionesha sampuli zote 11 zilizojaribiwa zilikuwa na mshindilio kati ya asilimia 75 hadi 94, kinyume na viwango maalumu vinavyotaka kiwango cha chini cha mshindilio kuwa asilimia 96.3.

Nina mtazamo kwamba, barabara tajwa inaweza kuharibika mapema kwasababu ya tabaka dhaifu la changarawe na kusababisha muda wa baarabara kupungua. Hivyo nashauri menejimenti ya Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini, kuchukua hatua za haraka kurekebisha mapungufu, ili kuepuka uharibifu wa barabara unaotokana na udhaifu wa tabaka la changarawe.

Sura ya Tisa

Ukaguzi wa Manunuzi na Usimamizi wa Mikataba

9.1 Utangulizi

Manunuzi ya Umma ni nguzo muhimu ya kimkakati inayotakiwa kuzingatiwa katika utoaji wa huduma bora Serikalini. Kwa kuwa Manunuzi ya Umma yanatumia kiasi kikubwa cha fedha za umma, usimamizi wake ni muhimu kuzingatiwa ili kuleta ufanisi na tija katika sekta ya Umma.

Viwango vya uzingativu wa sheria za manunuzi vinaendelea kuwa chini katika Taasisi za Serikali Kuu kwa kuendelea kutozingatia taratibu za manunuzi. Hali hii isiposhughulikiwa kwa kina, kuna uwezekano wa kutofikia malengo yaliyowekwa na serikali ya utoaji wa huduma bora kwa umma. Ununuzi wa bidhaa na huduma ni muhimu kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali na Sekretarieti; Kesi za rushwa zilizowahi tokea nchini zinaonesha kuwa, eneo la manunuzi ni hatarishi zaidi katika kufanya udanganyifu na ubadhiribifu. Rushwa yoyote katika manunuzi haileti tu hasara za kifedha kwa Taasisi za Serikali Kuu, bali pia huleta madhara katika taasisi za umma kwa kuharibu sifa na taswira ya Taasisi za Umma na kutokuaminika katika utoaji huduma kwa jamii.

Mamlaka ya CAG kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 48 (3) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma, 2011 ni kuhakikisha kuwa michakato ya manunuzi katika Sekta ya Umma inafanyika kwa haki na uwazi; na kwamba, kwa ujumla mahitaji ya Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.7 ya mwaka 2011 na Kanuni zake za msingi za Mwaka 2013 zinazingatiwa.

Utekelezaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 7 ya Mwaka 2011 (iliyorekebishwa mwaka 2016) pamoja na Kanuni zake za msingi za mwaka 2013 hutoa mfumo wa kisheria unaosimamia taasisi na mchakato wa manunuzi katika sekta ya umma. Licha ya kuwapo kwa sheria, vyombo vingine vya serikali bado havizingatii kikamilifu Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011 na Kanuni zake za Mwaka 2013.

Sura hii inaonesha matokeo ya ukaguzi kuhusu manunuzi na usimamizi wa mikataba kutokana na ukaguzi uliofanyika. Katika ripoti hii nimejumuisha pia ripoti ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Manunuzi ya Umma na Taarifa ya Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali.

9.2 Hoja zitokanazo na Usimamizi wa Manunuzi

9.2.1 Manunuzi Yaliyofanyika bila Ushindanishi Sh. 4,615,040,383.12

Kwa kipindi cha mwaka huu wa ukaguzi Taasisi za Serikali Kuu kumi (10) zilibainika kufanya manunuzi ya bidhaa na huduma zenye thamani ya Sh. 4,615,040,383.12 bila kuzingatia Kanuni ya 163 na 164 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013 inazoitaka Taasisi za Umma zinazofanya Manunuzi kuzingatia upatikanaji wa nukuu za bei zisizopungua tatu kutoka kwa Wazabuni/Wakandarasi tofauti.

Pia, nilibaini matumizi yaliyofanyika kupitia njia za manunuzi isivyostahili kama vile kutoka chanzo kimoja au kushindanisha wazabuni wachache kinyume na Kanuni ya 159 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013. Orodha ya Taasisi ambazo hazikufuata Kanuni hizi zimeoneshwa kwenye Kiambatisho Na. 43

Katika mwaka wa fedha wa 2017/2018 Taasisi za Serikali Kuu ambazo zilifanya manunuzi yasiyokuwa shindanishi zimepungua kutoka Sh. 6,536,468,043 hadi Sh. 4,615,040,383.12 za mwaka wa fedha wa 2017/18. Pia idadi ya Taasisi zimepungua kutoka kumi na moja(11) zilizobainika mwaka uliopita hadi kumi (10) kwa mwaka huu.

Kitendo cha Taasisi za serikali kuu kutofuata taratibu za ushindanishi kinatia shaka kuwa haki haikutendeka vema katika manunuzi; na huenda hazikulipa bei stahiki katika manunuzi yaliyofanyika.

Kwa hiyo nashauri taasisi za serikali kuu kuhakikisha kwamba zinajitahidi zaidi kuzingatia kikamilifu Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 ili kuwezesha manunuzi yote yanayofanyika pakiwa na ushindanishi wa bei ili kuboresha ushindanishi. Hivyo, kuweza kupata thamani ya fedha katika bidhaa na huduma zinazonunuliwa. Vilevile, nashauri taasisi za serikali kuu kutotumia njia zisizofaa za

kununua kutoka kwa mzabuni mmoja au kufanya zabuni zisizo za wazi kwa kuwa ziko kinyume na matakwa ya Kanuni ya 159 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013 ili kuwezesha kuwapo kwa utendaji haki na uwazi katika manunuzi ya umma. Orodha ya Taasisi ambazo hazikufuata Kanuni hizi ni zimeoneshwa kwenye Kiambatisho Na. 43

9.2.2 Manunuzi Yaliyofanyika Bila ya Kupata Kibali/Idhini ya Bodi ya Manunuzi yenye Thamani ya Sh 5,373,435,190.36

Kwa mwaka huu wa fedha, ukaguzi wa uzingatiaji wa kifungu cha 35(3) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 na Kanuni 55 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za 2013 kuhusu zabuni za manunuzi kuidhinishwa na bodi ya manunuzi umebaini kuwa, taasisi mbalimbali zilifanya manunuzi mbalimbali ya bidhaa na huduma bila ya kuidhinishwa na bodi ya zabuni. Kutokufuata sheria ya manunuzi kumeonekana katika taasisi nane (8) kwa mwaka 2017/2018 zenye thamani ya Sh. 5,373,435,190.36 ilihali kwa mwaka 2016/17 zilikuwa Sh. 2,997,009,109. Taasisi mbalimbali zilizofanya manunuzi bila idhini ya Bodi ya Zabuni husika zimeorodheshwa kwenye Kiambatisho Na. 44

Taasisi za Serikali Kuu zimeendelea kufanya vibaya katika eneo hili kwa kutozingatia kanuni, hivyo katika mwaka huu wa fedha, taasisi nane (8) za Serikali Kuu zilifanya manunuzi yenye thamani ya Sh. 5,373,435,190.36 ambayo hayakufuata kanuni ya manunuzi. Hii inaonesha ongezeko la taasisi moja (1) kutoka saba (7) zilizobainika mwaka jana zenye thamani ya Sh. 2,997,009,109. Hii imeonesha ongezeko la utendaji mbovu la Sh. 2,376,426,081.36 sawa na asilimia 79.29% ikilinganisha na ilivyobainika katika ukaguzi wa mwaka jana.

Manunuzi yanayofanyika bila idhini ya bodi ya zabuni husababisha kuingia mikataba na wazabuni au wakandarasi wasiokuwa na sifa; hivyo kuwa na athari kubwa katika suala la uwazi, ufanisi na tija.

Kwa maelekezo yaliyopo katika kifungu cha 35 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011, napendekeza menejimenti za taasisi husika zifuate kikamilifu ushiriki wa Bodi ya Zabuni katika kuidhinisha manunuzi ili kuepuka manunuzi yasiyokuwa na tija au mikataba isiyotekelezeka.

9.2.3 Malipo yaliyofanyika bila bidhaa, kazi na huduma kutolewa Sh. 5,356,549,884.76

Katika ukaguzi wangu nilibaini kuwa taasisi za serikali kuu kumi na tatu (13) zimelipia bidhaa, huduma na kazi mbalimbali; zenye thamani ya Sh 5,356,549,884.76 ambazo bidhaa hazijapokelewa, wala huduma haijatolewa na kazi hazijafanyika.

Kutokana na manunuzi kulipiwa bila bidhaa na huduma kupokelewa au kazi kutokufanyika, thamani ya fedha na tija havikuweza kupatikana za manunuzi hayo. Bila kuwapo kwa thamani ya fedha kwenye manunuzi yaliyofanyika ni sawa na fedha kutumika bila kuwa na manufaa kwa umma au kama vile zimepotea. Manunuzi ya jinsi hii ni kinyume na makubaliano yaliyofanyika kati ya Wazabuni/Wakandarasi na Taasisi za Serikali Kuu ambayo imeweka bayana kwamba malipo yasifanyike kabla ya kazi kufanyika, bidhaa kuletwa na huduma kutolewa. Kwa maelezo ya taasisi husika angalia Kiambatisho Na. 45.

Kutokana na uwepo wa kasoro katika manunuzi nimeshindwa kubaini kama manunuzi yaliyofanywa kazi au huduma iliyotolewa au bidhaa zilizopokelewa vilikuwa sawa au hapana. Kwa kufanya malipo bila kupokelewa kwa bidhaa, kazi kutofanyika na huduma kutolewa, matarajio ya manufaa yaliyotaraiwa hayawezi kupatikana. Hii ni hatari katika kufanya manunuzi ya umma kwa kuwa bidhaa yawezekana zisipokelewe kabisa au kazi na huduma kutofanyika au vikafanyika kwa muda usiokuwa muafaka.

Ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2016/17, idadi ya taasisi za Serikali Kuu zilizokuwa na kasoro kwenye manunuzi zimeongezeka toka taasisi nane (8) hadi kumi na tatu (13) kwa mwaka huu wa fedha; hilo ni ongezeko la asilimia 62.5.

Ninashauri menejimenti za taasisi za Serikali Kuu kufanya jitihada za kufuatilia bidhaa ambazo hazijapokelewa ili kuokoa fedha za umma. Hii ni pamoja na kuwachukulia hatua za kisheria Wazabuni/Wakandarasi ambao watashindwa kufanya kazi au kutoa huduma.

9.2.4 Manunuzi ya Vifaa, Kazi na Huduma kutoka kwa Wazabuni Wasioidhinishwa Sh. 5,356,549,884.76

Kanuni ya 131 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka za 2013 imeweka wazi kuwa taratibu za kununua bidhaa na huduma kutoka kwa Wazabuni walioidhinishwa na Wakala wa Manunuzi wa Serikali (GPSA).

Pia, Kanuni ya 137 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013 imebainisha nakuelezea namna ya kufanya matengenezo ya Magari ya Serikali kupitia TEMESA. Vilevile Kanuni za 139-141 za manunuzi ya Umma za Mwaka 2013 zinatoa mwongozo kwa taasisi za Serikali kununua madawa kutoka Bohari Kuu ya Madawa (MSD).

Katika ukaguzi wa mwaka huu nilibaini kuwa taasisi tano (5) za Serikali zilikiuka kanuni ya kununua bidhaa na huduma ya Sh. 432,737,939,877.68 kutoka kwa Wazabuni ambao hawajapata kibali au kuidhinishwa na GPSA, TEMESA, na MSD; na wengine hawajasajiliwa na Bodi ya Usajili wa Wakandarasi (CRB). Kwa maelezo Zaidi, angalia Kiambatisho Na. 46

Nimebaini ongezeko la uzingatiaji wa Kanuni ya 131 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma, kuna upungufu wa asilimia 38 ya Taasisi za serikali kuu ambazo hazikuzingatia; ambapo mwaka 2016/2017 zilikuwa taasisi nane (8) zenye manunuzi yenye thamani ya Sh.402,496,986, wakati huo huo kwa mwaka ulioishia 2018 zilikuwa taasisi tano (5) zenye thamani ya Sh. 432,737,939,877.68

Nashauri Maafisa Masuuli wa taasisi za Serikali Kuu kuhakikisha kwamba manunuzi ya umma yanafanywa kwa kuwatumia wazabuni na wakandarasi ambao wameidhinishwa na wamesajiliwa na mamlaka husika. Pia, kuhakikisha kwamba Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011 na Kanuni zake na marekebisho yake zinazingatiwa na kutekelezwa kikamilifu.

9.2.5 Mapokezi ya Bidhaa na huduma bila Kukaguliwa Sh 628,364,144.05

Kwa mwaka huu wa ukaguzi, jumla ya Taasisi kumi na nne (14) zilibainika kufanya manunuzi ya bidhaa na huduma zenye thamani ya

Sh 628,364,144.05 ambazo hazikufanyiwa ukaguzi na zikapokelewa kinyume na Kanuni ya 244 (1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013 ambayo inaelekeza kuwa manunuzi yote yanayofanywa na taasisi za umma yawe yanakaguliwa ili kuweza kubaini kama yamefikia viwango vilivyowekwa kwenye mkataba husika.

Pia, Kanuni ya 245 ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 imeweka maelezo bayana kwamba Afisa Masuuli anatakiwa kuteua Kamati ya Ukaguzi na Mapokezi ya vifaa ambayo itawajibika kukagua, kuthibitisha ubora wa vifaa au huduma na kupokea mara zinaponunuliwa kutoka kwa Wazabuni mbalimbali.

Katika ukaguzi wa mwaka huu, nimebaini bado uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi uko chini ingawa mwaka huu taasisi zimefungua kidogo. Mwaka huu ni taasisi kumi na nne (14) ambazo hazikuzingatia Sheria. Nimebaini kuwa tathmini ya ubora wa bidhaa za thamani zenye Sh 628,364,144.05 haikuweza kufanyika. Wakati mwingine, Maafisa Masuuli hawakuweza kuunda kamati za Kaguzi na Mapokezi kwa ajili ya kukagua bidhaa, huduma kutoka jkwa wazabuni. Taarifa zaidi zinapatikana kwenye Kiambatisho Na. 47

Katika mwaka huu wa fedha, ikilinganishwa na mwaka jana, nimebaini kuwa uzingatiaji wa sheria za manunuzi umeongezeka kwa kiasi fulani, Hii ni kwasababu mwaka 2016/2017 ni taasisi za serikali kuu ndizo zilikiuka kanuni za manunuzi zikiwa kumi na nne (14) thamani ya Sh. 1,688,784,207.90; ambapo kwa mwaka huu wa fedha ni taasisi kumi na nne (14) zilifanya manunuzi ya thamani ya Sh 628,364,144.05 bila ya manunuzi hayo kukaguliwa na TEMESA au kamati ya ukaguzi na upokeaji.

Kufanya manunuzi ya bidhaa na huduma bila idhini ya Bodi ya Zabuni kunaweza kuathiri kazi kutolewa kwa wazabuni/wakandarasi wasiokuwa na uwezo, hivyo kusababisha uwazi, ufanisi na tija kukosekana katika manunuzi.

Ili kuhakikisha kwamba uvunjifu wa sheria za manunuzi katika taasisi za serikali kuu hauedelei kufanywa, nashauri kila taasisi ihakikishe kuwa inaunda kamati ya ukaguzi na upokeaji iliyo madhubuti ili kuzingatia utekelezaji wa sharia za manunuzi zilizokiukwa.

9.2.6 Manunuzi ya Kazi, Bidhaa na Huduma bila Mkataba Sh 1,174,767,341

Kanuni ya 10(4) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za 2013 imeweka bayana kuwa malipo kwa wazabuni yafanywe mapema kwa ukamilifu na kuzingatia masharti yaliyowekwa kwenye mikataba iliyoingia taasisi. Kutokana na kutokuwapo kwa mikataba halali kati ya taasisi za Serikali Kuu na Wazabuni/Wakandarasi, sikuweza kubainisha kama taratibu za kuingia mikataba zilifanyika kwa usahihi ili kuwapa kazi wazabuni mbalimbali kama isemavyo Kanuni ya 60(8) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya 2013.

Katika mwaka wa fedha huu, kinyume na sharia, nimebaini idadi ya taasisi tano (5) zilizofanya manunuzi ya Sh 1,174,767,341 bila ya kuwa na mikataba na Wazabuni na Wazabuni. Kuwapo kwa mkataba ni kigezo cha kila upande kuwajibika kisheria. Taasisi zilizobainika kwenda kinyume sheria ya manunuzi zipo katika Kiambatisho Na. 48

Nimebaini kuboreka kwa uzingatiaji wa taasisi za serikali kuu ikilinganishwa na mwaka uliopita wa 2016/2017 ambapo kulikuwa na taasisi kumi na mbili (12), ambapo mwaka huu zipo taasisi tano (5). Kwa hiyo, zimepungua taasisi saba (7) sawa na asilimia 58, ikilinganishwa na mwaka jana. Kupungua huko kunaashiria kuongezeka kwa maboresho katika uzingatiaji wa sheria za manunuzi katika mwaka huu wa ukaguzi.

Ninashauri menejimenti za taasisi za Serikali Kuu kuhakikisha kwamba manunuzi yote yanayofanyika yawe na mikataba ili itokeapo kuna upande utakaokiuka mkataba au sehemu ya mkataba iwe rahisi kuwajibishwa kisheria na itasaidia manunuzi yote kufanyika kisheria.

9.2.7 Kutokuandaliwa kwa Ripoti za Manunuzi

Kifungu 38 (n-q) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011 kimeweka bayana kwamba Kitengo cha manunuzi kinatakiwa kufanya yafuatayo: Kuandaa ripoti ya mwezi na kuwasilisha kwenye bodi ya zabuni, kuandaa ripoti ya robo mwaka kuhusiana na utekelezaji wa mpango wa manunuzi wa mwaka, na kuwasilisha kwenye manejimenti, na kuandaa ripoti za manunuzi zinazotakiwa kuandaliwa kila wakati.

Vilevile Kanuni ya 137(4)(b) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya 2011 inataka taasisi zinazofanya manunuzi ziandae ripoti za robo mwaka za manunuzi yaliyofanyika ikionesha majina ya wazabuni/wakandarasi, maelezo ya huduma au bidhaa na thamani yake na kuwasilisha kwa Mamlaka ya Manunuzi ya Umma (PPRA).

Katika ukaguzi wangu wa mwaka huu nimebaini kuwepo kwa udhaifu wa utekelezaji wa hii sheria kwenye taasisi za serikali kuu ambapo zimeshindwa kuandaa na kuwasilisha ripoti zinazotakiwa kupelekwa kwenye Mamlaka zinazohusika. Ripoti hizo ni Kuto kuandaa na kutopeleka ripoti ya manunuzi ioneshao jina la mzabuni, huduma iliyofanyika, na thamani, kutokuandaa ripoti za manunuzi za robo mwaka, Mpango wa manunuzi wa mwaka haukuwasilishwa PPRA ndani ya siku 14 baada ya kumalizi mchakato wa bajeti.

Katika mapungufu hayo ya kutokuzingatia Sheria zilizotajwa hapo juu, idadi ya taasisi zilizobainika ni nane (8) ambazo zimeainishwa kwenye Jedwali hapo chini:

Jedwali Na. 71: Taasisi ambazo hazikuandaa Ripoti za Manunuzi

Na	Fungu	Taasisi Husika
	37	Ofisi ya Waziri Mkuu
	41	Wizara ya Katiba na Sheria
	31	Ofisi ya Makamu wa Rais
	89	Sekretarieti ya Mkoa wa Rukwa
	16	Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali
	80	Sekretarieti ya Mkoa wa Mtwara
	52	Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto
	43	Wizara ya Kilimo

Chanzo: Ripoti ya Ukaguzi kwa Menejimenti 2016/2018

Hata hivyo, menejimenti za taasisi za Serikali Kuu zilikubaliana na ushauri wa CAG kuhakikisha kuwa zinazingatia sheria tajwa hapo juu; kwamba, kwa kipindi kijacho wataandaa ripoti za manunuzi na kuziwasilisha kwenye Bodi za Zabuni, menejimenti na PPRA ili kuendana na uhitaji wa Kifungu cha 38 cha Sheria ya manunuzi ya umma ya mwaka 2011 na Kanuni 137(4)(b) ya Kanuni za manunuzi ya umma za 2013.

9.2.8 Mpungufu katika Usimamizi wa Manunuzi, Mikataba na Miradi Sh 119,228,294,260.45

Kanuni ya 114 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 inazitaka taasisi zinazofanya manunuzi ya Umma kusimamia manunuzi yote ya bidhaa, huduma au Ujenzi ifanye yafuatayo: Kufuatilia gharama na upatikanaji wa bidhaa na huduma kwa muda na ubora ulioainishwa kwenye mkataba, Kufuatilia maendeleo na kukamilika kazi kwa wakati kwa mujibu wa masharti ya kila mkataba, kuchukua hatua za kusahihisha mapungufu yaliyojitokeza katika kutekeleza masharti ya mkataba Kuhakikisha majukumu yaliyobainishwa kwenye mikataba yanatekelezwa yote.

Pia, Kanuni ya 192 (1 na 2) na 232 (2) za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013 zimebainisha kwamba nyaraka za zabuni ziweke bayana muda halali wa maombi ya zabuni, Pia utoaji wa zabuni unatakiwa ufanyike ndani ya kipindi halali cha kushughulikia zabuni; ambapo mzabuni atajulikana kama ndiye aliyeomba kwa bei ya chini au bei ya juu baada ya tathimini kufanyika na mshindi wa zabuni atapewa ndani ya kipindi hicho.

Kinyume na Kanuni zilizotajwa hapo juu, nilibaini mapungufu yaliyojitokeza katika usimamizi wa mchakato wa manunuzi, mikataba na utekelezaji wa miradi. Taasisi zilizobainika kuwa na udhaifu ni kumi na tatu (13) kwa thamani ya Sh. 119,228,294,260.45 Taasisi zenye madhaifu hayo zimeorodheshwa kwenye Kiambatisho Na. 49 hapo chini:

Ikilinganishwa na matokeo ya ukaguzi na mwaka wa fedha 2016/2017 na 2017/2018, idadi ya taasisi za serikali zimepungua toka kumi na nane (18) hadi kumi na tatu (13), ikionesha kupungua kwa taasisi tano (5). Kupungua toka taasisi 18 hadi 13 kunaonesha ongezeko kidogo la Taasisi za Serikali Kuu katiko uzingatiaji wa sheria za manunuzi. Nazishauri taasisi za serikali kuu;-

Ziendeele kuboresha usimamizi wa mchakato wa manunuzi, kazi za wakandarasi na wazabuni kwenye miradi mabalimbali kwa ufasaha na kwa kuzingatia sheria na mikataba iliyowekwa.

Pamoja na kwamba TBA imepewa mamlaka ya kujenga majengo ya Serikali, TBA haitakiwi kupuuza au kutozingatia vigezo na masharti yaliyomo kwenye mikataba iliyosainiwa na TBA pamoja na Sheria ya Manunuzi ya umma ya 2011 na Kanuni zake za 2013 zinatakiwa kuzingatiwa kwa ujumla wake.

9.2.9 Kuchelewa Kukamilika kwa Miradi ya Ujenzi yenye thamani ya Sh. 2,878,272,902.49

Katika ukaguzi wa mwaka huu nilibaini kuchelewa kukamilika kwa miradi yenye thamani ya Sh. 2,878,272,902.49 kinyume na muda ulioainishwa kwenye mikataba. Jumla ya Wizara, Idara na Sekretariati za Mkoa nne (4) ziliingia katika makubaliano ya Mikataba na Wakandarasi katika ujenzi wa miradi mbalimbali. Tazama Kiambatisho Na. 50

Kuchelewa kukamilika kwa miradi kunaweza kusababisha Serikali kuingia gharama zisizo za lazima. Hii ni kutokana na mfumuko wa bei, hatimaye unasababisha vifaa vya ujenzi kuongezeka bei ambayo huongeza gharama ya mradi. Kwa hiyo menejimenti za taasisi husika zinashauriwa kuzingatia Kanuni ya 114 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za 2013 na kusimamia ipasvyo mikataba ya manunuzi.

Pia, nashauri menejimenti kusimamia kikamilifu mikataba inayoendelea ili kuhakikisha inakamilika kwa wakati bila kuchelewa. Nazishauri Taasisi ziendeele kufanya juhudi za ufuatiliaji rasilimali fedha kutoka Hazina ili kuweza kutekeleza miradi iliyopangwa katika bajeti. Nashauri pia miradi yenye fedha kidogo itekelezwe kwa hatua ili kurahisisha usimamizi wa miradi na ulipaji wake. Zaidi ninapendekeza ujenzi ufanyike kwa awamu ili kuwezesha kulipa madeni, hivyo kuepuka kulipa gharama kwa riba.

9.2.10 Vifaa vilivyounuliwa bila kuingizwa kwenye vitabu Sh 339,232,939

Kanuni ya 198 na 203 ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma za 2001 zinahitaji kupokea bidhaa, kutoa bidhaa na kuandika taarifa za kiasi cha bidhaa kilichobaki stoo kwenye kurasa tofauti katika leja za stoo. Wakati wa ukaguzi wangu, nilishindwa kuthibitisha matumizi ya bidhaa zenye thamani ya Sh 339,232,939 zilizonunuliwa na taasisi

kumi na mbili (12) zilizokaguliwa. Hii ni kutokana na kutokuwapo kwa kumbukumbu sahihi katika leja za stoo na daftari la kudhibiti mwenendo wa matumizi ya gari na matumizi ya mafuta baada ya kupokelewa.

Ulinganisho wa utendaji wa Taasisi za Serikali Kuu kwa miaka miwili unaonesha kwamba katika mwaka wa fedha wa 2016/2017 kulikuwa na Taasisi kumi na nne (14) ambazo zilifanya vibaya; ambapo kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018 kuna Taasisi kumi na mbili (12). Kwa hiyo, zimepungua taasisi mbili (2), sawa na asilimia 14 ukilinganishwa na mwaka jana.

Orodha ya taasisi zilizounua vifaa bila kuingizwa kwenye vitabu inapatikana kwenye Kiambatisho Na. 51

Kutokana na kukosekana kwa kumbukumbu za Stoo kuhusu jinsi Bidhaa na Mafuta yalivyotumika, sikuweza kujua namna matumizi ya Bidhaa/Mali zilizolipiwa.

Kutokana na kuwapo kwa kiasi kikubwa cha fedha za umma zilizotumika kununua vifaa na mafuta ambavyo havikuingizwa kwenye Leja ya Stoo na Kitabu cha Gari, napendekeza kwamba Taasisi zote za Serikali Kuu zihakikishe zinaingiza mali/bidhaa kwa wakati katika Leja ili kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali katika kutoa huduma kwa wakati kwa watumiaji wa vifaa vya stoo na kuingiza mafuta katika daftari la kuratibu mwenendo wa Gari na matumizi ya mafuta.

9.3 Taarifa ya PPRA -Kuhusu Uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka, 2011 na Kanuni zake za, 2013

Mamlaka ya Udhibiti wa manunuzi ya Umma (PPRA) ilianzishwa chini ya kifungu cha 9(1)(i)cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011. Kwa mwaka ulioishia 30 Juni, 2018 Mamlaka ilifanya ukaguzi wa manunuzi katika Wizara na Idara za Serikali. Ukaguzi ulilenga kuangalia na kujiridhisha kama taratibu, mifumo na kumbukumbu za kuingia mikataba ilifanyika kufuatana na Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 na Kanuni zake za 2013 na marekebisho yake ya mwaka 2016. Pia kuhakiki fomu ya mkataba iliyoidhinishwa na PPRA na kama manunuzi yalifanywa kuzingatia uchumi, ufanisi na tija pamoja na thamani ya fedha.

9.3.1 Matokeo ya Ukaguzi ya Uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi

Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi (PPRA) ilifanya ukaguzi kuhusu uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi kwa kutumia vigezo saba ambayo ni:- Kuanzishwa kwa kitengo cha manunuzi na utendaji kazi wake, kuandaa na kutekeleza mpango wa manunuzi wa mwaka, usahihi katika mchakato wa zabuni, usimamizi wa mikataba, utunzaji wa kumbukumbu za manunuzi, kutumia mifumo iliyoanzishwa na Mamlaka ya Manunuzi ya Umma; pamoja na ufuatiliaji wa Malalamiko.

9.3.1.1 Kiasi cha Manunuzi Kilichokaguliwa

Jumla ya mikataba 3,763 yenye thamani ya bilioni 805.68 ilifanyiwa ukaguzi na PPRA kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2018. Kati ya hiyo; mikataba 171 yenye thamani ya Sh bilioni 436.85 ilikua ni ya Ujenzi sawa na asilimia 4.5, mikataba 339 yenye thamani ya Sh bilioni 270.99 ilikua ni ya Bidhaa sawa na asilimia 9.01, na mikataba 97 yenye thamani ya Sh bilioni 51.36 ilikua ni ya Ushauri sawa na asilimia 2.58.

Mikataba mingineyo 227 yenye thamani ya Sh bilioni 27.61 ilikaguliwa ambayo siyo ya huduma ya kiushauri sawa na asilimia 6.03 na mikataba 2929 yenye thamani ya Sh bilioni 18.87 ya manunuzi madogo madogo sawa na asilimia 77.84. Pia ulifanyika ukaguzi wa zabuni ya kuuza mali za umma zenye thamani ya Sh milioni 81.22.

Kati ya mikataba yote iliyokaguliwa mikataba 612 yenye thamani ya Sh bilioni 403.72 sawa na asilimia 50 ya thamani yake, ilihusiana na taasisi 11 ilikuwa ya taasisi zenye manunuzi makubwa.

9.3.1.2 Viwango vya uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi

Uchambuzi wa uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi uliofanywa na PPRA ulijikita kwenye taasisi 58 kwa kutumia vigezo saba vinavyotakiwa kuzingatiwa. Matokeo ya ukaguzi huo ni kama ifuatavyo; wastani uliofikiwa wa uzingitiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma ulikuwa wa kiwango cha asilimia 74% ambao kwa mwaka 2016/2018 ulikuwa kwa kiasi hicho hicho. Wastani huo wa asilimia 74 ni chini ya makisio ya asilimia 80 iliyokadiriwa kwa mwaka 2017/2018.

Uzingatiaji wa sheria za manunuzi kwenye Taasisi za Serikali Kuu umeshuka kutoka asilimia 78 ya mwaka jana hadi asilimia 75 kwa

mwaka huu wa 2017/2018. Matokeo ya ukaguzi kwa Taasisi za Umma katika kila kigezo katika vigezo saba ni kama ifuatavyo; Kuanzishwa kwa Kitengo cha Manunuzi na utendaji kazi wake ni asilimia 78 ambayo ni nzuri kiasi; kuandaa na kutekeleza mpango wa manunuzi wa mwaka ni asilimia 79; ilikuwa asilimia 81 kwenye usahihi katika mchakato wa zabuni; usimamizi wa mikataba ni asilimia 81; utunzaji wa kumbukumbu za manunuzi ni asilimia 68; kutumia mifumo iliyoanzishwa na Mamlaka ya Manunuzi ya Umma ni asilimia 41. Hii inamaanisha kwamba uzingatiaji wake ni mbaya;

Mapendekezo:

Mafunzo ya sheria za manunuzi ya umma pamoja na kanuni za manunuzi ya umma zinatakiwa zifundishwe kwa wafanyakazi wa Kitengo cha Manunuzi, wajumbe wa Bodi ya Zabuni, na Wakaguzi wa Ndani.

PPRA inatakiwa iandae mwongozo unaoelekeza muda unaotakiwa kuzingatiwa na Kitengo cha Manunuzi juu ya muda unaotakiwa katika kila hatua kwenye mchakato wa zabuni kwa kila njia ya manunuzi hasa kwenye maeneo ambayo kuna ucheleweshaji mkubwa ambao hauna mwongozo wa kisheria.

Taasisi za Serikali Kuu zinatakiwa kuzingatia muda wa zabuni uliopangwa kwenye mpango wa manunuzi uliopitishwa ili pawe na ufanisi katika utekelezaji wa mipango na mairadi ya maendeleo.

9.3.2 Muhtasari Wa Matokeo Ya Uchunguzi Uliofanywa Na Ppra Kwa Mwaka Wa Fedha Ulioishia 30 Juni, 2018

9.3.2.1 Utangulizi

Kifungu cha 10 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.7 ya Mwaka 2011 kinatoa mamlaka kwa PPRa kufanya uchunguzi inapotokea tuhuma za Manunuzi yenye mapungufu. Uchunguzi unaweza kufanywa na PPRa kwa kutumia juhudi binafsi au kupitia tuhuma zilizowasilishwa kwa Mamlaka.

Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Mamlaka ilifanya uchunguzi katika Taasisi sita (6) zenye mikataba ishirini na nne (24) yenye

thamani ya Sh bilioni 280. Uchunguzi huo ulifanyika kutokana na maelekezo kutoka ngazi za juu; na Taasisi nyingine zenyewe ziliomba uchunguzi huo ufanyike kwenye Taasisi zao.

Hata hivyo, Taasisi za Serikali Kuu zilizofanyiwa uchunguzi ni tatu (3) kati ya sita (6) zilizofanywa na PPRA. Kwa hiyo, Mamlaka ya Manunuzi na Udhhibiti wa Umma ilifanya chunguzi katika Taasisi za Serikali kuu kama ilivyooredheshwa hapa chini kwenye Jedwali Na. 72 hapa chini

Jedwali Na. 72: Taasisi zilizotakiwa kufanyiwa uchunguzi na PPRA

NA	Taasisi	Idadi ya chunguzi	Idadi ya Tenda/Zabuni
1	TANROADS	1	15
2	Wakala wa Umeme Vijijini (REA)	1	4
3	Wiazara ya Elimu, sayansi na teknolojia	1	5
	Jumla	3	24

9.3.2.2 Taasisi: Wakala wa Umeme Vijijini (REA)

PPRA ilifanya uchunguzi baada ya kupokea taarifa toka vyanzo mbalimbali kutokana na ukiukaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma katika kupata Wakandarasi wa zabuni za kununua vifaa, kusimika transifoma, kuunganisha njia za umeme za wa kati na msongo mdogo wa umeme pamoja na kuunganishia umeme kwa wateja kwenye vijiji vya Tanzania bara ambavyo havina umeme. Uchunguzi huo ulijikita katika zabuni ya kazi ya ushauri na zabuni tatu za kupata Wakandarasi katika loti 29. Zabuni zilizochunguzwa zilikuwa katika mradi wa REA wa awamu ya tatu na thamani ya mikataba iliyokuwa inachunguzwa Sh 984,345,001,450.

Uchunguzi ulibaini yafuatayo:

- i) REA iliingia mkataba na mshauri aitwaye SMEC ambaye hakuwaamesajiliwa kwenye bodi ya wakandarasi; kwa hiyo, ikaleta mashaka kwa mkataba ulioingiwa;
- ii) Zabuni ya kupata Wakandarasi ilitangazwa kwa Wazabuni kabla ya maandalizi ya nyaraka za zabuni na usanifu wa mradi kukamilishwa na mshauri;

- iii) Tathimini ya kuwapata wakandarasi haikufanyika vizuri kwa kuwa ilikuwa na mapungufu kadhaa;
- iv) Majadiliano na mapendekezo ya wazabuni kupewa kandarasi hayakufanyika vizuri;
- v) Makisio ya vifaa vilivyohitajika kutokana na BoQ ni vichache kuliko zilizooneshwa katika mikataba sita iliyosainiwa na wakandarasi na zilizoandaliwa na wakandarasi, Hii ilibainika baada ya kutembelea mradi ambayo jumla ya tofauti ni Sh bilioni 99.07 kwa mikataba yote.
- vi) Mkataba ulioingiwa kati ya REA na M/s Urban and Rural Engineering Limited uliandika mara mbili kodi ya ongezeko la thamani (VAT) ambayo ni Sh 3,834,378,471;
- vii) Mkataba ulikuwa na utata wa nani anawajibika kulipia gharama za kuingiza vifaa nchini.
- viii) Uhalali wa zabuni zilizowasilishwa na M/s Sengerema Engineering Limited ulikuwa na dosari nyingi;
- ix) Gharama ya mkataba iliyopitishwa na bodi ya zabuni katika zabuni Na. 9 Loti 9 inatofautiana na ilivyoshauriwa na kamati ya tathmini;
- x) Vijiji 55 ambavyo tayari vilishapata umeme viliingizwa tena kwenye mikataba mingine ili wakandarasi waitekeleze katika mikoa ya Tanga, Shinyanga, Arusha, Manyara na Mwanza.
- xi) Kulikuwa na mashaka kwamba viwanda vya ndani havitaweza kukidhi mahitaji ya wakandarasi kama vile transifoma, nyaya na nguzo katika kutekeleza miradi.

Maelekezo ya PPRA: REA ilipewa maelekezo sita (6), Kati ya maelekezo hayo sita (6) maelekezo matatu (3), sawa na asilimia 50, yametekelezwa na mengine matatu (3), sawa na asilimia 50, ya maelekezo yote hayajatekelezwa kama ripoti ya REA ilivyowasilishwa PPRA na kuhakikiwa. Maelekezo ambayo bado hayajatekelezwa ni;

- i) Kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya maafisa waliokiuka sheria ya manunuzi ya umma walipokuwa wanatekeleza

majukumu yao. Maafisa hao ni kama vile Afisa Masuuli, bodi ya zabuni, Mkuu wa kitengo cha manunuzi, timu ya tathimini, na timu ya majadiliano.

- ii) Kufanya tathimini ya wazalishaji wa ndani wa nguzo, transiFoma, nyaya, na kuhakikisha kwamba mahitaji yote ya mradi yanapatikana pindiyanapohitajika;
- iii) Kuomba ushauri kwa Mwanasheria Mkuu juu ya uhalali wa mkataba ulioingwa kati ya REA na SMEC International Pty.

9.3.2.3 Taasisi: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

Uchunguzi: Zabuni zilizotekelezwa mwaka wa fedha 2015/16 - 2017/18

Uchunguzi katika Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ulifanyika baada ya Mheshima Waziri mwenye dhamana kubaini kuwa kuna ukiukaji wa sheria za manunuzi na usimamizi wa mikataba. Baada ya hapo, wizara iliwasiliana na PPRA ili uchunguzi wa kina wa zabuni hizo ufanyike na ushauri uweze kufanyika.

Uchunguzi huo ulihusisha zabuni tano (5) kwa ajili ya: kununua printa za mashine za kuchapa vitabu na nyaraka zinginezo; kuandaa mzungira kwa watu wenye uhitaji maalum; kununua kemikali na vifaa vya maabara kwa ajili ya vyuo vya ualimu saba vyuo hivyo ni: chuo cha Tabora, Kleruu, Morogoro, Mpwapwa, Butimba, Mtwara na Monduli. Kemikali na vifaa vya maabara kwa ajili ya vyuo vinne vya ualimu ambavyo ni chuo cha Songea, Kleruu, Mpwapwa na Morogoro; na samani za ukumbi wa kutolea mihadhara katika vyuo vya Morogoro, Butimba, Kasulu na Marangu. Mawanda ya ukaguzi yalikusisha mapitio ya uwezo wa kiutendaji wa kitengo cha manunuzi (PMU) kama kina uwezo wa kukabili shughuli za manunuzi na utendaji wa Bodi ya Zabuni ya wizara. Vilevile, uchunguzi wa utumiaji wa Bodi ya Zabuni kutumia ‘circular resolution’ katika kutoa zabuni kwa kutumia “force account” katika kutekeleza miradi ya maendeleo.

a) Zabuni ya kununua mashine ya kuchapa vitabu:

- i) Manunuzi ya mashine ya kuchapa vitabu na nyaraka zinginezo hayakuwa kwenye Mpango wa Manunuzi wa Mwaka wa wizara

- ii) Nyaraka za zabuni zilizotumia hazikuwa za kiwango kinachotakiwa
- iii) Mahitaji ya kiufundi hayakuainishwa kwenye makisio ya kinachohitajika; na viliandaliwa ili kumpendelea Mazabuni mmoja aliyeomba hiyo zabuni.
- iv) Kulikuwa na utata wa taarifa ya vyanzo vya fedha kwa ajili ya manunuzi hayo; pia vigezo vya tathimini ya zabuni havikuwepo kwenye nyaraka za zabuni,
- v) Zoezi la tathmini halikufanyika vizuri bila kuwapo kwa wataalamu kwenye taaluma husika na mapungufu katika urekebishaji wa tarakimu zenye makosa,
- vi) Kutokuzingatia ushauri unaotolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwenye rasimu za mikataba.

Maamuzi na Maelekezo ya PPRA: PPRA iliagiza kuwa wizara iwe inaweka mahitaji yote ya manunuzi kwenye Mpango wa Manunuzi wa Mwaka na kuwa na mapitio ya Mpango wa Manunuzi ya Mwaka kwa kuingiza mahitaji yaliyojitokeza; kutumia nyaraka za zabuni zenye kukidhi viwango vilivyowekwa kwenye nyaraka za zabuni na ziandaliwa vizuri; kuandaa vigezo mahsusi vya kiufundi visiyokuwa na upendeleo; na tathimini ya zabuni ifanywe na wataalam wenye weledi wa kitaaluma wa zabuni inayofanyika. Maamuzi mengine yanayofanywa na Kitengo cha Manunuzi (PMU) kama inavyotakiwa na Kifungu cha 38 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya 2011 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2016); na usahihi na uhalali wa mkataba uliosainiwa na M/s Achelis.

b) Zabuni ya Manunuzi ya Huduma za Wanafunzi wenye Uhitaji Maalum

- i) Timu ya tathmini ya zabuni ilitumia vigezo ambavyo havimo kwenye nyaraka za maombi ya zabuni
- ii) Muda wa uhalali wa zabuni haukuongezwa wakati Bodi ya Zabuni ilipokuwa ikisubiria kufanya maamuzi;
- iii) Kutokuweka wazi, kutoandaa na kutoweka vizuri mahitaji ya manunuzi yanayotakiwa;

- iv) Bodi ya Zabuni ilifanya maamuzi ya kufuta zabuni kimakosa;
- v) Ubalozi wa Swideni ulipewa taarifa yenye utata juu ya vigezo vilivyotumika wakati wa tathmini ya Mzabuni M/s Mbesa Bookshop.

Maamuzi na maelekezo ya PPRA: PPRA iliagiza kwamba; tathimini ya zabuni iwe inafanyika kwa kutumia vigezo vilivyowekwa kwenye nyaraka za zabuni husika na tathimini ya zabuni iwe inafanywa na maafisa wenye weledi kufuatana na taaluma zao. Pia, kitengo cha Manunuzi (PMU) kinatakiwa kitimize wajibu wake kama matakwa ya Kifungu cha 38 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 (iliyorekebisha mwaka 2016). Vilevile, iliagizwa kuhakikisha kwamba zabuni na nyaraka zake ziandaliwe kwa ustadi, ikiwa ni pamoja na makisio ya mahitaji mbalimbali kwa uhalisia pamoja na njia ya manunuzi itakayotumika ili kuwezesha ushindani unakuwapo katika manunuzi.

- c) **Zabuni ya Manunuzi ya Kemikali na Vifaa vya Maabara kwa Vyuo vya Ualimu.**
 - i) Mzabuni aliyependekezwa kupewa mkataba hakukidhi baadhi ya vigezo vilivyowekwa,
 - ii) Mzabuni hakuwasilisha kibali cha mzalisha bidhaa zilizotakiwa kununuliwa,
 - iii) Mzabuni alishindwa kutekeleza ipasavyo mkataba wake, kwani alikadhi kemikali na vifaa baada muda wa mkataba kuisha,
 - iv) Baadhi ya kemikali na vifaa vyenye thamani ya Sh 846,700 muda wake wa matumizi ulikuwa ni chini ya miaka miwili tangu tarehe ya kupokelewa, kinyume na matakwa ya mkataba;
 - v) Vifaa vyenye thamani ya Sh 9,932,600 vilikabidhiwa vikiwa tofauti na vilivyokuwa vinahitajika; na
 - vi) Kulikuwa na utunzaji mbaya wa nyaraka za manunuzi.

Maamuzi na Maagizo ya PPRA: PPRA iliagiza na kutoa maelezo yafuatayo:

- i) Mahitaji ya vifaa vilivyooneshwa kwenye nyaraka za zabuni hazikuwa za kweli; pia kemikali za ziada zilipokelewa katika Chuo cha Ualimu Tabora ambazo zinatakiwa zipelekwe kwenye vyuo vingine vya walimu vyenye upungufu wa kemikali hizo.
 - ii) Tathmini ya zabuni ifanywe na wafanyakazi wenye weledi kwa kutumia vigezo vilivyowekwa kwenye nyaraka za zabuni.
 - iii) Kiasi cha cha Sh 19,854,345 kikatwe katika malipo yatakayofanyika kwa M/s Scientific Centre kwa sababu ya kuleta kemikali ambazo zilipokelewa zikiwa na muda wa matumizi ambao ni chini ya miaka miwili kuanzia tarehe ya kupokelewa.
 - iv) Kuhakikisha kwamba, usimamizi wa mikataba unakuwa mzuri
- d) Zabuni ya Manunuzi ya Kemikali Vifaa vya Maabara kwa vyuo vya Ualimu Vinne**

Uchunguzi ulibaini mapungufu yafuatayo:

- i) Baadhi ya Kemikali zilionunuliwa za thamani ya Sh 1,059,250 muda wake wa matumizi ulikuwa chini ya miaka miwili kuanzia tarehe zilipopokelewa ambayo ni kinyume na mkataba unavyotaka.
- ii) Kemikali zenye thamani ya Sh 34,695,000 hazikupokelewa toka kwa Mzabuni M/s Scientific Center ingawa malipo yalishafanyika;
- iii) Kazi ya tathmini ya zabuni ilikuwa na mapungufu. Hii ni pamoja na timu ya tathimini kushindwa kurekebisha makosa kwenye bei iliyowasilishwa na Mzabuni; ambapo bei ya zabuni ilizidi kwa Mzabuni kwa kiasi cha Sh 4,608,000.

Maamuzi na Maelekezo ya PPRA: PPRA ilielekeza wizara kuhakikisha kuwa vyuo vya Ualimu vihakikishe vinakuwa na makisio sahihi ya vifaa na kutumia njia za manunuzi zenye ushindani ili kupata bei nzuri iliyo shindanishi. Wizara iliagizwa kuhakikisha inafidiwa Sh 40,362,250 iliyolipwa kwa M/S Scientific Centre kwa malipo yaliyolipwa zaidi kutokana na makosa ya kutokujumlisha vizuri tarakimu za kihesabu kwenye zabuni yake ya maombi; na kwa Kemikali zilizopokelewa

muda wake wa kutumika ukiwa chini ya miaka miwili; pamoja na Kemikali ambazo hazikupokelewa kutoka kwa Mzabuni, na kuhakikisha kuna umakini katika maandalizi ya mikataba na usimamizi wa mikataba iliyosainiwa.

e) Zabuni za Manunuzi ya Samani kwa ajili ya Ukumbi wa Kutolea Mihadhara

Uchunguzi umebaini kuwa:

- i) Mzabuni Jaffery Ind. Saini Limited aliwasilisha hati kifani kwa Wizara kabla ya Afisa Masuuli hajaidhinisha uanzwaji wa taratibu za manunuzi.
- ii) Vikao vya Bodi ya Zabuni kuidhinisha Wazabuni bila akidi (idadi ya wajumbe) inayohitajika kukamilika.
- iii) Kitengo cha Manunuzi kutoa taarifa zisizo za kweli kwa Bodi ya Zabuni ili kuidhinisha mikataba, wakati zabuni husika haziwahi kuanzishwa kwa taratibu zilizopo.
- iv) Kujua mahitaji ya samani ilifanyika baada ya mkataba na mzabuni kusainiwa.
- v) Mapendekezo ya kitengo cha sheria cha Wizara kuhusu kuwepo kwa hati ya dhamana hayakuzingatiwa kwenye mikataba iliyosainiwa .
- vi) Bei ya viti iliyoonyweshwa na Mzabuni haiendani na bei iliyopo sokoni.

Maamuzi ya PPRA: PPRA imeelekeza Wizara kuhakikisha inabainisha mahitaji na makadirio kabla ya kuanza taratibu za manunuzi. Vilevile imeelekezwa kuwe na uwazi na ushindani katika manunuzi ya Samani zilizobaki.

f) Tathimini ya Uzingatiaji wa Sheria za Manunuzi na Viashiria vya Rushwa.

PPRA ilifanya tathimini katika zabuni tano zilizofanyiwa uchunguzi kubaini kiwango cha Wizara katika uzingatiaji wa Sheria na kanuni za manunuzi. Tathimini imebaini uzingatiaji upo kwa kiwango cha

asilimia 50 ambacho ni utekelezaji usioridhisha kwa viwango vilivyowekwa na Mamlaka.

Vilevile, tathmini ya viashiria vya rushwa imeonyesha kuwa na wastani wa asilimia 28, ambapo vigezo vilivyowekwa na PPRA inaonyesha kuwa manunuzi yanayofanywa na Wizara yana viashiria vya rushwa. Kwa muktadha huo, taarifa husika imepelekwa TAKUKURU kwa uchunguzi zaidi kulingana na Kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya 2011 kama ilivyoboreshwa mwaka 2016.

Maamuzi ya PPRA: PPRA imeelekeza Wizara:

- i) Kuhakikisha inabainisha mahitaji na makadirio kabla ya kuanza taratibu za manunuzi.
- ii) Kuhakikisha kuna uwazi na ushindani katika manunuzi ya Samani zilizobaki.
- g) Tathimini ya Uwezo wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, Bodi ya Zabuni na Kitengo cha Manunuzi**

PPRA ilifanya tathimini ya ufanisi kwenye ukaguzi wa ndani, Bodi ya Zabuni na kitengo cha manunuzi na kubaini;

- i) Kitengo cha Manunuzi inaongozwa na mtu ambaye hana kiwango cha taaluma inayohitajika, idadi ndogo ya watumishi na kutokuwapo kwa mafunzo juu ya sheria za manunuzi.
- ii) Utunzaji mbovu wa nyaraka za manunuzi na mikataba kwenye kitengo cha manunuzi.
- iii) Wajumbe wa Bodi ya Zabuni hawana uelewa wa sheria za manunuzi ya Umma juu ya namna ya kusimamia manunuzi.
- iv) Kitengo cha ukaguzi wa ndani hawana uelewa wa kutosha wa sheria ya manunuzi ambapo inasababisha kutokuwa na uwezo wa kukagua manunuzi.

Maamuzi ya PPRA: PPRA inapendekeza kwa Wizara;

- i) Pawe na uwazi na ushindani kwenye manunuzi yote yanayotakiwa kushindanishwa ili kupata thamani ya fedha.

- ii) Mkuu wa kitengo cha Manunuzi awe mtu mwenye sifa zinazohitajika.
- iii) Maofisa wanaohusika na usimamizi wa mikabata wapate mafunzo ya Sheria ya manunuzi ya Umma.
- iv) Kitengo cha manunuzi pamoja na ukaguzi wa ndani kiwe na wafanyakazi wa kutosha kuweza kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.
- v) PPRa ilielekeza kuwachukulia hatua za kinidhamu wajumbe wa Bodi ya Zabuni, kamati ya tathimini waliotadhimini zabuni na wafanyakazi wawili waliokuwa wanakaimu ukuu wa kitengo cha manunuzi waliohusika katika kutokuzingatia sheria.

9.3.2.4 Uchunguzi uliofanywa sampuli ya Zabuni - Wakala wa Barabara Arusha

Mamlaka ilifanya uchunguzi wa Zabuni zilizotolewa na Wakala wa Barabara Arusha kwa miaka wa fedha 2015/16-2016/17 baada ya kupokea mashitaka yanayohusu uvunjwaji wa taratibu za manunuzi ya umma kutoka Sekiretarieti ya Maadili. Uchunguzi ulijumuisha zabuni 118 za kiasi cha Sh 25,378,235,540 na LPO 139 zenye thamani ya Sh 286,143,984. Vilevile zabuni kumi na tano (15) kati ya zilizofanyiwa uchunguzi zilipatikana na matatizo ya kutokufuata sheria. Mamlaka iliamua kupitia zabuni zote kumi na tano (15) ili kubaini kama taratibu, mchakato na utunzaji wa nyaraka za manunuzi na utoaji wa kandarasi kulingana na Sheria ya Manunuzi ya Umma ya 2011 (iliyorekebishwa 2016) na Kanuni ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2013.

Mamlaka ilibaini mambo yafuatayo:

- i) Kuna kutokufuata sheria kwenye hatua za awali za zabuni na madhaifu katika usimamizi wa mikataba.
- ii) Tathmini za zabuni hazikufanywa vizuri kwa kufuata vigezo vilivyoainishwa kwenye zabuni, hivyo kusababisha kutoa zabuni kwa mkandarasi asiyekidhi vigezo.

- iii) Wakala wa Barabara Arusha ilivunja mkataba na Mkandarasi A & E Building and Civil Engineering Limited mkataba Na. AE/001/16-17/AR/TEN/W/08 kutokana na kushindwa kutekeleza mkataba husika. Kutokana na nyaraka zilizopitiwa ilibainika kuwa Mkandarasi A & E Building and Civil Engineering Limited hakuwa amekidhi vigezo vilivyokuwa vimeanishwa wakati wa kufanya tathimini za zabuni zilizopokelewa. Kama tathimini ya zabuni ingefanywa ipasavyo angepatikana mkandarasi ambaye ana viwango vinavyotakiwa na kutekeleza majukumu ya kimkataba inavyotakiwa.
- iv) Wakala wa Barabara - Arusha haikufuata taratibu katika kutoa kazi kwa Mkandarasi mwenza (sub-contracting) mkataba Na.AE/001/16-17/AR/CON/W/47 na 05 baada ya Mkandarasi aliyeingia mkataba kushindwa kutekeleza majukumu yake hivyo kuhamisha majukumu ya kimkataba kwa Mkandarasi mwingine.
- v) Wakala wa Barabara - Arusha kushindwa kumsimamia kwa umakini Mkandarasi A & E Building and Civil Engineering Limited hivyo kushindwa kulipa kiasi cha Sh 63,151,174 baada ya kuvunja mkataba;
- vi) Kuwepo kwa ripoti ya uwongo wakati wa makabidhiano ya mradi kumesababisha Mkandarasi Luneco Investment Limited kulipwa kwa ajili ya kazi ambayo haikukaguliwa kupitia mkataba Na. AE/001/15-16/AR/CON/W/31 na 74.
- vii) Kazi ya ujenzi wa miundombinu ya maji katika mkataba Na.AE/001/15-16/AR/CON/W/31 na 74 haikutengenezwa kulingana na viwango viliyopo kwenye mkataba na matokeo yake wakati wa mvua miondombinu ikaharibika kiasi cha kutokufaa tena. Hii imetokana na usimamizi hafifu wakati wa ujenzi wa miundombinu na kupelekea Mkandarasi kujenga chini ya kiwango.
- viii) Mfanyakazi mmoja wa Wakala wa Barabara ni mmiliki mmojawapo wa Wincom Enterprises Company Limited ambayo

iliingia mkataba na Wakala wa Barabara Arusha, kinyume na matakwa ya Kifungu 84 (3) cha Sheria ya Manunuzi ya 2011.

Maamuzi ya PPRA: Mamlaka imeelekeza Wakala wa Barabara Arusha:

- i) Wajumbe wa kamati ya tathmini na kitengo cha manunuzi wawajibike kwa kuwa na upendeleo kwa wazabuni; wakala wa barabara Arusha wafuate taratibu wanapoingia mikataba midogo (sub-contracting) na wakandarasi ili kuondokana na ucheleweshaji wa miradi na kuongezeka kwa gharama.
- ii) Wakala wa Barabara Arusha wadai kutoka kwa Mkandarasi A & E Building and Civil Engineering Limited kiasi cha Sh 63,151,174 kilicholipwa kwa kutumia taarifa ya uongo katika ukaguzi wa mwisho.
- iii) Wakala wa Barabara Arusha wahakikishe Mkandarasi Luneco Investment Limited anarekebisha mapungufu yote kulingana na mkataba Na. AE/001/15-16/AR/CON/W/31 and 74
- iv) Wakala wa Barabara Arusha wafanye tathimini kujua kiasi halisi cha fedha kilichotumika kwenye mkataba Na. AE/001/2015-16/AR/CON/W/31 na 74 na hatua stahiki.
- v) Hatua za kinidhamu zichukuliwe juu ya mtumishi wa Wakala wa Barabara Arusha ambaye ni mmoja wa wamiliki wa Wincom Enterprises Company Limited iliyoingia mkataba na Wakala wa Barabara Arusha kinyume na Kifungu 84 (3) cha sheria ya manunuzi ya umma 2011.
- vi) Pia, hatua za kinidhamu kuchukuliwa kwa watumishi wote walioandaa taarifa ya uongo wakati wa ukaguzi wa mwisho wa Mradi mkataba Na. AE/001/15-16/AR/CON/W/31 na 74; na
- vii) TAKUKURU wafanye uchunguzi kwenye mkataba Na. AE/001/16-17/AR/CON/W/08, 05; Mkataba Na. AE/001/15-16/AR/CON/W/31 Na mkataba Na AE/001/15-16/AR/CON/W/74.

9.4 Makosa Katika Manunuzi na Usimamizi wa Stoo kama Iliyotaarifiwa katika Taarifa ya Mhakiki Mali wa Serikali

Katika kutekeleza majukumu yangu ya Ukaguzi, nimetumia taarifa ya Mhakiki Mali za Serikali ambaye amepewa jukumu la kuhakiki Mali za Serikali kupitia Kanuni ya Fedha za Umma Kifungu 239-249 ya Mwaka 2001 ambayo inataka Mhakiki Mali kufanya uhakiki huru wa mali za serikali katika Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoza na kutoa taarifa ya uhakiki huo. Katika mwaka wa fedha wa 2016/2017, alitoa taarifa inayoonesha makosa mbalimbali yenye thamani ya Sh 6,223,172,903.53 katika Taasisi za umma ishirini (20) ukilinganishwa na mwaka wa fedha 2017/2018 iliyokuwa na thamani ya kiasi cha Sh 968,085,433.63 katika Taasisi 20 (ishirini). Mwaka huu wa ukaguzi yamekuwa pungufu kwa kiasi cha bilioni 5.26 ambayo ni sawa na asilimia 84.44. Hii inamaanisha kuwa Taasisi zimeongeza uzingatiaji wa sheria katika usimamizi wa stoo ukilinganisha na mwaka wa fedha uliopita.

Mapungufu katika manunuzi na usimamizi wa Stoo kama ilivyotolewa katika taarifa ya Mhakiki Mali wa Serikali yenye athari ya kifedha yameelezewa katika na Kiambatisho Na. 52, ambapo makosa yasiyokuwa na athari za kifedha yapo katika Kiambatisho Na. 53

Hoja zilizotolewa katika taarifa ya Mhakiki Mali wa Serikali ni vyema zikafuatiliwa na kutatuliwa, kwani zinaleta viashiria vya usimamizi mbovu ambao unaweza sababisha kupotea kwa mali za umma. Maafisa Masuuli wanashauriwa kuyaondoa mapungufu yote yaliobainishwa na Mhakiki Mali wa Serikali

Ili kupunguza au kuepuka upotevu wa mali kupitia wizi na matumizi mabaya, ninazishauri Taasisi husika kuongeza udhibiti wa ndani kwa kuhakikisha mali zote zinaingizwa katika kumbukumbu, na ziwe tayari kwa ukaguzi au kuonekana muda wowote itakapohitajika

Sura ya Kumi

Usimamizi wa Matumizi

10.1 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa mambo muhimu ya ukaguzi yaliyojiri pamoja na mapendekezo juu ya usimamizi wa matumizi kwa mwaka wa fedha unaoishia 2017/18. Sura hii inathibitisha kwa ujumla namna Maafisa Masuuli husika walivyozingatia Sheria mbalimbali, Kanuni, Maelekezo na Miongozo ya Serikali. Hivyo sura hii inatoa mrejesho wa namna rasilimali zilivyotumika na kusimamiwa na hivyo, kupelekea Serikali kuimarisha Uangalizi, Uwazi, Uwajibikaji, Utawala bora na kuchochea usimamizi bora wa rasilimali fedha katika nyanja zote za utendaji katika Wizara, Idara, Mabalazi na Sekretarieti za Mikoa.

Matokeo ya ukaguzi na mapendekezo, yakiwamo maelezo ya kina ya ukaguzi vimejadiliwa na Maafisa husika wa Wizara, Idara na Wakala wa Serikali; na maelezo yao yamezingatiwa katika kuandaa hii sura.

10.2 Dosari katika Matumizi yaliyofanywa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwenda kwenye Kampuni Binafsi za Kisheria Sh. 4,665,410,500

Katika ukaguzi wangu nimebaini kuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imetumia Sh. 4,665,410,500 kulipia ada za kisheria kwa kampuni tatu za kisheria, yaani M/S Curtis-Mallet, Prevost, Colt & Mosle LLP ya Londoni na Usharika kati ya Crax na kampuni ya uwakili ya Rweyongeza. Malipo yalikuwa kwa ajili ya kuiwakilisha Serikali ya Tanzania kwenye kesi ya usuluhishi kati ya Benki ya Standard Chartered (Hong kong) na Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye kesi Na. ICSID ARB/15/41. Mapitio ya nyaraka za malipo na viambatisho vingine yamebaini mapungufu yafuatayo:

- i) Kiasi kilichohojiwa cha ada za kisheria Sh. 4,665,410,500 hakikustahili kulipwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa niaba ya IPTL. Nimebaini kuwa, kulingana na vigezo vya kutoa hela katika Akaunti ya 'Escrow' ya Tegeta, IPTL ilikubali kulipia gharama za baadaye juu ya madai ambayo yangehusiana na hela iliyotolewa. Hata hivyo, Wanasheria

walipowasiliana na IPTL, Kampuni ilidai kuwa na hali tete ya kifedha. Aidha, barua ya IPTL ilieleza kuwa ingeweza kupata fedha kutoka kampuni nyingine zenye mahusiano lakini hilo halikuwezekana kwani lilihitaji kuapo kwa Mwenyekiti Mtendaji, jambo ambalo lilishindikana kwa sababu ya mashitaka yanayoendelea dhidi yake.

- ii) Malipo yaliyokatwa ya 15% ya Kodi ya zuio iliyopaswa kulipwa TRA kwa mujibu wa kifungu cha 83(1)(c)(ii) cha Sheria ya Kodi ya 2004 (iliyorekebishwa mwaka 2017). Hata hivyo, kampuni ya Curtis-Mallet ilidai tena kulipwa bila kukata kodi ya zuio, na hivyo kumlazimu Mwanasheria Mkuu wa Serikali kulipa kiasi kilichokuwa kimekatwa kama kodi ya zuio Sh. 512,073,000 kwa maelezo kuwa kiasi hicho kitakatwa kwenye malipo mengine: hivyo, kukiuka matakwa ya Sheria ya kodi.
- iii) Kutoshughulikiwa ipasavyo Mgongano wa maslahi tarajiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kabla ya kukubaliana na Kampuni za kisheria. Nimebaini kuwa, tarehe 20/11/2015 kupitia barua yenye kumbukumbu Na. AGC/C.130/1/68/70, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliwasiliana na kampuni ya kisheria ya Crax na RK Rweyongeza juu ya Kuwepo Kwa mgongano wa maslahi na kampuni ya Uingereza kwani Benki ya Standard Chartered (Hong Kong) ni kampuni tanzu na Benki ya Standard Chartered (Uingereza).Hata hivyo, menejimenti ilijibu kuwa hakuna mgongano wa maslahi.
- iv) Aidha kulikosekana ushahidi wa kama huduma za kisheria zilipatikana kiushindani kulingana na matakwa ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 na kununi zake za mwaka 2013 kwa kampuni zote tatu. Hii ni kwa sababu menejimenti iliamua kutumia manunuzi yasiyo ya wazi.
- v) Ni maoni yangu kuwa, kiasi kilichotumika Sh. 4,665,410,500 hakikupaswa kulipwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, bali IPTL. Kutolipa kodi ya zuio huizua Serikali kukusanya kodi zake. Mapungufu katika kutathmini mgongano wa maslahi kabla ya makubaliano huweza kuathiri uwakilishi kwenye kesi dhidi ya Serikali. Pia, manunuzi yasiyo na

ushindani yanayohusu huduma za kampuni za Sheria yanaweza kusababisha tozo kubwa ambazo haziwezi kuthibitishwa kwa kiwango kinachoridhisha.

- vi) Hivyo, nashauri menejimenti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kudai Sh. 4,665,410,500 kutoka IPTL ili kuendana na makubaliano kabla ya kutoa hela kwenye akaunti ya ‘Escrow’ ya Tegeta. Pia idai Sh. 512,073,000 kama kodi ya zuio kutoka kwa kampuni ya Curtis-Mallet. Pia, menejimenti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inashauriwa kuhakikisha inafanya uchambuzi wa kina na wadau wa Sheria juu ya uwezekano wa kuwapo kwa mgongano wa maslahi katika hatua za awali. Aidha, Ofisi izingatie Sheria ya manunuzi ya umma ya mwaka 2011 na kanuni zake za mwaka 2013 juu ya manunuzi ya huduma za Kisheria. Zaidi, kuhakikisha vihatarishi vinadhitiwa kikamilifu kabla ya kufanya malipo.
- vii) Vilevile, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pia itoe hali ya sasa ya kesi inayosikilizwa ICSID na kufanya ufuatiliaji wa karibu kuhakikisha kwamba makampuni yaliyohusishwa yanatuwakilisha kwa umakini na kulinda maslahi ya Nchi.

10.3 Mapungufu katika Usimamizi wa Ankra za Matibabu Nje ya Nchi Sh. 7,013,014,856.65

Ukaguzi wa Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto umebaini kuwa Sh. 7,013,014,856.65 zilitumika kwenye matibabu katika Hospital ya AHEL-India bila kuwa na uthibitisho kwa kiwango kinachoridhisha. Ankra zilizowasilishwa zinapingana na Aya ya 2 ya kifungu cha 2.2 cha makubaliano kati ya AHEL na MOHS (Kwa sasa MHCDGEC) kinachotaka mgonjwa kuruhusiwa AHEL baada ya kupokea nakala ya barua ya kibali inayotolewa na MHCDGEC. Mgonjwa atakayetibiwa anapaswa kuwa na nakala ya barua ya kibali ili AHEL waweze kutumia kibali hicho kuhakiki sifa za wagonjwa. Kwa lengo la udhibiti, baada ya kumaliza matibabu Wagonjwa wanapaswa kusaini ankra zao kabla ya kurejea Tanzania mara tu baada ya kuruhusiwa. Kwa kuongezea, kwenye ankra ambazo hazikusainiwa, madai mengine hayakuhakikiwa na kamati ya ufundi ya Ukaguzi wa kitabibu. Zaidi,

hapakuwa na nyaraka toshelezi na kutoingiza ankra kwenye rejista ya Wizara kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali Na. 73 hapo chini.

Jedwali Na. 73: Muhtasari wa mapungufu yaliyobainika kwenye ankra za matibabu

Na	Mapungufu yaliyoibuliwa	Kiasi(TZS)
1	Ankra ambazo hazikupitiwa na timu ya Wakaguzi wa Kitabibu	3,785,840,959.33
2	Ankra ambazo hazikusainiwa na Wagonjwa	3,046,539,912.50
3	Ankra zisizo na viambatisho	121,497,661
4	Ankra ambazo hazikuingizwa kwenye rejista	59,136,323.82
Jumla		7,013,014,856.65

Chanzo: Barua ya Mapungufu ya MHCDGEC ya mwaka 2017/2018

Wizara ilijibu kuwa imewaagiza matabibu ambata kusimamia udhibiti kwa kuhakikisha kuwa ankra zote zinasainiwa kulingana na tarehe za kuruhusiwa wagonjwa; zile ambazo hazina viambatisho menejimenti ilihaidi kuziwasilisha kwa ajili ya uhakiki. Menejimenti haikufanyia kazi mapendekezo yangu ya miaka ya nyuma, kwani ankra za matibabu zinaelendelea kujirudia bila kuwa na mkakati wa kuziepuka.

Kwa maoni yangu, naamini kuwa kushindwa kuwajibika kwenye matibabu nje ya nchi kunaweza kutengeneza mianya ya matumizi mabaya ye fedha za umma kupitia madai hewa kwa gharama ya mlipa kodi, hivyo, thamani ya fedha haiwezi kufikiwa.

Hivyo, nashauri menejimenti ya MOHCDGEC kuhakikisha kuwa ankra zote zinapitiwa kitaalamu na kiuledi na Maafisa tabibu. Aidha, timu ya Ukaguzi wa Kitabibu kabla ya malipo ihakikishe kwamba madai yote yasiyo ya kweli yanaondolewa. Pia, ufuatiliaji wa ankra/hati za madai ambazo zinakosekana kutafutwa na ankra zote za kweli na kumbukumbu zake zinaingizwa kwenye rejista ya ankra. Madai yote yaliyohojiwa yanapawsa kuwasilishwa ipasavyo kwa ajili ya uhakiki.

10.4 Miamala yenye utata katika Sekretarieti ya Wilaya ya Tarime Sh. 514,000,000.

Katika Ukaguzi wangu katika Sekretarieti ya Wilaya ya Tarime, nimebaini kuwa Sh. 514,000,000 zilipokelewa na DAS Tarime kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya Hospitali ya Wilaya ya Tarime na kupima eneo lililopendekezwa kwa ajili ya kilimo cha miwa na kiwanda cha sukari kama ilivyoenezwa katika Jedwali Na. 74 hapo chini

Jedwali Na. 74: Mihutasari wa miamala yenye utata

Tarehe	Maelezo	Kiasi(Sh)
29-04-2017	Malipo kwa DAS kupitia NMB akaunti Na. 30410008369 kutoka kwa kampuni ya Biashara ya North Mara Comm kwa lengo la kupima eneo la kupanda miwa na kujenga kiwanda cha miwa	214,000,000
3-08-2017	Halmashauri ya Wilaya Tarime ilihuisha fedha kwenda akaunti Na. 30410008369 kama mchango wa Halmashauri wa kukarabati na kuboresha Hospitali ya Wilaya ya Tarime	300,000,000
Jumla		514,000,000

Chanzo: Barua ya mapungufu ya RAS-Mara kwa mwaka wa fedha 2017/18

Kama ilivyoenezwa hapo juu, nimebaini dosari zifuatazo:

- i. **Kufungua akaunti ya benki NMB bila kibali cha Mamlaka husika**

Nimebaini kuwa akaunti Na.30410011011 haikufunguliwa chini ya mamlaka husika kwa mujibu ya kifungu cha 15 cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001(Iliyorekebishwa 2004) kinachotaka akaunti ya umma au akaunti ya ofisi kutofunguliwa bila mamlaka ya maandishi kutoka kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali kama ilivyoenezwa zaidi na kanuni ya 155(1) ya Kanuni za fedha za Umma ya mwaka 2001 inayotaka pia Ofisa wa umma kutofungua akaunti ya benki ya amana, kuihifadhi au kutoa fedha za umma au fedha nyingine ambazo Afisa husika anawajibika nazo kulingana na majukumu ya ofisi au kwa ajili ya kufanya miamala ya kibenki bila kibali kutoka kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali

ii. Utata katika kuhaulisha Sh. 300,000,000

Tarehe 14 Agosti, 2017 ofisi ya DAS Tarime alihawilisha Sh. 300,000,000 kutoka Akaunti ya DAS NMB Na 30410008369 kwenda kwenye akaunti ya biashara iliyofunguliwa Na. 30410011011 kwa jina la Akaunti ya Mageuzi ya Hospitali ya Tarime. Lakini tarehe hiyohiyo (14 Agosti, 2017) Sh. 300,000,000 zilihawilishwa tena kutoka akaunti Na. 30410011011 kwenda kwenye akaunti ya Zacharia Wambura. Nina shaka juu ya mzunguko wa hizi fedha kupitia kwenye akaunti iliyotajwa ambayo inamhusisha Zacharia Wambura anayehusika na ukarabati wa Hospitali ya Wilaya Tarime bila kuwa na ushaidi wa nyaraka. Kukosekana kwa nyaraka kunaacha kiasi kilicholipwa kuendelea kuwa chini ya muamala wenye utata.

iii. Kutohakikiwa kwa maelezo ya matumizi ya fedha zilizochangwa na kampuni ya Biashara ya North Mara Comm Sh. 214,000,000

Sikuweza kuhakiki maelezo ya matumizi ya Sh. 214,000,000 zilizochangwa na kampuni ya Biashara ya North Mara Comm. Hii ni kwa sababu, hati za malipo na viambatisho vyake yaliyofanywa na DAS kutoka akaunti Na. 30410008369 zilichukuliwa na ofisi ya PCCB. Nimeshindwa kupata uhakika wa kiasi kilichohojiwa kwa sababu ya kukosekana kwa nyaraka. Madhara yake ni kwamba, mawanda yangu ya Ukaguzi yameathiriwa kwa kiwango kikubwa katika nyanja zote.

iv. Kukosekana kwa uthibitisho wa taratibu za manunuzi

Nimebaini kuwa ofisi ya DAS Tarime haina Kitengo cha Manunuzi ambacho kinglezingatia mchakato wa manunuzi kwa mujibu wa kifungu cha 31(1) cha Sheria ya manunuzi ya umma ya 2011. Kwa sababu hiyo, nimeshindwa kupata uhakika kama manunuzi ya vifaa vya Hospitali yamezingatia matakwa ya kifungu cha 64(1) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 na kanuni zake za mwaka 2013.

Menejimenti ya RAS ilitoa maoni kwamba, udhaifu ulisababishwa na uelewa hafifu wa ofisi ya DAS juu ya namna ya kuendesha michakato ya manunuzi. Zaidi ya hilo, kulikuwa na kikwazo cha mawasiliano kati ya ofisi ya DAS na Katibu Tawala wa Mkoa juu ya namna ya kutekeleza

miradi iliyoanzishwa Matokeo yake hakupewa taarifa vizuri juu ya miamala iliyopitishwa kwenye akaunti husika.

Ni mtazamo wangu kuwa, kukosekana kwa ushahidi wa nyaraka za kuthibitisha miamala iliyofanyika kunaweza kutengeneza mianya ya matumizi mabaya ya fedha za umma.

Kwa hiyo, nashauri menejimenti ya Sekretarieti ya Mkoa wa Mara, kwa kushirikiana na DAS Tarime, kuhakikisha:

Kuzingatia matakwa ya Sheria ya Fedha za Umma ya 2001 (Iliyorekebishwa mwaka 2004) juu ya kufungua akaunti na Sheria ya Manunuzi ya umma ya mwaka 2011 na kanuni zake za mwaka 2013 RAS anashauriwa kuingilia kati na kuchunguza suala hili kwa ukaribu; na

Hatua stahiki zichukuliwe ili kutatua mapungufu yaliyobainika ili mbinu za kupunguza hayo mapungufu zinaanzishwa ili kuzuia kutokea mambo yaleyale kwa siku za usoni.

10.5 Malipo yasiyo ya kawaida ya posho mbalimbali yaliyofanywa na Tume ya Huduma za Walimu Sh. 721,050,000

Ukaguzi umebaini kuwa, wafanyakazi mbalimbali wa Tume ya Huduma za Walimu walilipwa posho inayofikia Sh. 721,050,000 kwa lengo la kutekeleza shughuli za ofisi, kwa kulipa posho ya safari kwa siku 324, posho ya kazi za ziada kwa siku 365 na posho za vikao kwa siku 127. Hii si kwamba inaashiria matumizi yenye mashaka bali kutokuwa na uhakika kama wafanyakazi walikuwa nje ya kituo cha kazi kwa mwaka mzima wakati rejista ya mahudhurio imeonesha Wafanyakazi hao walikuwapo ofisini kwa kipindi hicho.

Ni mtazamo wangu kwamba, mapungufu haya yamesababishwa na udhibiti wa ndani na uaminifu hafifu juu ya kulinda na kutumia fedha za umma, ambapo kama hatua hazitachukuliwa yanaweza kuchochea matumizi mabaya ya fedha za umma.

Kwa sababu ya udhaifu ulioibuliwa hapo juu, nashauri menejimenti ya Tume ya Huduma za Walimu kuanzisha mifumo imara ya udhibiti wa ndani ikiwamo huduma za ukaguzi wa ndani, yenye vitendea kazi

vya kutosha na mgawanyo imara wa majukumu ambao unaweza kuwa na umuhimu katika kupunguza vihatarishi vilivyotambuliwa.

Nashauri zaidi Ofisi ya Raisi Tawala za Mikoa na Serikali za mitaa kuchunguza kwa ukaribu suala hili, na itakapohitimishwa wahusika watapaswa kuwajibika.

10.6 Kuongezeka kwa gharama za kukodi magari katika Balozi za Tanzania Moroni na Brasilia Sh 87,461,046.99

Ukaguzi wangu umebaini kuwa, Balozi za Moroni na Brasilia zimekuwa zikikodi magari kwa ajili ya shughuli za kila siku za Baloz; hivyo kukinzana na kanuni ya 84 ya kanuni za Huduma za Umma (Huduma za Nje ya Tanzania) ya mwaka 2016 inayotaka kutoa gari sahihi la uwakilishi kwa Mkuu wa Balozi na gari jingine linatolewa kwa ajili ya huduma za jumla. Katika ukaguzi wa mwaka husika, Balozi zililipa Sh. 87,461,0546,99 kwa ajili ya kukodi magari.

Menejimenti za Balozi husika zimekuwa zikifanya ufuatiliaji wa karibu na Wizara mama kupitia barua yenye kumbukumbu Na. CJB111/162/02/16 ya tarehe 8 Novemba, 2017 na CKCA.41/65/01/III ya tarehe 15 Januari 2019, mtawalia, lakini hakuna kilichofanywa na Wizara ili kumaliza tatizo hili kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali Na. 10.3 hapo chini

Jedwali Na. 10.3: Muhtasari wa gharama za kukodi magari

Na	Fungu	Mkaguliwa	Kiasi(Sh.)
1	2034	Ubalozzi wa Tanzania Moroni	63,848,500.00
2	2031	Ubalozzi wa Tanzania Brasilia	23,612,546.99
Jumla			87,461,046.99

Chanzo: Barua za mapungufu kwa mwaka wa fedha 2017/2018

Naamini kuwa, gharama za kukodi zinazofikia Sh. 87,461,046.99 zingeweza kuepukwa kama magari mapya yangenunuliwa na kutolewa kwa Balozi husika.

Kwa hiyo, nashauri menejimenti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuachana na ongezeko la gharama za kukodi magari kwenye Balozi kwa kununua magari yake.

10.7 Malipo yasiyo na nyaraka toshelezi Sh. 4,369,240,033.86

Katika Ukaguzi wa mwaka wa fedha 2017/18, nimebaini kuwa Taasisi arobaini (40) zilifanya malipo ya Sh. 4,369,240,033.86 ambayo hayakuwa na nyaraka toshelezi kama vile hati za madai, hati za kukiri kupokea huduma, hati za malipo na kadhalika. Kukosekana kwa hizi nyaraka kulizuia mawanda yangu ya ukaguzi katika kuthibitisha usahihi wa matumizi yaliyofanywa; hivyo kukinzana na kanuni ya 95 ya kanuni za fedha za umma ya mwaka 2001 inayotaka malipo kuwa na nyaraka zinazojitosheleza. Kiambatisho Na. 54.


Ni maoni yangu kuwa, malipo yasiyo na nyaraka toshelezi kwa kiwango kikubwa yamezuia mawanda yangu ya ukaguzi; hivyo uhalali wa malipo hauwezi kuthibitishwa katika kiwango kinachoridhisha.

Nawashauri Maafisa Masuuli husika kukumbuka kuwa malipo yasiyo na nyaraka kisheria yanachukuliwa kama ni hasara ya fedha taslimu ambayo Mhasibu mkuu wa Serikali anapashwa kuijumuisha kwenye taarifa ya hasara ya mwaka ili kuchunguzwa na PAC kulingana na kanuni ya 18(1)(f) & (2) ya Kanuni za fedha za umma za mwaka 2001. Kwa sababu hiyo, Maafisa Masuuli wanawajibika na kutakiwa kuleta nyaraka zilizohojiwa kwa ajili ya uhakiki.

Maafisa Masuuli pia wanashauriwa kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani ya kumbukumbu za fedha kutoka hatua za awali za kutengeneza nyaraka, kuhifadhi, kutafuta na kuharibu nyaraka hizo. Hivyo, hatua za masahihisho kwa mujibu wa kanuni ya 24 ya Kanuni ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 zinapaswa kuzingatiwa

Kwa kulinganisha na Ripoti ya Jumla ya mwaka uliopita 2016/17 kiasi kilichohojiwa kimepungua kutoka Sh. 6,895 milioni mpaka Sh. 4,369 milioni ijapokuwa idadi ya taasisi imeongezeka kutoka 27 mpaka 40. Katika mwaka huu nimejumuisha malipo yote yasiyo na viambatisho toshelezi kama vile malipo yasiyo na hati za malipo, na kukosekana kwa nyaraka. Hivyo kiasi kilichokuwa kimeoneshwa kwa utengano mwaka uliopita kimejumlishwa kwa lengo la ulinganisho. Kupitia ulinganisho huu, Maafisa Masuuli wamezingatia kwa kiwango kikubwa mapendekezo yangu kama inavyooneshwa hapo chini:

Kielelezo Na. 3: Ulinganisho wa malipo yasiyo na nyaraka toshelezi kwa miaka 8 mfululizo



10.8 Kodi za zuio ambazo hazikudaiwa Sh. 722,173,494.09

Ukaguzi wangu umebaini kuwa, Taasisi 7 zilishindwa kukata kodi ya zuio na kulipa TRA kama inavyotakiwa na kifungu cha 83(1)(c)(ii) cha Sheria ya Mapato ya mwaka 2004 (Iliyorekebishwa mwaka 2017) kinachotaka kukata kodi za zuio kwenye ada za huduma na malipo ya mikataba na kupeleka kwa Kamishna ndani ya siku saba baada ya kila mwisho wa mwezi kodi yoyote iliyokuwa imezuiliwa kulingana na kifungu cha 84(1) cha sheria hiyohiyo ya kodi ya mapato. Ukaguzi wangu umebaini kuwa Sh. 722,173,494.09 hazikukatwa kama kodi ya zuio; hivyo kukinzana na utii wa kodi kwa hiari kwenye vifungu vilivyotajwa hapo awali. Maelezo yametolewa kwenye Jedwali Na. 75 hapo chini.


Jedwali Na. 75: Muhtasari wa Kodi za Zuio ambazo hazikukatwa

Na	Fungu	Mkaguliwa	Kiasi(Sh.)
1	78	Sekretarieti ya Mkoa wa Mbeya	12,578,443
2	16	Mwanasheria Mkuu wa Serikali	512,073,000
3	54	Sekretarieti ya Mkoa wa Njombe	37,414,077
4	67	Ofisi ya Rais-Sekretarieti ya Ajira	57,615,961
5	96	Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo	56,420,478
6	3	Tume ya Taifa ya mipango ya Matumizi ya Ardhi	14,000,000
7	70	Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha	32,071,535
Jumla			722,173,494

Chanzo: Barua za mapungufu kwa mwaka wa fedha 2017/2018

Ikilinganishwa na Ripoti ya Jumla ya mwaka uliopita (2016/17), hakuna maboresho juu ya kuzingatia sheria za kodi. Hii ni kwa sababu kiasi kilichohojiwa kimeongezeka kutoka Sh. 109 milioni hadi Sh. 722 milioni kama ilivyooneshwa kwenye picha hapo chini. Idadi ya taasisi ambazo hazijazingatia kifungu cha 83(1) imepungua kutoka taasisi 10 hadi 7.

Kielelezo Na. 4: kodi za zuio ambazo hazikudaiwa kwa miaka 4 mfululizo




Ni maoni yangu kuwa, kutozingatia vifungu vya 83(1) na 84(1) vya Sheria ya Kodi kunafanya taasisi zilizohojiwa kuwajibika kisheria kulipa kodi hizo ambazo zilipaswa kuwa zimezuiwa katika namna hiyohiyo. Hivyo, mgawanyo wa bajeti uliokuwa umeidhinishwa kwa malengo mengine unaweza kuathiriwa kwa gharama ya kushindwa kutii Sheria za Kodi.

Napendekeza kuwa, Menejimenti za Taasisi husika zihakikishe kodi za zuio ambazo hazikukatwa zilipwe bila kuchelewa; na kwa siku za usoni, kodi hizo zinapaswa kuwa zinakatwa kwa usahihi na kupelekwa kwa Kamishna kama inavyotakiwa na vifungu vilivyotajwa hapo awali.

10.9 Malipo yasiyo na risiti za kielektroniki (EFD) Sh. 1,432,407,818.97

Ukaguzi wangu umebaini kuwa Taasisi 20 zililipa Sh. 1,432,407,818.97 kwa Wazabuni mbalimbali wa bidhaa na huduma bila kudai risiti za kielektroniki kama inavyotakiwa na kifungu cha 36 (1) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015 na Kanuni ya 28(1) ya Sheria ya Kodi ya Mapato (Vifaa vya Kielektroniki) kanuni za mwaka 2012 zinazotaka Wazabuni wote na Wanunuzi kutoa na kudai risiti za kielektroniki. Hii ni kwa sababu, Serikali ina sera ya kuhakikisha miamala yote inaunganishwa na mifumo ya kielektroniki ili kuwa na ukusanyaji stahiki kupitia kudai risiti za kielektroniki wakati wa kununua bidhaa au huduma. Hivyo, Ukaguzi wangu umeshindwa kuthibitisha kama wazabuni hao wamesajiliwa kutoa risiti za kielektroniki. Rejea Kiambatisho Na. 62



Ikilinganishwa na Ripoti kuu ya mwaka jana (2016/17) kiasi kilichohojiwa kimepungua kidogo kutoka TZS 1,533 milioni mpaka Sh. 1,432 milioni. Vilevile idadi ya taasisi ambazo hazizingatii vifungu vya Sheria za Kodi vilivyotajwa imepungua kutoka taasisi 29 hadi 20. Kwa kipindi cha miaka 6, mwendelezo unaonesha kuna maboresho katika kuzingatia mambo ya kodi kama ilivyooneshwa kwenye chati ya hapo juu.

Ni mtazamo wangu kuwa, kutodai risiti za kielektroniki kunaweza kutengeneza mianya ya kupoteza mapato ya serikali ikitokea miamala iliyohojiwa haitatamkwa na Wazabuni wakati wa kujaza mawasilisho ya makadirio ya kodi (Tax returns). Inapaswa kueleweka kuwa kushindwa kudai risiti za kielektroniki ni kosa kwa mujibu wa kanuni ya 50 na 55 ya Kanuni za Usimamizi wa Kodi (Kanuni za Jumla) za mwaka 2016.

Napendekeza kuwa Maafisa Masuuli husika washughulikie na wazabuni wanaotumia mashine za kielektroniki au hati za madai zilizounganishwa na TRA. Zaidi, katika siku za usoni uzingatiaji wa sheria za kodi unapaswa kuzingatwa ipasavyo.

10.10 VAT ya 18% ambazo hazijadaiwa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwenye Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji Sh. 49,285,014.88

Mapitio ya ukaguzi wa malipo yaliyofanywa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji yamebaini kuwa, Wzara ilifanya malipo kwa wazabuni mbalimbali wa bidhaa na huduma, ambapo Sh. 49,385,014.88 ilitumika kama VAT ambayo ilipaswa kurejeshwa tena. Hii ni kulingana na Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania na Washirika wa Maendeleo katika utekelezaji wa mradi wa WSDP wa kutumia makubaliano ya utekelezaji wa kawaida; ambapo Serikali ya Tanzania ilikubali kusamehe matumizi yote halali ya bidhaa, ujenzi na huduma zinazofadhiliwa na WSDP katika kodi zinazotozwa moja kwa moja na zisizotozwa moja kwa moja na Serikali ya Tanzania. Pia, barua yenye kumbukumbu Na. TRA/HQ/CG/L.3 ya tarehe 7 Septemba, 2015 na Sheria mpya (VAT Na.5 ya 2014) moja kwa moja vinasamehe kodi kwenye bidhaa zinazoagizwa nje na kutosamehe moja kwa moja bidhaa za ndani kwa kutaka VAT ilipwe kwanza na baade idaiwe chini ya kifungu cha 85 cha Sheria. Hivyo kusamehe kabisa bidhaa za nje na ndani. Menejimenti ilijibu kuwa imedai marejesho ya VAT kutoka TRA kupitia barua Na.CA.362/547/05B, CA.362/547/05B/02 na CA.362/547/05B/03. Hata hivyo, mpaka muda wa kuhitimisha ukaguzi wangu, Januari 2019, kiasi hicho kilikuwa hakijarejeshwa Wizarani.

Kwa maoni yangu, wanufaika wa WSDP waliokusudiwa hawakunufaika na matokeo ya mradi kwa kiwango sawa na kiasi ambacho hakijadaiwa Sh. 49,385,014.88.

Napendekeza menejimenti ithibitisha marejesho ya VAT iliyolipwa awali na kuleta taarifa za marejesho kwa ajili ya uhakiki.

10.11 Malipo ya madeni ya nyuma ambayo awali yalikuwa hayajaoneshwa Sh. 145,067,788.50

Kanuni ya 85(3) ya Kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2001 inayotaka matumizi kuingizwa kwa usahihi katika mwaka husika wa matumizi na hayapaswi kusogezwa mbele kwa lengo la kukwepa matumizi ya ziada yanayotolewa kwenye makadirio. Kinyume na kanuni hiyo, Ukaguzi wangu umebaini kuwa malipo ya Sh. 145,067,788.50 yaliingizwa kwenye matumizi ya mwaka huu japo miamala husika ilifanyika kwenye mwaka wa fedha uliopita; na matumizi hayo hayakuingizwa kwenye taarifa za fedha zilizopita. Zaidi ya hayo, nimebaini kuwa, madai hayakuingizwa kama madeni katika mwaka husika. Hivyo, kukinzana na Viwango vya Kimataifa vya Uhandaji wa Hesabu za Umma kwa Msingi usio Taslimu (Aya ya 7 ya IPSAS 1) inayotaka miamala na matukio mengine kutambuliwa inapotokea; na si lazima mpaka taslimu au taslimu linganishi ziwe zimepokelewa au kulipwa; na inapaswa kuingizwa kwenye mwaka husika. Taasisi husika zimeorodheshwa kwenye Jedwali Na. 76 hapo chini.


Jedwali Na. 76: Malipo ya madeni ya nyuma ambayo hayakuoneshwa

Na	Mafungu	Mkaguliwa	Kiasi (Sh.)
1	73	Sekretarieti ya Mkowa wa Iringa	16,139,800.00
2	81	Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza	64,991,818.00
3	72	Secretarieti ya Mkoa wa Dodoma	48,407,704.00
4	85	Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora	11,683,115
5	62	Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano	3,845,351.50
Jumla			145,067,788.50

Chanzo: Barua za mapungufu kwa mwaka wa fedha 2017/2018

Ikilinganishwa na Ripoti kuu iliyopita ya 2016/17, idadi ya taasisi ambazo hazijazingatia kanuni ya 85(3) ya kanuni za Fedha za Umma

za mwaka 2011 na aya ya 7 ya IPSAS 1 zimeongezeka kutoka 2 hadi 5. Hii inaonesha kuwa, hakuna maboresho katika kuzingatia kanuni na viwango. Kiasi kichohojiwa kimeongezeka kutoka Sh. 23 milioni hadi Sh. 145 milioni kama ilivyooneshwa hapo chini. Hii sio ishara nzuri katika usimamizi wa matumizi



Naamini kuwa bajeti kwa ajili ya shughuli zilizobainishwa kutekelezwa katika mwaka huu zimeathirika vibaya kwa kiwango cha Sh. 145,067,788.50; hivyo kukinzana na makadirio ya bajeti iliyotengwa.

Napendekeza kuwa, Maafisa Masuuli wachambue shughuli zote ambazo hazikutekelezwa kutokana na madhara ya kulipa madeni ya nyuma na kuhakikisha zinaingizwa tena kwenye bajeti ijayo. Menejimenti za Taasisi zilizohojiwa zinashauriwa muda wote kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu za Umma kwa Msingi usio Taslimu na kanuni ya 85(3) ya kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001

10.12 Fedha ambazo hazijarejeshwa kwenye akaunti za amana Sh. 562,635,234.24

Ukaguzi wangu wa malipo umebaini kuwa Wizara, Idara na Sekretarieti 10 zilihaulisha Sh. 562,635,234.24 kutoka kwenye akaunti

za amana za ndani zilizokopwa kutoka kwenye akaunti za amana na miradi iliyotengwa kwa matumizi mahsusi kwa lengo la kuzirejesha tena. Kinyume chake, mpaka mwisho wa mwaka (30 Juni, 2018) kiasi kilichokopwa kilikuwa hakijarejeshwa kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali Na. 77 hapo chini:

Jedwali Na. 77: Fedha ambazo hazijarejeshwa kutoka kwenye akaunti ya Amana

Na	Fungu	Mkaguliwa	Kiasi(Sh.)
1	73	Sekretarieti ya Mkoa wa Iringa	66,529,840
2	46	Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia	223,200,000
3	77	Sekretarieti ya Mkoa wa Mara-Hospitali ya Rufaa ya Mkoa	6,500,000
4		Sekretarieti ya Mkoa wa Mara	48,172,339
5	81	Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza	69,856,588
6	83	Sekretarieti ya Mkoa wa Shinyanga	18,332,000
7	40	Mahakama ya Tanzania	25,448,248
8	36	Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga	28,740,000
9	85	Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora	11,861,672
10	70	Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha	14,529,662
			49,464,885
Jumla			562,635,234

Chanzo: Barua za mapungufu kwa mwaka wa fedha 2017/2018

Nimebaini kuwa, kuchelewa kurejesha fedha zilizokopwa kunaweza kusababisha kuchelewa au kutotekelezwa kwa shughuli zilizopangwa. Hivyo kusababisha kutofanikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa

Kwa hiyo, napendekeza kuwa Maafisa Masuuli wanapaswa kurejesha fedha zilizokopwa ili kurahisisha utekelezaji wa shughuli zilipopangwa kutekelezwa.

10.13 Dosari katika Usimamizi wa Masurufu Sh. 6,356,450,927.45

Masurufu ni fedha taslimu ambazo Serikali hutumia kulipia vitu vidogovidogo na matumizi ya mara kwa mara. Pia humaanisha fedha za awali anazopewa mtu kwa lengo mahsusi. Ijapokuwa masurufu yanaweza kuhusisha kiasi kidogo, bado usimamizi wake unapaswa kuangaliwa kwa umakini kwani inaweza kuvutia udanganyifu na ubadhirifu katika kuyarejesha. Wakati wa Ukaguzi, nimebaini dosari zifuatazo:

- a) Ucheleweshaji wa kurejesha masurufu muda wake unapofikia ukomo;
- b) Masurufu yaliyolipwa moja kwa moja kama matumizi kwenye vifungu vya matumizi;
- c) Kutotumia mfumo wa Epicor 9.05 wakati wa kutoa masurufu (Moduli za masurufu);
- d) Rejista zinaandaliwa kwa mkono, hivyo kuwa katika hatari ya marejesho ya masurufu yenye udanyanyifu;
- e) Masurufu yaliyotolewa kwa majina tofauti na Maofisa waliopokea
- f) Masurufu yaliyorejeshwa na watu tofauti na waliopewa masurufu;
- g) Kuwapo kwa mazingira yalisababisha tarehe ya marejesho kuwa ya awali kuliko tarehe ya kulipa masurufu kwa wahusika; na
- h) Baadhi ya waajiriwa walipewa masurufu mengine wakati wameshikilia masurufu ambayo hayajarejeshwa kinyume na Kanuni ya 103 (7) ya Kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2001

Katika Ukaguzi wangu, nimebaini kuwa, Wizara, Idara, Balozi na Sekretariaeti za mikoa 28 zilifanya malipo yanayofikia Sh. 6,356,450,927.45 ambayo hayakuwa na uwajibikaji stahiki; hivyo, kuashiria kuwa kuna uwezekano wa matumizi mabaya ya fedha za Umma.

Kwa hiyo, napendekeza menejimenti za taasisi husika kuhakikisha masurufu yanafanyiwa marejesho mara tu baada ya lengo la hayo masurufu kukamilika; na muda haupaswi kuzidi siku 14 za kazi. Vinginevyo kiasi kilichosalia kinapaswa kurejeshwa kutoka kwenye mshahara au stahiki au malipo mengine ambayo hajapewa mshika masurufu kama inavyotakiwa na kanuni ya 103(3) ya Sheria ya Kanuni za fedha za Umma ya mwaka 2001. Tazama Kiambatisho Na. 56

10.14 Malipo yaliyofanyika kimakosa katika vifungu visivyostahili Sh. 885,994,926,713.82

Kanuni ya 42(2) ya Kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2001 inataka Bunge mara tu baada ya kuidhinisha makadirio, kutunga sheria ya matumizi itakayompa mamlaka Waziri kutumia kiasi kilichoidhinishwa kwenye makadirio na kuzigawa kwenye mafungu yaliyoelezwa kwenye sheria. Sheria hiyo inataka kila matumizi na mapato kuoneshwa kwa usahihi kulingana na maelezo ya bajeti iliyoidhinishwa. Kinyume chake, katika Mwaka huu wa Ukaguzi nimebaini kuwa Sh. 885,994,926,713.82 zililipwa kimakosa kutoka kwenye vifungu visivyostahili kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali Na. 78 hapo chini.

Jedwali Na. 78: Malipo yaliyofanyika kimakosa kwenye vifungu visivyostahili


Na	Fungu	Mkaguliwa	Kiasi(Sh.)
1	36	Sekretarieti ya Mkoa wa Katavi	25,358,936.00
2	91	Mamlaka ya Udhhibiti wa Madawa ya Kulevya	24,975,375.98
3	92	Tume ya Kuzuia UKIMWI Tanzania	13,040,000.00
4	81	Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza	11,392,600.00
5	33	Ofisi ya Rais, Sekretariaeti ya Viongozi wa Umma	24,756,381.84
6	2034	Ubalozi wa Tanzania -Moroni	430,859,250.00
7	85	Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora	4,816,700.00
8	13	Kitengo cha kuzuia Fedha Haramu	40,210,165.00
9	48	Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi	27,700,000.00
10	22	Deni la Taifa na Huduma za Jumla	885,391,817,305.00
Jumla			885,994,926,713.82

Chanzo: Barua za mapungufu kwa mwaka wa fedha 2017/2018

Hii si tu inaonesha kwamba mchakato wa bajeti hauna uhalisia, bali pia inaashiria upotoshaji wa taarifa za fedha za taasisi zilizokaguliwa.

Nimebaini kuwa malipo yaliyofanyika kimakosa kwenye vifungu visivyostahili imeongezeka kwa kiwango kikubwa sana kutoka Sh. 751,946,000 hadi Sh. 885,994,926,713.82 kutoka mwaka jana 2016/17 hadi 2017/18. Taasisi zilizohusika zimeongezeka kidogo kutoka taasisi 7 hadi 10 kama ilivyooneshwa katika chati ya hapo chini. Tofauti hii imechangiwa zaidi na fungu Na. 22-Deni la taifa na Huduma za jumla.

Kielelezo Na. 5: ulinganisho wa matumizi yaliyolipwa kimakosa kutoka kwenye vifungu visivyostahili



Narudia mapendekezo yangu ya miaka ya nyuma na kushauri Maafisa Masuuli kutoendelea kuchepusha fedha na kuzingatia matumizi yanakuwa kwenye vifungu vya bajeti iliyoidhinishwa. Pale inapotokea uchepushaji haukwepeki, kibali cha kubadili matumizi lazima kiombwe kutoka kwenye mamlaka husika kwa mustakabali na kifungu cha 41 cha Sheria Na.11 ya Bajeti ya 2015.

10.15 Matumizi yasiyo na tija Sh. 668,764,264.53

Kama ilivyotafsiriwa na kanuni ya 21 ya Kanuni za fedha za Umma za 2001, malipo yasiyo na tija ni yale yaliyofanywa kwenye huduma hewa (zisizo na manufaa), na ambayo yangeepukika kama umakini wa hali ya juu ungetiliwa maanani. Kwa maana hiyo, nimebaini kuwa taasisi 3 zimetumia Sh. 668,764,264.53 kama matumizi yasiyo na tija kama ilivyofupishwa katika Jedwali Na. 79 hapo chini.


Jedwali Na. 79: Orodha ya malipo yasiyo na tija

Na	Mafungu	Mkaguliwa	Kiasi(Sh.)	Uhalisi wa matumizi
1	89	Sekretarieti ya Mkoa wa Rukwa	10,359,430.00	Matumizi ya ziada yasiyo muhimu kutokana na kununua mashine mbovu ya kufulia nguo
2	71	Sekretarieti ya Mkoa wa Pwani	657,949,308.53	Tozo, adhabu na riba zitokanazo na kushindwa kuzingatia matakwa ya mikataba
3	52	Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto	5,455,521.00	Ikiwa ni 50% ya riba kwa menejimenti kushindwa kupeleka makato kwa wakati kwenda PSPF
Jumla			668,764,264.53	

Chanzo: Barua za mapungufu kwa mwaka wa fedha 2017/2018

Nimebaini kuwa matumizi yasiyo na tija yameongezeka kutoka Sh. milioni 61 mpaka Sh. 668, 764,264.53 kutoka mwaka 2016/17 hadi 2017/18 kwa mtawalia. Idadi ya taasisi zilizohusika zimebaki zilezile tatu.

Kielelezo Na. 6: matumizi yasiyo na tija kwa miaka miwili



Maoni yangu ni kwamba, matumizi haya yasiyo na tija yangeweza kuepukika, na kiasi hicho cha fedha kutumika katika shughuli nyingine muhimu kwa kutumia vizuri fedha za walipa kodi.

Hivyo, nawashauri Maafisa Masuuli husika kutumia vizuri sana fedha za umma katika kufanya malipo ndani ya muda unaotakiwa; na kuepuka adhabu zisizo za lazima na matumizi mengine yasiyo na tija.

10.16 Malipo yaliyofanywa bila kuidhinishwa Sh. 193,182,333.28

Ukaguzi wangu wa mwaka wa fedha 2017/18 umebaini kuwa taasisi 6 zilifanya malipo ya Sh. 193,182,333.28 ambayo nyaraka zake za malipo hazikuidhinishwa kabla ya malipo. Hii ni kinyume na kanuni ya 88(1) ya Kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2001 inayotaka Afisa Masuuli au mtu yeyote kusaini/kuidhinisha hati za malipo kabla ya kufanya malipo. Malipo ambayo hayajaidhinishwa yameorodheshwa kwenye Jedwali Na. 80 hapo chini.

Jedwali Na. 80: Malipo yaliyofanyika bila kuidhinishwa

Na	Mafungu	Mkaguliwa	Kiasit(Sh.)
1	89	Sekretarieti ya Mkoa wa Rukwa	89,240,219
2	41	Wizara ya Katiba na Mambo ya Sheria	34,000,000
3	74	Sekretarieti ya Mkoa wa Kigoma (Hospitali ya Rufaa Maweni)	11,472,320
4	80	Sekretarieti ya Mkoa wa Mtwara	1,400,000
5	70	Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha	51,919,753
6	2	Tume ya Huduma za Waalimu	5,150,041
Jumla			193,182,333

Chanzo: Barua za mapungufu kwa mwaka 2017/2018

Ni maoni yangu kuwa, malipo ambayo hayajaidhinishwa yanaweza kusababisha matumizi mabaya ya fedha. Aidha, Wafanyakazi wasio waaminifu wanaweza kutumia mianya hii kufanya malipo hewa bila menejimenti kugundua.

Nawashauri Maafisa Masuuli wanaohusika kuhakikisha malipo yote yanaidhinishwa ipasavyo katika ngazi zote ili kupunguza viatarishi vinavyohusiana na mifumo dhaifu ya uhibitwa wa ndani

10.17 Malipo yasiyostahili kutoka kwenye akaunti za amana Sh. 192,582,796.42

Kanuni ya 132 ya kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2001 inasisitiza fedha zilizo kwenye amana kutumika kulingana na malengo ya kuweka fedha hiyo kama inavyoelezwa na kumtaka Ofisa muidhinishaji kujiridhisha kama malengo ya amana hiyo yametimizwa Ofisa huyo atapaswa kujiridhisha mwenyewe marejeo ya nyaraka halisi zilizotolewa, kwamba mtu anayedai amana ni mhusika halisi au vinginevyo anastahili kurejeshewa. Kinyume chake Sh. 192,582,796.42 zililipwa kutoka kwenye akaunti za Amana kwa ajili ya shughuli ambazo hazina uhusiano na malengo yaliyowekwa kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali Na. 81 hapo chini.

Jedwali Na. 81: Malipo yasiyostaki kutoka kwenye akaunti za amana

Na	Fungu	Mkaguliwa	Kiasi(Sh.)
1	82	Sekretarieti ya Mkoa wa Ruvuma	14,937,160
2	63	Sekretarieti ya Mkoa wa Geita	7,467,300
3	87	Sekretarieti ya Mkoa wa Kagera	35,872,189
4	77	Sekretarieti ya Mkoa wa Mara	36,118,000
5	80	Sekretarieti ya Mkoa wa Mtwara	87,877,622
6	71	Sekretarieti ya Mkoa wa Pwani	10,310,525
Jumla			192,582,796

Chanzo: Barua za mapungufu kwa mwaka 2017/2018

Ni mtazamo wangu kuwa, usimamizi duni wa amana husababisha kuwa na matumizi mabaya ya fasha taslimu kinyume na malengo yaliyowekwa.

Menejimenti na Maafisa Masuuli husika wanapaswa kuweka jitihada zaidi katika kuanzisha mifumo imara ya udhibiti wa ndani.

10.18 Bakaa ya fedha za amana ambazo hazijatumika kwa muda mrefu Sh. 2,532,574,210.92

Kanuni ya 133(1) ya Kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2001 inataka 'Bakaa ya amana yoyote iliyobaki muda mrefu bila kudaiwa kwa miaka mitano inaweza, kwa kibali cha Mhasibu Mkuu wa Serikali, kulipwa kwenye akaunti ya mapato; na Mhasibu Mkuu wa Serikali anaweza kurejesha fedha ya amana kwa mtu yoyote anayestahili kama amejiridhisha kwamba madai ni sahihi. Nimebaini kuwa, Taasisi 5 zimebakiza bakaa za amana bila kuomba kibali ili kutumia bakaa hiyo kwenye kazi nyingine muhimu kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali Na. 82 hapo chini:

Jedwali Na. 82: Bakaa la Amana ambayo hazijatumika muda mrefu

Na	Mafungu	Maelezo	Kiasi(Sh.)
1	53	Ofisi ya Huduma ya Mashtaka ya Umma	447,825,930.31
2	2018	Ubalozi wa Tanzania, Washington, D.C	231,781,467.00
3	50	Wizara ya Fedha na Mipango	203,423,657.91
4	43	Wizara ya Kilimo	95,698,152.25
5	2002	Ubalozi wa Tanzania- Bertini	1,553,845,003.45
Jumla			2,532,574,210.92

Chanzo: Barua za mapungufu kwa mwaka wa fedha 2017/2018

Ni maoni yangu kuwa malengo yaliyokusudiwa yamekamiliwa. Hivyo, fedha za amana zinapaswa kuhamishiwa kwenye akaunti ya mapato au kutumika kwa shughuli nyingine baada ya kuomba kibali kutoka kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali; vinginevyo, bakaa iliyopo inaweza kutumiwa vibaya kwa siku za usoni.

Napendekeza kwamba, Menejimenti za taasisi husika kutumia bakaa za amana zilizokaa muda mrefu kwenye akaunti za amana au kuzihawilishia kwenye akaunti ya mapato kulingana na Kanuni ya 133 (1) ya kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2001.

10.19 Hasara ya fedha za umma kutokana na makosa ya kujaza madai ya NHIF Sh. 291,933,248

Mapitio yangu ya madai ya kurejeshewa fedha kutoka NHIF nimebaini kuwa Sekretarieti za Mkoa zimepata hasara inayofikia Sh. 291,933,248 kutokana na dosari katika kujaza madai, hivyo kukinzana na kifungu cha 27(2) ya Sheria ya NHIF ya mwaka 1999. Zifuatazo ni Sekretarieti za Mkoa zinazohusika kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali Na. 83 hapo chini.


Jedwali Na. 83: Orodha ya Taasisi zenye madai yaliyokataliwa

Na	Mafungu	Mkaguliwa	Kiasi(Sh.)
1	77	Sekretarieti ya Mkoa wa Mara	16,014,180
2	81	Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza	49,029,655
3	86	Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga	119,159,625
4	82	Sekretarieti ya Mkoa wa Ruvuma	41,091,435
5	75	Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro (Hospitali ya Rufaa Mawenzi)	33,637,340
6	95	Sekretarieti ya Mkoa wa Manyara	9,850,218
7	85	Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora	23,150,795
Jumla			291,933,248

Chanzo: Barua za mapungufu kwa mwaka wa fedha 2017/18

Kwa ulinganisho, Nimebaini kuwa hasara zilizotokana na kukataliwa kwa madai imepungua kutoka Sh. milioni 343 hadi Sh. milioni 292 katika mwaka 2016/17 hadi 2017/18, mtawalia, kama ilivyooneshwa katika chati hapo chini. Taasisi zilizotumika zimepungua kidogo kutoka 9 hadi 7

Kielelezo Na. 7: mwenendo wa hasasa kutokana na kukataliwa kwa marejesho ya fedha kutoka NHIF



Ni maoni yangu kuwa, kama menejimenti za Sekretariati za Mikoa husika na Hospitali hazitafanya usimamizi na kuhakikisha kwamba fomu za madai zinajazwa vizuri na kwa uwajibikaji zinaweza kuathiri utoaji wa huduma kwa gharama ya madai yaliyokataliwa. Madhara ya kutojaza vizuri fomu za madai ya NHIF yamepelekea kukataliwa kwa madai yanayofikia Sh. milioni 292 ikiashiria kuwa taasisi zilizohojiwa zimepata hasara kwa kiwango sawa na madai yaliyokataliwa.

Nashauri menejimenti ya NHIF kuwa inatoa mafunzo ya mara kwa mara; na pale itakapowezekana, kila Hospitali ya Rufaa ipangiwe Afisa atakayewajibika ili kurahisisha zoezi la kujaza fomu.

10.20 Malipo yaliyozidishwa kiasi kinachotakiwa Sh. 133,528,196.68

Kanuni ya 87 ya Kanuni za Fedha za Umma ya 2001 inataka Afisa anayesaini nyaraka za malipo kuthibitisha usahihi wa kila maelezo ya malipo; kinyume chake, nimebaini kuwa taasisi 6 zililipa Sh. 133,528,196.68 kununua bidhaa na huduma kwa kulipa zaidi ya kiasi kilichokuwa kinatakiwa. Kitendo hiki kinaonesha upotoshaji wa taarifa za fedha kwenye taasisi husika. Masuala haya yalijadiliwa kwa

kila Mkaguliwa, ambapo Maafisa Masuuli waliahaidi kudai hela iliyolipwa zaidi kama ilivyooneshwa katika Jedwali Na. 84 hapo chini.


Jedwali Na. 84: Matumizi yaliyolipwa zaidi

Na	Fungu	Mkaguiwa	Kiasi(Sh.)
1	73	Sekretarieti ya Mkoa wa Iringa (Hospitali ya Mkoa wa Iringa)	25,636,500.00
2	2040	Ubalozi wa Tanzania- Tel Aviv, Israel	14,093,750.00
3	88	Sekretarieti ya Mkoa wa Dar es Salaam	16,874,258.68
4	56	Ofisi ya Rais, Tawala za mikoa na Serikali za mitaa	19,717,800.00
5	70	Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha	4,485,888.00
6	02	Tume ya Huduma za waalimu	52,720,000.00
Total			133,528,196.68

Chanzo: Barua za Mapungufu kwa mwaka wa fedha 2017/2018

Kwa kulinganisha na ripoti yangu iliyotangulia mwaka 2016/17 kiasi kilichohojiwa kimepungua kutoka Sh. 306 milioni hadi Sh. milioni 133. Vilevile, idadi ya taasisi ambazo hazikuzingatia kanuni ya 87 imebaki ileile ya taasisi 6. Kwa miaka 5 mwenendo unaashiria kuwa kuna maboresho kidogo kwenye usimamizi wa matumizi kama ilivyooneshwa kwenye chati hapo chini.

Kielelezo Na. 8: linganisho la malipo yaliyozidishwa kwa miaka 5 mfululizo



Kwa mtazamo wangu, kiasi kilicholipwa kilisababishwa na udhibiti hafifu wa ndani katika mchakato wa malipo ambao labda ungesababisha nyaraka za malipo kuandaliwa kwa kutumia hati

zilezile za madai na hati nyingine za madai kulipwa zaidi ya kiasi kilichokuwa kinatakiwa. Hivyo, nashauri yafuatayo:

- a) *Menejimenti za taasisi husika kuimarisha udhibiti wa ndani wa mifumo ya kuchakata malipo*
- b) *Kiasi kilicholipwa mara mbili na kilicholipwa zaidi kinapaswa kurejeshwa na kufanya usuluhishi ili kurekebisha malipo yaliyozidishwa.*

10.21 Hitimisho

Katika kupitia udhaifu uliyooneshwa hapo juu, nahitimisha kuwa, udhaifu na dosari vinaweza kuondolewa au kuwa katika kiwango kinachostahimilika kama tu ufanisi wa udhibiti wa ndani utasisitizwa kwa umakini, vihatarishi vinatathminiwa ipasavyo na Sheria husika zinazingatiwa kikamilifu.

Sura ya Kumi na Moja

Ukaguzi wa Mali na Madeni ya Wazabuni na Watumishi

11.1 Utangulizi

Sehemu hii ya ripoti inatarajia kuonyesha muhtasari wa matokeo muhimu ya ukaguzi na mapendekezo husika kutokana na ukaguzi wa usimamizi mali na madeni kwa mwaka 2017/18.

11.2 Usimamizi wa Mali za Kudumu

Mali za Kudumu zinachangia sehemu kubwa kwenye Mali za Serikali. Kwa hivyo, kuna haja ya kuhakikisha kunakuwa na ufanisi katika usimamizi wake.

Wizara ya Fedha imeweka miongozo mbalimbali inayoelekeza na kuweka mahitaji maalum kwa kuzingatia matakwa ya kitaaluma ili kuwe na ufanisi katika usimamizi na udhibiti wa Mali za Umma.

Mapitio yangu yalibaini maeneo kadhaa ambayo yanatakiwa kuimarishwa katika usimamizi wa Mali za Kudumu za Umma. Maeneo hayo ni:

11.2.1 Majengo yaliyotelekezwa, Ujenzi usiokamilishwa na Viwanja visivyoendelezwa

Nilibaini kuwa Serikali ina majengo yaliyotelekezwa, viwanja ambavyo hajijaendelezwa kwa kipindi kirefu, ujenzi wa majengo kwa kipindi kirefu bila kukamilishwa na kutorekebishwa kwa mapungufu yaliyojitokeza katika kipindi cha matazamio. Nilibaini Taasisi saba (7) zimetelekeza majengo na mengine ujenzi umesitishwa; saba (7) zina majengo yanayojengwa pole pole sana na Ofisi za balozi tatu (3) zina viwanja ambavyo havijaendelezwa kwa muda mrefu kama zilivyoainishwa kwenye Tazama Kiambatisho Na. 57

Miradi ya ujenzi isiyokamilishwa katika kipindi kilichopangwa inakuwa na athari nyingi, zikijumuisha kuongezeka kwa gharama za ujenzi, ucheleweshwaji wa huduma, mazingira hatarishi ya kufanya kazi na utolewaji wa huduma hafifu.

11.2.2 Kuwapo kwa Rejista ya Mali za Kudumu Isiyo Timilifu

Katika sampuli ya Taasisi 28 mapitio ya Ukaguzi wa Rejista za Mali za Kudumu nilibainisha mapungufu yafuatayo; mali zisizo na nambari za utambulisho, kukosekana kwa tarehe ya manunuzi, aina ya mali, muda wa matumizi ya mali, uchakavu uliotolewa kwa mwaka ukilinganishwa na taarifa ya uchakavu wa Mali kwa miaka ya nyuma. Njia ya uchakavu na kiwango cha kutumia, Thamani halisi ya Mali, Uhamisho wa Mali, kuuzwa kwa Mali na kuziondoa Mali, hayo yote hayakuonyeshwa kwa Rejista ya Mali, kinyume na sehemu ya 5.2 ya muongozo wa Mali za Kudumu za Serikali 2012. Taasisi zilizobainika na mapungufu hayo zimeonyeshwa katika Kiambatisho Na. 58.

Kazi muhimu ya usimamizi ni kuhakikisha mali za Taasisi zinalindwa kutokana na tishio lolote ambalo linaweza kuzuia Taasisi husika kufikia malengo yake.

Kazi hii muhimu haiwezi kufikiwa ikiwa hakuna mfumo mzuri ulioanzishwa wa kusimamia Mali.

Ninashauri Taasisi husika kurekebisha taarifa kwenye Regista ya Mali kwa wakati ili kuwe kwa mfumo sahihi wa kufuatilia mali ili kutoa repoti sahihi ya Mali za Taasisi.

Regista ya Mali za Kudumu yenye taarifa sahihi inatumika kama kidhibitisho cha ukaguzi ili kutoa maoni juu ya usahihi wa taarifa za Fedha.

11.2.3 Magari ambayo hayatumiki kwa muda mrefu bila kufanyiwa matengenezo au kuuzwa

Kufuatia ukaguzi wa Mali za Kudumu uliofanyika kwenye Taasisi ikijumlisha Ofisi za Ubalozi Nje ya Nchi, nilibaini magari 264 na Mali zingine zipatazo 66 ambapo taratibu za kuziondosha kwa mujibu wa Kanuni Na.254 (1) ya Kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2001 haikufuatwa. Magari pamoja na Mali zingine vinachukua nafasi katika majengo ya Taasisi husika kwa muda mrefu pia vinaendelea kuharibika zaidi. Kwa taarifa Zaidi tazama Kiambatisho Na. 59

Usimamizi wa hali ya Magari na Mali zingine za Serikali yanaangaliwa na watumiaji pale tu ubovu unapojitokeza. Hata hivyo hakuna

taratibu zilizowekwa za kuhakikisha kunakuwapo na uchunguzi wa hali za magari na mali nyingine mara moja kwa mwaka na hakuna taratibu ya kuwa na kumbukumbu juu ya taarifa za uchunguzi wa kila gari au mali nyingine.

Hali hii si kuwa tu inaongeza gharama za uendeshaji kwa Taasisi, bali pia inapelekea kutoa taarifa ya thamani za Mali za Kudumu isiyosahihi.

Naishauri Serikali kuanzisha taratibu za uchunguzi wa hali za Magari na Mali nyingine mara moja kwa mwaka; na kuwa na utaratibu wa kuweka kumbukumbu kuhusu taarifa za uchunguzi wa kila gari au mali nyingine kwenye Regista. Hii itasaidia Afisa masuuli kufanya maamuzi juu ya kuondoa kwenye matumizi Magari na Vifaa chakavu kwa wakati.

11.2.4 Ukosefu wa Nyaraka za Umiliki wa Ardhi na Majengo ya Umma

Barua yenye kumbukumbu Na.CAB142/626/01/A/42 kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi ya tarehe 26/09/2014 na barua kumbukumbu Na.CNA.32/572/01/96 kutoka kwa Msajili wa Hazina ilielekeza kwa Taasisi zote za Umma zinafuatilia nyaraka za umiliki wa Ardhi wanazomiliki.

Ardhi na Majengo yanayomilikiwa na Wizara na Sekretarieti za Mikoa hadi sasa hazina nyaraka za umiliki licha ya mapendekezo yangu ya awali. Jedwali Na. 85 linaonyesha orodha ya Taasisi ambazo hazijapata Hatimiliki kutoka kwa Mamlaka husika za Serikali.

Jedwali Na. 85: Ukosefu wa Nyaraka za Umiliki wa Ardhi na Majengo ya Umma

Na.	Fungu	Jina la Taasisi
1	46	Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi
2	41	Wizara ya Katiba na Sheria
3	78	Sekretarieti ya Mkoa wa Mbeya
4	52	Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto
5	50	Wizara ya Fedha na Mipango

Chanzo: Taarifa za Mapungufu Kwa Menejimenti za Taasisi Husika kwa Mwaka 2017/18

Hatimiliki inampa mmiliki uhalali kisheria kumiliki ardhi, bila hatimiliki Taasisi zinaweza kukosa haki pale inapotokea mgogoro wa mipaka ukizingatia kuwa Hati ndiyo inayothibitisha kisheria uhalali wa kumiliki ardhi.

Ninashauri Mkurugenzi wa Usimamizi ya Mali za Umma chini ya Wizara ya Fedha na Mipango afuatilie Taasisi husika na kuhakikisha nyaraka za umiliki zinapatikana kwa kufanya ufuatiliaji wa karibu kwa mamlaka zinazohusika.

11.2.5 Ukosefu wa Mpango wa Matengenezo na Kumbukumbu za Matengenezo ya Mali za Kudumu

Kanuni Na.254 (1) ya kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2001 (rejeo 2004) inahitaji kuwa, pamoja na matengenezo ya magari na mitambo, kuwe na taarifa za kila gari au mtambo kuhusu historia, utendaji, matengenezo pia kufanya ulinganifu kati ya utendaji wake na gharama zinazotumika kuitunza.

Ukaguzi umebaini Taasisi 13 ambazo hazikutengeneza Mpango wa matengenezo ya Mali za Kudumu wala kuandaa Taarifa za matengenezo yake kinyume na Kanuni Na.254 (1) ya Kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2001 (rejeo 2004) pamoja na Aya ya 11 ya muongozo wa Mali za Kudumu wa 2012.

Orodha ya Taasisi ambazo zimepatikana na mapungufu zimeonyeshwa katika Jedwali Na. 86 hapo chini:

Jedwali Na. 86: Taasisi ambazo hazina Mpango wa Matengenezo na Kumbukumbu za Matengenezo ya Mali za Kudumu

Na	Fungu	Jina la Taasisi
1	68	Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia
2	31	Ofisi ya Makamu wa Rais
3	90	Sekretarieti ya Mkoa wa Songwe
4	34	Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki
5	46	Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi
6	40	Mahakama
7	85	Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora
8	71	Sekretarieti ya Mkoa wa Pwani
9	2041	Ubalozi wa Tanzania -Doha
10	48	Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi
11	2019	Ubalozi wa Tanzania -Brussels

Na	Fungu	Jina la Taasisi
12	2020	Ubalazi wa Tanzania-Umoja wa Mataifa, Geneva
13	69	Wizara ya Maliasili na Utalii

Chanzo: Taarifa za Mapungufu Kwa Menejimenti za Taasisi Husika kwa Mwaka 2017/18

Nashauri Wizara, Ofisi za Ubalazi na Sekiretarieti za Mikoa kuweka taratibu za kuweka kumbukumbu za matengenezo na kuandaa mpango wa matengenezo wa Mali za Kudumu kila mwaka.

11.2.6 Kushindwa kufanya mapitio ya thamani na muda uliobaki wa matumizi ya Mali za Kudumu

Mwongozo wa kusimamia Mali za Kudumu za Serikali Na. 6(3) uliotolewa na Mlipaji Mkuu tarehe 10 Desemba, 2012 ulielekeza, “kama thamani ya Mali za Kudumu imekuwa sifuri kwenye vitabu na bado inaendelea kutumika, hiyo inamaanisha muda wa matumizi uliokadiriwa mwanzoni haukuwa sahihi. Hivyo muda wa matumizi ya Mali za Kudumu lazima urekebishwe”.

Aya ya 67 ya Viwango vya Kimataifa vya kuandaa Taarifa za Fedha za Umma (IPSAS 17) inahitaji Taasisi kupitia angalau mara moja kwa mwaka muda uliobaki kutumika Mali za Kudumu ikilinganishwa na thamani yake iliyobaki.

Ukaguzi umebaini Taasisi ishirini na mbili (22), zikiwamo Wizara nne (4) na Balazi kumi na nane (18) zilishindwa kukagua thamani ya muda wa Mali za Kudumu ikilinganishwa na thamani yake iliyobaki, na kupelekea Taasisi kuwa na Mali za Kudumu ambazo bado zinatumiwa lakini zimeripotiwa zikiwa na thamani sifuri.

Orodha ya Taasisi ambazo zimepatikana na mapungufu zimeonyeshwa kwenye Jedwali hapo chini:

Jedwali Na. 87: Taasisi ambazo zimeshindwa kufanya mapitio ya thamani na muda uliobaki wa matumizi ya Mali za Kudumu

Na	Fungu	Jina la Taasisi
1	34	Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki
2	43	Wizara ya Kilimo
3	46	Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi
4	52	Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto
5	2002	Ubalazi wa Tanzania -Berlin

Na	Fungu	Jina la Taasisi
6	2006	Ubalozi wa Tanzania- London
7	2007	Ubalozi wa Tanzania - Lusaka
8	2008	Ubalozi wa Tanzania -Maputo
9	2009	Ubalozi wa Tanzania -Moscow
10	2010	Ubalozi wa Tanzania- New Delhi,India
11	2016	Ubalozi wa Tanzania -Stockholm
12	2019	Ubalozi wa Tanzania -Brussels
13	2022	Ubalozi wa Tanzania -Harare,Zimbabwe
14	2031	Ubalozi wa Tanzania -Brasilia
15	2023	Ubalozi wa Tanzania- Nairobi
16	2024	Ubalozi wa Tanzania- Riyadh,
17	2025	Ubalozi wa Tanzania -Pretoria
18	2029	Ubalozi wa Tanzania -Muscat
19	2030	Ubalozi wa Tanzania -Lilongwe
20	2032	Ubalozi wa Tanzania -Kuala Lumpur
21	2028	Ubalozi wa Tanzania -Bujumbura
22	2026	Ubalozi wa Tanzania - Kigali

Chanzo: Taarifa za Mapungufu Kwa Menejimenti zaTaasisi Husika kwa Mwaka 2017/18

Kushindwa kufanya tathmini ya thamani na muda wa matumizi ya Mali za Kudumu angalau mara moja kwa mwaka ni kutozingatia matakwa ya Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa hesabu katika Sekta za Umma (IPSAS 17).Hali hii husababisha taarifa za fedha kuwa na mapungufu.

Wizara na Ofisi za Ubalozi zinatakiwa kufuata matakwa ya Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa hesabu katika Sekta za Umma (IPSAS 17) na mwongozo wa Mali za Kudumu Na.6 (3) katika kuandaa taarifa za fedha.

11.2.7 Mapungufu yaliyoonekana katika usimamizi wa Mali zilizotaifishwa

Mali kutaifishwa ni kitendo cha mali kuwa chini ya umiliki wa Umma kutokana na uhalifu.

Kusudi la kutaifisha mali ni kuvuruga shughuli za uhalifu kwa kuchukua mali ambazo zinaweza kuwa na manufaa kwa mtu binafsi au shirika kulingana na Sheria ya Uhalifu (Cap 256 R.E.2002)

Nilibaini mapungufu mbalimbali katika usimamizi wa Mali za Kudumu zilizotaifishwa katika sampuli ya Mikoa iliyotembelewa, mapungufu hayo yanahitaji kurekebisha ili kukabiliana na vihatarishi vinavyohusiana na Mali za Kudumu zilizotaifishwa ili kuwe na usimamizi mzuri. Mapungufu yameainishwa kwenye Jedwali Na. 88 hapo chini.

Jedwali Na. 88: Taasisi zilizoonekana na mapungufu katika usimamizi wa Mali zilizotaifishwa

Na.	Mkoa	Mapungufu
1.	Mbeya, Lindi, Mtwara, Mwanza, Bukoba, Arusha, Manyara, Dodoma, Morogoro, Mara, Kilimanjaro, Tanga, Ruvuma na Shinyanga,	Mali zilizotaifishwa kutokusajiliwa kama Mali za Umma
2.	Arusha, Mbeya, Morogoro, Dar es salaam, Shinyanga, Tanga, Mtwara, Lindi, Dodoma na Bukoba.	Mali zilizotaifishwa kutohaminishwa ili kujua thamani yake
3.	Mbeya, Lindi, Mtwara, Mwanza, Bukoba, Arusha, Manyara, Dodoma, Morogoro, Mara, Kilimanjaro, Tanga, Ruvuma na Shinyanga	Mali zilizokamatwa na kuachwa muda mrefu bila kutunzwa
4.	Tanga, Arusha Kilimanjaro, Manyara na Ruvuma	Uchelewashwaji taratibu za ukamilishaji wa kutaifisha Mali kutokana na kukosekana kwa Hati ya kutaifisha Mali.
5.	Manyara na Mtwara	Mali zilizotaifishwa na zilizoorozeshwa kutoonekana wakati wa uhakiki.
6.	Morogoro na Mbeya	Kutokuwa na taarifa muhimu kwenye rejista ya Mali zilizotaifishwa
7.	Lindi , Mtwara, Mwanza, Bukoba, Arusha, Manyara, Dodoma, Mara, Kilimanjaro, Tanga , Ruvuma na Shinyanga	Kutokuwa na rejista ya Mali zilizotaifishwa

Chanzo: Taarifa za Mapungufu Kwa Menejimenti za Taasisi Husika kwa Mwaka 2017/18

Serikali inashauriwa kuanzisha taratibu za udhibiti kuhakikisha mashauri ya kutaifisha Mali yanafanywa kwa wakati na kwa utaratibu unaofanana ili kuwe na usimamizi mzuri.

Vilevile, Msajili wa Hazina anashauriwa kuhakikisha Taasisi zinazohusika wanaweka kumbukumbu sahihi za mali zilizotaifishwa

kwa ukamilifu na kwa wakati ili kukidhi matakwa ya sheria zilizopo na kuwa na utunzaji endelevu wa Mali zilizotaifishwa.

11.2.8 Mapato ambayo hayajapokelewa Sh. 222,695,169,207.36


Mapato ambayo hayajapokelewa yanahitaji usimamizi mzuri ili kupunguza vihatarishi kama ubadhirifu, makosa na hasara. Makusudi ya kuwa na usimamizi mzuri wa ndani ni kuhakikisha ufanisi katika usimamizi wa makusanyo ya mapato ambayo hayajakusanywa.

Hadi kufikia 30 Juni, 2018 jumla ya Taasisi ishirini na nane (28) zilionekana kuwa na mapato ambayo hayajapokelewa kiasi cha Sh.222,695,169,207.36 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2016/2017, kuna ongezeko la mapato ambayo hayajapokelewa kiasi cha Sh.28,485,427,666.62

Taasisi ambazo zilionekana na mapato ambayo hayajapokelewa zimeonyeshwa kwenye Kiambatisho Na. 60

Nimebaini kuwa asilimia 59 ya mapato ambayo hayajapokelewa katika yapo Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Fungu 98, ikifuatiwa na Wizara ya Madini na Nishati yenye asilimia 20 kama inavyooneshwa kwenye kielelezo hapa chini

Kielelezo Na. 9:



Kwa maoni yangu, kutokukusanywa kwa mapato haya kunaleta athari katika kuihudumia jamii. Sio kwamba hupunguza tu uwezo wa kutoa huduma, bali pia huongeza madeni yasiyolipwa na kuwa mzigo kwa Taasisi husika.

Nashauri Wizara na Menegimenti za Sekretariati za Mikoa kuanzisha mkakati wa kuhakikisha mapato ambayo hayapokelewa kwa wakati yanakusanywa. Maafisa Masuuli wanaohusika wanashauriwa kuwa na mfumo dhabiti wa ndani wa kukusanya mapato yasiyopokelewa.

11.3 simamizi wa Madeni

Usimamizi imara wa madeni ni eneo muhimu katika kusimamia madeni ya Nchi. Katika mwaka huu wa fedha, nilibaini mapungufu yafuatayo kwenye kaguzi za Taasisi.

11.3.1 Madeni tarajiwa (Kesi ambazo hazijafanyiwa maamuzi)

Madeni tarajiwa ni moja ya vyanzo vikuu vya vihatarishi vya kifedha kutokana na matarajio ya wajibu wa kulipa utakaotokana na matokeo tarajiwa. Usimamizi wa madeni kwa ufanisi ni muhimu katika kuhakikisha uthibiti wa fedha za Umma.

Kuna viashiria vya hatari katika kuongezeka kwa madeni tarajiwa kwenye Wizara na Idara. Taasisi hazitengi bajeti kwa ajili ya madeni tarajiwa, ikiwa inatokea madeni tarajiwa yanakuwa madeni itabidi yalipwe kutoka kwenye bajeti ya Taasisi badala ya kutoa huduma na pia kuifanya Taasisi isiwe na uwezo wa kifedha.

Nimebaini Taasisi kumi na moja (11) ambazo zina madeni tarajiwa yanayofikia kiasi cha Sh. billioni 52.6 zikisubiria maamuzi ya mahakama dhidi ya Makampuni na Watu binafsi.

Taasisi zenye kesi za madeni tarajiwa zimeodhoreshwa kwenye Jedwali 8 hapo chini.

Jedwali Na. 89: Taasisi zenye madeni tarajiwa

Na	Fungu	Jina la Taasisi	Kiasi (Sh.)
1	37	Ofisi ya Waziri Mkuu	6,846,922,629.49
2	43	Wizara ya Kilimo	5,675,170,155.00
3	46	Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi	572,677,709.00

Na	Fungu	Jina la Taasisi	Kiasi (Sh.)
4	49	Wizara ya Maji na Umwagiliaji	3,510,957,248.70
5	52	Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto	2,696,360,000.00
6	57	Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa	3,486,904,375.50
7	64	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi	42,000,000.00
8	65	Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu	21,890,260.00
9	69	Wizara ya Maliasili na Utalii	23,399,564,809.00
10	96	Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo	525,351,200.00
11	98	Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano	5,853,828,010.00
Jumla			52,631,626,396.69

Kiasi kikubwa cha madeni tarajiwa kipo katika Wizara ya Maliasili na Utalii kikiwa ni Sh.23,399,564,809.00 sawa na asilimia 44 ya kiasi chote cha madeni tarajiwa. Ya pili ni Ofisi ya Waziri Mkuu, kiasi cha Sh.6,846,922,629.49 sawa na asilimia 13. Ikifuatiwa na Wizara ya Kilimo yenye madeni tarajiwa Sh.5,675,170,155 sawa na asilimia 11 ya madeni tarajiwa yote.

Kuna hatari ya kuingia katika matumizi yasiyo na manufaa kwa Wizara kutokana na faini au adhabu ambayo inaweza kuamriwa na Mahakama kama Wizara zitashindwa kesi hizi.

Kama nilivyopendekeza katika taarifa zangu zilizopita, naendelea kupendekeza Serikali ihamasishe kila taasisi ya serikali iwe na mikakati thabiti ya usimamizi wa madeni kulingana na mazingira yao kwa ajili ya kuhakikisha hatari zilizopo katika Taasisi zao zinasimamiwa na kupunguzwa mpaka kufikia kiwango cha kudhibitiwa.


11.3.2 Matumizi ambayo hayajalipwa Sh.3,109,419,395,085.00

Matumizi ambayo hayajalipwa ni gharama ya huduma mbalimbali ambazo Taasisi ilizipata lakini haikuzilipia katika kipindi cha mwaka wa Fedha husika.

Mpaka kufikia tarehe 30 Juni 2018 jumla ya Taasisi 92 zilikuwa na madeni kiasi cha Sh.3,109,419,395,085.00 ikilinganishwa na mwaka uliopita uliokuwa na madeni yaliyofikia Sh.2,658,415,707,437.81 kuna ongezeko kubwa la madeni la kiasi cha Sh.451,003,687,647.19 sawa na ongezeko la asilimia 16.


Mwenendo wa madeni kwa kipindi cha miaka minne yameonyeshwa katika kielelezo hapo chini:

Kielelezo Na. 10: Matumizi ambayo hayajalipwa kwa kipindi cha miaka minne



Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Fungu Na 57 ina asilimia 33, sawa na Sh.1,037,443,513,359; Ya pili ni Jeshi la Polisi Fungu Na 28 lina asilimia 24, sawa na Sh.752,922,769,459 ikifuatiwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania Fungu 38 lina asilimia 10 sawa na Sh. 300,802,361,005 ya jumla yote ya matumizi ambayo hayajalipwa kama zilivyoonyeshwa katika kielelezo hapo chini:

Kielelezo Na. 11: Taasisi ambazo zina matumizi ambayo hayajalipwa



Chanzo: Taarifa za Mapungufu Kwa Menejimenti za Taasisi Husika kwa Mwaka 2017/18

Matumizi ambayo hayajalipwa yanajumuisha matumizi ya Wizara ya Afya ya gharama za matibabu ya wagonjwa waliotibiwa katika Hospitali za rufaa nchini India. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2018 gharama za hospitali zilikuwa kiasi cha Sh.29,172,371,931.26 ukilinganisha na mwaka wa fedha uliopita gharama zilikuwa kiasi cha Sh.28,609,803,615.40 kuna ongezeko la kiasi cha Sh.562,568,315.80, sawa na asilimia mbili (2) kama ilivyoonyeshwa kwenye Jedwali Na. 90 hapo chini;

Jedwali Na. 90: Mtiririko wa deni la Hospitali za India

Maelezo	Kiasi (Sh)
Kiasi cha mwanzo cha Madai 01/07/2017	28,609,803,615.40
Madai yaliyopokelewa 2017/18	20,920,066,404.80
Jumla Madai	49,529,870,020.20
Kutoa- Malipo yaliyofanyika 2017/18	20,357,498,089.00
Madai ambayo hayajalipwa 30/06/2018	29,172,371,931.20

Chanzo: Taarifa ya Ukaguzi wa 2016/17 na 2017/18

Napongeza juhudi za Serikali kwa kulipa deni kiasi cha Sh. 20,357,498,089 kwa hospitali za India, ikiwa ni asilimia 41 kwenye kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018. Hospitali zenye madeni zimeonyeshwa kwenye Jedwali Na. 91 hapa chini.

Jedwali Na. 91: Madeni ya Hospital za India

Na.	Jina la Hospital	Madai (Sh)
1	Apollo Bangalore	778,255,768.28

Na.	Jina la Hospital	Madai (Sh)
2	Apollo Chennai	6,109,299,977.04
3	Apollo Hyderabad	8,423,732,616.20
4	Apollo Delhi	9,954,451,448.29
5	Apollo Ahmedabad	2,327,339,250.49
6	Madras Medical Mission	1,579,292,870.96
Jumla		29,172,371,931.26

Chanzo: Taarifa za Wizara ya Afya za Madeni ya Hospitali za India

Orodha ya taasisi zenye matumizi ambayo hayajalipwa kwa muda mrefu zimeonyeshwa kwenye Kiambatisho Na. 61

Pamoja na juhudi kubwa za Serikali kulipa madeni hayo ya muda mrefu, madeni katika Taasisi za Serikali kwa mwaka 2017/2018 yamezidi kuongezeka kwa kiasi cha Sh.451,003,687,647.19 kulinganisha na mwaka uliopita.

Napendekeza yafuatayo kwa Serikali:

- a) Matumizi ambayo hayajalipwa yaingizwe kwenye mfumo (Epicor) pale yanapotokea. Ili kufanikisha hili, nashauri Wizara ya Fedha pamoja na Mzabuni wa Mfumo (SOFTECH) kuutengeneza Mfumo (Epicor) ili Taasisi ziweze kuingiza kwenye mfumo matumizi yasiyolipwa pale yanapotokea ili kuyadhibiti kulingana na Bajeti. Pia, kukidhi viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu katika Sekta za Umma (IPSAS Accrual).
- b) Kuingiza madeni yote ya miaka ya nyuma kwenye makisio ya miaka ijayo ili yaweze kulipwa na kuondoa migogoro ya Wazabuni na wadau wengine.
- c) Kutoa fedha kwa mujibu wa makisio yaliyoidhinishwa na mahitaji husika ya Taasisi, hivyo kuzisaidia Taasisi kutokuzalisha madeni mapya katika utendaji wake.

Sura ya Kumi na Mbili

Kaguzi Maalum na Ukaguzi wa Vyama vya Siasa

12.1 Utangulizi

Sura hii inaonesha masuala yaliyojitokeza na mapendekezo yanayohusu Kaguzi Maalum na Ukaguzi wa Vyama vya Siasa kwa mujibu wa mamlaka yaliyoainishwa kwenye Kifungu cha 29 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 na Kifungu cha 14(1) cha Sheria za Vyama vya Siasa Na.5 ya mwaka 1992 (iliyorekebisha mwaka 2015), mtawalia.

12.2 Kaguzi Maalum

Kwa mujibu wa Kifungu cha 29 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008 na Kanuni 79(1) ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma ya Mwaka 2009. Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza kufanya Ukaguzi Maalum kufutia maombi kutoka kwa Afisa Masuuli, mtu yeyote, Taasisi, Mamlaka ya Umma, Wizara, Idara, Wakala, Mamlaka ya Serikali za Mtaa na Vyombo vingine. Aidha, mawanda ya Ukaguzi huu maalum huandaliwa na muombaji. Hata hivyo, Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza kufanya maboresho ya mawanda ya kaguzi hizi maalum kwa kuzingatia umuhimu na ufanisi kama ilivyoainishwa katika Kanuni 80(2) ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma ya Mwaka 2009.

Katika Mwaka huu wa fedha, nilifanya Kaguzi maalum zifuatazo;

- i) Ukaguzi Maalum wa Ununuzi wa Mfumo wa Kidijitali wa Kusajili Wapiga Kura (BVR) uliofanywa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).
- ii) Ukaguzi Maalum wa Ununuzi wa Mfumo wa Utambuzi wa Alama za Vidole (AFIS) uliofanywa na Jeshi la Polisi Tanzania.
- iii) Ukaguzi Maalum wa Tuhuma za Ubadhirifu wa Fedha za Umma wakati wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege Songwe uliofanywa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA)
- iv) Ukaguzi Maalum wa Ununuzi wa Sare za Polisi uliofanywa na Jeshi la Polisi Tanzania.

- v) Ukaguzi Maalum wa Masurufu uliofanyika katika Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi (Fungu 43), Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu Na. 46), Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Fungu Na. 52) na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Fungu Na. 98)
- vi) Ukaguzi Maalum wa Ununuzi wa Magari 777 aina ya Ashok Leyland uliofanywa na Jeshi la Polisi Tanzania.
- vii) Ukaguzi Maalum wa Tuhuma za Matumizi Mabaya ya Marejesho ya Mikopo kutoka Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF) Tawi la Morogoro.

Masuala yaliyojitokeza kwenye Kaguzi hizi maalum yamebainishwa kwenye kila ripoti ya Mkaguliwa na kuwasilishwa kwenye Mamlaka zilizoomba Kaguzi hizi maalum. Kwa muhtasari masuala yaliyojitokeza katika kila Ripoti yameainishwa katika Aya zifuatazo:

12.2.1 Ukaguzi Maalum wa Ununuzi wa Mfumo wa Kidijitali wa Kusajili Wapiga Kura (BVR) uliofanywa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iliombwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kupitia barua yenye Kumb. Na. PCCB/HQ/RB/122/2017/OP3B ya tarehe 14 Mei 2018 kufanya ukaguzi maalum kuhusu ununuzi wa Vifaa vya kidijitali vya kusajili wapiga kura (BVR) 8,000 uliofanywa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Mawanda ya ukaguzi huu yalilenga kubaini kama vifaa vya kidijitali vya kusajili wapiga kura (BVR) 5,000 zilivyotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) vilipokelewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na kubaini kama kulikuwa na haja ya ununuzi wa leseni mpya za Windows na Biometric Algorithms uliofanywa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA). Pia, Ukaguzi huu pia ulilenga kubaini gharama halisi zilizotumiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kufanya manunuzi ya vifaa vya kidijitali vya kusajili wapiga kura (BVR), na kubaini hasara iliyopata Serikali. Hadidu za rejea za ukaguzi huu ziliandaliwa na TAKUKURU na kuboreshwa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT), na ulihusu miaka ya fedha 2013/2014, 2014/2015, 2015/2016 na 2016/2017, 2017/2018 kwenye

Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA). Katika ukaguzi huu, nimebaini mapungufu yafuatayo:

12.2.1.1 Mfumo wa kidijitali wa kusajili Wapiga kura (BVR) wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) Haukuunganishwa na BVR za Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) na Malipo yasiyokuwa na tija ya manunuzi ya leseni za windows na biometric algorithms kiasi cha Sh.862,085,100

Mnamo tarehe 19 Machi 2014 makubaliano kuhusu kuunganishwa kwa Mifumo ya kidijitali ya kusajili wapiga kura (BVR) kati ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Mamlaka ya Vitambulisho (NIDA) na RITA (Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini) yalifikiwa. Aidha, mnamo tarehe 15 Mei 2014, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) iliingia mkataba na kampuni ya Lithotec Exports LTD kwa ajili ya ununuzi wa vifaa 10,500 vya kidijitali vya kusajili wapiga kura kupitia Mkataba Na. IE/018/2012-2013/HQ/G/19 na kuwekwa kwa vigezo vya kiufundi vinavyolandana na mfumo wa BVR ya NIDA na RITA. Aidha, mnamo tarehe 11 Desemba 2014, mkataba wa nyongeza ulisainiwa na kupunguza idadi ya vifaa vya BVR na kufikia 8,000. Hadi kufikia Mei 2015, jumla ya vifaa vya kidijitali 8,000 vya kusajili wapiga kura vilipokelewa toka kwa mzabuni Lithotec Exports LTD; ambapo jumla ya vifaa 5,000 vilipelekwa NIDA kwa Hati ya kutolea vifaa Stoo Na. 2996707 na 2996714 ya tarehe 11 Machi 2016 na 23 Mei 2016, mtawalia. Vifaa vilivyopokelewa toka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) vilikuwa havilandani na mfumo wa BVR wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), kinyume na makubaliano ya kimkataba.

Pia, nilipitia Hati tatu (3) za malipo pamoja na Ankara za madai na kubaini kiasi cha Sh.862,085,100 kilitumiwa na NIDA kwa ajili ya manunuzi ya leseni mpya za Windows na Biometric Algorithms ili kubadilisha mfumo kwenye BVR 5,000 zilizopokolewa ili ziweze kulandana na mfumo wa BVR wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).

Kwa kuwa vigezo vya kiufundi vya mfumo wa BVR vilibainishwa kabla ya kusainiwa kwa mkataba, usimamizi dhaifu wa mkataba huu

uliofanywa na maafisa wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) umesababisha serikali kupata hasara kwa kufanya malipo yasiyokuwa na tija.

Kuhusiana na suala hili, naishauri Serikali kuongeza usimamizi wa mikataba kwa ukaribu ili kupunguza matatizo yatokanayo na ubadhirifu na matumizi mabaya ya rasimali za umma.

12.2.1.2 Malipo zaidi kwa Mzabuni ya jumla ya Dola za Kimarekani 148,243.73

Mnamo tarehe 15 Mei 2014, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) iliingia Mkataba Na. IE/018/2012-2013/HQ/G/19 na Mzabuni Lithotec Exports LTD kwa ajili ya ununuzi wa Mfumo wa Kidijitali wa Usajili wa Wapiga Kura (BVR kits) 10,500 kwa gharama ya Dola za Kimarekani 89,094,407.05. Aidha, mnamo tarehe 11 Desemba, 2014 mkataba wa nyongeza ulisainiwa na kupunguza idadi ya BVR kuwa 8,000 pamoja na gharama za mkataba kupungua hadi kufikia Dola za Kimarekani 72,154,907.05. Hata hivyo, nilipitia malipo yaliyokwishalipwa kwa Mzabuni kati ya Juni 2014 na Aprili 2015 na kubaini jumla ya Dola za Kimarekani 72,303,150.78 (sawa na Sh.128,252,142,319) zililipwa na Tume ya Taifa ya uchaguzi (NEC), na kubaini malipo ya ziada ya Dola za Kimarekani 148,243.73. Nilifanya mahojiano na Menejimenti ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ili kubaini kama kuna mkataba wa nyongeza au vifaa vipya vilivyonunuliwa nje ya mkataba. Hata hivyo, hadi mwisho wa Ukaguzi wangu hakuna mkataba wa nyongeza wala orodha ya vifaa vipya iliyowasilishwa kwa ajili ya uhakiki.

Malipo zaidi ya gharama za mkataba yalikuwa ni kinyume na mkataba; na yanaonesha viashiria vya rushwa na ubadhirifu wa mali za umma.

Nashauri fedha zaidi zilizolipwa kwa Mzabuni zirejeshwe, na hatua kali za kisheria na kinidhamu zichukuliwe kwa Maafisa wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) walioshirikiana na Mzabuni kupora Mali za Umma.

12.2.1.3 Malipo ya Mafunzo ambayo hayakufanyika ya Jumla ya Dola za Kimarekani 358,650

Kifungu Na. 13 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba (GCC) ya Mkataba Na. IE/018/2012-2013/HQ/G/19 kati ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Lithotec Exports LTD kilielekeza kufanyika kwa mafunzo ya mfumo kwa watalaamu kumi na tano (15) kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) nchini Uholanzi. Hadi kufikia Aprili 2015, jumla ya Dola za Kimarekani 72,303,150.78 (sawa na Sh.128,252,142,319) zililipwa kwa Mzabuni, ikijumuisha gharama za mafunzo ya kiasi cha Dola za Kimarekani 358,650. Hata hivyo, nilifanya mahojiano na maafisa wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na kupewa taarifa kuwa mafunzo haya hayakufanyika nchini Uholanzi; badala yake, mzabuni alileta timu ya wataaluma wake na kufanya mafunzo ya majaribio wakati wa zoezi la uandikishaji wa wapiga kura. Niliomba kupatiwa ushahidi wa mafunzo haya, lakini hakuna ushahidi wowote uliowasilishwa kwa ajili ya uhakiki.

Serikali imepata hasara ya jumla ya Dola za Kimarekani 358,650 kwa ajili ya malipo ya mafunzo ambayo hayakufanyika.

Kuhusiana na hili, nashauri Mzabuni arejeshe kiasi tajwa. Aidha, hatua za Kinidhamu na kisheria zichukuliwe kwa Maafisa wote wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) waliohusika kufanya malipo bila mafunzo kufanyika.

12.2.2 Ukaguzi Maalum Kuhusu ununuzi wa Mfumo wa Utambuzi wa Alama za Vidole (AFIS) uliofanywa na Jeshi la Polisi Tanzania

Ukaguzi huu maalum umefanyika kufuatia maombi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupita barua yenye Kumb Na.PMP/1567/24/25 ya tarehe 23 Aprili 2017 kwa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT). Ukaguzi huu maalum ulilenga kubaini mapungufu yaliyojitokeza wakati mchakato wa manunuzi ya Mfumo wa Utambuzi wa Alama za Vidole (AFIS), kutathimini utekelezaji wa mradi mzima wa mfumo wa utambuzi wa alama za vidole (AFIS), pamoja na kutambua vifaa vizima na vibovu. Mawanda ya ukaguzi huu yalihusu

mwaka ya fedha 2011/2012 mpaka 2017/2018. Katika Ukaguzi huu, nimebaini yafuatayo:

12.2.2.1 Vigezo vya Kiufundi zilivyoandaliwa na Mtumiaji Mfumo wa utambuzi wa Alama za Vidole (AFIS) Havikuzingatiwa wakati wa Tathmini ya Zabuni

Nimepitia vigezo vya Kiufundi vya Zabuni Na. ME.014/PF/2011/2012/G/12 Lot 1 kwa ajili ya manunuzi ya Mfumo wa Utambuzi wa Alama za Vidole (AFIS) vilivyoandaliwa na mtumiaji mfumo na kuwasilishwa kwa Inspekta Jenerali wa Polisi na kubaini kwamba, vigezo husika havikuzingatiwa wakati wa tathmini ya Zabuni. Zaidi, ukaguzi umebaini kuwa vigezo vilivyotumika wakati wa tathmini ya zabuni hii ni vile vilivyowasilishwa na Mzabuni Lugumi Enterprises Limited wakati wa mapendekezo ya kuomba Zabuni kupitia barua yenye Kumb Na.LE/GC/VOL I/5/11 ya tarehe 14 Juni 2011 kwa Inspekta Jenerali wa Polisi. Hii ikiwa ni kinyume na Kifungu 36(1) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2004 (imefutwa) ambayo ilitamka vigezo vyote kwa ajili ya manunuzi ziandaliwe na mtumiaji.

Kutozingatia vigezo vya utumiaji mfumo kumesababisha Jeshi la Polisi kununua mfumo usiokuwa na tija.

Kuhusiana na suala hili, nashauri manunuzi mapya yote kufuata mahitaji kama ilivyoelekezwa kwenye kifungu 39(1)(b)-(d) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011 ili kuweza kupata thamani halisi ya fedha. Pia, nasisitiza mamlaka husika zichukue hatua stahiki kwa maofisa wote waliohusika.

12.2.2.2 Vifaa vya aina Moja vyenye Sifa na Uwezo unaolingana vilitozwa Bei Tofauti na Kusababisha Mzabuni Kulipwa zaidi ya Sh.556,647,610

Mnamo tarehe 28 Oktoba 2011, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani aliingia Mkataba Na. ME.014/PF/2011/2012/G/12 Lot 1 na Kampuni ya Lugumi Enterprises Limited kwa ajili ya ununuzi wa Mfumo wa Utambuzi wa Alama za Vidole (AFIS) kwa gharama ya kiasi cha Sh.37,163,940,127.70. Hata hivyo, mapitio yangu yalibainisha kuwa, vifaa vya mfumo wa utambuzi wa alama za vidole (AFIS)

vilivyoorodheshwa kwenye jedwali la mahitaji vyenye uwezo, sifa na ufanyaji kazi sawa na kutengenezwa na kampuni moja viliuzwa kwa bei tofauti na kusababisha Mzabuni kulipwa zaidi ya kiasi cha Sh.556,647,610.

Malipo haya ni matumizi mabaya ya fedha za walipa kodi.

Nashauri hatua za kisheria na kinidhamu zichukuliwe kwa maafisa wote wa Jeshi la Polisi waliosababishia Serikali hasara ya jumla ya Sh.556,647,610.

12.2.2.3 Zabuni yenye Kumb Na. ME.014/PF/2011/2012/G/12 Lot 1 kwa ajili ya Ununuzi wa Mfumo wa Utambuzi wa Alama za Vidole (AFIS) ilitolewa kwa Mzabuni Asiyekuwa na Sifa.

Nimepitia Kifungu Na. 13.3 (b) na (d) cha Maelekezo ya Jumla kwa Wazabuni na Kifungu 14 na 15 cha Masharti Maalumu kwa Wazabuni cha mkataba Na. ME/014/PF/2011/2012/G/12 Lot 1 kati ya Katibu Mkuu, Wizara ya Mambo ya Ndani na Lugumi Enterprises Limited na kubaini hitaji la uzoefu wa miaka mitatu kwa mzabuni kwa utekelezaji wa mradi unaofanana na mfumo wa utambuzi wa alama za vidole (AFIS). Aidha, nilipitia kabrasha la zabuni pamoja na ripoti ya tathmini ya zabuni na kubaini kutokuzingatiwa kwa kipengele cha uzoefu wa miaka mitatu kutoka kwa Mzabuni.

Vilevile, nilipitia ripoti ya Ukaguzi iliyotolewa na Idara ya Kodi za Ndani pamoja na nyaraka za usajili wa Kampuni na kubaini kuwa Kampuni ya Lugumi Enterprises haikusajiliwa kufanya biashara ya ununuzi na ufungaji wa Vifaa vya upelelezi na udukuzi (Forensic Tools). Nina maoni kwamba, hakukuwa na weledi wakati wa tathmini ya zabuni hii na kusababisha kununua mfumo usiokuwa na manufaa.

Kutokuwa na uangalizi wa kutosha kwenye vigezo vilivyowekwa imesababisha kununua mfumo (AFIS) kwa Mzabuni asiyekuwa na sifa na aliyeshindwa kutekeleza.

Kwa mantiki hii, nashauri vigezo vilivyowekwa kwenye Zabuni vitumike wakati wote wa tathmini, uidhinishaji na utoaji wa Zabuni kama ilivyoelekezwa na Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011 pamoja na Kanuni zake za Mwaka 2013. Nasisitiza wajumbe wa Kamati

za Tathmini za Zabuni kuwa huru na kutumia weledi wakati wote wa utekelezaji wa majukumu yao.

12.2.2.4 Manunuzi ya Mfumo wa Utambuzi wa Alama za Vidole Hayakuwa Kwenye Bajeti ya Jeshi la Polisi

Nimepitia nyaraka za bajeti za Jeshi la Polisi kuanzia mwaka wa fedha 2011/2012 hadi 2013/2014 na kubaini kuwa hakukuwa na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu ununuzi wa Mfumo wa Utambuzi wa Alama za Vidole (AFIS) uliotekelezwa na Jeshi la Polisi. Hata hivyo, nilibaini kuwa ununuzi huu ulitekelezwa kwa malipo ya jumla ya kiasi cha Sh.40,300,000,000 zilizohamishwa kutoka Hazina (Fungu Na. 21) kwenda Jeshi la Polisi (Fungu Na. 28) kwa mwaka wa fedha 2011/2012 hadi 2012/2013; ambapo, jumla ya kiasi cha Sh.34,000,000,000 kililipwa kwa Mzabuni Lugumi Enterprises Limited. Fomu zilizotumika kuhamisha fedha kutoka Hazina kwenda Jeshi la Polisi hazikuwa halisi, na ziliidhinishwa na Afisa asiyehusika. Zaidi, hapakuwa na ushahidi wa kibali kutoka Bunge kuhusu uhamisho wa fedha hizi.

Manunuzi nje ya bajeti yalikuwa kinyume na Sheria ya Matumizi ya Fedha za Umma (Appropriation Act) kwa mwaka 2011/2012 na 2012/2013 na kusababisha shughuli zilizobajetiwa kutotekelezwa.

Kuhusiana na hili, nashauri matumizi yote yatokane na bajeti iliyopitishwa na kuidhinishwa na bunge; na uhamisho wowote ufuatale taratibu zilizoainishwa kwenye kifungu Na. 41 cha Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015.

12.2.2.5 Kutofungwa Kwa Vifaa Vya Utambuzi wa Alama za Vidole (AFIS) Vya Gharama Ya Sh.1,736,056,030.45 Kwenye Magereza 35

Nilipitia Jedwali la Mahitaji la Mkataba na ME/014/PF/2011/2012/G/12 Lot 1 kwa ajili ya ununuzi wa Mfumo wa Utambuzi wa Alama za vidole (AFIS) kati ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani na Lugumi Enterprises Limited na kubaini kuwa vifaa vya thamani ya Sh.1,736,056,030.45 kwa ajili ya Magereza 35 havijafungwa kwenye Magereza husika. Aidha, vifaa hivyo

vilihamishwa toka kwa Boharia Mkuu wa Jeshi la Polisi na kuhifadhiwa kwenye Idara ya Upelelezi ya Makao Makuu ya Jeshi la Polisi (CID).

Hali ya vifaa hivi kuendelea kuhifadhiwa inaonesha ni jinsi gani Jeshi la Polisi halikuandaa Mpango kazi kabla ya kufanya Manunuzi ya Mfumo huu wa Utambuzi wa Alama za Vidole (AFIS); hivyo hakuna thamani halisi ya fedha za umma kwenye manunuzi haya.

Nashauri vifaa hivi kufungwa kwenye Magereza 35 yaliyoainishwa bila kuchelewa.

12.2.2.6 Mafunzo kwa Wataalamu 30 wa Mfumo Yaliyogharimu Sh.604,390,244 Hayakufanyika

Nimepitia Mkataba na. ME.014/PF/2011/2012/G/12 Lot 1 unaohusu ununuzi wa Mfumo wa Utambuzi wa Alama za Vidole (AFIS) ulioingiwa baina ya Katibu Mkuu, Wizara ya Mambo ya Ndani na Mzabuni Lugumi Enterprises Limited na kubaini kati ya gharama ya mkataba ya Sh.37,163,940,127.70, gharama za mafunzo na elimu zilikuwa Sh.4,101,680,000 (ikijumuisha kodi ya ongezeko la thamani) kwa waendeshaji 382 na wataalamu 30 wa mfumo. Pia, nilibaini Hati za kupelekea Mzigo Na. 0161 na 0174 za tarehe 20 Februari 2012 na 30 Aprili 2012 kutoka kwa Mzabuni zilipitishwa na Mkuu wa Kitengo cha Uchunguzi wa Kisayansi cha Jeshi la Polisi (Forensic Unit) na kuidhinisha malipo ya Sh.604,390,244 kwa ajili ya mafunzo ya wataalamu 30. Aidha, niliomba nyaraka za mafunzo ili kujiridhisha kama mafunzo husika yamefanyika. Hata hivyo, nyaraka hizo hazikuwasilishwa wakati wa Ukaguzi wangu. Hivyo, kutokana na kukosekana kwa nyaraka hizo, nimeshindwa kuthibitisha kama mafunzo husika yamefanywa na mzabuni Lugumi Enterprises Limited. Serikali imepata hasara kwa kulipia mafunzo ambayo hayakufanyika.

Kwa mantiki hii, nashauri Mzabuni Lugumi Enterprises Limited ama akamilishe mafunzo ya wataalamu 30 au arudishe gharama za mafunzo alizolipwa.

12.2.2.7 “Monitor” 58 Aina ya L2250p zenye ukubwa wa inchi 22 na zenye thamani Ya Sh.159,166,100 Hazikuonekana Wakati wa Ukaguzi

Nimepitia Jedwali la Mahitaji la Mkatoba Na. ME.014/PF/2011/2012/G/12 Lot 1 unaohusu ununuzi wa Mfumo wa Utambuzi wa Alama za Vidole (AFIS) na kubaini kuwa miongoni mwa orodha ya vifaa, kulikuwa na “monitor” 271 aina ya Dell optiplex zenye ukubwa wa inchi 21.5 pamoja “monitor” nyingine 271 aina ya Dell optiplex zenye ukubwa wa inchi 22 zote ziligharimu jumla ya Sh.2,513,029,651. Vilevile, nilipitia Hati ya malipo Na. 28VC1108240, Hundi Na. 256885/6, Hati ya kuletea Mzigo Na.0176, 0177 na taarifa ya Kamati ya Ukaguzi na Mapokezi ya Vifaa ya tarehe 25 Mei 2012 na 20 Februari 2012, mtawalia. Nilibaini uletwaji wa vifaa na malipo ya jumla ya kiasi cha Sh.159,166,100 kwa mzabuni Lugumi Enterprises Limited kwa “monitor” 58 aina ya Dell optiplex moduli L2250P yenye ukubwa wa inchi 22 “wide hybrid” 0282 TCO-5.0 1680X105075HZ. Pia, nimepitia Hati jumuifu ya kuombea na kutolea Vifaa na kubaini “monitor” 58 aina za Dell zilihamishwa toka kwa Boharia Mkuu wa Jeshi la Polisi na kupelekwa Ofisi ya upelelezi ya Makao Makuu ya Jeshi la Polisi tarehe 21 Februari 2012. Hata hivyo, monitor hizo hazikuonekana wakati nilipofanya Ukaguzi katika Ofisi ya Upelelezi ya Makao Makuu ya Jeshi la Polisi (CID). Aidha, mahojiano na Viongozi wa Ofisi ya Upelelezi (CID) hayakuweza kubainisha taarifa yoyote kuhusiana na suala hili.

Malipo kwa vifaa ambavyo havikuonekana kunaonesha ubadhirifu na matumizi mabaya ya rasilimali za umma.

Kuhusiana na suala hili, napendekeza hatua za kisheria na kinidhamu zichukuliwe kwa maafisa wote wa Ofisi ya Upelelezi Makao Makuu ya Jeshi la Polisi walioshindwa kutunza “monitor” 58 aina ya Dell optiplex modeli L2250P yenye ukubwa wa inchi 22.

12.2.2.8 Malipo ya Huduma ambayo Haikufanyika Sh.3,304,000,000

Nimepitia Kifungu cha 52 cha Jedwali la Mahitaji ya Mkatoba ME.014/PF/2011/2012/G/12 Lot 1 kwa ajili ununuzi wa Mfumo wa

Utambuzi wa Alama za Vidole (AFIS) na kubaini huduma ya matengenezo na uwezeshaji ya kipindi cha miaka tatu (3) kwa vifaa vyote vya Mfumo wa Utambuzi wa Alama za Vidole kwa mpangilio ufuatao; matengenezo na uwezeshaji mwaka wa kwanza, uwezeshaji wa kiufundi mwaka wa pili na wa tatu. Pia, nilipitia Hati ya Malipo Na. 28VC12008548/9, Hati ya Madai Na. 0148, Hati ya kupelekea vifaa Na. 0161, Hundi Na.273071/2 ya tarehe 20 Februari 2012 na 28 Mei 2013, mtawalia. Nilibaini kuwa malipo ya Sh.3,304,000,000 yalilipwa kwa mzabuni Lugumi Enterprises Limited kwa ajili ya huduma ya matengenezo na uwezeshaji.

Hata hivyo, wakati wa kipindi cha ukaguzi kwenye mikoa ishirini na sita (26), nilibaini hakukuwa na huduma ya matengenezo na uwezeshaji kwenye Mikoa minane (8) ya Temeke, Mwanza, Simiyu, Rukwa, Tabora, Kigoma, Geita na Kinondoni, katika Mikoa 18, Maafisa wakuu walinitaarifu kuwa huduma ya matengenezo na uwezeshaji ilifanyika kati ya mara moja mpaka mbili, kinyume na matakwa ya mkataba yaliyomtaka Mzabuni kutoa huduma hiyo kwa awamu tatu tofauti.

Kwa sababu ya kutokuwapo kwa usimamizi wa kutosha wa kimkataba uliofanywa na Kitengo cha Upelelezi cha Makao Makuu ya Jeshi la Polisi, huduma ya matengenezo na uwezeshaji haikukamilika kwa mikoa yote ishirini na sita (26), hivyo kusababisha hasara ya kiasi cha Sh.3,304,000,000 kwa Serikali.

Hivyo, nashauri huduma ya matengenezo na uwezeshaji ikamilishwe na Mzabuni Lugumi Enterprises Limited kwenye mikoa yote ishirini na sita (26) kama ilivyoelekezwa kwenye maktaba.

12.2.2.9 Malipo ya Monitor 213 Aina ya Dell yenye Ukubwa wa Inchi 22 (Modeli L2250P 22 Wide Hybrid 0282 TCO-5.0 1680X105075HZ) zenye Gharama ya Sh.431,658,635 ambazo Hazikuletwa

Nimepitia Mkataba wa nyongeza na. ME.014/PF/2011/2012/G/12 Lot 1 kwa ajili ya ununuzi wa Mfumo wa Utambuzi wa Alama za Vidole uliorekebisha gharama ya Mkataba toka Sh.41,475,728,579.50 na kuwa Sh.37,742,913,007.34 na kubaini orodha ya Dell Monitor 213

aina ya optiplex zenye modeli L2250P na ukubwa wa inchi 22. Zaidi, nimebaini Mzabuni Lugumi Enterprises alikwishalipwa jumla ya Sh.34,000,000,000 kabla ya kusaini kwa mkataba huu wa nyongeza. Aidha, jumla ya kiasi cha Sh.236,436,952.84 hakikuwa kimelipwa na Jeshi la Polisi kwa Mzabuni Lugumi Enterprises Limited. Hata hivyo, Ukaguzi wangu niliofanya Mwezi wa Juni 2018 ulibaini kuwa, kati ya vifaa vyote vilivyoletwa na Lugumi Enterprises Limited, “monitor” 213 aina ya Dell hazikuletwa licha ya mzabuni kulipwa malipo yote. Kwa maoni yangu, hakukuwa na haja ya kuletwa kwa “monitor” hizi 213 zenye ukubwa wa inchi 22 kwani tayari “monitor” zenye ukubwa wa inchi 21.5 zilishafungwa kwenye vituo vya Polisi 184 nchi nzima, ikiwamo Zanzibar.

Nimebaini malipo zaidi ya jumla ya kiasi cha Sh.195,221,682 kwa Lugumi Enterprises Limited kwa “monitors” ambazo hazikuletwa na zisizokuwa na matumizi kwenye mfumo wa Utambuzi wa Alama za Vidole na kusababishia Serikali hasara.

Kuhusiana na suala hili, nashauri Jeshi la Polisi kutopokea Monitors 213 ambazo hazina matumizi yoyote kwenye Mfumo wa Utambuzi wa Alama za Vidole. Hivyo, Lugumi Enterprises Limited arejeshe kiasi cha Sh.195,221,282 kilicholipwa zaidi.

12.2.3 Ukaguzi Maalum wa Tuhuma za Ubadhirifu wa Fedha za Umma wakati wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Songwe uliofanywa na Mamlaka ya Viwanja Vya Ndege (TAA)

Kwa mujibu wa Kifungu cha 29 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008, nilianzisha Ukaguzi huu Maalum kufutia tuhuma za ubadhirifu zilizojitokeza wakati wa ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu alioifanya uwanja wa ndege wa Songwe mkoani Mbeya. Ukaguzi huu ulilenga kubaini mapungufu kwenye malipo yaliyohusu ujenzi wa uwanja wa ndege Songwe kupitia mkataba Na. TAA/C/19/2008/2099 uliosainiwa baina ya Mamlaka ya Viwanja Vya Ndege (TAA) na Mkandarasi dp Shapriya & Co Limited. Ukaguzi huu umehusu mwaka wa fedha 2013/2014 mpaka 2017/2018. Yafuatayo ni mapungufu yaliyojitokeza:

12.2.3.1 Malipo ya Shughuli za Ujenzi ambazo Hazikuidhinishwa na Mhandisi Mshauri ya Sh. 5,482,610,339.86 na Malipo yenye Udanganyifu ya Sh.570,508,125

Nimepitia Hati za Malipo ishirini na tatu (23) na kubaini malipo ya jumla ya Sh. 13,084,303,177.77 yalilipwa kwa Mkandarasi dp Shapriya & Co LTD kati ya mwaka wa fedha 2012/2013 na 2015/2016. Hata hivyo, kati ya Hati za Malipo ishirini na tatu (23) nilizozikagua, nimebaini kuwa jumla ya Hati za Malipo kumi na sita (16) zenye thamani ya Sh.7,601,692,837.91 ziliidhinishwa na Mhandisi Mshauri wakati Hati za Malipo saba (7) zenye thamani ya Sh.5,482,610,339.86 hazikuidhinishwa na Mhandisi Mshauri, kinyume na kifungu 60.2 cha Masharti ya jumla ya Mkataba Na. TAA/C/19/2008/2009. Hivyo basi, nimeshindwa kuthibitisha kama kazi husika zilifanyika kama Hati za Malipo saba (7) hazikuidhinishwa na Mhandisi Mshauri.

Mbali na hilo, nilipitia Hati kumi na sita (16) zilizoidhinishwa na Mhandisi Mshauri na kubaini mwajiri (TAA) aliongeza madai zaidi juu ya yale yaliyoidhinishwa na Mhandisi Mshauri kwenye Hati za Malipo 223/6, 98/8 za tarehe 24 Juni 2014 na 15 Agosti 2013, mtawalia, zenye jumla ya Sh.570,508,125.

Malipo zaidi yaliyoidhinishwa na Mhandisi Mshauri ni viasharia vya rushwa na ubadhirifu wa mali za umma.

Kuhusiana na suala hili, napendekeza Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) kuanzisha uchunguzi kwenye Hati za Malipo Na. 10 na 03 kabla ya kukabidhiwa kwa Mradi na urejeshaji wa pesa zilizoshikiliwa kwa matazamia (Retention money) kwa Mkandarasi.

12.2.3.2 Kutorejeshwa kwa Malipo ya Awali ya Kuanzisha Shughuli za Ujenzi Sh.1,528,200,879.98

Nimepitia Hati za Malipo 98/8, 77/4 na 23/4 na kubaini malipo ya awali ya Sh. 1,704,766,352.25 yalilipwa kwa Mkandarasi dp Shapriya & Co LTD kabla ya kuanza shughuli za ujenzi tarehe 10 Aprili 2013. Vilevile, nilipitia Hati za Malipo Na. 126/9 ya tarehe 19 Septemba 2014 na kubaini kiasi cha Sh.176,565,475.27 ndicho kilichorejeshwa kati ya jumla ya Sh.1,704,766,352.25 kilicholipwa kwa Mkandarasi kama Malipo ya awali, kinyume na Kifungi 60.7 cha Mkataba Na.

TAA/C/19/2008/2009 baina ya Mamlaka ya Viwanja Vya Ndege (TAA) na Mkandarasi dp Shapriya & Co LTD.

Kama hatua za haraka za urejeshaji hazitachuliwa, kuna uwezekano mkubwa kiasi husika kutorejeshwa.

Kuhusiana na hili, nashauri mwajiri (TAA) kurejesha kiasi husika kwenye Hati za Madai ambazo Mkandarasi hajalipwa.

12.2.3.3 Malipo kwa Mkandarasi ambayo Hakustahili Sh.3,383,387,095

Nimepitia Hati za Malipo Na. 171/10, Hati za Madai za Mkandarasi (IPC) Na. 9 na 10 za tarehe 15 Oktoba 2014 na kubaini malipo ya Sh.629,081,268.95 na Sh.804,305,826.51, mtawalia, yalilipwa kwa Mkandarasi dp Shapriya & Co LTD. Hata hivyo, wakati wa Ukaguzi niligundua malipo yote hayo yalishalipwa kwa Mkandarasi kupitia Hati za Malipo Na. 167/5 na 223/6 za tarehe 21 Mei 2014 na 24 Juni 2014, mtawalia. Aidha, vitendo vya udanganyifu vilivyofanywa na Maofisa wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) kwa kushirikiana na Mkandarasi dp Shapriya & Co LTD vimesababisha malipo mara mbili ya Sh.1,433,387,095.46.

Vilevile, nilipitia jumla ya malipo yote ya Sh.13,084,303,177.77 aliyolipwa Mkandarasi dp Shapriya & Co LTD na kubaini kiasi cha Sh.1,950,000,000 kililipwa kupita Hati ya Malipo na. 48/3 bila ya kuwapo kwa Cheti cha Madai kilichoidhinishwa na Mhandisi Mshauri pamoja na Jedwali la Vipimo, kinyume na Kifungu 56.1,60.1 na 55.1,53.3 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba Na. TAA/C/19/2008/2009 kati ya Mamlaka ya viwanja vya Ndege (TAA) na Mkandarasi dp Shapriya & Co LTD.

Malipo mara mbili ya Sh.1,433,387,095.46 na malipo ya Sh.1,950,000,000 bila ya Cheti cha Madai kilichoidhinishwa ni udanganyifu ambao Mkandarasi hakustahili kulipwa. Hivyo, rasilimali za umma za jumla ya Sh.3,383,387,095 zilitumiwa vibaya na Maaofisa wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA).

Kuhusiana na suala hili, nashauri Mkandarasi dp Shapriya & Co LTD arejeshe kiasi cha jumla ya Sh.3,383,387,095 ambazo hakustahili

kulipwa, ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua za kinidhamu na kisheria kwa Maafisa wote wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) waliohusika.

12.2.4 Ukaguzi Maalum wa Ununuzi wa Sare za Polisi uliofanywa na Jeshi la Polisi

Nilifanya Ukaguzi huu kufutia maombi kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKURURU), na kwa mujibu wa Kifungu 29 na 36 ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya 2008. Kazi hii ilifanyika kwa kuongozwa na hadidu za rejea zilizoandaliwa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Lengo la Ukaguzi huu lilikuwa kubaini kama Manunuzi ya sare za Jeshi la Polisi yalitekelezwa kwa kufuata sheria na kanuni za Manunuzi ya Umma, na kuthibitisha kama malipo aliyolipwa Mzabuni Daissy General Traders ni halali na yalihusu Sare alizoleta, kupokelewa na kuhifadhiwa na Boharia Mkuu wa Jeshi la Polisi. Katika Ukaguzi huu, yafuatayo ndiyo mambo ya msingi yaliyoibuka:

12.2.4.1 Maoni ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Hayakuzingatiwa

Nilipitia mawasiliano ya barua kati ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani na kubaini maoni ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusiana na uwasilishaji wa Hati ya Nguvu ya Kisheria (Power of Attorney) na leseni halali hayakuzingatiwa na katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani wakati wa kusaini Mkataba Na. ME.014/PF/2015/2016/G/30 Lot 2 kwa ajili ya ununuzi wa Sare za Polisi mnamo tarehe 2 Novemba 2015 na Mzabuni Daissy General Traders.

Kushindwa kuingizwa kwa maoni ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwenye rasimu ya Mkataba kunakinzana na matakwa ya kanuni 59(1)(5) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2013 na kufanya mkataba uliosainiwa kuwa batili kwa mujibu wa Kanuni 59(1)(2) ya Sheria hiyo.

Hivyo, nashauri Jeshi la Polisi mara zote kufanya manunuzi kwa kuzingatia sheria, ikiwa ni pamoja na kujumuisha maoni ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali mara baada ya kuhakiki rasimu za mikataba.

12.2.4.2 Malipo ya Sare za Polisi ambazo Hazikuletwa Kwa Boharia Mkuu wa Jeshi la Polisi Sh.16,660,000,000

Nilipitia Mkataba Na. ME.014/PF/2015/2016/G/30 Lot 2 kwa ajili ya manunuzi ya Sare za Jeshi la Polisi yenye thamani ya Sh.22,918,880,600 uliosainiwa tarehe 2 Novemba 2015 baina ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani na Mzabuni Daissy General Traders na kubaini yafuatayo:

- a) Mkataba ulitekelezwa kwa utaratibu wa Oda zenye uhitaji (Call off Order), ambapo Mzabuni mara tu apokeapo Oda zenye uhitaji huagiza mzigo wa Sare za Polisi kutoka kwa mtengenezaji aliyeko nchini China na kuzileta kwa Boharia Mkuu wa Jeshi la Polisi kwa kipindi kisichozidi siku 180 kutoka siku aliyopokea Oda. Mchakato wa manunuzi ulianza kwa Oda ya hitaji Na. MOHA/PF/2015/2016/08 ya tarehe 04 Novemba 2015 kwenda kwa Mzabuni Daissy General Traders. Mnamo tarehe 06 Novemba 2015 Mzabuni Daissy General Traders aliwasilisha Hati ya Madai Na. 0403 na Hati ya kupokelea mzigo Na. 0106 akidai malipo kwa bidhaa alizoleta.
- b) Mnamo tarehe 09 Novemba 2015, kiasi cha Sh.16,660,000,000 kililipwa kwa Mzabuni Daissy General Traders kupitia Hundi Na.369695, 369696,369701 za Sh.8,000,000,000, Sh.8,600,000,000, na Sh.60,000,000, mtawalia. Hata hivyo, katika mazingira yasiyo ya kawaida nilishindwa kukubali kuwa uagizwaji toka China na upelekaji wa Sare za Polisi kwa Boharia Mkuu wa Jeshi la Polisi ulichukua siku mbili (2) kutoka siku ya upokeaji wa oda za uhitaji.
- c) Kukosekana kwa nyaraka za kuthibitisha uletaji wa mzigo. Niliomba Hati ya kupokelea Shehena ya Mzigo Bandarini (Bill of Lading), Hati ya Madai kutoka kwa Mtengenezaji (Commercial Invoice), Hati ya Mzigo ulipotoka (Certificate of Origin), orodha za mali zilizopo kwenye meli (Packing List) na cheti cha ukaguzi wa bidhaa (Inspection Certificate) kutoka kwa Mzabuni Daissy General Traders kwa ajili ya kujiridhisha kama bidhaa husika zililetwa nchini. Hata hivyo, Mzabuni alishindwa kuwasilisha nyaraka hizo. Aidha, nilipitia Mfumo wa Forodha (TANCIS) wa

Mamlaka ya Mapato (TRA) na kubaini kuwa hapakuwa na shehena yoyote kutoka kwa Mzabuni Daissy General Traders mwezi Novemba 2015.

- d) Vilevile, nilifanya mahojiano na Maofisa wa Bohari kuu ya Jeshi la Polisi na kubaini hakukuwa na Sare zozote zilizoletwa na Mzabuni Daisy General Traders mwezi Novemba 2015.

Hivyo, Serikali imepata hasara kubwa kwa kufanya malipo ya Sare za Polisi ambazo hazikuletwa na Mzabuni.

Kuhusu suala hili, nashauri Mzabuni Daissy General Traders arejeshe kiasi alicholipwa kwa kutoleta Sare za Polisi na hatua stahiki za kinidhamu na kisheria zichukuliwe kwa Maofisa wote wa Jeshi la Polisi kwa kuisababishia Serikali hasara.

12.2.5 Ukaguzi Maalum wa Masurufu Katika Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi (Fungu Na. 43), Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu Na. 46), Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Fungu Na.52) na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Fungu Na. 98)

Nilifanya ukaguzi huu maalum wa usimamizi wa Masurufu kwenye Wizara ya Kilimo, Mifugo, na Uvuvi (Fungu Na.43), Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu Na. 46), Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Fungu Na.52) na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Fungu Na.98) pamoja na Taasisi zake kwa mujibu wa Kifungu cha 29 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya Mwaka 2008. Lengo la ukaguzi huu lilikuwa kubaini utoshlezaji wa mifumo ya udhibiti wa ndani kuhusiana na uidhinishaji wa masufuru, kubaini kama Mfumo wa masufuru ndani ya “Epicor” umewezeshwa kudhibiti utoaji na urejeshaji wa Masurufu na kuhakiki uhalali wa nyaraka za marejesho za masurufu yaliyotolewa ikiwa ni pamoja na kuangalia utunzaji wake. Ukaguzi wangu umehusu masurufu yote yaliyotolewa na kurejeshwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015 hadi 2016/2017 na yafuatayo yamebainika katika Ukaguzi huu:

12.2.5.1 Masufuru ambayo Hayajarejeshwa Sh.245,194,247.8

Kipindi cha Ukaguzi wangu, nimebaini jumla ya masufuru ya Sh.245,194,247.8³³yalitolewa kwa Maofisa wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi (Fungu Na. 43), na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Fungu Na. 52) kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kiofisi ambayo hayakurejeshwa hadi kipindi cha ripoti hii Agosti 2018. Hata hivyo, nilibaini hakuna hatua za urejeshaji au za kinidhamu zilizochukuliwa kwa Maafisa wote waliotajwa kwa mujibu wa Kanuni 103(2) ya Kanuni za Fedha za Umma za Mwaka 2001. Chini ya Kanuni hii, masufuru ambayo hayakurejeshwa hadi kufunga kwa mwaka wa fedha yanapaswa kurejeshwa na wahusika kutoka kwenye mishahara.

Nilishindwa kuthibitisha kama masufuru husika yalifanya kazi iliyokusudiwa.

Hivyo, napendekeza Maafisa Masuuli wa Wizara zilizotajwa kuhakikisha kuwa masufuru ambayo hayajarejeshwa yakatwe kwenye mishahara ya Watumishi husika kama ilivyoelekezwa na Kanuni 103(2) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001.

12.2.5.2 Masufuru yalitolewa kwa Shughuli ambazo Hazikuwa kwenye Bajeti Sh. 32,529,895

Nimepitia nyaraka za Bajeti na Ripoti ya matumizi ya Mradi wa ERPP uliopo Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi (Fungu Na. 43) kutoka mwaka wa fedha 2014/2015 hadi 2916/2017. Nimebaini jumla ya Sh.32,529,895 kutoka mradi wa ERPP ilitumika kulipia shughuli za Wizara ambazo hazikuwa kwenye bajeti, kinyume na Kanuni 97(1) ya Sheria za Fedha za Umma ya Mwaka 2001 (iliyorekebisha mwaka 2004). Kiasi hicho hakijarejeshwa hadi muda wa Ukaguzi wangu mwezi wa Agosti 2018. Kwa mujibu wa kanuni 97(1), Masufuru yanapaswa kutolewa kwenye shughuli zote zilizopo kwenye bajeti iliyoipitishwa na Bunge.

³³ Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi (Fungu Na. 43) ,Sh. 72,147,077 na Wizara ya Afya ,Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Fungu Na. 52) ,Sh. 173,047,170.80

Shughuli za mradi wa ERPP zenye thamani ya jumla ya Sh.32,529,895 hazikutekelezwa kwenye kipindi husika na kuathiri matokeo ya mradi.

Kuhusiana na suala hili, nashauri Afisa Masuuli (Fungu Na. 43) kutoa Masufuru kwenye matumizi ambayo yamebajetiwa na kuhakikisha masurufu ya mradi wa ERPP yanarejeshwa.

12.2.5.3 Masufuru ambayo Yameshughulikiwa nje ya Mfumo wa “Epicor Imprest Module” Sh.11,756,128,459.71

Nimepitia mfumo wa “Epicor” pamoja na mwongozo wa uendeshaji na kubaini jumla ya Masufuru ya Sh.11,756,128,459.71 kutoka Wizara ya Kilimo,Mifugo na Uvuvi (Fungu Na. 43), Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46), Wizara ya Afya,Maendeleo ya Jamii,Jinsia,Wazee na Watoto (Fungu Na. 52) na Wizara ya Ujenzi,Uchukuzi na Mawasiliano (Fungu Na.s 98) yalitolewa na kurejeshwa nje ya mfumo wa “Epicor ” licha ya kuwapo kwa Moduli ya Masufuru “Imprest Module” ambayo leseni yake Serikali imegharamia jumla ya Sh.5,371,391,852.05³⁴ toka mwaka wa fedha 2010/2011 hadi 2015/2016. Masufuru ambayo hayakupita kwenye mfumo yameorodheshwa hapa chini.

Jedwali Na. 92: Masurufu ambayo hayakupita kwenye mfumo - Wizara

Jina la Taasisi	Miaka			Jumla (Sh.)
	2014/2015	2015/2016	2016/2017	
Wizara ya Ujenzi,Uchukuzi na Mawasiliano (Fungu Na. 98)	431,967,675.44	116,342,938.84	300,087,161.71	848,397,775.99
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu Na. 46)	1,394,229,597.96	959,375,982.66	1,066,834,668.14	3,420,440,248.76
Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi (Fungu Na. 43)	3,249,313,912.00	909,748,870.00	937,652,465.00	5,096,715,247.00
Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Fungu Na. 52)	282,902,098.16	469,458,321.20	1,338,619,851.60	2,090,980,270.96
JUMLA	5,358,413,283.50	2,454,926,112.70	3,643,194,146.45	11,456,533,542.71

Chanzo: Nyaraka za Masurufu kutoka mwaka 2014/2015 mpaka 2016/2017

Hakuna thamani halisi ya fedha kwenye ununuzi wa Mfumo wa “Epicor” kama “Imprest Module” haitumiki kushughulikia masurufu.

³⁴ Malipo ya leseni ya Epicor yaliyolipwa na Serikali, 2011: Sh. 670,844,160,2012: Sh.699,269,760,2013: Sh.699,269,760,2014: Sh. 980,943,673.05,2015: Sh.1,074,410,001, na 2016: Sh. 1,246,654,498

Nashauri Maafisa Masuuli wote kushughulikia masufuru yote ndani ya mfumo wa “Epicor Imprest Module” ili kuwe na thamani halisi ya fedha ya ununuzi wa mfumo wa “Epicor”

12.2.5.4 Masufuru yaliyorejeshwa ambayo yana Nyaraka Pungufu au yasiyokuwa na Nyaraka Sh. 3,282,748,190.42

Nimepitia utaratibu wa masufuru kwenye Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Fungu Na.52), Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu Na. 46) na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi (Fungu Na.43) pamoja na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2014/2015 hadi 2016/2017 na kubaini masufuru ya jumla ya Sh. 2,610,449,214 yalirejeshwa bila kuwapo kwa nyaraka za msingi kama vile fomu ya maombi ya masurufu, risiti za mafuta, tiketi na fomu za marejesho. Zaidi, nimebaini masufuru jumla ya Sh.672,248,976.80 kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu Na. 46), na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Fungu Na. 52) yalirejeshwa pasipokuwa na nyaraka zozote. Maelezo yameonyeshwa hapa chini.

Jedwali Na. 93: Maelezo yenye nyaraka pungufu au yasiyokuwa na nyaraka

Jina la Taasisi	Masurufu yenye nyaraka pungufu		Masurufu yasiyokuwa na nyaraka	Jumla (Sh.)
	Fungu	Taasisi		
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu Na. 46)	820,058,107.60	430,997,000.00	61,215,000.00	1,312,270,107.60
Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi (Fungu Na. 43)	-	582,767,616.50	-	582,767,616.50
Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Fungu Na. 52)	776,676,489.52	-	611,033,976.80	1,387,710,466.32
Jumla	1,596,734,597.12	1,013,764,616.50	672,248,976.80	3,282,748,190.42

Chanzo: Nyaraka za masurufu kutoka mwaka 2014/2015 mpaka 2016/2017

Kutokana na kutokuwapo kwa nyaraka muhimu za masufuru, nimepata kikwazo kutambua kiasi cha masurufu kilichotolewa na kuthibitisha kama masufuru yalitumika kwenye shughuli za matumizi zilizohusiana na masufuru hayo.

Kuhusiana na suala hili, nashauri Afisa Masuuli kuwawajibisha Maafisa wote ambao wamerejesha masufuru yenye nyaraka pungufu, na wale ambao wamepoteza nyaraka za masufuru.

12.2.6 Ukaguzi Maalum wa Ununuzi wa Magari 777 aina ya Ashok Leyland uliofanywa na Jeshi la Polisi Tanzania.

Kifungu 27 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya Mwaka 2008 kinawezesha Mdhambi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi wa kiuchunguzi baada ya kutambua dalili za ubadhirifu kama zipo katika taasisi fulani. Kwa suala hili, niliombwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani kwa barua yenye Kumbukumbu Na. CAB 89/369/01 ya tarehe 22 Februari 2018 kufanya uchunguzi wa ununuzi wa magari ya polisi yenye thamani ya Dola za Kimarekani 29,606,100 (sawa na Sh.47,953,296,231). Nilianzisha uchunguzi huu kwa lengo la kupata uhakika kama magari 777 yaliyoagizwa na Jeshi la Polisi yalipokelewa, kuona utekelezaji wa mkataba pamoja na namna iliyotumika kupata mkopo kupitia Mkataba wa Mkopo (Buyers Credit Agreement). Katika Ukaguzi huu nilibaini yafuatayo:

12.2.6.1 Mapugufu yaliyojitokeza kwenye ununuzi wa magari 777 aina ya Ashok Leyland yenye thamani ya Dola za Kimarekani 29,606,100

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani aliingia mkataba Na. ME.014 / PF / 2012/2013 / G / 40 na kampuni ya Ashok Leyland kwa ajili ya ununuzi wa magari 777 yenye thamani ya Dola za Kimarekani 29,606,100 (sawa na Sh.47,953,296,231) mnamo tarehe 5 Septemba 2013. Zaidi, nilibainisha kuwa mkataba wa nyongeza na mkataba wa mwisho ulisainiwa tarehe 07 Desemba 2015 na 15 Februari 2017, mtawalia. Hata hivyo, muda wa utekelezaji mkataba haukubainishwa wazi wazi kwenye kiambatisho cha Mkataba wa nyongeza na Mkataba wa mwisho.

Ukaguzi wangu ulibainisha kuwa ununuzi wa magari uligharamiwa na mkopo wa Dola za Kimarekani 29,606,100 (sawa na

Sh.47,953,296,231) zilizokopwa toka benki ya Exim India kupitia makubaliano ya mikopo yaliyosainiwa tarehe 19 Juni 2015 kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Benki ya Exim India. Ukaguzi wangu pia ulibaini kuwa kabrasha na barua ya mwaliko ya Zabuni vilipelekwa kwa kampuni ya Ashok Leyland tarehe 15 Aprili 2013 kabla ya idhini ya mkopo kutolewa na Wizara ya Fedha tarehe 30 Aprili 2014.

Pia, nilibainisha kwamba masharti ya mkopo huu yalikuwa ya kibiashara. Hata hivyo, licha ya masharti hayo kuwapo, mkopo ulipendekezwa na kuidhinishwa na Kamati ya Kiufundi ya Usimamizi wa Madeni (TDMC), Kamati ya Taifa ya Usimamizi wa Madeni (NDMC) na Wizara ya Fedha, mtawalia. Kwa kuongezea, nilibaini kuwa masharti ya malipo yaliyotajwa kwenye Mkataba wa usambazaji ni tofauti na yale yaliyotajwa katika Mkataba wa mkopo.

Hadi kufikia Desemba 2018, jumla ya mkopo wa Dola za Kimarekani 16,128,529,70 kati ya Dola za Kimarekani 29,606,100 ulitumiwa na Serikali na kuacha bakaa ya Dola za Kimarekani 13,477,570,30 ambazo hazikutumiwa na kusababisha gharama za kujitolea (Commitment charges) za Dola za Kimarekani 287,087.17 (sawa na Sh.642,256,630.39) ambazo hazijalipwa na Serikali. Ukaguzi wangu zaidi ulibainisha masuala yafuatayo:

- a) Pamoja na ufuatiliaji wa kutosha, hakuna ushahidi uliowasilishwa ili kuthibitisha kama uhitaji wa magari ulianzishwa na Idara ya Usafiri na Lojistiki ya Jeshi la Polisi kabla ya kuanza kwa taratibu za ununuzi kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 36 (1) (a) - (d) ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004 (imefutwa). Mbali na hilo, nilibaini kwamba Ashok Leyland ilikuwa haina uwezo wa kuleta magari haya kwani anaweza kuleta magari 507 (sawa na asilimia 65) yenye thamani ya Dola za Kimarekani 25,498,100 kati ya magari 777. Magari 270 (sawa na asilimia 35) yenye thamani ya Dola za Kimarekani 4,103,000 yalipatikana kutoka kampuni ya Great Wall Motors ya nchini China.
- b) Kwa Kuongezea, nimebaini magari 314 yenye thamani ya Dola za Kimarekani 7,436,194 yalipatikana bila ya kutathminiwa na Kamati ya Tathmini kulingana na Kanuni ya 90 ya Kanuni za

manunuzi wa Umma ya mwaka 2005 (imefutwa). Pia, Mkataba ulijumuisha Vipuri vya Magari vyenye thamani ya Dola ya Kimarekani 7,105,791 ambavyo aina zake hazikubainishwa kwenye Mkataba. Ilibainika wakati wa ukaguzi kwamba, vipuri vilikuwa vikiletwa kulingana na busara ya mzabuni. Hadi kufikia mwezi Februari 2019, vipuri vya thamani ya Dola za Kimarekani 1,595,362, sawa na asilimia 22.45, vilipokelewa na Jeshi la Polisi la Tanzania bila kuwapo kwa ushahidi wa maombi kutoka Jeshi la Polisi.

- c) Ukaguzi wangu pia ulibaini kuwa mikataba yote iliyosainiwa ilikosa Jedwali la uletaji. Zaidi, muda wa mkataba haukuelezwa bayana katika mkataba wa awali, nyongeza ya mkataba na mkataba wa mwisho uliorekebishwa; Matokeo yake, magari yaliletwa kwa kuchelewa kwa kipindi kisicho cha kawaida. Hadi kufikia Desemba 2018, ni Magari 497 pekee yenye thamani ya Dola za Kimarekani 15,740,961 yalipokelewa na Magari 280 yenye thamani ya Dola za Kimarekani 6,759,648 hayakuletwa; ambapo yalitakiwa kuletwa hadi kufikia Septemba 2014.
- d) Magari yote yaliyoletwa hayakuwa na ripoti za Ukaguzi. Kwa hiyo, hakuna uhakika kwamba magari hayo yalifanyiwa ukaguzi kabla ya kuwasili Bandari ya Dar es Salaam, kinyume na kifungu cha 9 cha Mkataba uliosainiwa. Pia, nilibaini Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) alifanya ukaguzi wa magari yote yaliyopokelewa; ambapo magari 181 yenye thamani ya Dola za Kimarekani 7,447,428 yalikuwa na hitilafu. Hivyo, hakuna uhakika kama magari hayo yalikuwa mapya au la. Aidha, magari 22 yenye thamani ya Dola za Kimarekani 572,506 yalipatikana kuwa na kasoro, na hayakukubaliwa na Jeshi la Polisi la Tanzania.
- e) Pia, ilibainika kwamba magari yote 497 yalitolewa katika Bandari ya Dar es Salaam bila ya Hati ya Kutolea Mzigo kutoka Idara ya Forodha na Ushuru, kinyume na taratibu za Idara ya Forodha na Ushuru CED-702-F. Hiyo pia imesababisha taratibu za bandari kukiukwa na kusababisha madeni ya kodi na ada ya jumla ya Sh.6,858,417,450 na Sh.1,216,824,288 toka Mamlaka ya Mapato na Mamlaka ya Bandari zikiwa ni kodi (Kodi la Ongezeko la thamani na tozo za Bandari) na Ada za Bandari (gharama za

hifadhi na ubebaji), mtawalia. Fedha hizi zilikuwa hazijalipwa na Jeshi la Polisi hadi muda wa ukaguzi mwezi Februari 2019. Ukaguzi wangu wa Mfumo wa forodha na Mfumo wa utoaji wa mzigo pale Mamlaka ya Mapato na Mamlaka ya Bandari imethibitisha magari yaliyotolewa bado yapo chini ya miliki ya Forodha licha ya kuwa yameondolewa kutoka Bandari ya Dar es Salaam.

- f) Manunuzi ya magari 777 yalilenga kutumika wakati wa uchaguzi mkuu wa mwezi Oktoba 2015. Hata hivyo, nilibaini magari 104 tu kati ya 777 yaliletwa hadi kufikia mwezi Oktoba 2015. Magari mengine 393 yaliletwa kati ya mwezi Aprili 2016 na Mei 2018. Hadi kufikia Desemba 2018, nilibaini magari 280 yalikuwa bado hayajaletwa na Mzabuni Ashok Leyland. Kutokana na upungufu wa magari, mnamo mwezi Septemba 2015 Jeshi la Polisi lilipatiwa fedha za ziada jumla ya Sh.42,930,801,479 ili kuunua magari mengine 276 ili kufuta upungufu uliokuwapo hadi kufikia mwezi Oktoba 2015. Hivyo, nimebaini hakuna tija yoyote ya mkopo huu kwa Serikali.

Ununuzi wa magari haya ya Ashok Leyland ulikuwa ni wa gharama kubwa, isiyokuwa na tija na ufanisi. Hivyo, malengo yaliyokusudiwa hayakupatikana.

Kwa suala hili, napendekeza magari 22 yenye thamani ya Dola za Kimarekani 572,506 yaliyopatikana na kasoro na kukataliwa na Jeshi la Polisi yabadilishwe. Magari 280 yenye thamani ya Dola za Kimarekani 6,759,648 na vipuri vya thamani ya Dola za Kimarekani 5,510,429 viletwe mara moja ili kuepuka ongezeko la gharama za kujitolea (commitment charges) za mkopo wa Dola za Kimarekani 13,477,570,30 ambao haujatumiwa. Ninahimiza Serikali daima kuchambua mikopo yote kwa ufanisi na kuachana na mikopo yenye masharti ya kibiashara ambayo inaonekana kuwa ya gharama kubwa. Zaidi, ninahimiza Kamati za Usimamizi wa Madeni za Kitaifa kufanya kazi kitaalum na kutekeleza taratibu zote kama zilivyoainishwa kwenye Sheria ya mikopo ya Serikali, Dhamana na Ruzuku ya Mwaka 1974 (marekebisha ya mwaka 2003) na Kanuni zake.

12.2.7 Ukaguzi Maalum Kuhusiana na Tuhuma za Matumizi Mabaya ya Marejesho ya Mikopo Katika Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF) Tawi la Morogoro

Mnamo tarehe 17 Aprili 2018, Katibu Mkuu Kiongozi aliandika barua yenye Kumbukumbu Na. CAB 218/433 / 01D/ akiniomba kufanya Ukaguzi Maalum juu ya madai yanayohusiana na matumizi mabaya ya fedha katika Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF) Tawi la Morogoro. Tarehe 04 Oktoba 2018 niliagiza Ukaguzi huo kwa mujibu wa Kifungu Na.27 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008.

Ukaguzi wangu katika shughuli za PTF ulilenga tuhuma kwamba kulikuwa na matumizi mabaya ya fedha kuhusiana na utoaji na marejesho ya mikopo. Uchambuzi wa kina wa taarifa za kifedha ulifanyika, ikiwa ni pamoja na uthibitisho kutoka nje. Ukaguzi ulibaini mambo mbalimbali, yakiwamo:

12.2.7.1 Matumizi mabaya ya Fedha Wakati wa Kulipa Marejesho ya Mikopo ya Jumla ya Sh.67,489,000

Nilibaini kumbukumbu za TPF Tawi la Morogoro zinaonesha mikopo iliyotolewa kwa vikundi 26 ya kiasi cha Sh.196,900,000 kwa kipindi kinachozia tarehe 01 Januari 2016 hadi 31 Desemba 2017. Kiasi cha Sh.128,642,800 kimebainishwa kurejeshwa, na kilipokelewa kupitia akaunti ya PTF, Benki ya NMB No.22306600227. Uthibitisho kutoka kwa wajumbe wa vikundi husika ambao ndio walipaji wa mikopo husika ulibainisha kuwa, marejesho ya Sh.196,131,800 ya mikopo yamefanyika hadi kufikia Mwezi Desemba 2017. Hata hivyo, kiasi cha Sh.67,489,000 cha marejesho yaliyothibitishwa na wajumbe hakikubainishwa katika nyaraka za PTF wala kuanishwa kupokelewa Benki. Kutoanishwa kwa kiasi kilichopokelewa na Maafisa wa PTF Tawi kunathibisha ubadhirifu wa fedha hizo Sh.67,489,000.

Namshauri Katibu Mkuu Kiongozi kuhakikisha kuwa Uongozi wa PTF unasimamia kikamilifu urejeshaji wa fedha kiasi cha Sh.67,489,000. Pia, achukue hatua stahiki za kisheria kwa Watumishi husika.

12.2.7.2 Mikopo Iliyotolewa Isiyothibitika Kupokelewa na Walengwa Sh.2,500,000

Nilibaini kuwa, kumbukumbu za PTF Tawi la Morogoro zinaonesha kuwa Kikundi cha wanachama 16 "Nyota na Ing'ae" kilipewa mkopo wa Sh.15,500,000 tarehe 7 Desemba 2016 kupitia akaunti ya Benki ya NMB Na.22110032165. Hata hivyo, nilibaini baadhi yawanachama walipokea mikopo kiasi cha chini ya kile kilichobainishwa katika mfumo wa Fedha wa PTF uitwao "CRDB Finance Solution". Zaidi, nilibaini wanachama wengine walipokea mikopo kiasi kinachozidi kile kilichoidhinishwa, pia wanachama wengine hawakupokea kiasi chochote cha mkopo kilichoidhinishwa.

Wanachama wa kikundi walibaini kuwa, jumla ya Sh.2,500,000 ililipwa kwa Meneja wa PTF Tawi kwa ajili ya marejesho ya ulipaji wa deni la mkopo la nyuma licha ya kuwa Kikundi husika hakikuwahi kuchukua mkopo kabla.

Ninapendekeza Menejimenti ya PTF kupitia mfumo wake wa uendeshaji kwa mtazamo wa kudhibiti uwezekano wa matumizi mabaya ya mikopo.

12.2.7.3 Risiti za Malipo ya Marejesho Zilizopatikana kwa Wakopaji Zisizoainishwa Katika Kumbukumbu za Malipo ya Marejesho ya TPF Kiasi cha Sh.76,560,550

Mwongozo wa Uendeshaji wa PTF unahitaji kutolewa kwa Risiti ya malipo kwa mlipaji kutokana na malipo husika ambapo PTF hubaki na nakala (duplicate) ya risiti halisi. Risiti halisi za malipo yenye thamani ya Sh.76,560,550 zilizotolewa kwa wakopaji wakati wakirejesha mikopo hazikuwepo katika nyaraka/kumbukumbu za PTF. Stakabadhi zilizotolewa kwa Wanachama wa Vikundi wakati wa marejesho zimesainiwa na maafisa wa PTF Tawi, jambo linalothibitisha kuwa maafisa husika walipokea fedha hizo. Hata hivyo, maafisa husika wa PTF tawi la Morogoro hawakuthibitisha wala kukana mapokezi ya fedha za marejesho ya mikopo husika.

Ufafanuzi uliotolewa na maafisa wa PTF kwamba utunzaji wa vitabu vya risiti vya mapato ni mgumu kwa kutokuwa na chumba cha kuhifadha nyaraka hadi kufikia Mwaka 2017, unathibitisha kuwa tatizo hilo halikupewa kipaumbele na Menejimenti ya PTF.

Kutotunzwa wala kunukuliwa kwa kumbukumbu za urejeshwaji mikopo na PTF kunathibitisha ubadhirifu wa fedha husika uliofanywa na Maafisa wa Tawi la Morogoro.

Ninapendekeza Katibu Mkuu Kiongozi kuhakikisha kwamba, kiasi hicho kilichotumika isivyostahili kinarudishwa na hatua stahiki zinachukuliwa.

12.2.7.4 Udanganyifu kwa Kutumia Nyaraka za Wanachama wa Kikundi cha Mkopo Katika Maombi ya Mkopo Sh.15,000,000

Ukaguzi wangu katika nyaraka ulibaini kuwapo kwa udanganyifu wa utambulisho katika nyaraka za maombi ya mikopo ya wanachama 5 wa kikundi cha “Kilakala Kijana Jiajiri”. Nyaraka hizo zilitumiwa na Kampuni ya M / s Mwale Cleaners katika kuomba mkopo wa Sh.15,000,000 uliowekwa katika akaunti ya NMB ya Benki Na.22110042631 chenye marejesho ya Sh.20,062,500 (Mtaji na riba). Watumishi wa Tawi la PTF Morogoro na Mwenyekiti wa Mwale Cleaners Group walihusika katika udanganyifu wa utambulisho, kuidhinisha maombi ya mkopo, na hatimaye, kufanya malipo ya mkopo.

Utoaji wa Mkopo uliofanywa kiudanganyifu kwa Mwale Cleaners unasababisha kukosekana kwa yakini katika urejeshaji wa mkopo huo.

Ninapendekeza Katibu Mkuu Kiongozi kuhakikisha kuwa Uongozi wa PTF unasimamia urejeshaji wa mkopo wa Sh.20,062,500 na kuchukua hatua stahiki kwa waliohusika katika udanganyifu.

12.2.7.5 Kuunda Kikundi Hewa na kupatiwa Mkopo kwa Njia ya Udanganyifu Sh.5, 000,000

Nilibaini kuwa, Uongozi wa Tawi la PTF ulitoa Mkopo wa jumla ya Sh.7,000,000 kwa Wanachama 14 wa kikundi cha “Raha Kikoba” ambacho kilifanya marejesho kikamilifu. Katika kupitia nyaraka zaidi, nilibaini kuwa kulikuwa na utengenezaji wa kikundi hewa cha “Maendeleo Uhuru Two” ambacho kiliundwa kwa kutumia utambulisho wa wanachama kumi (10) wa “Raha Kikoba Group” isivyostahili katika kuomba na kulipa mkopo. Udanganyifu huo ulihusisha kughushi mwandiko, kuiga saine, kubandua na kubandika

picha za Wanachama kumi (10) kutoka “Raha Vikoba” kwenda faili la kikundi cha “Maendeleo Uhuru Two”, ambapo Meneja wa Tawi alihusika.

PTF Makao Makuu ililipa mkopo wa Sh.5,000,000 ulioombwa kupitia Akaunti ya Benki NMB Na. 22110032491 ya Kikundi kiitwacho “Maendeleo Uhuru” (kinachoshabihiana) kwa maelezo ya Meneja wa Tawi kwamba muombaji “Maendeleo Uhuru Two” ni kundi tanzu la “Maendeleo Uhuru” lisilokuwa na Akaunti ya Benki. Baadaye, Meneja wa Tawi aliwajulisha wanakikundi wa “Maendeleo Uhuru” kuhusu kulipwa kimakosa katika akaunti yao ya Benki. Hivyo, kuwataka kutoa kiasi hicho cha pesa taslimu na kukikabidhi kwake ili kilipwe mahala husika, “Maendeleo Bigwa Group”. Hata hivyo, hakukuwa na kumbukumbu zozote za mkopo wa fedha hizo kwenye ofisi za PTF Tawi.

Ninapendekeza menejimenti ya PTF kuhakikisha fedha hizo zinarejeshwa katika Mfuko. Pia, kuchukua hatua za kisheria dhidi ya aliyekuwa Meneja wa tawi la Morogoro kwa kushiriki katika shughuli za ubadhirifu.

12.3 Ukaguzi Wa Vyama Vya Siasa

Nimefanya Ukaguzi wa Vyama vya Siasa kwa mujibu wa Kifungu cha 14(1) (i) cha Sheria za Vyama vya Siasa Na.5 ya mwaka 1992 (iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2015) ili kuongeza kiwango cha kujiamini kwa wadau waliokusudiwa. Ukaguzi wangu umehusisha taratibu za kupata ushahidi kuhusu kiasi na ufafanuzi wake kama ilivyooneshwa kwenye Taarifa za Fedha, kutathmini ufanisi wa sera za uhasibu zilizotumika, na uwazi wa makadirio ya hesabu.

Nimezingatia mifumo wa udhibiti ya ndani katika uandaji wa Taarifa za Fedha za Vyama vya Siasa na kubuni miongozo mbalimbali iliyoniwezesha kufanya Ukaguzi; na wala sio kutoa Maoni kuhusu ubora wa Mifumo ya udhibiti wa ndani wa Vyama vya Siasa. Wakati wa Ukaguzi wangu, nilibaini masuala muhimu ambayo yamefupishwa hapa chini:

12.3.1 Kutowasilishwa Kwa Taarifa za Fedha kwa ajili ya Ukaguzi

Kifungu cha 14 cha Sheria ya Vyama vya Siasa Na. 5 ya Mwaka 1992 (Iliyofanyiwa marekebisho Mwaka 2015) kinataka kila Chama cha Siasa kilichosajiliwa kuhifadhi Mahesabu ya fedha na Mali za Chama na kuwasilisha Taarifa za Fedha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa ili Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali afanye ukaguzi.

Wakati wa Ukaguzi wangu wa Vyama vya Siasa, sikupokea Taarifa za Fedha kutoka Vyama vya Siasa vinne (4) kati ya Kumi na Tisa (19) vyenye usajili wa kudumu; kinyume na matakwa ya kifungu 14(1) cha Sheria ya Vyama vya Siasa Na. 5 ya Mwaka 1992 (iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2015). Hivyo basi, sina uhakika Fedha zilizopokelewa kutoka kwa wanachamana au Serikalini zilitumika ipasavyo. Vyama hivyo ni NRA, ADC, Demokrasia Makini na TLP. Kuhusu CUF, nilipokea Taarifa za Fedha, lakini sikuweza kufanya Ukaguzi kwa sababu ya migogoro iliyopo ndani ya chama hicho inayosubiri maamuzi kutoka mahakamani.

Nimebaini kuwa, hakuna uboreshaji katika eneo hili, kwani Vyama vya Siasa ambavyo havikuwasilisha Taarifa za Fedha mwaka huu ni vile vile ambavyo havikuwasilisha mwaka uliopita.

Kwa hiyo, nasisitiza Uongozi wa Vyama vya Siasa kuwasilisha Taarifa za Fedha kwa ajili ya Ukaguzi. Kwa, Vyama visivyozingatia kuwasilisha Taarifa za Fedha, nasisitiza Msajili wa Vyama vya Siasa kuvilazimisha kufuata sheria na kuvichukulia hatua zinazostahili kulingana na Mamlaka yaliyotajwa katika Sheria ya Vyama vya Siasa Na. 5 ya mwaka 1992 (iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2015).

12.3.2 Hakuna Nyaraka za Kuthibitisha Mkopo wa Sh.147,760,080 (Dola za Kimarekani 63,720)

Mnamo tarehe 30 Machi 2017, Bodi ya Wadhamini ya Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) iliingia Mkataba na Kampuni ya AMC Tanzania Limited kwa ajili ya ununuzi wa gari jipya aina ya Nissan Patrol Y61 Series yenye moduli ya GRX kwa bei ya Dola za Kimarekani 63,720 (sawa na Sh.147,760,080). Kifungu cha 1 cha Mkataba uliosainiwa kilitamka gari litakalonunuliwa lisajiliwe kwa jina la Bodi

ya Wadhamini ya CHADEMA. Hata hivyo, gari hilo lilisajiliwa kwa jina la Mbunge, kinyume na Sharti la 1 la Mkataba uliosainiwa.

Vilevile, nilipitia Rejista ya Mali za Chama na kubaini hakukuwa na kumbukumbu za gari aina ya Nissan Patrol Y61 Series yenye Moduli ya GRX kwenye Rejista ya Mali za Chama, licha ya gari hilo kutumika na CHADEMA. Zaidi ya hayo, gari lililonunuliwa liliingizwa kwenye Taarifa za Fedha za Chama kama Mkopo uliotolewa kwa Mbunge bila ya makubaliano yoyote kati ya Mbunge na Bodi ya Wadhamini wa CHADEMA.

Aidha, nilibaini kuwapo kwa mawasiliano ya barua kati ya Mbunge na CHADEMA kuhusu kusitishwa kwa Mkataba wa Mkopo na urejeshwaji wa gari hilo. Jambo hili lilitokea mapema tu baada ya kutoa hoja ya Ukaguzi. Hata hivyo, wakati wa ukaguzi wangu Februari 2019, Mkataba wa Mkopo huo haukuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.

Maoni yangu ni kwamba, kuonesha thamani ya gari kama mkopo kwa Mbunge kunapotosha watumiaji wa Taarifa za Fedha za chama.

Kwa mantiki hiyo, usajili wa gari husika ufanyike kwa jina la mmiliki ambaye ni Bodi ya Wadhamini wa CHADEMA na deni hili liondolewe kwenye Taarifa za Fedha za chama.

12.3.3 Hakuna Uthibitisho wa Nyaraka za Magari ambayo Hayajapokelewa Kutoka Nje ya Nchi ya Thamani ya Sh.172,227,083

Nimepitia Taarifa za Fedha zilizowasilishwa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na kubaini Magari yenye thamani ya Sh.172,227,083 hayajapokelewa kutoka nje ya nchi wakati wa Ukaguzi wangu mwezi wa Januari 2019. Aidha, niliomba nyaraka za manunuzi na uagizaji wa magari hayo ili kujiridhisha kama magari hayo yapo lakini hakuna nyaraka zilizowasilishwa kuthibitisha ununuzi wa magari hayo.

Kutokana na kutokuwapo kwa nyaraka za manunuzi, nilishindwa kuthibitisha idadi ya magari yaliyonunuliwa, taratibu za manunuzi zilizotumika na kama CHADEMA ni wamiliki halali wa magari hayo kwa gharama zilizotajwa.

Kuhusiana na jambo hili, nakishauri CHADEMA kufuata taratibu za manunuzi na kuhifadhi nyaraka zake za manunuzi.

12.3.4 Michango ya Unachama ya Jumla ya Sh 3,741,358,870.97 Haijawaasilishwa kwenye Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na Umoja wa Wanawake (UWT)

Kwa mujibu wa Kifungu cha 14(1) na (3) cha Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii Na. 28 ya Mwaka 1997, Mwajiri anapaswa kulipia michango ya wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii ndani ya kipindi cha mwezi mmoja toka mwezi wa uchangiaji kupita. Kushindwa kuwasilisha kwa wakati kutasababisha adhabu ya asilimia tano (5) kwa mwezi.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa, michango ya wanachama ya kila mwezi iliyokatwa kutoka kwenye mishahara ya wanachama wa NSSF haikuwasilishwa na UWT kwenye Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii, kinyume na Kifungu 14 (1) cha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Na. 28 ya Mwaka 1997. Hadi kufikia Mei 2018, UWT kulikuwa na madeni ya jumla ya Sh.3,741,358,870.97 yakiwamo madeni ya adhabu ya jumla ya Sh.2,730,509,964.73 yaliyosababishwa na ucheleweshaji wa uwasilishaji wa michango ya Wanachama. Kwa maoni yangu, kutokuwapo kwa ufuatiliaji kuhusu uwasilishaji wa michango ya Wanachama kwa wakati kumesababisha riba na adhabu kuwa kubwa.

Suala hili sio tu linapotosha taswira ya chama bali, pia linaweza kuondoa ari ya kufanya kazi kwa wafanyakazi; na linaweza kusababisha changamoto wakati wa kupokea mafao ya mwisho ya kustaafu.

Ninapendekeza UWT kulipa madeni yote ya Mfuko wa Taifa ya hifadhi ya Jamii. Aidha, Katibu Mkuu wa CCM aendelee kujenga utamaduni wa kulipa michango kwa wakati ili kuzuia mkusanyiko wa ada na adhabu.

12.3.5 Udhaifu Uliobainishwa kwenye Mradi wa Uwekezaji wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT)

Mnamo tarehe 09 Februari 2007, Bodi ya Wadhamini ya Umoja wa Wanawake (UWT) ya Chama cha Mapinduzi (CCM) iliingia Mkataba wa Ukodishaji wa ardhi na mwekezaji Manji Holdings Limited kwa ajili ya

kuendeleza mradi wa ujenzi (hivi sasa ZANRAN TOWER) kwenye ardhi yake iliyopo Kitalu Na. 41, Mtaa wa Morocco, Kinondoni, Dar es Salaam, chenye Hati ya Umiliki Na. 186158/45. Kwa mujibu wa Mkataba huu, kipindi cha ukodishaji kilikubalika kuwa miaka thelathini na tatu (33) itakayoanza Mwezi Julai 2009 na kumalizika Mwezi Novemba 2042. Mara baada ya muda wa Ukodishaji kumalizika, mradi huo utarudishwa kwa mmiliki (UWT) au kuingia makubaliano mapya na Mwekezaji. Pia, ilikubalika kuwa mwekezaji (Manji Holdings Limited) atalipa kodi ya upangishaji ya jumla ya Dola za Kimarekani 200,000 kwa mwaka. Kodi hiyo italipwa mapema kila robo ya mwaka kuanzia tarehe 1 Desemba 2009 na kuongezeka kwa asilimia 10 kwa mwaka kwa kipindi cha miaka mitano; na kama kodi hiyo haitalipwa kwa wakati uliopangwa, riba ya asilimia 10 itatozwa kwa mujibu wa Kifungu cha 7(b na c) cha Mkataba wa ukodishaji. Wakati wa Ukaguzi wangu nilibaini yafuatayo:

a) Kodi ya upangishaji haikurekebishwa na kusababisha hasara ya Sh.230,000,000

Kulingana na Kifungu cha 7 (b) cha Mkataba wa Ukodishaji, malipo ya kukodisha yalipaswa kuongezeka kwa asilimia 10 mnamo Mwezi Desemba 2014. Hata hivyo, wakati wa Ukaguzi wangu mwezi wa Desemba 2018, nilibaini hakukuwa na marekebisho ya kodi yaliyofanywa kati ya UWT na Mwekezaji; hivyo, kusababisha kupotea kwa mapato ya Dola za Kimerakani 100,000 (sawa na Sh.230,000,000).

b) Mapato ya Dola za Kimarekani 10,000 (sawa na Sh.23,000,000) Yatokanayo na Ada ya Ucheleweshaji ya Asilimia 10 kwa Kipindi cha Miaka Mitano hayakukusanywa

Kwa kuwa makubaliano ya kukodisha hayakurejewa tena na ongezeko la kodi la asilimia 10 halikulipwa. Hivyo, wakati wa ukaguzi wangu nimebaini kwa muda wa miaka mitano kiasi cha Dola za Kimarekani 100,000 hazikulipwa na kupokelewa na Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) hivyo kusababisha hasara ya kiasi kilichotajwa .

c) Vigezo vya Ukokotoaji wa Kodi ya Pango ya Dola za Kimarekani 200,000 kwa Mwaka (sawa na Sh.460,000,000) havikubainishwa

Vigezo vya ukokotoaji wa kodi ya pango havikubainishwa kwenye Mkataba wa upangishaji kati ya UWT na Mwekezaji Manji Holdings Limited. Hivyo, kodi ya upangishaji kwa mwaka ya Dola za Kimarekani 200,000 haikuweza kupimwa wakati wa Ukaguzi. Aidha, nilibaini mawasiliano ya barua kati ya UWT na Mwekezaji Manji Holdings Limited kuhusu marekebisho ya kodi ya upangishaji. Mwekezaji aliomba makubaliano hayo kukamilika mwaka 2017. Hata hivyo, hakuna makubaliano yoyote yaliyofanyika mpaka wakati wa Ukaguzi wangu Mwezi Desemba 2018.

d) Ukosefu wa Alama ya Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Kwenye Mkataba wa Ukodishaji

Mkataba wa Ukodishaji na Mradi wa jengo hauoneshi alama ya UWT ikilinganishwa na alama zilizowekwa za Mwekezaji Manji Holdings Limited na za mrithi wake ZANRAN Tower. Hata hivyo, Bodi ya Wadhamini ya Umoja wa Wanawake ilipendekeza kuwekwa kwa alama ya UWT. Mpaka kipindi cha uandishi wa ripoti yangu, Desemba 2018, alama ya UWT ilikuwa haijawekwa.

Maoni yangu ni kwamba, UWT ilikosa weledi wakati wa kufanya makubaliano ya kimkataba; hivyo, kuingia kwenye makubaliano yenye utata yaliyosababisha hasara ambayo ingeweza kuepukika.

Nashauri uongozi wa UWT na CCM kwa ujumla kufanya mashauriano mengine ya kikodi na kuingia makubaliano mapya yatakayounda ushirikiano wa pamoja wa kibiashara ambao utaleta manufaa sawa pande zote.

12.3.6 Kuwapo kwa Matatizo ya Ustamihilivu wa Kibiashara kwenye Kampuni ya Uhuru Publication Limited

Mapitio ya Taarifa za Fedha za Kampuni ya Uhuru Publication Limited, inayomilikiwa na Chama cha Mapinduzi (CCM) yamebaini kuwapo kwa matatizo stamihilivu ya kibiashara yanayohitaji kushughulikiwa. Kulingana na Mfumo wa Kihisibu, Taarifa za Fedha huandaliwa kwa dhana ya muendelezo wa shughuli za kibiashara, pamoja na kufuata

matakwa ya kisheria kwa kipindi kisichotabilika. Ukaguzi ulibaini matatizo yafuatayo:

a) Kupungua kwa Mwenendo wa Mapato Yaliyoripotiwa kwa Kipindi cha Miaka Mitatu (3) Mfululizo

Ukaguzi wangu wa Taarifa za Fedha kwa Miaka Mitatu kuanzia mwaka 2016 mpaka mwaka 2018 umebaini kupungua kwa uwezo wa kifedha kwenye kampuni ya Uhuru Publication Limited uliotokana na kupungua kwa mauzo, mapato ya matangazo na mapato mengine ya uendeshaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la hapo chini.

Jedwali Na. 94: Mwenendo wa Mauzo kutoka Mwaka 2016 to 2018

Maelezo	Mwaka 2016	Mwaka 2017	Mwaka 2018
Mauzo	502,196,091	341,426,133	264,807,046

Chanzo: Taarifa za mauzo na hesabu za mwaka 2016 mpaka Mwaka 2018

Kushuka kwa mapato kuna athari mbaya juu ya utendaji na uendelevu wa huduma muhimu.

b) Ongezeko la Gharama za uendeshaji Halifungamani na Mapato Yaliyotarajiwa

Kulingana na ukaguzi wangu wa Taarifa za utendaji, nimebaini kuwa Uhuru Publication Limited imekuwa ikifanya biashara kwa gharama kubwa ikilinganishwa na mapato yaliyopatikana kwa zaidi ya miaka mitatu; hivyo kusababisha nakisi ya muda mrefu kama ilivyooneshwa hapo chini:

Jedwali Na. 95: Mwenendo wa gharama za uendeshaji kutoka Mwaka 2016 mpaka 2018

Maelezo	Mwaka 2016	Mwaka 2017	Mwaka 2018
Matumizi yaliyoripotiwa Sh.	1,207,691,070	1,021,478,217	953,282,894
Hasara iliyoripotiwa Sh.	657,157,950	914,636,427	1,345,375,725

Chanzo: Taarifa za hesabu za mwaka 2016 mpaka 2018

Kutokana na mikakati dhaifu ya mauzo na masoko, mapato yamekuwa yakipungua kwa kiasi kikubwa; na hakuna fedha za kutosha

zinazozalishwa. Hivyo, wazabuni hawalipwi kwa wakati, na hakuna imani kutoka kwenye Taasisi za Fedha.

Nashauri uongozi wa CCM kuongeza mtaji ikiwa ni pamoja na kuandaa mikakati ya mauzo na masoko yenye ushindani ili kuweza kupata mafanikio tarajiwa ya kimasoko.

12.3.7 Majengo ya CCM Yanayomilikiwa kwa Majina ya Mwanachama

Ukaguzi wa Hati Miliki za majengo mbalimbali yaliyo chini ya miliki ya Chama cha Mapinduzi (CCM) huko Zanzibar ulionesha jumla ya nyumba 199 hazikusajiliwa kwa jina la Bodi ya Wadhamini wa CCM. Majengo hayo yalitambuliwa kwa majina ya maafisa wa chama badala ya jina la mmiliki ambaye ni Bodi ya Wadhamini.

Kwa hali hii, ikiwa hakuna hatua madhubuti zitakazotumika kufanya uhamisho wa majina, kuna uwezekano mkubwa wa majengo haya kumilikiwa na maafisa wa Chama bila Bodi ya Wadhamini kuwa na taarifa. Hii ni kwa sababu, Chama hakina Hati Miliki katika kuthibitisha umiliki wa majengo hayo. Aidha, endapo chama kitaingia kwenye migogoro, kuna uwezekano wa kupoteza majengo haya.

Kwa uzito mkubwa, ninapendekeza kwa Katibu Mkuu wa CCM kuanzisha hatua za haraka za kuhakikisha majina ya wanachama yaliyopo kwenye Hati Miliki za Majengo ya Chama yanabadilishwa na kusajiliwa kwa jina la Bodi ya Wadhamini.

12.3.8 Mapato Yasiyokusanywa Sh.1,457,173,050

Nilibaini kwamba CCM ina Majengo mbalimbali na vyanzo vingi vya mapato. Hadi kufikia Mwezi Juni 2018, jumla ya Sh.1,457,173,050 zilikuwa hazijakusanywa na CCM kutoka vyanzo mbalimbali nchi nzima. Zaidi, nimebaini kuwa hakuna utaratibu wa kutosha uliowekwa na Uongozi ambao ungesaidia ufuatiliaji na ukusanyaji wa mapato kwa wakati kutoka kwa wapangaji. Hali hii, sio tu inazorotesha hali ya kifedha, bali pia inapunguza fedha za uendeshaji Chama.

Hali hii inaweza kusababisha upungufu wa mapato. Hivyo, kusababisha shughuli za chama kutokamilika kama ilivyopangwa kwenye mpango kazi wa mwaka.

Uongozi wa CCM unashauriwa kuanzisha mfumo madhubuti ambao utahakikisha mapato yanakusanywa kwa wakati na kupunguza mwanya wa madeni sugu. Pia, hatua za kisheria zinapaswa kuchukuliwa dhidi ya wapangaji walioshindwa kulipa madeni yao.

12.3.9 Taratibu za Manunuzi hazikufuatwa wakati wa Ununuzi wa Huduma za Uchapishaji Sh.524,777,538

Mapitio yangu ya taratibu za Manunuzi ya Uhuru Publications Limited yalibaini kwamba, Kampuni ya FG Flint Graphics na Kill Deep Sea & Printing Services zililipwa jumla ya Sh.423,533,538 na Sh.101,244,000 ikiwa ni gharama za uchapishaji wa Magazeti ya Uhuru na Mzalendo. Nilithibitisha kuwa hakukuwa na Mkataba rasmi ulioingiwa kati ya Uhuru Publications Limited na FG Flint Graphics Company Limited.

Vilevile, Makubaliano na Kampuni ya Kill Deep Sea Printing Service hayakusainiwa wakati wa utoaji huduma Mwezi Mei 2018; badala yake, Mkataba ulisainiwa tarehe 3 Novemba 2018 miezi mitano (5) baadaye baada ya huduma kutolewa.

Kushindwa kufuata taratibu za ushindanishaji wa Zabuni kumesababisha Uhuru Publications Limited kukosa fursa ya kupata huduma au bidhaa bora; na wakati mwingine, kupata huduma iliyo chini ya kiwango.

Ninapendekeza kuwa, Katibu Mkuu CCM afuate taratibu za Manunuzi ya Umma wakati wa kufanya Manunuzi ili kupata thamani halisi ya fedha kwa kila manunuzi yatakayofanyika; hivyo, kujenga imani kwa wanachama.

12.3.10 Kukosena kwa Rejista ya Kuhifadhi Kumbukumbu za Mali ya Chama

Nilipitia usimamizi wa Mali za Vyama na kubaini kuwa Vyama vitano (5) (CCM³⁵, UDP, UPDP, CKK na African Democratic Alliance (ADA-TADEA)) havina Rejista ya kutunza kumbukumbu za Mali za Chama. Hii ni kinyume na Kifungu 14 (1) (b) (ii) cha Sheria ya Vyama vya Siasa Na. 5 ya mwaka 1992 (iliyorekebishwa Mwaka 2015) ambayo inataka

³⁵ Ofisi za CCM wilaya ya Ilala, Nyamagana, mkoa wa Mwanza, UVCCM (Makao Makuu), Zanzibar mjini, mkoa wa Mtwara, mkoa wa Ruvuma, Afisi Kuu Zanzibar, Afisi Mkoa wa Mjini na wilaya ya Urambo.

kila Chama cha Siasa kilichosajiliwa kuhifadhi na kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa tamko la Mali za Chama kila Mwaka.

Maoni yangu ni kwamba, kutokuwapo kwa kumbukumbu ya Rejista za Mali za Vyama vya Siasa kunaweza kuleta hatari ya wizi au matumizi mabaya ya mali zinazomilikiwa bila Uongozi wa juu kuwa na taarifa.

Ninapendekeza Vyama vya Siasa vilivyohojiwa kuweka kumbukumbu ya Rejista ya Mali kwajili ya kuweka Taarifa za Mali za Chama na Kukidhi Masharti ya Kifungu 14 (1) (b) (ii) ya Sheria ya Vyama vya Siasa Na.5 ya 1992 (iliyofanyiwa Marekebisho Mwaka 2015).

12.3.11 Matumizi Yenye Nyaraka Pungufu Sh.777,910,739.72

Wakati wa ukaguzi wangu wa usimamizi wa matumizi, nilibaini vyama vya siasa saba (7) vilifanya matumizi ya jumla ya Sh.777,910,739.72 bila kuwepo kwa nyaraka za kutosha, kinyume na mahitaji ya Kanuni 86 (1) na 95 (4) ya Kanuni za Fedha za Umma za Mwaka 2001. Hivyo, nimeshindwa kuthibitisha kama malipo hayo yalikuwa sahihi, yalitokea, au yalikuwa kamilifu, na yalihusu shughuli za kisiasa za chama. Orodha ya Vyama vya Siasa na malipo yenye nyaraka pungufu yameonyeshwa kwenye jedwali la 1 hapa chini:

Jedwali Na. 96: Orodha ya vyama vya siasa vyenye matumizi yenye nyaraka pungufu

Na.	Jina la Chama cha Siasa	Kiasi (Sh.)
1	CKK (Chama cha Kijamii)	10,948,800
2	CHADEMA (Chama cha Demokrasia na Maendeleo)	134,646,740
3	AAFP (Alliance for Africa Farmers Party)	9,475,000
4	Chama Cha Sauti ya Umma (SAU)	7,404,205
5	Union for Multiparty Democracy (UMD)	3,370,000
6	CCM ³⁶ (Chama cha Mapinduzi)	604,996,994.72

³⁶ Ofisi ya CCM; Mkoa wa Njombe Sh. 25,668,000, Ruvuma Sh. 96,922,000, Wilaya ya Njombe Sh. 13,832,000, Mtwara Sh. 20,523,350, Lumumba Sh. 429,419,044.72, na UWT Sh. 18,632,600.

Na.	Jina la Chama cha Siasa	Kiasi (Sh.)
7	Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA)	7,069,000
	Jumla	777,910,739.72

Chanzo: Taarifa ya Mapungufu ya Mwaka 2017/2018

Kuhusiana na suala hili, ninapendekeza Vyama vya Siasa kuhakikisha kwamba kila matumizi yatakayotumika yanathibitishwa kwa nyaraka ili kupata uhakika na usahihi wa matumizi hayo kama masharti ya kanuni 86 (1) & 95 (4) ya Kanuni za Fedha za Umma za Mwaka 2001 yalivyoainishwa.

12.3.12 Matumizi Yaliyofanyika bila ya Kuomba na Kuhifadhi Risiti za Kielektroniki Sh.85,168,705

Nilipitia kiwango cha ufuatiliaji wa Sheria na taratibu za kodi na kubaini kuwa, CCM, CHADEMA na ACT Wazalendo havikuomba na kuhifadhi risiti za kielektroniki za jumla ya Sh.85,168,705³⁷ kwa Mwaka wa fedha 2017/2018 na kutoka 2015/2016 hadi 2017/2018. Hii ni kinyume na mahitaji ya Kanuni 24 na 28 (1) ya Kanuni ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2012 (Vifaa vya Risiti za Kielektroniki). Aidha, maoni yangu ni kwamba vitendo vinavyofanywa na Vyama vya Siasa vya kutozingatia taratibu na kukwepa kodi vinapunguza mapato ya serikali.

Nashauri Vyama vya Siasa vilivyotajwa kuomba na kuhifadhi risiti za kielektroniki kama inavyotakiwa na Kanuni 24 na 28 (1) ya Kanuni za Kodi ya Mapato ya Mwaka 2012 (Vifaa vya risiti za kielektroniki).

12.3.13 Mikutano ya Bodi ya Wadhamini Haikufanyika

Nimepitia miongozo ya Bodi ya Wadhamini (Trustee deed) ya Vyama vya Kisiasa kumi na vinne (14) vilivyokaguliwa na kubaini kuwa idadi ya mikutano iliyotamkwa kwenye muongozo wa Bodi ya Wadhamini ya ACT Wazalendo haikutimizwa; kwani ni mkutano mmoja tu (1) kati ya mikutano minne (4) ulifanyika. Aidha, nimebaini, kuwa hakukuwa na mkutano wa Bodi ya Wadhamini wa Chama cha CCK tangu kiliposajiliwa. Nilibaini pia Chama cha SAU bado hakijasajili Bodi ya

³⁷ CCM (Mtwara), Sh. 19,820,000, CHADEMA, Sh. 44,347,177 na ACT Wazalendo Sh. 21,001,550

Wadhamini. Hii ni kinyume na mahitaji ya Kifungu 21 cha Sheria ya Vyama vya Kisiasa Na. 5 ya 1992 (iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2015) ambayo inahitaji kila Chama cha Siasa kilichosajiliwa na kupewa hati ya usajili wa kudumu kuteua Bodi ya Wadhamini kwa ajili ya usimamizi wa mali na biashara au uwekezaji wa Chama.

Maoni yangu ni kuwa, mikutano pungufu iliyofanywa na Bodi za Wadhamini za Vyama inapunguza fursa ya maamuzi kutoka ngazi za juu za chama kuhusu uwekezaji na masuala mengine yanayohusu chama kwa ujumla.

Napendekeza Bodi za Wadhamini za Vyama vya Siasa kufanya mikutano ipasavyo kama ilivyoelezwa kwenye miongozo yao ili kuleta ufanisi katika usimamizi wa Vyama vya Siasa.

12.3.14 Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha zenye Mapungufu

Ukaguzi wangu wa Vyama vya Siasa ulibaini kuwa, Taarifa za Fedha za SAU, UPDP, UMD, ADA (TADEA), NLD na AAFP zina kiwango cha juu cha kutofautiana na Mfumo wa uandaaji wa Hesabu za Umma Kwa Viwango vya Kimataifa (IPSAS conceptual framework).Ufuatao ni udhaifu uliobainika:

- c) Taarifa za Kifedha zilizopokelewa zilikuwa na mapungufu, kwani taarifa zinazohusiana na mizania, ufanisi, mtiririko wa fedha na bajeti hazikuwasilishwa.
- d) Taarifa za kifedha zilizowasilishwa zilitoa maelezo juu ya Mapato na Matumizi bila ya kuonesha msingi wa uandaji kama ulifuata mfumo wa Kihisibu wa uandaaji wa hesabu.
- e) Hakukuwa na Sera za Uhasibu na maelezo juu ya taarifa za mapato na matumizi hivyo, kupunguza uelewa kwa watumiaji.
- f) Hakukuwa na chati ya vifungu vya Taarifa za Fedha zilizoandaliwa. Hivyo, vitabu vya mahesabu havikutayarishwa kwa kufuata mzunguko wa taratibu za kiuhasibu.

Ripoti yangu inaonyesha kuwa idadi ya Vyama vya Siasa ambavyo havikuandaa taarifa kamili za kifedha kwa kufuata mfumo wa uandaaji wa hesabu za umma kwa viwango vya kimataifa zimepungua kutoka Vyama vya Siasa saba (7) hadi kufikia sita (6) mwaka huu.

Nimebaini uboreshaji mdogo kwa Vyama vya Siasa kuhusiana na suala hili.

Taarifa za Kifedha zilizotolewa kwa watumiaji zinatoa taarifa pungufu kuhusiana na ugawaji wa rasilimali zilizotolewa na wanachama wa vyama vya siasa.

Hivyo, ninahimiza sana Vyama vya Siasa kuandaa taarifa kamili za kifedha kwa kufuata Mfumo wa Kimataifa wa Uandaaji wa Hesabu za Umma ili kutoa uwajibikaji sahihi wa rasilimali zilizotolewa na wanachama.

12.3.15 Taarifa za Mwaka za Wajumbe wa Bodi ya Wadhamini Hazijawasilishwa kwa Kabidhi Wasihi (RITA)

Ukaguzi wangu wa mwaka wa mawasilisho ya taarifa za wajumbe wa Bodi ya Wadhamini, ilibaini kuwa chama cha UPDP, UDP na CCK havijawahi kufanya mawasilisho ya taarifa za wajumbe wa Bodi ya Wadhamini kwa Kabidhi Wasihi (RITA) kwa muda wa miaka tisa (9), kumi na nane (18) na miaka miwili (2), mtawalia, tangu tarehe ya kupata cheti za kudumu cha usajili wa Bodi ya Wadhamini. Hii ni kinyume na Kifungu cha 16(3) cha Sheria ya Usajili wa Bodi wa Wadhamini Sura 318 (iliyorekebishwa mwaka 2002) ambayo inahitaji kila Bodi ya Wadhamini yenye usajili kufanya mawasilisho ya taarifa za wajumbe wa Bodi ndani kwa kipindi cha mwezi mmoja mara baada ya kumalizika kwa muda wa miezi kumi na miwili tangu tarehe ya utoaji wa Cheti cha Usajili wa Bodi.

Kutokana na kushindwa kuwasilisha taarifa za Wajumbe wa Bodi ya Wadhamini, Kabidhi Wasihi (RITA) atachelewesha kufanya maboresho kwenye Rejista ya Bodi ya Wadhamini ikiwa maboresho hayo yataokea.

Hivyo, ninahimiza Vyama vya Siasa vyote vilivyosajiliwa kufuata matakwa ya Kifungu 16(3) ya Sheria ya Usajili wa Bodi ya Wadhamini Sura 318 (iliyorekebishwa mwaka 2002) kwa kuwasilisha taarifa za Wajumbe kwa Kabidhi Wasihi (RITA) kwa wakati. Mawasilisho ya taarifa hizo kwa wakati yatamwezesha Kabidhi Wasihi (RITA) kufanya maboresho wakati wowote yatakapojitokeza.

12.3.16 Hakuna Nyaraka za Kuthibitisha Madeni na Madai Mengine Jumla ya Sh.85,366,000

Kwa mujibu wa Kifungu 4.1 cha Mwongozo wa fedha wa Chama cha NCCR Mageuzi, kila shughuli za fedha zilizoelekezwa katika Taarifa za Fedha zinapaswa kuwa na nyaraka za chanzo. Katika mwaka huu wa ukaguzi, nilibaini kuwa Madeni na Madai mengine ya jumla ya kiasi cha Sh.85,366,000 yalitajwa katika Taarifa za Fedha bila kuwapo kwa nyaraka za kuthibitisha bakaa iliyoripotiwa. Hii ni kinyume na mahitaji ya Kifungu cha 4.1. Hivyo, nimeshindwa kuthibitisha uhalali wa madeni na madai yaliyotajwa kutokana na NCCR Mageuzi kushindwa kutoa nyaraka za chanzo. Mbali na hilo, hakuna jedwali la mchanganuo wa umri wa madeni liliohifadhiwa kwa ajili ya uainishaji wa bakaa za madeni kwa kufuata umri ili kurahisisha ufatiliaji na malipo kwa wakati.

Katika hali hii, matumizi yaliyofanywa hayakuweza kuthibitishwa. Kitendo hiki kinapotosha Taarifa za Kifedha, na kinaashiria mapungufu katika kuhifadhi kumbukumbu.

Kuhusiana na suala hili, napendekeza Uongozi wa Chama cha NCCR Mageuzi kuhifadhi kumbukumbu za nyaraka za kifedha kwa kila Muamala wa Kifedha unaotokea. Pia, kianzishe jedwali la umri wa madeni kwa urahisi wa uainishaji na malipo kwa wakati.

Viambatisho

13.1 Viambatisho - Sura ya Pili

Kiambatisho Na. 1: Orodha ya Taasisi Zenye Hati Zinazoridhisha

Na.	Jina	Fungu Na.	2017/18	2016/17	2015/16
1	Ofisi ya Rais - Bodi ya Mishahara ya Watumishi wa Umma	9	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
2	Tume ya Huduma za Mahakama	12	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
3	Kitengo cha Uchunguzi wa Fedha	13	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
4	Jeshi la Zimamoto na Uokoaji	14	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
5	Tume ya Usuluhishi na Maridhiano	15	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
6	Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali	16	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
7	Ofisi ya Rais - Ikulu	20	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
8	Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali	23	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
9	Tume ya Maendeleo na Ushirika	24	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
10	Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu	25	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
11	Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais	26	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
12	Msajili wa Vyama vya Siasa	27	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
13	Idara ya Huduma za Magereza	29	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
14	Ofisi ya Rais - Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri	30	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
15	Huduma ya Taifa ya Mashtaka	35	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
16	Sekretarieti ya Mkoa wa Katavi	36	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
17	Ofisi ya Waziri Mkuu	37	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
18	Jeshi la Wananchi wa Tanzania (TPDF)	38	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
19	Bunge la Tanzania	42	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha

Na.	Jina	Fungu Na.	2017/18	2016/17	2015/16
20	Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji	44	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
21	Sekretarieti ya Mkoa wa Simiyu	47	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
22	Wizara ya Maji na Umwagiliaji	49	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
23	Wizara ya Fedha na Mipango	50	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
24	Ministry of Home Affairs	51	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
25	Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora	55	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
26	Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa	56	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
27	Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania	59	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
28	Tume ya Taifa ya Uchaguzi	61	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
29	Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu	65	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
30	Ofisi ya Rais Tume ya Mipango	66	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
31	Ofisi ya Rais - Sekretarieti ya Ajira	67	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
32	Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano	68	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
33	Tume ya Kuzuia Ukimwi	92	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
34	Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo	96	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
35	Sekretarieti ya Mkoa wa Pwani	71	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
36	Sekretarieti ya Mkoa wa Dodoma	72	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
37	Sekretarieti ya Mkoa wa Iringa	73	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
38	Sekretarieti ya Mkoa wa Lindi	76	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
39	Sekretarieti ya Mkoa wa Mara	77	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
40	Sekretarieti ya Mkoa wa Morogoro	79	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
41	Sekretarieti ya Mkoa wa Mtwara	80	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha

Na.	Jina	Fungu Na.	2017/18	2016/17	2015/16
42	Sekretarieti ya Mkoa wa Shinyanga	83	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
43	Sekretarieti ya Mkoa wa Singida	84	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
44	Sekretarieti ya Mkoa wa Dar es Salaam	88	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
45	Ubalozi wa Tanzanian Nchini Ethiopia	2001	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
46	Ubalozi wa Tanzanian Nchini Ujerumani	2002	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
47	Ubalozi wa Tanzanian Nchini DRC, Congo	2004	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
48	Ubalozi wa Tanzanian Nchini Uingereza	2006	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
49	Ubalozi wa Tanzanian Nchini Urusi	2009	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
50	Ubalozi wa Tanzanian Nchini India	2010	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
51	Ubalozi wa Tanzanian Nchini Canada	2012	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
52	Ubalozi wa Tanzanian Nchini China	2014	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
53	Ubalozi wa Tanzanian Nchini Italia	2015	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
54	Ubalozi wa Tanzanian Nchini Swiden	2016	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
55	Ubalozi wa Tanzanian Nchini Japan	2017	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
56	Ubalozi wa Tanzanian Nchini Uganda	2021	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
57	Ubalozi wa Tanzanian Nchini Zimbabwe	2022	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
58	Ubalozi wa Tanzanian Nchini Kenya	2023	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha

Na.	Jina	Fungu Na.	2017/18	2016/17	2015/16
59	Ubalози wa Tanzanian Nchini Saudi Arabia	2024	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
60	Ubalози wa Tanzanian Nchini Afrika Kusini	2025	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
61	Ubalози wa Tanzanian Nchini Rwanda	2026	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
62	Ubalози wa Tanzanian Nchini Umoja wa Falme za Kiarabu	2027	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
63	Ubalози wa Tanzanian Nchini, Burundi	2028	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
64	Ubalози wa Tanzanian Nchini Malawi	2030	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
65	Ubalози wa Tanzanian Nchini Brazil	2031	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
66	Ubalози wa Tanzanian Nchini Malasia	2032	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
67	Ubalози wa Tanzanian Nchini Uholanzi	2033	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
68	Ubalози wa Tanzanian Nchini Comoro	2034	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
69	Wakala wa Mafunzo ya Takwimu Mashariki mwa Afrika	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
70	Wakala wa Mbegu za Miti Tanzania	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
71	Wakala wa Mafunzo ya Kimataifa	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
72	Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
73	Wakala wa Serikali Mtandao	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
74	Wakala wa Utafiti wa Miamba Tanzania	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
75	Wakala wa Usajili na Utoaji wa Leseni za Biashara	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha

Na.	Jina	Fungu Na.	2017/18	2016/17	2015/16
76	Wakala wa Uchimbaji wa Visima na Mabwawa	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
77	Wakala wa Elimu ya Uvuvi na Mafunzo	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
78	Chuo cha Mafunzo ya Mifugo	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
79	Wakala wa Umeme, Mitambo na Ufundi Tanzania	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
80	Wakala wa Vipimo Tanzania	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
81	Wakala wa Mbegu za Kilimo	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
82	Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
83	Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
84	Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
85	Wakala wa Afya na Usalama Sehemu za Kazi	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
86	Chuo cha Maji	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
87	Mamlaka ya Mapato Tanzania - Matumizi	Mamlaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
88	Bodi ya Bonde la Maji, Ziwa Rukwa	Bodi	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
89	Bodi ya Bonde la Maji Ziwa Victoria	Bodi	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
90	Bodi ya Bonde la Maji Ziwa Tanganyika	Bodi	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
91	Bodi ya Bonde la Maji Rufiji	Bodi	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
92	Bodi ya Bonde la Maji Ruvuma na Pwani ya Kusini	Bodi	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
93	Mfuko wa Misitu Tanzania	Mfuko	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
94	Mfuko wa Mikopo Hazina	Mfuko	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
95	Mfuko wa Kulinda Wanyamapori Tanzania	Mfuko	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha

Na.	Jina	Fungu Na.	2017/18	2016/17	2015/16
96	Mfuko wa Uwezeshaji Maendeleo ya Madini	Mfuko	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
97	Mfuko wa Maji	Mfuko	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
98	Mfuko wa Usimamizi na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika	Mfuko	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
99	Mfuko wa Taifa wa Usimamizi wa Majanga	Mfuko	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
100	Mamlaka ya Usambazaji Maji Safi na Maji Taka Wanging'ombe	Mamlaka ya maji	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
101	Mamlaka ya Usambazaji Maji Safi na Taka Handeni	Mamlaka ya maji	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
102	Mamlaka ya Usambazaji Maji Safi na Maji Taka Makonde	Mamlaka ya maji	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
103	Chuo cha Usimamizi wa Mahakama	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
104	Chuo cha Uongozi	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
105	Chuo cha Rasilimali Madini	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
106	Chuo cha Utafiti wa Mifugo Tanzania	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
107	Baraza la Wataalamu wa Mifugo Tanzania	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
108	Baraza la Wataalamu wa Macho	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
109	Bodi ya Uratibu wa Taasisi Zisizo za Kiserikali	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
110	Mkakati wa Kukuza na Kuratibu Biashara Tanzania	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
111	Taasisi ya Kuthibitisha Ubora wa Mbegu Tanzania	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
112	Mamlaka ya Vitambulisho vya Taaifa	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
113	Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha

Na.	Jina	Fungu Na.	2017/18	2016/17	2015/16
114	Mpango wa Kujitathmini Kwa Nchi za Afrika	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
115	Shirik la Uzalishaji Mali - Makao Makuu	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
116	Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
117	Chuo cha Maendeleo ya Tengeru	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
118	Baraza la Wataalamu wa Mionzi na Picha	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
119	Bodi ya Maabara Binafsi ya Afya	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
120	Bodi ya Ushauri Hospitali Binafsi	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
121	Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi	99	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo
122	Wakala wa Barabara Tanzania	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo
123	Wakala wa Umeme Vijijini	Wakal	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo
124	Chuo cha Sheria Tanzania	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo
125	Idara ya Ulinzi - SUMA	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo
126	Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha	70	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala mengine
127	Sekretarieti ya Mkoa wa Kigoma	74	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo
128	Sekretarieti ya Mkoa wa Ruvuma	82	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo
129	Manyara Regional Secretariat	95	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo
130	Ubalozi wa Kudumu Umoja wa Mataifa - Marekani	2011	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo
131	Ubalozi wa Tanzania Nchini Marekani	2018	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala mengine

Na.	Jina	Fungu Na.	2017/18	2016/17	2015/16
132	Taasisi ya Mafunzo ya Uhasibu Tanzania	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala mengine
133	Ofisi ya Makamu wa Rais	31	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo
134	Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora	32	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo
135	Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Maadili ya Umma	33	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo
136	Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki	34	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo
137	Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknologia na Mafunzo ya Ufundi	46	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo
138	Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto	53	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo
139	Wizara ya Nishati na Madini	58	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo
140	Ubalози wa Tanzania, Abuja	2005	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo
141	Ubalози wa Kudumu kwenye Umoja wa Mataifa Nchini Uswisi	2020	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo
142	Wakala wa Huduma za Misutu Tanzania	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo
143	Chuo cha Taifa cha Utalii	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo
144	Wizara ya Katiba na Sheria	41	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo	Hati inayoridhisha
145	Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake	Mfuko	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo na masuala mengine	Hati inayoridhisha
146	Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro	75	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo na masuala mengine	Hati inayoridhisha na masuala mengine

Na.	Jina	Fungu Na.	2017/18	2016/17	2015/16
147	Tume ya Taifa ya Umwagiliaji	5	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
148	Wakala wa mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam	Wakala	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
149	Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela Afrika	TN	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
150	Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto	52	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo
151	Wizara ya Maliasili na Utalii	69	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo
152	Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga	86	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo
153	Mahakama ya Tanzania	40	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
154	Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano	98	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
155	Mfuko wa Ufadhili wa Pembejeo za Kilimo	Mfuko	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha
156	Sekretarieti ya Mkoa wa Njombe	54	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo	Hati inayoridhisha
157	Wakala wa Majengo Tanzania	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo	Hati inayoridhisha na masuala mengine
158	Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo
159	Ofisi ya Rais - Idara ya Usimamizi wa Nyaraka na Kumbukumbu	4	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo	Hati inayoridhisha
160	Jeshi la Kujenga Taifa	39	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo	Hati inayoridhisha
161	Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano	62	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo	Hati inayoridhisha
162	Ubalozi wa Tanzania Nchini Msumbiji	2008	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo	Hati inayoridhisha

Na.	Jina	Fungu Na.	2017/18	2016/17	2015/16
163	Nyumbu	OI	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo	Hati inayoridhisha
164	Baraza la Wataalamu wa Maabara za Afya	OI	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo	Hati inayoridhisha
165	Tume ya Pamoja ya Fedha	10	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
166	Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi	43	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
167	Ofisi ya Rais- Tume ya Utumishi wa Umma	94	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
168	Sekretarieti ya Mkoa wa Mbeya	78	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
169	Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza	81	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
170	Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora	85	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
171	Sekretarieti ya Mkoa wa Kagera	87	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
172	Ubalozi wa Tanzania Nchini Misri	2003	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
173	Wakala wa Huduma za Manunuzi Serikalini	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
174	Bodi ya Bonde la Maji la Ziwa Nyasa	Bodi	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
175	Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo	Mfuko	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
176	Shirika la Mzinga	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
177	Shirika la Uzalishaji Magereza	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
178	Idara ya Kilimo na Viwanda-SUMA	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
179	Idara ya Zana za Kilimo - SUMA	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
180	Idara ya Ujenzi - SUMA	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
181	Mamlaka ya Mapato Tanzania - Mapato	Mamlaka	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
182	Kampuni Tanzu ya Mzinga	TN	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka
183	Ubalozi wa Tanzania, Kuwait	2035	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Haikuwepo
184	Hesabu Jumuiifu za SUMA JKT	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Haikuwepo
185	Bodi ya Filamu Tanzania	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Haikuwepo

Na.	Jina	Fungu Na.	2017/18	2016/17	2015/16
186	Baraza la Wataalamu wa Afya ya Mazingira	TN	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Haikuwepo
187	Sekretarieti ya Mkoa wa Songwe	90	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Haikuwepo
188	Mfuko wa Bodi ya Barabara (Fungu 98)	Mfuko	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Haikuwepo
189	Mfuko wa Maendeleo ya Hatimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea	Mfuko	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Haikuwepo
190	Ubalozi wa Tanzania Nchini Ufaransa	2013	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Haikuwepo
191	Ofisi ya Ushauri Mafuta na Gesi	11	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Haikuwepo
192	Mfuko wa Taifa wa Mambo ya Kale	mfuko	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha	Haikuwepo
193	Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzanai	TN	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo	Hati inayoridhisha	Haikuwepo
194	Mfuko wa Taifa wa Uwekezaji wa Maji	Mfuko	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo na masuala mengine	Haikuwepo
195	Mfuko wa Dhamana ya Rais	Mfuko	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo	Haikuwepo
196	Msajili wa Hazina	7	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo	Hati yenye shaka
197	Sekretarieti ya Mkoa wa Rukwa	89	Hati inayoridhisha	Hati inayoridhisha na masuala mengine	Hati isiyoridhisha
198	Wakala wa Ndege za Serikali	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
199	Wakala wa Maabara za Mifugo Tanzania	Wakala	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
200	Baraza la Madawa Tanganyika	TN	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha
201	Baraza la Famasia	TN	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Haikuwepo
202	Ubalozi wa Tanzania Nchini Ubeligiji	2019	Hati inayoridhisha	Hati yenye shaka	Hati inayoridhisha na masuala ya msisistizo
